

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Tatu – Tarehe 8 Mei, 2014

(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job J. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA,
UTAWALA BORA NA MAHUSIANO NA UTARATIBU:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 20

Kuhamisha Soko la Mwika

MHE. DKT. AUGUTINE L. MREMA aliuliza:-

Soko la Mwika liko barabarani na kuna hatari ya wananchi kugongwa na magari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta eneo kubwa na kuhamisha soko hilo ili kukwepa athari hizi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Mwika liko katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi karibu na barabara. Soko hili lina ukubwa wa ekari 2.5 na idadi ya wafanyabiashara wanaotumia soko hili ni kati ya 1,000 hadi 1,500. Kimsingi kuna ongezeko kubwa la wafanyabiashara kufuatia mahitaji ya walaji ambao wanajumuisha wananchi wa Kata ya Mwika Kaskazini na Mwika Kusini.

Kwa kutambua changamoto ya soko hili kuwa karibu na barabara, Halmashauri inaandaa mpango wa kuboresha soko hilo ili liwe la kisasa na kuondoa athari za ajali katika eneo hilo. Mpango uliopo wa Halmashauri ni kukopa katika Bodi ya Mikopo katika Serikali za Mitaa, yaani the *Local Government Loans Board* ili kutekeleza mpango huo. Kwa sasa Halmashauri iko katika hatua ya upembuzi yakinifu wa eneo hilo ili kujua gharama zitakazohitajika kukamilisha kazi hiyo. Wakati mpango wa muda mrefu wa kuboresha soko hilo unaendelea, Halmashauri imewasilisha maombi kwa Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Kilimanjaro kwa barua ya tarehe 17 Januari, 2014 ili iweze kuruhusu ziwekwe alama na tahadhari kwa maana ya kuonyesha maeneo ya kuvukia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuona umuhimu wa kuchukua tahadhari na kuona haja ya kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao katika soko hilo. Aidha, napenda kutoa rai kwa wananchi kuzingatia Sheria za Barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima. Vilevile wafanyabiashara wote wanakumbushwa kutumia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya biashara na kuacha kuweka bidhaa barabarani kwa ajili ya usalama wao na mali zao.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Kwa kuwa, wewe Naibu Waziri wa TAMISEMI na umefanya kazi nzuri kwenye Jimbo langu hasa ulivyonisaidia ile barabara ya Uchira, Kisomachi, Kwalaria, kuna Shilingi milioni 300 zilitaka kuibiwa ukazizuia, sasa naomba nikuulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni kuhusu ushuru unaotozwa kwa wafanyabiashara pale Mwika Sokoni. Tumeona kwamba biashara wanayofanya, wanafanya barabarani. Mwanzoni walivyokuwa wanapakia maparachichi na nini, tani moja ya Fuso ilikuwa inatozwa Sh. 20,000/= wakapandisha kuwa Sh. 40,000/=. Fuso *diff* mbili wakapandisha kutoka Sh. 20,000/= mpaka Sh. 60,000/= wakafanya wale wafanyabiashara wanahangaika, hawajui wafanye nini. Hilo la kwanza. Sijui ni nini msimamo wa Serikali kuhusu huo ushuru.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

La pili, ni wale wafanyabiashara wadogo wadogo akina mama wetu ambao walinichagua mimi na Mheshimiwa Rais; mtu ana ndizi kwenye malboro anatembea nazo tena hapo barabarani; karanga, nini anatozwa Sh. 300/= . Naomba niambiwe msimamo wa Serikali hii, itasaidiaje wale wananchi wa pale Sokoni Mwika waweze kufanya biashara kwa amani na kwa starehe? Jibu!

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwanri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Kwanza, namshukuru kwa shukrani zake lakini la pili kuhusu ushuru ambao Mheshimiwa Lyatonga Mrema anauzungumzia, hii siyo mara yake ya kwanza kuzungumzia hapa. Mara nyingi sana amekuwa akijitokeza hapa wakati wa Bajeti na kipindi hiki sasa tunamwona amerudi tena.

Tatizo hili lilikuwepo na tukazungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, anaitwa Mponzi, tukamwambia kumekuwa na haya malalamiko. Nami ninavyokumbuka, ushuru huu ulishuka kutoka Sh. 40,000/= kwa Fuso ukaenda kwenye Sh. 20,000/=. Ulibadilika huu. Sasa umeshuka, umerudi hapa. Mheshimiwa Mbunge utatusaidia kufuatilia kujua kwamba inaendelea hivyo au haiendelei hivyo.

La pili, hili swali la pili analoliuliza linalohusu kitu kinachoitwa Kodi Ushuru Wenye Kero, walikuwa wanaitwa *Nuisance Taxes*. Hili nataka niliseme hapa kwasababu nimemsikia Waziri wa Nchi akizungumzia kuhusu Halmashauri na mkakati wa kuongeza mapato ya Halmashauri. Wakati alipokuwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Bazil Mramba, ushuru huu uliondolewa kwasababu ulionekana unakuwa kero. Kwanza gharama ya kwenda kutoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alinituma Kigoma kurudi kule mara ya pili kwenda ku-*demonstrate*. Naomba ni-*demonstrate*. Wanaozungumzwa hapa ni wale wanaobeba samaki kwenye *ki-table* au kwenye ungo, kwenye *tray*, wanasema haya samaki! Haya samaki tena! Haya samaki! Wateja wanasema, samaki! Anakwenda anauza. Maana watatoka watu hapa watakwenda na magunia wamekaa pale wanasema tuwaambie ushuru walipe. Wale wanaouza vitumbua; haya vitumbua! Haya vitumbua! Vitumbuaaa! Ameshikilia hivi, hakai mahali pamoja; anatembea kwenye soko hivi, anatoka nje, anakwenda ndani. Ushuru huo umepigwa marufuku na Serikali! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mwananchi anayezungumzwa hapa ni mwananchi ambaye anakwenda kujikimu. Mwananchi huyu ukiangalia hata anapokwenda sokoni, haendi kwa kupanda pikipiki wala kwa kutumia bajaji, anakwenda kwa mguu. Akifika kule sokoni vitu anavyonunua; ananunua

utumbo wa taulo, utumbo mweupe, sabuni ya kuoga na kufua ni hiyo hiyo ya kufulia. Huyu mama akitoka pale anachukua mafuta ya taa kwa chupa ile ya Kilimanjaro nusu. Hawa wananchi ndiyo ambao Serikali imesema wasitozwe ushuru wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge mwende mkatusaidie kwenye hilo jambo. Mheshimiwa Lyatonga Mrema nakushukuru kwa kulileta hili jambo hapa. Lakini wale akina mama wanaokwenda na Fuso pale na mikungu ya ndizi inayotoka Vunjo, inakwenda Arusha na Tanga, wale wanalipa ushuru kwasababu wanafanya *business*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Kakoso.

Na. 21

Tatizo Sugu la Maji Mpanda Vijijini

MHE. MOSHI S. KAKOSO aliuliza:-

Kuna tatizo sugu la maji katika Jimbo la Mpanda Vijijini.

Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza tatizo hilo hasa katika vijiji vya Kamsanga, Bugwe, Sibwesa, Mpemba, Mwese na Bujombe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mpanda inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 179,136 ambapo kati yao wakazi 85,985 sawa na asilimia 48, wanapata huduma ya maji safi na salama. Hivyo bado iko changamoto ya upatikanaji wa huduma hii kwa wakazi wa Wilaya hii. Ili kutatua tatizo la maji katika vijiji, hivyo Serikali inatekeleza mradi wa maji wa kisima kifupi kimoja katika Kijiji cha Kamsanga na tayari upimaji wa eneo la kuchimba kisima kirefu umefanyika na kitachimbwa kabla ya mwezi Juni, 2014.

Vilevile katika Kijiji cha Bujombe katika bajeti ya mwaka 2013/2014 kimetengewa Shilingi milioni 8.0 kwa ajili ya kisima kifupi kimoja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Mwese Serikali kwa kushirikiana na Kanisa Katoliki katika mwaka 2013/2014 imepanga kutumia Shilingi milioni 65, kwa ajili ya ujenzi wa maji mserereko utakaohudumia wananchi wengi zaidi kukiwa na vituo vya kuchotea maji vitano.

Aidha, kijiji hiki pamoja na Kijiji cha Mpembe vimeingizwa katika Mpango wa Kuleta Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ambapo miradi ya maji yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.4 inatarajiwa kujengwa ifikapo 2015/2016.

Kijiji cha Sibwesa kina visima vifupi viwili, na mwaka huu wa fedha 2013/2014 Serikali imetenga Shilingi milioni 53 kwa ajili ya uchimbaji wa kisima na ujenzi wa lambo kwa matumizi ya mifugo kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imepokea kiasi cha Shilingi milioni 742.6 kwa mwaka wa fedha 2013/2014, fedha hizi zikiwa ni kuendelea kutekeleza miradi yote ya maji kama ilivyotajwa hapo awali.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kiasi cha fedha kilichobaki kiweze kupatikana kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Katika bajeti ya mwaka 2014/2015, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imetenga jumla ya Shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 15 Wilayani humo miradi hii itakapokamilika inatarajiwa kuhudumia wananchi wapatao 28,886.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vingine vikiwemo Kabage na Bugwe kufanyika kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado kuna changamoto kubwa sana ambazo Serikali imekuwa ikichelewa kupeleka fedha za miradi ya maji ina miradi ya maji ambayo mpaka sasa fedha zake bado hazijafika, mradi wa kijiji cha Majalila wenye thamani ya shilingi milioni minne na arobaini na tatu na mradi wa Kijiji cha Igagara wenye thamani ya Shilingi milioni 407. Bado hizo hazijafika kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa miradi iliyotengwa.

Vile vile kuna eneo la Kijiji cha Mwese, kwenye Kituo cha Afya bado zile fedha hazijafika, na ni eneo muhimu sana ambalo linahitaji kupata maji ukizingatia kwamba wananchi walio wengi wanahitaji huduma hasa wale

wanaokuwa na matatizo kwenye Kituo cha Afya: Je, Serikali itapeleka fedha hizo kwa wakati muafaka lini?

Swali la pili, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri alifika kwenye Kijiji cha Katuma na akatoa maagizo; mpka sasa eneo lile halina maji na yeye anafahamu: Je, ana majibu gani kwenye kijiji ambacho na yeye alikwenda kuwahakikishia wananchi wa pale?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso, majibu ya maswali hayo ya nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwanri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kakoso amesema kwamba tulikwenda wote. Huko kote ninakosema mpaka kule Mwese, Mpanda tumekwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hiyo Mwese, Mpanda anayozungumza hapa. Mwese Mpanda tumepeleka Shilingi milioni 65 ambazo tulikuwa tunasaidiana na Baba Padri pale anaitwa Martini Kapufi, amefariki dunia. Tukasimamisha lile zoezi tukasema tusimamishe kwanza mpaka tumalize mambo ya mazishi na nini. Ndiye aliyetupokea tukala chakula cha mchana pale nyumbani kwake. Hilo eneo analozungumza kwamba lina matatizo ya maji, huyu Padri ndiye aliyekuwa anashirikiana na sisi kutusaidia jambo hilo. Nichuke nafasi hii kuwapa pole wananchi wote wa Mwese kule Mpanda kwa msiba walioupata.

Kwa hiyo, zile fedha zimekwenda na tuna uhakika kwamba zimekwenda. Katika hivi vijiji vyote anavyozungumza na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anafuatilia kwa karibu jambo hili. Ukiacha Bugwe na ukiacha Kabage, haya maeneo mengine yote tunayozungumza hapa Mheshimiwa Kakoso yote yako kwenye programu.

Programu ya mwaka huu, Shilingi milioni 802 mwaka huu wa fedha unaokuja milioni 806. Mpango ule mkubwa wa *BRN* tunaozungumza, *1.4 billion*. Mimi naamini kwamba katika maeneo haya yote na lile aeneo ambalo anasema kwamba tulikwenda wote kwa pamoja nikatoa ahadi, tuna hakika kwamba tutalifanyia kazi na hizi hela zitapatikana kwa ajili ya kumaliza kazi hiyo.

Mimi naomba tu Mheshimiwa Mbunge aniamini kwasababu tumekwenda kule, anachosema Mheshimikwa Kakoso ni kweli. Hawa wananchi wana matatizo ya maji, wako mbali na Mji wa Mpanda hujapata kuona. Unaingia katika msitu, unakwenda kutokezea huko kwenye vijijiji. Kwa hiyo, nitashirikiana

naye kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa nchi kuhakikisha kwamba hata hiki kijiji alichokitaja hapa kinapata maji safi na salama.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee! Oh, hayupo. Basi kwa niaba yake Mheshimiwa Natse. *(Kicheko)*

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22 ya mwezi huu wa nne Mheshimkwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alifika Karatu na kuzindua mradi wa maji katika Mji mdogo wa Karatu. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri kuhakikisha kwamba huduma ya maji katika Mji mdogo wa Karatu siyo hisani bali ni wajibu wa Serikali.

Sasa ahadi ambazo zimetolewa ili kukamilisha ule mradi na wananchi wa Mji wa Karatu wapate maji, shilingi milioni 300 *plus* na milioni 700 kukamilisha ule mradi, naomba kusema kwamba Serikali itatekeleza ahadi hiyo ya Rais lini ili wananchi wa Karatu ndani ya mwaka huu wapate maji kama walivyoahidi?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mchungaji Natse. Mheshimiwa Waziri wa Maji Profesa Maghembe, majibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nijibu swali la nyongeza la Mchungaji Nassir Mbunge wa Karatu.

MBUNGE FULANI: Natse!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Natse! Nisamehe bwana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tarehe 22 Aprili, 2014 Mheshimiwa Rais alifungua mradi wa maji wa Karatu na kuhakikisha kuwa watu wa Karatu wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, alichofanya Mheshimiwa Rais, ni kweli sio kama anawapa zawadi au kitu cha namna hiyo, ila alikuwa anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huo unaendelea kutekelezwa sasa na katika mwaka wa fedha ujao hatua ya pili ya mradi huo itakamilika. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Tuendeleo Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, swali litaulizwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde.

Kukithiri kwa Rushwa Nchini

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Hivi karibuni Taasisi ya Kimataifa ya Kufuatilia Miendendo ya Rushwa Duniani (*Transparency International*) imetoa taarifa inayoonyesha Tanzania imepanda katika nafasi ya tatu kutoka ya nne kwa rushwa na ufiadini wa mali za Umma katika Ukanda wa Afrika Mashariki:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ili kuinusuru nchi yetu na janga hili linalozidi kuongezeka siku hadi siku?

(b) Je, Serikali imekithamini vipi chombo chake cha Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na kuona bado kina sifa ya kuendelea kushughulikia majanga haya ya rushwa?

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) (MHE. GEORGE H. MKUCHIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mhe. Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa zipo Taasisi za Kimataifa zinazojihusisha na masuala ya tathmini ya Utawala Bora katika nchi za Umoja wa Mataifa, katika nchi za Bara la Afrika na nchi za Afrika Mashariki. Matokeo ya tathmini hiyo kwa mwaka 2013 na nafasi ya Tanzania ni kama ifuatavyo:-

- *Transparency International*, imetathmini nchi 182 na Tanzania ilishika nafasi ya 111;

· Taasisi ya Mo Ibrahim, imetathmini nchi 53 za Bara la Afrika na Tanzania ilishika nafasi ya 17; na

· *Transparency International*, Tawi la Afrika Mashariki, jumla ya nchi tano za Afrika Mashariki, Tanzania imeshika nafasi ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo, takwimu hizi zinaonyesha kuwa Tanzania imeendelea kushika nafasi ya pili katika ukanda wa Afrika Mashariki na siyo nafasi ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maswali yake, sehemu (a) na (b):-

(a) Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua zifuatazo katika kupambana na janga la rushwa:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(i) Kurekebisha Sheria ya Kupambana na rushwa kwa kuongeza wigo wa makosa ya rushwa kutoka manne hadi 24 sasa;

(ii) Kutoa elimu kuhusu madhara ya rushwa kwa njia mbalimbali kama vile Mikutano, Semina, Makongamano, Vipidi vya Redio na Televisheni na kufungua Klabu za Kupambana na Rushwa katika Shule za Sekondari na Vyu;

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa kazi iliyofanyika inalingana na thamani ya fedha zilizotolewa; na

(iv) Kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria baada ya kuwa na ushahidi wa kuhusika kwao na vitendo vya rushwa.

(b) Serikali inathamini sana kazi inayofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Ili kuona chombo hiki kinafanya vizuri zaidi, Serikali imechukua hatua za kukiimarisha kwa kufungua Ofisi katika kila Mkoa na Wilaya Tanzania nzima, kuajiri Watendaji wapya wenye weledi na taaluma mbalimbali na kuwapa mafunzo mara kwa mara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib, swali la nyongeza.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Mwaka 2009 TAKUKURU ilipatiwa fedha, Shilingi bilioni sita kutoka mfuko wa PSPF kwa ajili ya kufanikisha shughuli zake za kupambana na rushwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya pesa hizi kutumika yalitegemewa kuwakamata na kupeleka panapotakiwa wahusika wa rushwa, matokeo yake tunaendelea kushuhudia anakamatwa na kushitakiwa kwa Hakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa kesi za Sh. 50,000/= wanakamatwa na *traffic* kwa kesi za Sh.10,000/= ilhali wala rushwa wakubwa wa nchi hii wanaendelea kuachiwa. (Makofi)

Je, hii ndiyo *value for money* ya pesa zilizotolewa kutoka mifuko yetu ya jamii? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kila anaendelea nafsi yake na kuitendea haki, hakuna asiyekubali tatizo la rushwa Tanzania linaongezeka. Je, Mheshimiwa Waziri, kuanzia wewe mwenyewe kabla sisi Wabunge hatujamshauri Mheshimiwa Rais akufute kazi kwa kushindwa kusimamia chombo hiki muhimu, huoni sasa ni muda muafaka wa kumwandikia Mheshimiwa Rais akufute kazi kwa sababu umeshindwa kusimamia Taasisi hii ya Kupambana na Rushwa Tanzania? (Kicheko/Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Mheshimiwa Mguchika, majibu.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu maswali mawili ya nyongeza, kwanza ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Haji kwa jinsi anavyofuatilia kuona nchi yetu inapambana vilivyo na madhara ya rushwa.

Baada ya hapo, ningependa kujibu maswali yake kama ifuatavyo:-

Kwanza anaeleza juu ya fedha zilizotolewa, lakini kikubwa anachosema ni kwamba nchi hii, watu wanaokamatwa na rushwa ni wale wanaofanya makosa madogo madogo na wakubwa wanaachwa. Ningependa nilikanushe hilo. Nakanusha hilo kwa sababu miongoni mwa watu ambao sasa wanatumikia vifungo ni pamoja na hao Viongozi wakubwa waliokuwepo katika Taasisi za Umma. Hivi tunavyozungumza, Mahakamani wapo Mawaziri, wapo Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, kwa hiyo, sikubaliani naye kwamba Serikali hii kuna watu inawaogopa wanapokwenda kinyume katika suala la rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la pili; kwa vile lile la mwanzo nimelikanusha na alitaka nijuzulu maana pesa zile hazikufanya kazi kwa sababu wanaoitwa mapapa hawakamatwi, mimi kwa sababu naendelea kuamini kwamba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na rushwa haibagui katika kukamata watu, sijaona sababu ya kujuzulu.

Mwisho, nataka niseme hivi, suala la kupambana na rushwa nchi hii, haliwezi kuwa la Waziri wa utawala bora peke yake wala Rais, wala Waziri Mkuu. Rushwa inafanyika Konde, Waziri wa utawala bora yupo Dar es Salaam na Dodoma. Ni jukumu la wananchi wa Konde, ni jukumu la Watanzania Bara na Visiwani, pale ambapo kuna vitendo vya rushwa kushirikiana na vyombo vya dola hasa Takukuru kwa kuwapa habari, kushirikiana kwakuwa tayari kutoa ushahidi Mahakamani. Watanzania wote tukishirikiana kupambana na rushwa, rushwa katika nchi yetu itapungua na siyo suala la Waziri peke yake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Lekule Laizer, swali la nyongeza!

MHE. LAIZER M. LEKULE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwakuwa suala la hili rushwa limekithiri na Serikali inajua na fedha za *World Bank* za maji Longido zimeliwa zaidi ya Shilingi bilioni moja na Serikali inafahamu na Waziri wa Maji anafahamu:

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wale walio kula hizo fedha na wananchi wa Longido hawana maji na bado wanadunda tu baada ya kumaliza Shilingi bilioni moja?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, namwona Waziri wa Maji Profesa Maghembe.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na udhaifu katika kutekeleza miradi ya Maji katika Wilaya ya Longido na kwamba tumeiandikia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali aweze kwenda kutuma timu maalum pale wafanye ukaguzi maalum.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, swali la nyongeza.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Suala la rushwa ni sawasawa na mwizi anapoiba, ni kwamba kuna mahali kuna soko. Sehemu kubwa sana za fedha zinazohamishwa katika nchi mbalimbali hunatokana na mabenki yaliyomo ndani ya nchi kushirikiana na mabenki yaliyomo nje.

Hivi karibuni Chama cha Wabunge kinachoshughulikia rushwa, kilipitisha Azimio kuomba nchi mbalimbali kwamba sasa hii rushwa kubwa ichukuliwe kama ni ile *crime against humanity*.

Je, nchi yetu inajipangaje katika kufanya hilo ili kupungua hii *illicit money* inayotoka katika nchi yetu kwenda nchi nyingine iweze kudhibitiwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Mkuchika.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Chama cha Wabunge Wanaopambana na Rushwa Duniani (APNAC), kimetoa pendekezo hilo la kufanya kwamba rushwa iwe ni *crime against humanity*. suala hili hata linaungwa mkono na APNAC Tawi la Tanzania.

Sasa kwamba Serikali tunajipanga vipi, sisi tunachukulia kwamba suala hili litatusaidia katika kupambana na rushwa. Kwa sababu moja kati ya matatizo tunayoyapata katika kupambana na rushwa katika nchi yetu ni pale ambapo ile kesi ya mtuhumiwa inahusika kufanya uchunguzi nchi za nje. Sasa ili ufanye uchunguzi nchi za nje, ni lazima upate ushirikiano wa ile nchi kule. Usipopata ushirikiano, ndiyo maana kesi hizi kubwa wakati mwingine inachukua muda mrefu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Sisi tumejipanga vipi kama Serikali? Jambo hili tunalikaribisha endapo litapita katika vikao na litafanikiwa na sisi Tanzania tunashiriki katika Mikutano ya Kimataifa ya kupambana na rushwa. Tutaunga mkono suala hili na likikubalika, tutafanya kazi bega kwa bega na nchi nyingine. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho, Mheshimiwa Leticia Nyerere!

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rushwa siyo linajitokeza hivi hivi. Ni lazima Serikali yetu iwe makini iangalie vyanzo vya rushwa ikiwemo mishahara midogo, mahitaji makubwa. Kwa mfano, Kiongozi wa ngazi ya juu unamshangaa anachukua rushwa, pengine mahitaji yake ni makubwa kutokana na wadhifa wake.

Kwa hiyo, Serikali sasa itakuwa tayari kutathmini upya kabisa mishahara na mapato ya wananchi wote wa Tanzania na hatimaye kufanya marekebisha ili tuondokane na aibu hii ya rushwa?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais utawala bora!

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yake, yeye anaamini kwamba nyongeza ya mishahara au mapato makubwa itafuta rushwa katika nchi hii.

Mimi ningeliomba kutofautiana naye kwa sababu kama nilivyoeleza pale awali, miongoni mwa watu ambao wapo Mahakamani, ni wale watu ambao wanalipwa vizuri sana sana ukilinganisha na Watanzania wengine.

Kwa hiyo, kudai na kupokea rushwa ni hulka, ni tabia ya mtu. Kwa hiyo, hata mishahara ikiwa mikubwa haimaanishi kwamba rushwa itatokomezwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyongeza ya mishahara, ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ni Sera ya CCM, ni Sera ya Serikali ya CCM mara kwa mara kuongeza mishahara ya watumishi, kuongeza mishahara hata ya wale waliojariwa katika sekta binafsi ili kuona kama wanaweza kumudu maisha.

Juzi tu Mheshimiwa Rais alikuwa mgeni rasmi katika Sikukuu ya Wafanyakazi, amehaidi nyongeza kwa watumishi. Tutakuwa tunafanya vile kila

mara ambapo uwezo upo. Kwa sababu kuna msemu wa Kiswahili kwamba, wema usizidi uwezo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa tuhamie Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki.

Na. 23

Mbolea Feki

MHE. WARIDE BAKARI JABU aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni mbolea feki isiyokidhi viwango imekuwa ikikamatwa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuikusanya na kuiteketeza mbolea hiyo feki ili kulinda afya za wananchi na uhifadhi wa mazingira?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Jimbo la Kiembe Samaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya kuwepo kwa pembejeo zisizokidhi viwango vya ubora katika soko, Serikali kupitia Sheria ya Mbolea Na 9. ya mwaka 2009 ilianzisha Mamlaka ya Udhubiti wa Mbolea (*Tanzania Regulatory Authority- TFRA*) ili kuhakikisha kuwa mbolea inayotumiwa na wakulima nchini inakuwa kwenye ubora unaotakiwa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhubiti wa mbolea Tanzania pamoja na mambo mengine hufanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa mbolea isiyo na viwango inateketezwa kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa chini ya Kanuni za Sheria ya Mbolea pamoja na Sheria ya Taifa ya Hifadhi ya usimamizi na mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kupitia ukaguzi huo uliofanyika mwaka 2012 na 2013, baadhi ya Makampuni ya Mbolea yaligundulika kuuza mbolea iliyokuwa chini ya viwango. Hatua zilizochukuliwa na Serikali dhidi ya Makampuni hayo ni kusimamisha leseni ya biashara ya mbolea, kusitisha mauzo ya mbolea hizo na kuhakikisha kuwa mbolea hizo zimeondolewa sokoni.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa mbolea hizo hazileti athari katika mazingira, *TFRA* iliyoamuru mbolea hizo zifungwiwe kwenye vyumba maalumu

vinavyolindwa wakati utaratibu wa kuziteketeza ukiandaliwa kwa kushirikiana na wadau wengine. Mamlaka (TFRA) inashirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba vyumba hivyo havifunguliwi na mtu yeyote na kupeleka mbolea hiyo isiyo na ubora sokoni.

Mheshimiwa Spika, kwakuwa mbolea ni kemikali, taratibu za uteketezaji wake zinahitajika umakini wa hali ya juu na wenye kuzingatia sheria za nchi na Mikataba ya Kimataifa inayosimamia mazingira ili kuepusha athari katika mazingira. Mamlaka ya Mbolea kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mkemia Mkuu wa Serikali inakamilisha mwongozo na taratibu za kitaalam zitakazotumika kusimamia uteketezaji wa mbolea zote zisizo na viwango nchini.

NAIBU SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Waride!

MHE. WARIDE B. JABU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Moja, ni Makampuni gani yaliyosimamishwa leseni ya biashara ya Mbolea? Naomba atutajie?

Pili, kwakuwa mbolea hii imekuwa inaathiri sana Wakulima: Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha mbolea hii isiyokuwa na viwango haiingii wala haisambazwi kwa wakulima? Ahsante!

NAIBU SPIKA: Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Zambi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Makampuni ambayo baada ya ukaguzi yalibainika na Mbolea zisizofaa au kuwa chini ya viwango ni pamoja na kampuni *STACO*, *SWISS Singapore* lakini pia ipo Kampuni ya *Mohamed Enterprises*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ya *Mohamed Enterprise* ilikuwa chini ya viwango lakini kupitia Baraza la Usuluhishi la Taifa iliruhusiwa itumike kwenye mashamba yao ya mkonge. Lakini zile nyingine ambazo zilioonekana kweli kabisa hazikidhi viwango, ndiyo hizo ambazo zilifungwa na taratibu nyingine za kuziteketeza zinasubiriwa.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Arfi!

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kumekuwepo na mbolea feki na mbolea zisizokuwa na kiwango na mbolea

ambazo hazihimili katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu na kuharibu ardhi: Je, kuna utafiti wa kina uliofanywa juu ya uharibifu wa ardhi kutokana matumizi ya mbolea hizo?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Zambi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakati mwingine imejitokeza kwamba baadhi ya mbolea zinazotumika maeneo fulani zinaweza zisikidhi viwango kwa sababu tu ya udongo kuwa tofauti kati ya eneo moja na eneo lingine. Lakini ni ukweli pia kwamba wataalam wetu wamekuwa wakijitahidi sana kufanya utafiti huo na mara nyingi mbolea tunapozipeleka kwenye matumizi katika maeneo mbalimbali huwa yanazingatia taarifa ambazo wataalam wetu wamekuwa wanatupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo ni kwamba unaweza kukuta katika eneo moja kuna maeneo mbalimbali ya tabaka, hivyo inaweza ikawa vigumu sana kama una maeneo tofauti tofauti katika eneo moja. Lakini kwa ujumla wataalam wetu wanajitahidi sana na ushauri wao ndiyo tunaotumia katika kusambaza mbolea hapa nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jitu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa naomba kuuliza: Je, ni lini Serikali itaweka maabara ya kupima udongo, mbolea na madawa ya kilimo katika sehemu mbalimbali ili haya matatizo tunayopata ya viwango vya mbolea, madawa na pembejeo nyingine ziweze kudhibitiwa huko huko katika maeneo ya karibu na wakulima waweze kutumia aina ya mbolea ambayo inahitajika kutokana na mahitaji katika udongo wao? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Ushirika.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jitu Soni anazungumzia kuhusu kuweka maabara ya kupima mbolea na udongo. Lakini naomba niseme kwamba tunao wataalam ambao kazi hizi wanazifanya, ndiyo sababu tunapokwenda kwa mfano kuchunguza mbolea ambayo haina viwango, maana yake Wataalam wana uwezo wa kupima na kubaini mbolea hizo kwamba hazifai. Tungekuwa hatuna wataalam, tungesema hizi tunazipeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu udongo, wataalam wetu wapo katika Vyuo vyetu vya Utafiti, hususan pale Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine,

ambapo Mheshimiwa Soni ni Mjumbe wa Bodi, anafahamu kabisa tunao wataalam ambao wana elimu ya kutosha kwa maana ya kupima udongo na kwamba ni udongo gani unafaa kwa kilimo cha namna gani katika nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa David Silinde, swali la mwisho kabisa katika eneo hili.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mbolea feki nchini imesambazwa kwa sababu nyingine wakulima wetu wamekuwa wakiitumia na matokeo ya wakulima waliotumia mbolea feki hususan kama kule Mbozi na Momba ni mazao yako kuungua na kukosa mavuno yaliyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ituambie ni namna gani inaweza kufidia wale wote walioathirika na mbolea feki?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya wakulima kule Mbozi kwa maana ya Mbozi Magharibi na Mbozi Mashariki na maeneo mengine nchini kwa kweli, wametumia mbolea ambayo baadaye ilikuja kuthibitika kwamba haikuwa na viwango au ilikuwa feki, inawezekana ikawa mbolea, mbegu au dawa zenyewe za kuua magugu. Sasa anasema tunafanya utaratibu gani kuwafidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa fidia una misingi yake na taratibu zake. Huwezi kumfidia tu mtu kwa sababu anasema mimi mbegu zangu hazikuota, mimi mbolea haikuwa sahihi, sijui dawa hizi hazikuua magugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni kwamba, kwanza tunawaomba wakulima wanaponunua mbolea, dawa na madawa yote wanayotumia kwenye kilimo, ni lazima wadai risiti kutoka kule wanakonunua. Wanapodai risiti kama ikithibitika sasa kwamba kweli mbolea hiyo ndiyo iliyosababisha, basi utaratibu ambao unaweza ukafanywa na Serikali ni kuwafidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wakumbuke kwamba ni Bunge hili hili, tumetunga Sheria ya Fidia. Tuliondoa sheria ya mwanzo ya mwaka 1962 ambayo ilikuwa hairuhusu fidia. Kwa hiyo, mwaka 2010 katika Bunge hili, tulitunga sheria ambayo inaruhusu fidia lakini tutafidia tu pale kama wakulima hawa watathibitisha kwamba mbolea hizo au mbegu hizo au dawa hizo ndizo zilizosababisha na baada ya wataalam wetu kutathibitishia na wao wakionesha vielelezo, basi Serikali itakuwa tayari kuwafidia.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Maswali yanatosha. Nilitarajia Waheshimiwa Wabunge mtauliza kuhusu ubora wa mbolea ya Minjingu lakini haikuwa hivyo.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondo Kaskazini.

Na. 24

Baadhi ya Mazao Kutosimamiwa na Bodi za Mazao

MHE. ZABEIN M. MHITA aliuliza:-

Baadhi ya mazao ya kilimo yanasimamiwa na Bodi ya Mazao hayo kama vile Pamba, Korosho na kadhalika:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu usimamizi wa mazao mengine ambayo wakulima hawanufaiki kutokana na wanunuzi wa kati kuingilia biashara hiyo kwa manufaa yao kuliko wakulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondo Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa kwa Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Na. 19 ya mwaka 2009. Madhumuni ya kuanzishwa Bodi hiyo ilikuwa ni kulisimua ushindani katika biashara ya nafaka na mazao mengine na kuwa chombo cha mfano katika biashara ya mazao hayo ili kuleta ushindani na sekta binafsi katika biashara ya nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ili kuwahakikishia wakulima soko la uhakika kwa mazao aina ya nafaka na mazao mchanganyiko ambayo hayakuwa na Bodi. Kuanzishwa kwa Bodi hii kunatoa fursa kwa wakulima wa nafaka pamoja na mazao mengine kuwa na soko la uhakika lenye bei ya ushindani.

Aidha, Bodi inaendelea kujenga uwezo ambapo watumishi 37 wameajiriwa pamoja na kufanya matengenezo katika kinu cha Iringa ili kutekeleza mpango mkakati wa Bodi wa kuwafikia wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iliyoanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, yaani *Cereals and other Produce Board* pia ilirekebisha sehemu

ya Sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka 1991 na kutoa fursa ya kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa nafaka na mazao mchanganyiko, yaani *Cereals and other Produce Regulatory Authority* yenye jukumu la udhibiti na usimamizi wa biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza mchakato wa uundwaji wa mamlaka hii ili ianze kutekeleza jukumu lake la udhibiti na usimamizi wa biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko kwa kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei nzuri na kudhibiti mwenendo wa biashara ya mazao nchini.

Aidha, mamlaka ya udhibiti wa nafaka na mazao mchanganyiko itashirikiana na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na Vyama vya Ushirika katika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei nzuri wakati wa kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko itashirikiana na *NFRA* kuanzisha usindikaji wa tani 30,000 za nafaka katika kinu cha Iringa. Utaratibu huu utapanua wigo wa soko la nafaka zinazozalishwa na wakulima, hususan mahindi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zabein Mhita!

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, pamoja na kuwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imeanzishwa, kusema kweli bado haifahamiki kwa wananchi walio wengi hasa wakulima. Je, Bodi ina mpango gani wa kujitangaza ili wakulima waweze kunufaika nayo? (*Makofi*)

Swali la pili, pamoja na kuwepo kwa Bodi, wakulima hawajanufaika nayo kwa sababu ulanguzi wa mazao ya wakulima unaendelea. Mfano, walanguzi kujipangia bei na mara nyingi bei inakuwa ni ya chini sana na hili linatendeka sana hususan katika Jimbo la Kondo Kaskazini na ninaamini kabisa kwamba hali hiyo ndivyo ilivyo katika maeneo mengi hapa nchini. Je, Bodi ina mpango gani wa kudhibiti hali hiyo ya ulanguzi kwa wakulima wetu?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Zambi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Bodi haijaitangaza ni kweli inawezekana Bodi hii haifahamiki kwanza kwa sababu ya changamoto za kawaida za kibajeti, lakini sasa tumeanza mkakati wa kutosha kabisa na tumeshaelekeza Bodi yenyewe ianze

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kujitangaza kwa maana ya kuhakikisha kwamba inafanya kazi zake sawasawa. Ndiyo sababu pia tuna Ofisi za Kanda katika maeneo mbalimbali, na Dodoma ni moja ya eneo ambalo tuna Ofisi ya Kanda ya Bodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge aitaafute Ofisi ilipo au anitaafute nimwelekeze Ofisi zilipo ili tuweze kuzungumza nao. Lakini kimsingi tumewapa Bodi jukumu la kuhakikisha kwamba wanafika kwa wakulima na kuweza kuhakikisha kwamba mazao yao yanasimamiwa vizuri. Kwa sababu moja ya jukumu, ni wao kuhakikisha kwamba wanafahamika na wakulima waweze kuwatafuta pale wanapokutana na changamoto za soko kwa maana ya mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, anazungumzia kwamba pamoja na kwamba Bodi imeundwa lakini bado kuna ulanguzi kwa mazao haya mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa naomba nikubaliane naye, lakini naomba niwashauri wakulima na wote ambao wapo kwenye soko hili kwamba dawa pekee ambayo tunaweza tukakabiliana na soko kwa maana ya wanunuzi, wale walanguzi, ni vizuri tukajiunga kwenye vikundi vya ushirika. Tukijiunga kwenye vikundi vya ushirika kwa mazao hata haya mchanganyiko, tunaweza tukawa na nguvu ya soko na nguvu pia za kuweza ku-*bargain* bei na kuhakikisha kwamba tunauza mazao yetu kwa bei nzuri zaidi. Kwa hiyo, tukifanya hilo inaweza ikasaidia sana.

Pia tunao utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Utaratibu huu unaruhusu mazao yote, hasa wakulima wakiweza kujiunga pamoja hususan kwa zao la mahindi, wakikusanya mazao yao, wakati wakisubiri labda bei nzuri ya soko, basi ikawa ni njia moja ya kukabiliana na wale wanunuzi ambao nia yao ni kujinufaisha wao wenyewe wakati wakulima wanaumia.

Kwa hiyok, tuwasihi sana Wakulima waone kwamba umoja ni nguvu lakini pia utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mwaka 2013 kulikuwa na tatizo kubwa sana la soko la mazao mchanganyiko hasa ukizingatia

wakulima wa mahindi na mpunga Mbarari na maeneo mengine walipata shida sana ya soko la mazao yao, na msimu huu ndiyo tunaelekea huko. Je, Serikali inajipangaje kuona kwamba tatizo hilo halijrudii tena?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme kwamba ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote wakajua kwamba Serikali kimsingi haitakuwa na haina uwezo wa kununua mazao yote ya wakulima. Serikali kitu ambacho inafanya ni kuweka mazingira mazuri ya soko kwa ajili ya mazao ya wakulima na ndiyo sababu kama nilivyosema awali nikijibu swali la Mheshimiwa Zabein Mhita, nimesema kwamba ni vizuri wakulima wakajiunga kwenye vikundi vya ushirika, wakawa na utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ili kuhakikisha kwamba wanauza mazao yao pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, tutakachojitahidi ni kuona kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko inafanya kazi yake vizuri kwa kusimamia mazao ya wakulima.

Pia naomba niwaambie wakulima wa Tanzania wote ambao wanajihusisha na biashara ya kilimo na wakulima kwa ujumla kwamba Serikali pia imefungua soko kwa ajili ya kuuza mazao yao nje ya nchi. Kwa hiyo, ni vizuri wafike Wizarani, wajue utaratibu ambao wanaweza kutumia katika kuuza mazao yao nje ya nchi na yote hii itakuwa ni kuhakikisha kwamba wanapata bei nzuri zaidi kwa ajili ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda naomba tuendeleo na utambulisho wa wageni ambapo tuna mgeni wa Mheshimiwa Stephen Wassira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, Ndugu Msafiri Majige kutoka Bunda, karibu sana.

Wageni saba wa Wabunge wa Mkoa wa Pwani kutoka Chama cha Mpira wa Miguu kutoka Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Henry Mpemba. Karibu wale wageni saba kutoka Mkoa wa Pwani, karibuni sana. (Makofi)

Wageni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 250 na Walimu 13 kutoka Kiracha Holly, *Childhood Pre and Primary School*, karibuni sana. Imeandikwa hapa Kiracha naamini siyo Kilaracha. Karibuni sana watoto wetu Bungeni. (Makofi/Kicheko)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ndugu Baraka Chambua Mwakilishi wa *the New Hope Community Development Organization* kutoka Dar es Salaam, karibu pale ulipo.

Wanafunzi 125 na Walimu 5 kutoka *Gonzaga Pre and Primary School* Dar es Salaam. Wale wanafunzi wa *Gonzaga* karibuni sana, mnapendeza kweli na *uniform* zenu. Karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi, Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Luhaga Mpina anaomba mkutane saa 7.00 mchana ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu wakutane Ukumbi Na. 136 Saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi Na. 229 ghorofa ya pili jengo la Utawala saa 7.00 mchana. Katibu tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya Waziri Mkuu Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Kwa kutumia Kanuni ya 68 (7) naomba mwongozo wako juu ya tabia ya Serikali kuleta majibu ya mkato bila kuzingatia taarifa za ukaguzi za CAG na zile taarifa ambazo zinatolewa na Kamati hapa Bungeni, hasa tukizingatia kwamba CAG anafanya kazi kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kipindi cha maswali na majibu, katika swali la nyongeza ambalo ameliuliza Mheshimiwa Lekule Laizer na ambalo lilipatiwa majibu na Mheshimiwa Waziri wa Maji kuhusiana na rushwa na ufiisadi unaofanyika pale Longido katika miradi ya maji, Waziri alisema kwamba atamwomba CAG aende akakague pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ambazo zilitoka kwa mwaka 2011/2012 za CAG tayari zilishaonesha hali halisi ya ufidadi wa miradi ya maji Wilaya ya Longido na hata Kamati yetu ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilishafika Longido na ilishatoa taarifa. Kati ya visima 12 ambavyo vilichimbwa pale, ni visima vitano tu ambavyo vinatoa maji. Mbali ya hilo, kisima kikuu cha Tembo ambacho kiligharimu Shilingi milioni 500 kimefanyiwa ufidadi na kisima kile hadi leo hakina tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Naibu Waziri kwa kutumia Kiti chako utoe mwongozo wako kuhusiana na Serikali kutozingatia taarifa za CAG na taarifa ambazo zinatolewa na Kamati.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Alikuwa ni yeye peke yake, ili tuweze kuendelea? Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu katika hili ni kwamba kwa vile tupo katika kipindi hiki cha bajeti, basi itakapofikia Wizara ya Maji pamoja na mambo mengine watatoa ufafanuzi zaidi kuhusiana na hiki kinachoendelea na miradi ya maji katika Wilaya ya Longido.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa tuendelee na uchangiaji, dakika saba saba kama kawaida. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Waziri Magufuli na atafuatiwa na Mheshimiwa Keissy.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ilivyowasilishwa hapa Bungeni kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya masuala yaliyojitokeza katika kuchangia hoja ya Waziri Mkuu, Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu hali halisi ya mvua zilizonyesha katika maeneo mbalimbali. Napenda nitoe taarifa kwamba Serikali inaendelea kufanya juhudi zote za kuhakikisha zinarudisha mawasiliano katika maeneo yote ambayo ni karibu Mikoa 14 ambapo mvua kubwa sana zimenyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara ya Ndundu Somanga kufikia jana magari zaidi ya 150 yalikuwa yamekwama na juhudi ya kuyatoa zilifanyika. Hata ninavyozungumza kwa sasa hivi mvua zinaendelea kunyesha na tulipopeleka magreda pale nayo yalikuwa yanakwama ndani. Kwa bahati nzuri kufikia jana usiku, mabasi yote 18 yalikuwa yamekwama pale tumeyavuta na yameondoka na malori zaidi ya 23 nayo yote yameondoka. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulihakikishia Bunge hili kwamba ikifika muda wa saa nane hivi leo, tutahakikisha njia yote hiyo itakuwa inajifungua kwa sababu watalaam wapo pale na pia Naibu Waziri nimeituma ameondoka jana usiku, wapo pale kwa ajili ya kuhakikisha mawasiliano katika sehemu hiyo ambayo ni ya kilomita mbili kutoka Somanga inarudi katika hali yake halisi.

Katika sehemu ya Ifakara kwenda Mahenge, pale napo pametokea mvua kubwa sana. Karibu Kilomita tisa zote za kutoka kwenye daraja kwenda kwenye Mji wa Ifakara imefunikwa na maji. Lile tuta lote limefurikwa na maji na kile kivuko imebidi tukisimamisha kwa sababu maji yanayoenda pale ni *speed* kubwa sana. Hata mkandarasi anayejenga daraja pale la Kilombero imebidi ile *draft* ya kwanza aliyokuwa ameiweka kwa ajili ya kutengeneza aito kwa sababu ingeweza kuchukuliwa na maji. Kwa hiyo, tumefanya hivyo na mvua zimeanza kunyesha tangu siku ya Jumapili.

Kwa hiyo hili liko nje ya uwezo wetu, imebidi tusebiri kwanza ili maji yapungue kwa sababu hata lile tuta na yale maji hata mawe huwezi ukayaweka kwenye ziwa ambalo tayari limeshajitengeneza pale. Tuliitaka tutumie feri kuivusha pale kuwa inakuja mpaka karibu kabisa kwenye Mji wa Ifakara, lakini napo isingeweza kufika kwa sababu kuna tuta. Lakini pia hatujatengeneza mahali pa *parking area* kwa ajili ya feri. Kwa hiyo, feri tumeiweka nanga, wananchi wasubiri, wavumilie, hali maji yatakapopungua tutaweza kuishughukia.

Sehemu nyingine ni ya Mafinga-Temeta katika sehemu ya Kinyanabo. Pale napo kuna *landscaping*, barabara ile nayo imejifunga, lakini tunajaribu kutafuta njia ni namna gani mvua zitakapopungua tuweze kuitatua.

Sehemu nyingine ni ya kutoka kwa Mheshimiwa Kibona, kutoka Mpemba hadi Isongole kuelekea mpaka Kasumulo. Pale pametoka *landscaping*, ile milima imeteremka kama ambavyo ilifanyika kule Afghanistan, milima imeteremka, kama ilivyofanyika kule Marekani milima ikateremka, sehemu hii nayo imetokea *landscaping* na ikaziba barabara yote.

Ni kutokana na mvua zilizotokea ile barabara nayo tumeifunga lakini tunajaribu kuangalia wataalam wetu wa *TANROAD* na wengine wote tunashughulika katika kuhakikisha kwamba barabara hii nayo tunairudisha katika hali yake kama inavyotakiwa. Sehemu nyingine ni barabara ya Sonye-Makete ambayo nayo imeharibika sana kutokana na mvua zilizonyesha, pamoja na eneo la barabara ya kutoka Kyela kwenda *Matema Beach* ambayo nayo imekatika kwa kiasi hicho.

Kwa hiyo Serikali kwa ujumla tunafanya juhudi kubwa katika kuhakikisha maeneo haya yote tunayarudisha. Yalitokea hivyo hivyo katika Mkoa wa Dar es

Salaam na kwa Mkoa wa Pwani. Kwa bahari nzuri ndani ya siku tatu yale matuta yote yaliyokuwa yamepelekwa na maji tuliweza kuyarudisha na barabara zile zinapitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe tu taarifa kwamba mvua za mwaka huu kama zilivyokuwa zimetabiriwa na Watabiri wa Hali ya Hewa hazikuwa za kawaida. Mvua zilinyesha kiasi kikubwa na kwa bahari nzuri katika mvua zote zilizonyesha hakuna daraja lililokuwa limejengwa liliondoka. Kwa sababu *design life* ya madaraja yetu ni zaidi ya miaka 100. Kilichokuwa kinapelekwa ni matuta ambayo yalikuwa yanaunganisha kwenye madaraja pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua hizi hazikuletwa na CCM, hazikuletwa na Kikwete, hazikuletwa na nani, ni mvua ambazo zimekuja kutokana na hali halisi. Mvua za namna hii zimekuwa zikijitokeza hata katika nchi nyingine.

Nchi ya Uingereza iliwahi kukumbwa na mafuriko zaidi ya wiki nne. Marekani iliwahi kukumbwa na mafuriko na watu wakafariki. Afghanistan sasa hivi wamekufa zaidi ya watu mamia kutokana na mafuriko; Japan palitokea mafuriko; na Afrika Kusini palitokea mafuriko. Kwa hiyo, hatua kubwa zinachukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba maeneo yote yaliyoharibika yanarudishwa katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nichangie hili katika kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba watuvumilie na wananchi wavumilie katika maeneo ambayo kwa sasa hivi Serikali inajipanga katika kuhakikisha kwamba inarudisha mawasiliano yake kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ningeomba kabisa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ipitishwe haraka ili zipatikane fedha zikaweze kushughulikia haya masuala mengine ambayo sisi tunaona yanaweza kuleta ukombozi mkubwa katika maeneo ambayo yamejifunga kwa sababu Kitengo cha Maafa kiko ndani ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba kushukuru na naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Magufuli, nakushukuru sana. Naomba niwakumbushe ile Kamati ya Miundombinu, ule Ukumbi Namba 136 ni Hazina Ndogo. Ukumbi Na, 136 ambako mtakutana saa 7.00 mchana ni ukumbi ambao uko Hazina Ndogo. Sio hapa hapa kwenye majengo ya Bunge. Mheshimiwa Kessy atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashimu.

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika. Ahsante sana. Muda wote miaka minne barabara ya Sumbawanga – Kanazi – Kanazi - Kibaoni. Nashangaa hii barabara haipevi kipaumbele. Tena ni barabara sijui kuna bifu kati ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ujenzi. Maana yake ukiangalia kule anakokaa Waziri Mkuu ndipo inakoanzia barabara, ni mashimo ya panya matupu. Miaka minne haijapewa pesa. Juzi juzi nasikia imepeleka pesa kiduchu kudanganya wananchi. Miaka yote imekuwa Wachina, sasa wamekuwa waganga wa kienyeji kule kwetu wanauza kokoto. *(Kicheko/Makofi)*

Kitu cha ajabu kabisa, barabara zote zinapewa kifungu, lakini barabara inayotoka kwa Waziri Mkuu kwenda Kanazi, hakuna chochote kinachopelekwa, mpaka Wachina wamekimbia. Nataka Waziri wa Ujenzi aeleze, kuna nini kati yake na Waziri Mkuu? Hii ni kwa sababu ni hoja ya Waziri Mkuu kumgandamiza asionekane anafanya kazi kwa sababu ni kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya mwaka 2013 hapa, nimezungumza kuhusu maji Nyamanyere, akatoka Profesa Maghembe, Waziri wa Maji mpaka Namanyere wakati Bunge linaendelea kwa pesa ya Serikali kwenda kufanya Mkutano Namanyere na kudanganya wananchi wa Namanyere kwamba maji yanakuja. Akaulizwa swali na kijana mmoja anaitwa Tepeli Afonei Tepeli, Profesa unasema ukweli? Akasema mimi Profesa siwezi kudanganya. Mpaka leo hakuna kilichofanyika Namanyere. Sasa je, uprofa umefika wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri aeleze Bunge lako, kadanganya wananchi wa Namanyere moja kwa moja na ametoa gari hapa hela za Serikali mpaka Namanyere kutoka Dodoma kwenda kufanya Mkutano wa hadhara na kudanganya wananchi wangu na hakuna chochote kilichokwenda.

Kuhusu Mji wa Namanyere, vigezo na masharti vyote vimeshatimia kutoka Mji mdogo kwenda Halmashauri ya Mji. Naomba Serikali izingatie sasa Namanyere iwe Halmashauri ya Mji kuanzia sasa. Vigezo vyote tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Maji Lwanfi, haikupata pesa, wanasema Namanyere Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi sijui imepata hasara. Inatuhusu nini sisi hasara? Wakamateni! Wananchi wanataka kulima mpunga kule. Hawategemei mvua. Mvua ya Mwenyezi Mungu ni shida. Kuna mto maalum kabisa pale wa Masoro, lakini pesa haiendi eti Halmashauri imekula pesa. Sasa Halmashauri imekula pesa, watu wa Kilando ndio wamekula pesa za Halmashauri? Naomba Wizara itimize Skimu ya Lwanfi mara moja kuwapeleka pesa ili watu waanze kumwagilia wapate mpunga wa kutosha. Kuhusu meli. Nimesoma kwenye kitabu cha Waziri Mkuu ni ukarabati wa meli tu za Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, wakati walituhidi meli mpya kwenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

maziwa yote matatu. Naomba Serikali itimize ahadi yake kutuletea meli mpya kwenye maziwa yote matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni nchi yetu ya wote, Tanzania ni moja Mikoa yote ni moja. Tunaomba Serikali bajeti yake izingatie Mikoa iliyokuwa nyuma, ipewe pesa zaidi kuliko mikoa ambayo iko mbele. Haiwezekani kabisa wenzetu wako peponi sisi tuko motoni. Inawezekana wapi wananchi wanaishi mwambao mwa Ziwa Tanganyika hawana barabara? Nenda Lake Victoria, wote wana barabara za lami. Hii imekuwa ni nchi ya upendeleo kiasi gani? Lazima bajeti tupendeleo Mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo ili na sisi tupige hatua kama Mikoa mingine. Hii ni nchi yetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kipili imeshakamilika, lakini hakuna barabara. Sasa faida yake ni nini? Kilomita saba tu, barabara hakuna. Watu waende kwa miguu Bandarini? Wabebe mizigo kilomita saba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema elimu imeshuka, wacha ishuke, kwa sababu Wakaguzi hawapewi pesa. Wakaguzi wamekaa hamna pesa, watafanya nini? Watakagua nini? *(Kicheko/Makofi)*

Wenyeviti wa Vitongoji hawalipwi mishahara wala posho. Nimezungumza miaka yote hii. Nchi gani ulimwenguni inamtumikisha mtu bila kumlipa? Hata ukimtaka mtu akutoe jicho leo akupige viboko, anakwambia nipe pesa. Itakuwa Mwenyekiti anaendesha Mikutano, Songambebe sijui nini, halipwi chochote! Mungu hapendi, dhambi! Mbona masherehe mnafanya makubwa makubwa, mnatumia mabilioni ya pesa? Huu ni uonezi wa hali ya juu. Hawafanyi maandamano tu kwa sababu wako mbalimbali. Au wangeacha tu. Nani atafanya kazi bure? Hapa tunalipwa posho, nani anafanya kazi bure? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu dakika ni ndogo, mimi nazungumza nakwenda kulenga sikuja hapa kubabaisha babaisha. Nimeeleza Wakaguzi wapewe pesa wakague Walimu wanafanya nini. Namanyere tunataka iwe Halmashauri ya Mji, vigezo vyote viko Ofisini.

La tatu, meli mpya kwenye maziwa yote matatu jinsi ahadi ile ya Rais ilivyotimia. Siyo ukarabati wa meli. Liemba ina miaka 100, utakarabati nini? Mwisho, itakuja kuua watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kipili inataka barabara pale mwambao mwa Ziwa Tanganyika vijiji vyote kama Ziwa Victoria. Huu siyo upendeleo! Hawajaona gari miaka 50! Tuondoke hapa, Kasombo hawajaona gari, Isaba hawajaona gari, Chamkotako hawajaona gari, Kalila hawajaona gari, Mkondo hawajaona gari tangu kuzaliwa!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika Tunafanya masherehe Shilingi bilioni 70. Unafanya sherehe ndugu yangu, wewe unafanya *Birth Day* watoto wako hawana viatu! Watoto wako hawana chakula! Hatuna uchungu na wananchi wetu! Watu hawana maji. Visima 10 vya *World Bank* havina maji. Hakuna hata kimoja kina maji. Wametaka tena usanifu urudiwe upya wale hela mara ya pili. Wamechimba mitaro ya milioni 200 imekuja mvua imefukia, Mkandarasi hana bomba hata moja. Kachimba mitaro, visima vyote Wilaya ya Nkasi, hela imeliwa! Hakuna hata kisima kimoja ambacho kimetoa maji, eti usanifu ufanywe upya. Usanifu wa kwanza umekula pesa. Uonevu wa hali ya juu nchi hii! Wanakula pesa vibaya nchi hii! Hawana huruma kabisa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka majibu kwa Waziri wa Maji kuhusu Namanyere. Kadanganya wananchi Namanyere. Yeye mwenyewe katoka hapa moja kwa moja, kafanya Mkutano, kaitisha watu. Anasema mimi ni Profesa, sisemi uongo, na wamemrekodi. Leo utasema nini? Namanyere maji yapo? Umelidanganya Bunge hapa mimi nitasema nini? Wabunge mpaka wengine hapa wakanionea wivu, wewe utapate hela? Hela zipo wapi? Wameniuza mbuzi kwenye gunia! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maelezo mengi. Lakini nimeuziwa mbuzi kwenye gunia. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Jaku Hashim, atafuatiwa na Mheshimiwa Suzan Lyimo. Mheshimiwa Jaku, Mheshimiwa Suzan jiandaye.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa kunipa pumzi zake kuweza kupumua, huu si ujanja wangu, wala uwezo wangu, wengine hivi sasa wako *ICU* wanasaidiwa pumzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa siyo mwingi wa wafadhila kama sitakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na vile vile nikupe pole kwa mambo yaliyotokea Kibwajuga na baadhi ya Wajumbe wako tumevunjiwa magari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nataka nichangie katika ukurasa wa 15. Tunatambua changamoto zilizopo na tumeweka utaratibu nzuri wa vikao ili kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo za vikao hivyo kuhusu suala la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea masuala haya ya kero za Muungano kwa upande wa Zanzibar zitazingatiwa. Hiki kilio kimekuwa cha muda mrefu na vikao hivi vimekaa sijui mara ngapi; kama mara 15 au mara 20 lakini bado umekuwa ni Wimbo wa Taifa. Changamoto zimekuwa ni nzito na hasa suala la *TRA*.

Mwenzangu Mheshimiwa Keissy alizungumza kwamba Tanzania ni nchi moja, tunatumia mfumo mmoja wa kodi, tuna mamlaka moja ya kusimamia kodi, yaani *TRA* ina Sheria moja, tuna viwango vimoja vya kodi, lakini cha kushangaza, mzigo ukitoka Dar es Salaam kwenda Dodoma hauna matatizo. Dar es Salaam kwenda Zanzibar hauna matatizo. Hapo utakiona cha mtema kuni, mzigo utoke Zanzibar kwenda katika Bandari ya Dar es Salaam. Usumbufu, mateso ya hali ya juu. Hivi sasa kuna mizigo karibu nusu mwaka iko Bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kilio kikubwa cha Wazanzibar cha wafanya biashara, wanasumbuka, wanaendelea kuteswa. Ikiwa Tanzania ni nchi moja, *formula* tunayotumia ni ya *TRA*; Zanzibar pamoja na udogo wake, tunachotegemea ni biashara, hakuna tunachokitegemea zaidi hapo.

Wenzetu Tanzania Mwenyezi Mungu kwa ukubwa wake kaineemesha kwa neema chungu nzima. Kuna mbuga, kuna madini ya *Uranium*, kuna dhahabu, kuna almasi; sasa mkitubana kiasi hiki ndugu zangu, mtatuweka katika hali nzito! Zanzibar tunategemea suala la biashara, mtupe angalau kupumua! (*Makofi*)

Hebu tufikiri ni jamani! Leo hospitali ya Mnazi mmoja hospitali ambayo ni hospitali kubwa kitanda kimoja kinalaza wagonjwa wawili mpaka watatu. Huo ndiyo ukweli, hospitali ya rufaa hiyo! Kero hizi zimekuwa ni za muda mrefu. Vikao vimefanywa, vinaendelea kufanyika. Lakini hakuna suluhu iliyopatikana. Mimi ningepomba pangekuwa na *formula* maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka hapo nije kwenye kero nyingine ya pili, nayo ni nzito kuhusu suala la Ubalizi na watendaji wake. Zanzibar kama nchi pamoja na udogo wake suala la Ubalizi na Watendaji wake pafanywe haki kidogo. Pawe na *formula* maalum ya Mabalizi kutoka Zanzibar. Leo tuna Mabalizi watatu tu! Suala hili lifikiriwe nalo! (*Makofi*)

Tuje suala la tatu, elimu ya juu ambalo ni suala la Muungano vile vile. Elimu ya Juu mwanzo ilikuwa ikitoa mkopo kwa wanafunzi wanaosoma suala la dini, hivi sasa imezuia. Tuione Zanzibar pamoja na ukubwa wake asilimia 95, 98 ni Waislamu, *formula* ile naomba irejeshwe tena. (*Makofi*)

Mtu aangaliwe uwezo wake, asiwe anapangiwa utaratibu maalum wa masomo ya kwenda kusoma. Asilimia 95 narudia tena ni Waislamu na wengi huenda kusoma dini ili kuja kuendelezwa na dini yao. Sasa *formula* hiyo imezuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije tena katika eneo lingine la mgao wa nafasi za kazi katika Taasisi za Jamhuri ya Muungano. Pawe na Sheria Maalum asilimia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ngapi Zanzibar wanapewa. Asilimia ngapi Tanzania Bara inanufaika. Hayo ndiyo mambo ya kuja kuzungumza Mheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije suala la *TFF*, Chama cha Mchezo wa Mpira, kwa masikitiko makubwa, kuna pesa zinatoka *FIFA* dola laki mbili na nusu kila mwaka, kuna dola laki moja zinatoka *CAF* kila mwaka, sijui Zanzibar inanufaika na kitu gani? Tukaye tufikiriane baadhi ya mambo jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naona nisipoteze muda. Mchango wangu ni mfupi, mdogo, lakini nzito. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jaku. Kwanza tukuombe radhi na utusamehe sana Jimbo la Kongwa pale kwa gari yako kupata matatizo wakati ukipita. Ni matatizo ya vijana ambayo hayatajirudia tena.

Mheshimiwa Ngeleja, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi wa Msekwa 'B' saa 7.00 mchana.

Sasa namwita Mheshimiwa Suzan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba muhimu sana ya Waziri Kuu pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara hii ni Wizara kubwa sana na ina majukumu makubwa sana katika nchi yetu. Lakini ukiangalia ni wazi kwamba fedha ambazo zilitolewa mwaka 2013 ni asilimia 60 tu ambazo tayari zimefika na wote tunajua kwamba Halmashauri zetu zinahitaji sana fedha hizi ili ziweze kufanya kazi kwa ajili ya wananchi na kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Lakini kwa masikitiko makubwa sana ni kwamba fedha hazijafika na kwa maana hiyo Halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kutimiza au kutekeleza yale ambayo tuliyapitisha hapa mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningepomba niongelee masuala machache lakini kubwa nianze na la msongamano wa magari Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na ni ushahidi kwamba, Wabunge wengi wanapita Dar es Salaam na wengi wanaishi Dar es Salaam, lakini ni wazi tumeona kuwa kuna matatizo makubwa sana ya msongamano wa magari Dar es Salaam na wote tunatambua kwamba Mkoa wa Dar es Salaam zaidi ya asilimia 70 ya pato la Taifa linapatikana Dar es Salaam, lakini kutokana na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

msongamano mkubwa wa magari na pamoja na hatua ambayo Serikali inazichukua, bado hatua hizi zinasuasua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge wa Dar es Salaam tulikuwa tumeomba sana *feeder roads* na *ring roads* ziweze kutengenezwa ili magari yaweze kupita, lakini cha kusikitisha mpaka leo tunavyoongea bado tatizo hili ni kubwa sana lakini kibaya zaidi. Barabara zinatengenezwa chini ya kiwango. Barabara ambazo zimetengenezwa mwaka 2013, mwaka 2012, sasa hivi zote hazipitiki. Lakini wote tunajua kutokana na matatizo makubwa ya mafuriko mwaka huu, hali imekuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, mimi ni mtaalamu wa Saikolojia, nimekuwa napata kesi nyingi sana za ndoa. Sasa hivi wanaume hawarudi nyumbani mapema kwa sababu ya msongamano. Wanatoka kazini saa 11.00 wanafika nyumbani saa 6.00 ya usiku. Hii ni kwa sababu wameamua sasa, kwa kuona foleni hizo wanaamua kwenda kwenye mabaa ili foleni zipungue, kwa hiyo, wanaanza safari saa 5.00 za usiku.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba sana barabara hizi ziweze kutengenezwa mapema ili kunusuru ndoa hizi. Ndio sababu tunaona hata watoto wasiokuwa na wazazi sasa hivi wanakuwa wengi. Hii ni kutokana na msongamano wa magari Dar es Salaam. Kwa hiyo, kwa kweli, hili ni janga. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa wanaohusika wahakikishe kwamba tatizo la msongamano Dar es Salaam linakwisha kwa sababu ni janga la Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye suala la elimu. Ni kweli kwamba kiwango cha elimu kinashuka, lakini ni wazi kwamba matokeo ya kidato cha IV mwaka 2014 yanaonesha kwamba idadi ya ufaulu imeongezeka. Lakini tunaona wazi kiuhalisia haijaongezeka; imeongezeka kwa asilimia, lakini ukiangalia kiuhalisia siyo sahihi kwa sababu kilichofanyika ni kuongeza alama na kubadilisha madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba Tanzania siyo kisiwa. Watoto wetu wanaomaliza wanaenda kwenye maeneo mbalimbali, wanaenda kwenye soko la Kitaifa na Kimataifa. Kwa hiyo, ni hatari sana tunapongeza upana wa goli ili kuweza kuweka vijana wengi zaidi waingie Kidato cha V wakati tuna hakika kwamba bado tatizo la elimu ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yetu Tanzania bado ni duni, lakini kubwa zaidi nimekuwa nikiongea suala la elimu ni lazima tuboreshe elimu, na katika kuboresha elimu ni lazima tuboreshe maslahi ya Walimu. Kikubwa, mpaka leo maslahi ya Walimu bado hayajaboreshwa, na tatizo lingine kubwa ni ajira za

Walimu. Bado tuna shule; na nitolee mfano, nashukuru Mheshimiwa Ridhwani Kikwete ameingia humu ndani kama Mbunge wa Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeenda kwenye Jimbo lile, kuna shule ambazo zinakuwa na Mwalimu mmoja darasa la kwanza mpaka la sita, shule inayoitwa Pera na nyinginezo, hata Bagamoyo kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na shule nyingine nyingi Tanzania. Haiwezekani shule yenye Darasa la Kwanza mpaka la Saba iwe na Mwalimu mmoja na Mwalimu huyo anaweza akaugua, kwa hiyo, watoto wanaenda likizo wakati wenzao wanaendelea na shule. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kabisa kwa Wizara inayohusika na elimu ambayo ni Wizara ya Elimu pamoja na *TAMISEMI* wahakikishe kwamba hizi ajira zilizotolewa sasa hivi, Walimu wanaenda kwenye shule ambazo hazina Walimu.

Ni jambo la kusikitisha sana kwamba pamoja na kwamba, tuna Walimu ambao wamemaliza masomo yao ya Ualimu, lakini hawajapata ajira, wako Mitaani wanalalamika kwamba pamoja na kwamba, kuna ajira zimetolewa, lakini bado kuna Walimu ambao wameachwa nje, lakini naomba sana Serikali ihakikishe kwamba wanatoa ajira kwa Walimu ambao bado wako nje. Kwa sababu, tuna hakika bado kuna shule nyingi sana hasa vijijini ambazo zina upungufu mkubwa sana wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la maji. Suala la maji ni suala la maji ni suala la uhai. Maji ni uhai! Lakini ni wazi kwamba, tatizo la maji pamoja na kwamba mwaka 2013 kwenye bajeti tuliongeza bajeti ya maji, lakini bado kuna maeneo mengi sana hayana maji, lakini pamoja na kutokuwa na maji, bado miradi hiyo imekuwa ikifisadiwa kama ambavyo amezungumza Mbunge wa Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Mkoa wa Dar es Salaam, kuna tatizo kubwa sana la maji hasa maeneo ya Mbezi, Kimara, Kawe na Kinondoni, tuna tatizo kubwa sana la maji. Tuna mabomba makubwa yanawekwa, lakini maji hakuna. Watu wamekaa miaka 10 hawapati maji. Naomba sana Waziri wa Maji ahakikishe kwamba ule mradi mkubwa unaoanzia Ruvu Chini sasa maji yaanze kutoka kwa sababu kwa kweli tunaona mabomba lakini maji hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa katika bajeti yake ya mwaka huu, wananchi wa Dar es Salaam ambao ni zaidi ya asilimia 60 hawana maji, watapata maji kwa sababu imekuwa ni kero kwa nchi nzima. Mwanamke anaenda kuchota maji zaidi ya saa 7.00 hajapata maji, shughuli nyingine za maendeleo hafanyi kwa sababu ya maji. Tunaomba sana maji na ninashukuru kwamba yako katika Sekta ya kipaumbele, hivyo ihakikishwe kwamba,

tunaenda kwenye bajeti hii tukihakikisha kwamba mwaka huu 2014 wananchi angalau asilimia 70 ya Watanzania wanapata maji salama na safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuongelea suala zima la ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Suala hili limeongelewa kwa muda mrefu, lakini bado hatujapata...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Mama Magreth Sitta, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake ya Huduma za Jamii wakutane saa 7.00 Ukumbi wa Msekwa 'C'.

Kama Mheshimiwa Mkiwa hayupo, aah yupo eeh, ahsante. Endelea Mheshimiwa Mkiwa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia nguvu na uhai mpaka kwa siku hii ya leo nami nikaweza kuchangia kwenye Bunge lako hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kusema neno moja; mtu anaposema *TAMISEMI* au Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni sawa kabisa na kusema hii ni Serikali ya Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? *TAMISEMI* imegusa maeneo yote, imegusa sehemu zote na ndiyo Wizara kubwa katika nchi hii na huenda ikachukua zaidi ya robo ya bajeti ya Serikali ya Tanzania. Kwa kuwa, *TAMISEMI* ina eneo kubwa sana na kwa kuwa *TAMISEMI* inajigusa katika maeneo mengi katika kuhudumia wananchi wa Tanzania, naomba katika Mfuko wa Barabara ambao *TANROAD* wanapewa asilimia 70 na *TAMISEMI* wanapewa asilimia 30, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hili aliangalie upya, angalau *TAMISEMI* wazewe kuongezwa angalau wafikie asilimia 40 na *TANROAD* waweze kupewa asilimia 60, kwani wakulima wanaposema wanashindwa kutoa mazao mashambani ni kwamba, *TAMISEMI* wanashindwa kuhudumia barabara za vijijini, wanashindwa kuhudumia barabara ambazo ziko kando kando kwa sababu ya asilimia ndogo wanayoipata. *(Makofi)*

Nilikuwa naiomba Serikali iliangalie hili na ilitolee maamuzi mara moja. Kwa sababu, Wizara ya Ujenzi tunapowaambia wachukue barabara

wazipandishe daraja, wanakataa na barabara hizo zinzendelea kuachwa *TAMISEMI*, wakati tunafahamu kabisa *TAMISEMI* uwezo wao ni mdogo na wao wanachukua asilimia kubwa. Kwa maana hiyo, ningepomba kabisa kwa hili, Serikali iangalie upya waongezewe *TAMISEMI* asilimia angalao ifike 40 kwa kuanzia na ikiwezekana tutakapoenda iwe asilimia 50 kwa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuongelea suala la ardhi. Naiomba Wizara ya *TAMISEMI* kupitia kwa Waziri husika aangalie zaidi watendaji wa Halmashauri kwa upande wa ardhi kwa sababu ardhi imekuwa tatizo kubwa. Kwa sababu, tatizo hili limekuwa kubwa kupita kiasi, ni vema sasa Waziri wa *TAMISEMI* akawa macho zaidi kwa sababu, wananchi wanadhulumika sana. Katika malipo, wananchi wanafidiwa kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa nikiishukuru Kamati ya *TAMISEMI* na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza katika mradi wa Monze. Sasa kuurudisha na waweze kuuandaa upya ili wananchi wapate haki zao halali na stahiki zao zinazostahiki. Kwa hili Mheshimiwa Waziri kwa kukubaliana na Kamati, napenda kukushukuru na kukupongeza kwa kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza pia, ili tuweze kuendana na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwananchi akubaliane wazi na mtu ambaye anataka kuchukua ardhi yake. Siyo kwenda mwananchi akapimiwa ardhi yake kwa kushikiwa bunduki na kuambiwa kwamba, ni lazima ardhi ipimwe. Hii siyo haki, haikubaliki na wala haitakubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuongelea suala la makusanyo ya fedha. Tunaiomba Wizara sasa kwa sababu, ndiyo nimesema hii ndiyo Tanganyika, iwasimamie Watendaji wakusanye mapato kwa kadiri inavyowezezana; na wakusanyie mapato kwenye Mfuko wa *TAMISEMI* na wala wasikusanyie mapato kwenye mifuko yao. Mheshimiwa Waziri tunamwomba, suala hili litakapogundulika wafanyakazi wale wasiishie kufukuzwa kazi tu, wachukuliwe hatua za kinidhamu, ikiwezekana hata kufilisiwa mali ambazo wanazipata kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mapato yaendeleo kushuka wakati vyanzo vya mapato viko vingi. Tunawaomba *TAMISEMI* waweze kuwawezesha wakusanyaji mapato ili waweze kufahamu ni nini wanachotakiwa kukifanya na ni nini ambacho kinatakiwa kipatikane kwa kuweza kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kodi zinakusanywa, wananchi wanalipa ushuru, lakini mpaka leo wanafunzi wa kitanzania bado wanagombania mawe kukalia darasani. Hii ni aibu! Kwa sababu pesa zinazokusanywa hazifiki kwa wakati. Nanafikiri kwa ule mkakati wa Kamati asilimia 60 zitumike kwa

maendeleo katika Halmashauri, nina imani kabisa wanafunzi wataweza kusoma kwa raha na wataweza kukalia madawati.

Ni juzi tu shule 13 Geita, wanafunzi wanagombania mawe kukalia darasani. Hii ni kweli kabisa! Geita kuna migodi, Geita wana Ziwa, Geita wana rasilimali chungu nzima, wanashindwa nini kukusanya pesa na wanafunzi wakaweza kukalia madawati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma yawe wazi, nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma yaeleweke na siyo kwamba, iishie kukusanywa na kupelekwa kusikojulikana. Naiomba Serikali isimamie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeiomba Serikali, sisi kama Watanzania tunasema Tanzania ni nchi masikini, lakini mambo tunayoyafanya siyo ya kimasikini. Haiwezekani Halaiki ya Miaka 52 ya Uhuru wa Tanzania ikatumia Shilingi milioni 700. Halaiki ya Miaka 52 ya Uhuru wa Tanganyika ikatumia Shilingi milioni, yaani...

MBUNGE FULANI: Uhuru!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Siyo Muungano, ni Uhuru wa Miaka 52 wa Tanganyika tukatumia Shilingi milioni 700 na kitu, hapo sijakwambia Halaiki ya Muungano imetumia Shilingi ngapi?

MBUNGE FULANI: Hapo sasa!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Tunamwonesha nani? Au tunamweleza nani sisi tunajua kupiga miguu, yaani kupiga kila siku gwaride, sherehe zisizokwisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inastahiki wakati mwingine kuadhimisha, yaani kama tunaadhimisha miaka 52 ya uhuru wa Tanganyika, twende tukafanye kazi Mahospitalini, tufanye usafi, tufanye mambo mengine, hizi pesa ziende kwenye shughuli za maendeleo. Sio kupiga makofi na kucheza maparedi yasiyokwisha! Kuonesha vifaa vya kivita; mimi kwanza nashangaa sisi Watanzania tunaonesha zana zetu halisi za kivita. Tunamwonesha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni UKAWA, UKAWA hatuogopi, wale ni Jeshi ni letu sote, wanalipwa kwa kodi zetu sisi sote. Hii haimsaidii Mtanzania! Matanzania hahitaji *parade*, Mtanzania anahitaji maji, Mtanzania anahitaji elimu, Matanzania anahitaji afya bora, Mtanzania anahitaji barabara, Mtanzania anahitaji ni jinsi gani mazao yake yatatoka shambani na kuingia sokoni.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwe na matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala moja la Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Tukisema Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji, hawa ni Mabalazi wetu kule chini kunakoanzia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, nakushukuru sana.

Ni zamu ya Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. Mheshimiwa Maria Hewa! Hayupo *Miss Bunge!*

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwanza kwa kushukuru kunipa nafasi hii kwa sababu ni adimu sana na ni dakika saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombae kuunga mkono Hotuba ya Waziri Mkuu ipitie kwa sababu bila hivyo fedha hamna. Naomba kuiunga mkono Hotuba ili sisi tusonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, asiyeshukuru kwa kidogo hata ungempa kitu kikubwa namna gani, kwa maana ya maendeleo yake, atasema na hiki ni kibaya, atatamani labda cha kutoka Mbinguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mwanza tulipewa daraja pale Mabatini ambalo wananchi sasa wanapita kwa juu na barabara wanaacha wazi kwa maana ya magari. Inapendeza sana! Mwanza inapendeza! Nashukuru kwamba nililishupalia suala hili mpaka mwishowe mambo yamejipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuomba tena lingine tuweze kupata daraja la namna hiyo pale *Mission* pale, panajulikana kwa jina la *Mission Street*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lile panajengwa sasa soko kubwa sana ambalo nadhani litakuwa la Kimataifa; zuri, kubwa! Lakini hapo hapo ndiyo njia ya kutokea uwanja wa Kirumba, hapo hapo ndiyo kuna Hospitali zimezunguka eneo, hapo hapo ndiyo kuna Makanisha kama hayo yanayowindwa sasa kwa njia za mabomu yale. Sasa pale patakuwa na watu wengi sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwenye Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Waziri wangu Magufuli, fikiria hilo pia, mimi ni mwombaji wa vitu vidogo vidogo tu, vikubwa siviwezi. Naomba mtupatie kidaraja tena cha pili kwa namna hiyo, ili Mwanza iendelee kufunguka kwa sababu, ina barabara tatu tu na watu ni wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza ina mzunguko wa fedha. Naomba pia hapo mtufikirie, tutaendelea kushukuru tu. Watu wa Mwanza ni wapole na wamejaa shukrani. Tunaomba daraja la namna hiyo tena liwekwe pale *Mission*, ili mbele ya safari soko litakapoanza kufanya kazi pafunguke kabla ya kuanza ma-congestion makali makali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mfupi! La tatu, ni reli ya kati. Reli ya kati kwa Waziri Mkuu nadhani anaelewa kabisa, ndani ya Kitabu chake katika bajeti yake ameeleza kwamba, kutanunuliwa na mabehewa ya mizigo nadhani 204 hivi, lakini wakati huo huo amesema kutanunuliwa na vichwa vipya 12. Tumesikia muda mrefu sana habari ya kununuliwa vichwa hivi. Hivi hata kimoja kimeshaingia? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hizi kauli ziwe za ndani ya dhamira ya utekelezaji. Kabisa! (Minong'ono)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vichwa vya treni! Waone! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naomba vichwa 12 vya treni, basi viingie. Mimi mara ya kwanza niliambiwa vinatoka Ujerumani. Sijui ndiyo hivyo? Naomba sana, katika kipindi hiki, pamoja na kupitisha fedha ndani ya Wizara yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi iweko dhamira ya utekelezaji ili hii reli ya kati ifanye kazi. Unajua kwa nini? Mimi mwishowe inaniweka mahali nawazia, katika mafuriko haya, yameilainisha; yaani kwa sababu barabara zetu zinapitwa na magari makubwa mazito, sasa yamekuja mafuriko juu yake, lami imelowana.

Sasa hivi mabarabara ni mashimo kuanzia Dar es Salaam mpaka nenda Bara. Yote hiyo ni kwa sababu ya mvua nyingi, lakini nadhani kwa sababu lami yetu iliguswa na magari mazito; mtanisahihisha, lakini ukweli ni kwamba lami sasa inabanduka. Naomba, naomba, naomba!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni masuala ya Walimu jamani! Walimu wako TAMISEMI. Wlimu hawa madai yao kutwa nzima wanalia jamani. Mtu anayeomba chake, mumfikirie! Mumfikirie kabisa! Wote kimsingi tunahitaji Walimu. Wote humu tumepitia mikononi mwa Walimu. Hebu tuwafikirie hata kwa awamu basi siyo lazima tuwalipe zote kwa mkupuo, lakini kwa awamu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Naomba kipindi hiki, mnapokezana vijiti jamani! Hebu kweli iwe agenda ya kudumu, hata angalau robo yao au nusu ya malipo yao wafikiriwe jamani!

Wanapogoma kutufundishia watoto wetu, hasara ni ya nani? Hasara ni yetu na anadai jamani! Mtu haendi njaa kufanya kazi, anakula kwanza ndiyo anaenda! Naomba tuwafikirie Walimu kabisa! Maana a, e, i, o, u inatoka mikononi mwao ndiyo unakuja hata kama ni Mbunge, hata kama ni nani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, mambo ya uzazi bora. Wanawake jamani wanajifungua hawana huduma yoyote. Unaingia Hospitali, anaenda tu kusukuma mtoto, inaisha. Tunaomba matibbabu ya sindano za kuzuia *bleeding*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Nakushukuru sana Mheshimiwa Maria Hewa hasa baada ya kutujulisha kwamba watani wangu kule Mwanza kumbe nao wana barabara za juu.

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nawapa pole watu wote waliokumbwa na mafuriko kwenye Jimbo langu na Majimbo yote nchini. Tuko pamoja na nyie na Mwenyezi Mungu atapunguza adhabu hii ya mvua ili wananchi wanusurike na mafuriko haya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kukwambia na niwaambie Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Waziri Mkuu. Mimi siungi mkono hoja hii mpaka pale Waziri Mkuu na Ofisi yake itakapotupa uhakika wa barabara kwenye Mkoa wa Dar es Salaam. Msongamano huu unaoletwa Dar es Salaam ni kutokana na miundombinu mibovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya uhuru, barabara za ndani Kariakoo, barabara za Mapipa, barabara za Temeke, barabara za Kinondoni lakini inapokuja hoja kui-*fund* Dar es Salaam kupata fedha za ziada Wabunge humu ndani mnakataa, nanyi Wabunge ndio mnaishi Dar es Salaam. Dar es Salaam mnatafuta nini? Kaeni kwenye Majimbo yenu huko, mkae na wananchi wenu huko! Msije Dar es Salaam halafu zikitolewa fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu, mnalalamika! Msije Dar es Salaam, kaeni huko huko mlkochaguliwa. (Makofi/Kicheko/Minong'ono)

Mheshimiwa Naibu Spika, habari ndiyo hiyo! (Kicheko/Makofi)

MBUNGE FULANI: Eeeh, Waambie. (Makofi/Kicheko)

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Ilala kuna mpango wa kujengewa uwanja wa michezo wa vijana. Namshukuru sana Waziri, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, namshukuru sana Rais, ndiye aliyekuja na mpangi huu. Namshukuru sana Katibu Mkuu TAMISEMI, naye analisimamia. Leo ameniahidi, ameandaa timu kwenda kuonana na wawekezaji kutazama pale ambako kuna mapungufu, basi wajaribu kuyanyoosha. Lakini haitatosha kama Watendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala wataachwa wapuuze maazimio ya vikao bila kuchukuliwa hatua.

Tunachelewa kupata mradi huu kutokana na ubinafsi tu wa Watendaji wanaharibu jina la Mheshimiwa Rais, wanaharibu jina la Waziri Mkuu, wanaharibu jina la Viongozi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi umetokea mtindo, Watendaji hawa wanasema, waacheni Wabunge wapige kelele, tukitoka nje sisi kazi kama kawaida. Hilo hatulikubali! Sisi tunapimwa na wananchi kila miaka mitano, wenzetu hawa hawana kipimo. Wakifika miaka 60 ndiyo wanastaafu. Kwa hiyo, wanajifanyia fujo wanazotaka, anahamishwa hapa, anapelekwa huku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba na Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa kama nilivyosema, mimi sitaunga mkono kwa hoja hiyo pamoja na zile Kata tatu za Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ufasidi mkubwa sana kwenye mradi huu wa Kigamboni. Malengo ya mradi huu sivyo yanavyotekelezwa! Nasi hatuwezi kukubali! (Makofi)

Kariakoo unavyoiona ile sasa hivi inachangia asilimia 20 ya pato la Taifa kutokana na biashara na majengo. Hakuna mtu aliyefukuzwa pale, wananchi wenyewe wameingia ubia na wawekezaji. Hata Kigamboni, Serikali ije na mpango, ije na *master plan* mwananchi aingie ubia na mwekezaji, kila mtu apate kuridhika katika shughuli ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *issue* ya usafi. Lipo zoezi linalofanywa sasa hivi Dar es Salaam. Hakuna Kiongozi, hakuna Mbunge, hakuna mwananchi anayetaka Mji wake uwe mchafu. Wote sisi tunataka Mji uwe msafi. Lakini ni lazima ifahamike, usafi huu anaufanya nani? Sisi Wabunge na Mameya, hatukubali *smart area* iendeshwe na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina mamlaka na ina majukumu ya Kisheria, hawawezi kuleta ripoti ya uongo kwenye RCC kwamba Mameya na Wakurugenzi wamekubaliana kwa Jiji la Dar es Salaam liteke maeneo ya Halmashauri. *Smart area* usafi utafanywa na Halmashauri zetu zinazohusika, siyo nanii. Nataka kumwuliza Mkuu wa Mkoa, yupo hapa; ni hatua gani atakayomchukulia Mkurugenzi kwa kuleta ripoti ya uongo kwenye RCC kuwa Halmashauri zimekubali suala hili la *smart area*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *smart area* hii lazima itazame na maeneo. Mji wetu huu; vijana wetu, watu wetu, uwezo wao wa kuwa na mitaji mikubwa hawana; leo zoezi hili ambalo sisi tunasema ni lazima usafi uwepo, haliendeshwi kwa mujibu wa taratibu za Sheria. Walemavu wako ndani, bodaboda wako ndani, Machinga wako ndani, Mama ntilie wako ndani; hawa wananchi wetu tunawasemea wapi? Leo mwananchi mlemavu anauza chakula Karume, anamwagiwa chakula chake. Hivi Karume ni *smart area*?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukija, maeneo yote ya Mjini yamemjaa matope. Kwa hiyo, *smart area* yale maeneo yatengwe, twenbde kwa *phases*. Ukitoka Move 'n' Peak *smart area*! Kwa hiyo, nasema na msimamo wetu ndiyo huo. *Smart area* ianze kuanzia UWT. Haya maeneo mengine mpaka wayaboreshe. (Makofi)

Mkurugenzi wa Jiji leo anavunja Sheria na hakuna mamlaka inayomwonya au kumkataza, anakusanya faini bila kuwa na mamlaka hayo, bila kuongozwa na Sheria, anatumia Sheria za Halmashauri kukusanya faini na anaachiwa tu. (Makofi)

Kwa hiyo, tunataka majibu haya. Mamlaka zinazohusika bodaboda, Machinga; hawa watu sisi ndio tunaishi nao Mitaani. Kama kuna Viongozi wanaona Kariakoo ni kero, huku nako msije. Kaeni huko huko *Oysterbay*. Mkitoka makazini kwenu, piteni barabara ya *Nyerere Road*, rudini makwenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana hawana maeneo ya kufanya biashara. Hakuna maeneo yaliyotengwa kufanya biashara. Wanakuja na mtaji mdogo sana! Unamkuta mtu anauza mhogo, yeye mwenyewe muhogo hali. Anaogopa akila anaharibu biashara yake. Leo mtu huyu anauza muhogo, ana mahitaji kama yangu mimi, kama yako wewe Naibu Spika, kama ya Wabunge humu ndani, ana mahitaji ya ada, ana mahitaji ya kwenda Hospitali, ana mahitaji ya kulipa kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulaya watu ambao wanakatazwa kufanya shughuli zao katika maeneo, wasiokuwa na kazi wanalipwa *social benefit*. Kwa vile sisi hatuna, tuvumiliane. Hatusemi wakifanya shughuli hizi wafanye uchafu,

hapana. Utaratibu ukisimamiwa na Serikali za Mitaa; kinachofanywa sasa hivi, ni kuingiza mpaka JKT kwenye Mitaa kuumiza akina Mama Lishe, kuumiza walemavu, kuumiza Machinga. Hili halikubaliki! Zoezi hili linafanywa kudhalimu watu. Sisi tunachaguliwa na hawa watu, tunawadanganya kutuchagua halafu tunashindwa kuwasimamia, tunashindwa kuwasemea. Lazima tusimame. Mambo makubwa kabisa yaliyofanywa wala hayachukuliwi, mradi wa chini wanaonewa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zungu, muda hauko upande wetu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, madawa. Hospitali za Dar es Salaam hazina madawa, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Namwita Mheshimiwa Puline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura, Mturura.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Naunga mkono hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, na hotuba zote ambazo zimesemwa ni hotuba ambazo Serikali inatakiwa iziangalie kwa makini na wachukue yale yote mazuri na naamini yote ni mazuri ili wayatekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendeleza pale Mheshimiwa Zungu alipoishia. Nilikuwa natafakari na nilikuwa nauliza wenzangu majirani hapa, hivi dalili za mtu aliyechoka ni zipi? Wakanitajia dalili zifuatazo:-

Kwanza, ni msahaulifu; pili, anafikia kikomo; tatu, anabweteka; nne, anapunguza mwendo na anakosa *control*. Lakini anakuwa analalamika anaumwa, ni mgonjwa, kumbe siyo mgonjwa. Ni mlegevu na analalamika ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii mambo hayaendi. Ukienda kwenye barabara baada ya mwaka zimeshababuka, zimeumuka. Lakini ukienda kwenye afya, tunaambiwa Hospitali za Mikoa zinajengwa ikiwemo ya Mkoa wangu wa Manyara, kila mwaka Serikali inapunguza zile fedha za maendeleo.

Mwaka 2013 Manyara tulitengewa Shilingi bilioni 1.4, mwaka huu wamepelekewa Shilingi milioni 500 lakini rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi tulikuwa tunahoji, kuna rushwa nyingine hazifanyiki sirini; ni wazi barabarani. Mabasi siku hizi hayasimami, trafiki anarushiwa, basi lipo kwenye *speed* ajali zaidi ya 23,000 mwaka huu zimetokea dalili za mtu aliyechoka, dalili ya Serikali iliyochoka. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini elimu yetu ndiyo imekuwa kichaka kabisa. Mnafahamu madaraja yalivyoongezwa, yaani mpaka sifuri huku tumeongezaongeza kwa sababu Serikali imekosa *control*.

Vile vile Maaskari Polisi wetu wanadai Serikali hata posho zao, wana rushwa. Ni Serikali iliyochoka. Maji usiseme mradi wa *World Bank*, ni rushwa tupu! Hakuna miradi, visima mnachimba maji hayatoki! Ni dalili za mtu aliyechoka! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa mara ya kwanza nashangaa, hata Tume ya Taifa ya Uchaguzi wanarushwa hela zao. Yaani mwaka 2010 wameendesha Uchaguzi, zaidi ya Shilingi bilioni mbili hawajalipwa mpaka leo; Kamati ya Katiba na Sheria wamesema. Yaani kwa Walimu msiseme, kwa wafanyakazi, msiseme hata Tume ya Taifa ya Uchaguzi inayowasaidia mkae madarakani mnawaibia! Ni watu wa namna gani nyinyi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dalili ya Serikali iliyochoka na imechoka kwenye mambo mengi sana. Hawa boda boda, naendeleza pale Mheshimiwa Zungu alikoishia.

Boda boda mwaka wa fedha uliopita tulisema tumewasemehe. Mapato yao chini ya milioni nne kwa mwaka, tumewasemehe. Nina *document* ya *TRA* kutoka Mkoa wangu wa Manyara, wanachajiwa laki moja bodaboda, wale guta; *TRA* wanadharau Bunge hili wanakwenda kuchaji hawa bodaboda wakati sisi tumewasamehe. Ni dalili ya Serikali iliyochoka! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana hawa wanakwenda Polisi pale wanaandikiwa *notification* kosa moja, mbili, tatu, nne zaidi ya laki na nusu wanalipa, wengine wanakimbizana na Maaskari wanapigwa. Serikali iliyochoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya, ni Serikali ambayo siyo sikivu; mwaka huu Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa, Erasto Mbwilo na Mkuu wa Wilaya wamekuja kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wananchi wale wa Tarangire, kila mwaka naongea. Hifadhi ile kila mwaka; miaka nane, miaka tisa, miaka kumi hawafanyiwi vilivyo. Wamekaa nje zaidi ya siku nne, wamekwenda huko wananiambia wameenda kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri Mkuu awasiliane na Mheshimiwa Rais atuambie hatma ya wale wananchi kama nyinyi ni wasikivu kwa sababu mimi sioni kama mnasikia kila mwaka tunawaambia. Haya mambo yanaudhi!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hali halisi ya mambo yanavyokwenda, hatuwezi tukavumilia tukaendelea kuwasifia kwamba kuna mambo mnafanya. Nasema ni wasahaulifu kwa sababu gani?

Sasa hivi uandikishwaji wa Daftari la Wakazi, Watendaji wa Wiji na wa Mitaa wameandikiwa na Wakurugenzi wakafanye kazi na Mabalozzi. Jamani, hili daftari la wapiga kura kwanza mmeshavunja taratibu na Sheria za nchi hii. Mnatakiwa muweze kuboresha lile daftari kwa miaka mitano mara mbili. Lakini tumepiga miaka minne hapa, mmenyamaza tu kimya, hamjachoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yanasikitisha! Halafu mwaka huu mnaanza kuboresha, mnatumia Mabalozzi. Mabalozzi wenyewe kuna Mabalozzi wa Vyama Vingi. Hata sasa hivi Serikali imesahau kwamba mwaka 1992 tulijiunga kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, mnatumia Mabalozzi wa CCM wa nini?

Naomba niwaambie wananchi wangu wa Babati na wa Mkoa wa Manyara waende wakajiandikishe, Mtendaji akikataa, hatulali mpaka kieleweke. Kila mmoja ajiandikishe, hawa watu waliochoka tuwaondoe hawatufai!

MBUNGE FULANI: Hatuondoki!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, mnasema hamwondoki lakini naomba tu niwaambie, mngesoma alama za nyakati kwa sababu kama nchi hii vurugu zitatokea zitaanzishwa na Chama cha Mapinduzi.

Acheni kuchepuka kaeni njia kuu mrekebishe haya mambo ambayo tunawaambia mrekebishe! Msipoyarekebisha, wananchi watachukua sheria mkononi!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mabalozzi, Waziri Mkuu awakemee nchi nzima waache Watendaji, waimarishe hilo daftari na waandikishe wananchi. Waache masuala ya kisiasa ili wananchi wafanye maamuzi kwenye masanduku ya kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba Serikali ijipange. Msipojipanga msilalamikie watu kwamba ndio wanalate vurugu. Amani ya nchi hii isiwe wimbo wakati mnachepuka hamfanyi yale ambayo yapo kwenye Sheria na hizi fedha; Waziri Mkuu tuambie, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa upo, haupo? Acha kutuvizia! Serikali acheni kutuvizia! Watanzania tupeni nafasi tufanye maamuzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa nini hamtulii njia kuu msirekebishe daftari? Kwa nini hamtoi fedha kwa wakati?

Kwa nini hampeleki fedha za maendeleo? Mjitafakari! Muangalie kama mnatosha, kama hamtoshi Watanzania wanawaona na watawashughulikia kweli kwenye sanduku la kupiga kura. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hayo kwa sababu hata kwenye TAMISEMI trilioni nne mnakusanya lakini fedha za maendeleo ni Shilingi bilioni 600. Hivi kweli mnatosha? Lakini misamaha ya kodi Shilingi trilioni 1.6, maendeleo kwenye Serikali za Mitaa Shilingi bilioni 600 tu, mmesamehe Shilingi trilioni moja na bilioni mia sita, mnatosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu hawatoshi kwa sababu wamechoka na naomba mjitafakari tu mwondoke kwa amani, hii Tanzania mtuachie ikiwa bado ya amani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Mtutura Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. *(Makofi)*

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimhakikishie tu Msemaji aliyepita kwamba CCM inatosha na itaendelea kuongoza nchi hii mpaka mwaka 3015. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Tunduru Kusini, wapiga kura asilimia 99 ni wakulima. Kwa hiyo, mchango wangu utaelekea katika kuwazungumzia hawa wapiga kura wangu wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri Mkuu, amekuwa akifanya ziara mbalimbali nje ya nchi na anapoona jambo zuri huwa anatuletea. Mojawapo ni ufugaji wa nyuki. Vile vile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Kikwete, naye anaposafiri nje ya nchi, anapoona mambo mazuri huwa anatuletea nchini kwetu.

Kwa mfano, alikwenda Ghana akagundua kwamba kuna mbegu nzuri sana ya mananasi, akasema wakulima wangu wa Tanzania nao ni wakulima wa mananasi akatuletea na mambo mbalimbali, misaada mingi mingi. Hii ni ishara kwamba mtu unapoona jambo zuri ni lazima upeleke nyumbani kwako. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, nataka kuzungumzia hili suala la Stakabadhi Ghalani, nimefanya mawasiliano na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Mtwara, wao wanasema wanaridhika kabisa na mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani; sitaki kumtaja ni Mbunge gani kwa sababu isije ikaleta mgogoro na wapiga kura wake. Lakini sisi watu wa Tunduru hatujaridhika kabisa na kitu kinachoitwa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Haijafanya vizuri kwetu! Imefanya vizuri mwaka mmoja tu kati ya miaka mitano ambayo Stakabadhi Ghalani imekuwa ikifanya shughuli zake katika Wilaya yetu ya Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu wa stakabadhi ghalani kisheria unavyoonekana, ukiisoma ile sheria ni nzuri kabisa ina lengo la kumkomboa mkulima lakini utekelezaji wake na usimamizi wake kwa Serikali kwa kweli tunasema umeshindwa kwa Wilaya yetu ya Tunduru, kwa maana hiyo hautufai.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita tumelazimika kuuza korosho zetu kwa mfumo ule wa zamani wa *cash* na wananchi wamefurahi na wameridhika. Sasa kama hii Sheria ya Stakabadhi Ghalani ambayo imemlenga mkulima wa korosho ambayo haimsaidii, bado anang'ang'anizwa itumike, kwa kweli sisi haturidhiki nayo. Tunaomba Serikali ijaribu kuangalia upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yake ni makubwa kwa sababu katika uzalishaji wa korosho mkulima analazimika kugharamia palizi, kupulizia viatilifu, dawa za kuulia wadudu pamoja na *surphur*, kuvuna, *ku-grade* lakini kutokana na mfumo wa stakabadhi ghalani bado mkulima analazimika kugharamia hata zile shughuli ambazo siyo za kwake. Korosho zikinunuliwa kwa *cash*, mkulima akishapeleka pale tayari ameshamaliza shughuli zake. Hata hivyo, kwa mfumo wa stakabadhi ghalani mkulima huyu analazimika kugharamia mambo mengine yasiyomhusu kama kununua gunia, kumlipa mlinzi, unyaufu na tozo mbalimali ambazo zinamgharimu mkulima kiasi kwamba hata gharama zile za uzalishaji zinaongezeka kutokana na huu mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa kweli wananchi wangu hawajaridhika na hawaupendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi kwa sababu ya kusubiri mfumo wa stakabadhi ghalani uendelee mkulima mpaka analazimika kuuza korosho zake kwa Kangomba. Kangomba ni kipimo ambacho siyo rasmi ambacho kwanza ujazo wake unazidi kilo moja na bei ambayo ananunua mchuuzi yule ni chini ya ile bei elekezi. Matokeo yake mwaka jana zaidi ya tani 2000 wananchi wamelazimika kuuza kwa Kangomba matokeo yake fedha nyingi zimeingia mfukoni mwa watu wajanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu, msimu huu ujao, Mheshimiwa Waziri kama vyama vyetu vya ushirika ambavyo havikopesheki, tunaomba maamuzi ya haraka ya Serikali yafanyike ili wananchi waweze kuuza korosho

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

zao cash ili masuala haya ya kuuza korosho kwa Kangomba yasiendelee kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika wa asilimia mia moja kwamba Chama cha Mapinduzi kitashinda uchaguzi ujao. Wananchi wa kijiji cha Nalasi ambao kipindi kile Mheshimiwa Rais amekwenda kuomba kura pale aliahidi kuboresha zahanati yao ya Nalasi iwe kituo cha afya, kiasi cha fedha ambacho kinatolewa mwaka hadi mwaka ni kidogo sana. Itaichukua Wilaya ile kuweza kujenga kile kituo miaka 15 kama kiwango cha pesa hakitaongezeka. Naomba kiasi hiki cha pesa ambacho kinatolewa Sh.80,000,000 kila mwaka kiongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunataka tusherehekee ushindi wa CCM mwaka 2015 tukiwa tunapita kwenye daraja la Mto Mbesa. Mwaka huu tumetenga kiasi cha fedha, naomba sana Wabunge wenzangu tukipitishie ili ujenzi wa daraja hili la Mbesa uweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, tunacho Kituo cha Afya cha Mkasale. Kituo hiki kila mwaka tumekuwa tukikitengea fedha lakini fedha hizi hazitoki matokeo yake sasa kile kituo cha afya ambacho kinahudumia wananchi wa kata zaidi ya tatu wanakosa huduma za maji. Naomba safari hii fedha hizi ambazo tumezitenga zaidi ya milioni ishirini na tano ziweze kupatikana ili wananchi wale waweze kupatiwa maji katika kituo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa sababu muda ni mfupi sana, ningependa sana nieleze kwa nini Serikali hii haijachoka lakini kwa bahati mbaya sana muda ni mdogo ngoja niongee mambo ya wana Kilindi. Hata hivyo, nadhani hata msemaji anajua kuwepo kwake hapa akipata posho, akiendesha gari la uhakika na kurudi kwa wananchi wake inaonesha dhahiri Serikali haijachoka ndiyo maana ana nguvu ya kuongea. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Serikali imechoka.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Serikali kwa kazi nzuri sana wanayoifanya hususani kwenye Jimbo letu la Kilindi. Wananchi wa Kilindi ni mashuhuda kwamba mambo mengi yanafanyika yakiwemo ya maji, afya na kadhalika lakini kwa sababu michakato inaendelea pengine inaweza

isionekane dhahiri. Naomba niwahakikishie wananchi wa Kilindi kwamba shughuli zinakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa tulilonalo Kilindi sasa hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu atusikie ni barabara. Barabara zote zilizokuwa zimejengwa madaraja, madaraja yamehama, barabara zimekatika, kwa kweli ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wa Kilindi na maendeleo ya Kilindi. Nimeongea na Mheshimiwa Magufuli kama Mbunge wa Kilindi, tayari amelifanyia kazi ametoa maelekezo TANROADS. Nilipenda mwenyewe angekuwepo hapa athibitishie lakini tayari kazi inafanyika wananchi wa Kilindi muwe na subira, Serikali yenu haijachoka kama ambavyo mmeona haijachoka siku zote na barabara zitakamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mema mazuri mengi yanayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tuelekee kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kinachosikitisha na nitaongea kwa kifupi sana, Wilaya yetu ya Kilindi mpaka sasa hivi hatuna watendaji, kuna vijiji 102, tuna watendaji 48 tu, vijiji 54 havina watendaji, wote ni Makaimu ambapo kwingine wanaondoka leo na kesho. Vilevile tuna kata 20 tuna Watendaji wa Kata tisa tu. Kwa hiyo, kwa kweli sijui huu uchaguzi utakuwaje, maeneo mengi hata kwenye Idara wako Makaimu. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumejitahidi sana. Kwa mfano, sasa hivi kwenye sekta ya afya tuliomba ajira ya watumishi 64, cha kusitisha mpaka sasa tumepata ma-nurse watatu tu. Tumeongea na Waziri, Waziri amesema tuandika barua haraka sana na kwa sababu mchakato wa ajira unaendelea basi tutaweza kuongezewa. Naomba niliseme hili na wananchi wa Kilindi muwe na subira. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametuorodhesha katika Halmashauri ambazo zilifanya vibaya katika makusanyo kwa mtiririko wa miaka mitatu. Naam, ukiongeza katika miaka mitatu inaweza ikaonekana kweli hatujafanya vizuri lakini naomba nitoe taarifa katika mwaka 2012/2013 tulikisia Sh.605,000,000 lakini tukakusanya Sh.451,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 65 ya makusanyo yote katika huo mwaka. Mwaka huu sasa tuionao hadi kufikia Machi, tuliongeza kipato kwa mara mbili kwamba tulikisia sasa Sh.1,300,000,000. Hadi kufikia Machi, tumekusanya Sh.705,000,000 sawa na asilimia 53, bado tuna mwaka. Wajumbe naomba hata muwapigie makofi wananchi wa Kilindi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji, hili ni tatizo sugu na wewe umelisema kwenye speech yako na umesema mikakati inafanyika. Utakumbuka mpaka wa Manyara na Mkoa wa Tanga ambapo tunapakana Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Kilindi, uliwahi kuagiza Tume ikafanya kazi wakati Mheshimiwa Lowassa akiwa Waziri Mkuu, ukaja wewe na kazi ile iliendelea na humu ndani ya Bunge ulitoa tamko la ile mipaka. Nisikitike

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kukuambia hadi leo ile mipaka haijaenda kuainishwa ambayo ni kero kubwa na watu wanapigana. Hivi karibuni kulikuwa na kikao cha Mkuu wa Mkoa wa Tanga na Wilaya zake na pia na upande wa Manyara. Wakuu wa Mikoa wale walifanya kazi nzuri, tumepeleka barua Wizara ya Ardhi, tunaomba wafuatilie suala hili na watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli migogoro ya ardhi imekuwa ni sugu sana na hasa siyo tu kwenye hii mipaka ya kitaifa lakini hata kata kwa kata, vijiji na vijiji. Nilikuwa naomba sana tuweze kusaidiwa ili angalau Maafisa Ardhi waweze kushuka kwa wingi. Kuna migogoro mingi sana, hasa pale Lukole ambapo Wenyeviti wa Vijiji, Mzee Hamza Abdallah wanafanya mambo ambayo yanawakera wananchi usiku na mchana na kuweka vitisho na watu kufungwa bila makosa, ni maeneo mengi ambayo yanatolewa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana Wizara ya Ardhi iweze kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikikaribia kumaliza nilitaka nilisemee moja, Wizara ya Maliasili kuna shida. Tumesikia mengi sana, kila siku unasikia mambo ya ile Wizara haijatulia. Sijui kama Waziri Mkuu anafahamu kwamba Maliasili kumetulia au kunafukuta nini na pale ndiyo chanzo cha mapato, tunaambiwa utalii unatupa zaidi ya 17.9 percent ya GDP yetu lakini unashangaa mambo yanayoendelea. Kupitia Kamati Ndogo ya Bunge tuliazimia hapa Mkurugenzi wa Wanyamapori, Profesa Songorwa akaondolewa. Hali kadhalika tukaazimia Waziri naye akaondolewa. Cha kushangaza Profesa Songorwa amerudishwa hatuoni sababu sasa na Waziri arudi kama sababu ni ileile, sioni kwa nini huyu arudishwe huyu asirudishwe wakati Azimio limetoka sehemu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo, hivi karibuni imeundwa Tume ya Mahakama ya kuchunguza mgogoro huu. Sasa hiyo Tume imeundwa lakini mtu yuko mezani, wataweza kumchunguza mtu yuko mezani? Naomba na hili nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha kabisa kwa kusema ninaomba sana Wilaya hizi ambazo ziko pembezoni Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia kwako Naibu Spika, niombe sana hizi Wilaya hizi ziangaliwe kwa macho mengine, watumishi wanakimbia, makazi hakuna. Umeme tuliofungiwa kila baada ya wiki mbili, siku moja umeme wote umekatika kunakuwa na giza, kweli tunakusudiwa kufanya maendeleo yanayotakiwa na makusanyo tutaweza kuyapata?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, yangu yalikuwa haya, kwa bajeti hii naunga mkono asilimia mia moja nikiahidi kushirikiana na Serikali tuweze kutatua hizi changamoto. Ndugu zangu wapendwa Wabunge kulalamika siyo hoja kikubwa ni kwenda kushirikiana na hawa Wizarani ili kuweza kuona tunafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Mheshimiwa Khatib Said Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Said Nkumba.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuongea machache kuhusu hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda, kwanza nitaanza kuzungumzia suala la Mfuko wa Jimbo. Naishukuru Serikali kupitia ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mifuko ya Jimbo hii tunayosaidiwa Wabunge ili tuweze kuendeleza maeneo yetu katika miradi mbalimbali, imesaidia kuchochea kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo langu ni kwa sisi Wabunge wa Zanzibar ambapo Mfuko wa Jimbo imekuwa kama ni sadaka ya Mwinyi Sadala. Mfuko wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar imekuwa ni hisani kwamba haina lazima sisi tupatiwe, tofauti na Sheria ya mfuko wa Jimbo inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa juzi na leo nataka niseme kwa uwazi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imezuia pesa ya Mfuko wa Jimbo kwa Wabunge wa Zanzibar ili hali pesa ile haiwahusu. Tunataka Waziri Mkuu atuambie, leo nimesoma kwenye vichwa vya habari vya magazeti, gazeti ya Serikali ya Zanzibar limeandika ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais haijazuia pesa za Mfuko wa Jimbo za Wabunge. Sasa kama haijazuia pesa hizi ziko wapi? Waziri Mkuu tupe jibu na kama hatukupata jibu, Mheshimiwa Waziri Mkuu tukitoka hapa, Balozi Seif Ali Idd atajua pesa pa kuzitoa, hatutakubali. Bahati mbaya sana leo hayupo hapa, kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wabunge tuna miradi tuliyoianzisha. Mimi kwenye Jimbo langu kuna soko najenga ambalo nasaidiwa na Mfuko huu wa Jimbo kiasi fulani, mimi mwenyewe nguvu zangu na Mfuko. Leo wakandarasi wanatishia kunipeleka Mahakamani, watu wangu wananiona mimi nimekula hela Mfuko wa Jimbo. Kwa nini wamechukua pesa zetu? SMZ kwa nini wameiba pesa zetu? Huu ni wizi! Yalisemwa na mimi nasema huu ni wizi. Pesa wamezajenga mnara wa Kisonge wazitoe. Walitaka mazuri wazurike wenyewe pesa hizi haziwahusu. Kiatu kibaya cha baniani huyu wa Muungano lakini kwetu dawa kinatusaidia. Nataka niwaambie, pesa hizi wasipozitoa eeh! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wanasema, mimi nasikitika sana, nataka niseme Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, nataka niseme hivi, yeye wanajua juhudi zilizofanywa na Rais Kikwete ya kupata Serikali ya Umoja wa Kimataifa Zanzibar, leo kwa ulevi tu wa madaraka kama alivyosema Mwalimu ulevi, ulevi tu, wanakwenda wanakaa pale wanasema wanafikiria kwenda kwenye Baraza la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wawakilishi kuvunja Serikali ya Umoja wa Kimataifa, nendeni kesho! Mnamtisha nani? Ninyi mkisema mna Serikali Zanzibar Obama aseme ana nini? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bajeti yake bilioni mia nne hamna! Serikali gani? Azam FC bajeti yake inashinda bajeti ya Zanzibar? Tunakaa hapa tunasema tuna Serikali, Serikali gani? Peleka hela zetu haraka sana kabla hatujaanza, usicheze na hiyo hela kabisa kabisa, hiyo hela ni yetu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala lingine moja ambalo linaniudhi sana. Mheshimiwa Mbunge wa Temeke alizungumza hapa kaka yangu Abbas Mtemvu, suala la wananchi wa Kurasini ambao Serikali kwa makusudi tu inawanyanyasa wananchi wale pasipo na sababu kutokana na mradi ule. Leo imekuwa ni suala la kila mwaka tunakuja hapa tunapigiana kelele kuhusu watu wale. Hebu kama ni ninyi hebu niwaambie, mnawahamisha watu pale, mnawaambia nendeni popote tu hamuwalipi maana yake nini? Shilingi bilioni kumi na moja zilizokuwemo kwenye bajeti iliyopita ambazo ilitakiwa watu wale wapewe muwalipe na kama hamuwalipi nawaomba sasa Wabunge wa Dar es Salaam msikubali bajeti hii ikapita, si mnawaonea huruma wale! Watu wahamishwe na watoto wao walikuwa wanasoma pale, watu wana maisha yao pale, wana wapangaji wao pale wameondolewa walikopelekwa hakujulikani. Mradi ambao tunasaidiwa ambao utatoa ajira kwa vijana 25,000 Serikali hii imeshindwa kutoa Sh.50,000,000,000 wakakamilisha kulipwa Wachina wakatujengea pale. Leo mkiambiwa mmechoka mnataka muambiweje? (Makofi)

Ndugu zangu niwaambie akili ya mgonjwa iko mikononi mwa mzima. Kwa hiyo, tunavyowaambia wamechoka wanakataa sasa sisi tuwasukume kwa namna nyingine. Hebu walipeni watu wale mliowahamisha pale Kurasini haki yao, wale ni Watanzania wenzetu wananyanyasika kwa nini? Kama mnaona mnaweka mradi ambao hamjawa na pesa ya kuufanya msihamishe watu, dhambi. Aliwahi kusema, nataka nimnukuu hapa baba wa Taifa moja, alisema:-

“Makosa ni makosa na dhuluma ni dhuluma. Japo watendao makosa hayo au dhuluma ile ni wakubwa au ni wengi au Chama kinachopenda ukweli hakina budi kiwape wanachama uhuru wake, uhuru wa nafasi ya kusahihisha makosa na kuondoa dhuluma. Wanachama hawanabudi waone kuwa ni wajibu wao kutumia uhuru huo na nafasi hiyo ila bila kuogopa au kuchukukiwa au kupoteza nafasi yao”.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno hayo alisema baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere kwenye kitabu chake cha Tujisahihishe. Hiki kitabu mlitungiwa nyie

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

jisahihisheni. Hiyo siyo haki. Wale watu wa Kurasini jamani wapeni haki yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nataka kuzungumzia kuhusu TAKUKURU. Leo asubuhi niliuliza swali hapa nikajibiwa ooh, tunashughulikia Mheshimiwa hamna! Leo hii, kwa ufupi tu hapa niwaambie, Serikali inaingia mkataba mradi wa shilingi bilioni moja, watu wanakurupuka mradi unapaa unafika shilingi bilioni sita. Kule Arusha kuna Chuo cha Uhasibu kilikasimiwa kitumie shilingi bilioni mbili, zimetumika shilingi bilioni sita bila ya maelezo TAKUKURU wako wapi? Hamlioni hili? Pale *Dar es Salaam Eda Estate, BRELLA* wamenunua kiwanja ambacho Mtathmini wa Serikali alisema kinunuliwe kwa Sh.1.2 bilioni, wanaume wamechota Sh.2.7 bilioni, TAKUKURU wako wapi? TAKUKURU hawapo hawayaoni haya? Kiwanda cha Urafiki pale, wanaume wamechota dola milioni ishirini na saba kwa kurekebisha kiwanda kile, zimeliwa zote, TAKUKURU wako wapi? Leo tukimwambia yule Mzee Mkuchika ondoka huwezi haya mambo, umechoka, anaona sisi tunamuonea. Jamani ukichoka pumzika. Mheshimiwa Waziri Mkuu wako vijana huko walete waongoze jahazi wazee wamechoka, kwisha kabisa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoyasema haya inaonekana utani, kama hamkubali hapa uwanjani, mkikaa vyumbani fikirieni kama haya tunayoyasema yana ukweli ni kwa faida ya Taifa hili na Watanzania wa leo na wa kesho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nizungumzie...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Bado, bado.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Khatib Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Ahsanteni, ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, muda hauko upande wako. Mheshimiwa Said Nkumba atafuatiwa na Mheshimiwa David Kafulila.

MHE. SAIDI J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwanza naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimesisima hapa nizungumzie suala moja la ajira za Maafisa Ugani. Tulikuwa na malengo mwaka 2015/2016 tutakapokuwa tumefika huko tuwe na Maafisa Ugani 15,082, hawa

wangetutosheleza katika kila kijiji na kila kata. Hata hivyo, utekelezaji wetu mpaka mwaka 2013 ambapo tulikuwa na wahitimu 8,659 walioajiriwa ni 4,595 jumla sasa tunao 7974 lakini kwa ujumla wake tuna upungufu wa Maafisa Ugani 7108.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu 2014, kimetolewa kibali cha ajira. Kibali kilichotolewa ni cha vijana 1,804 wanaotoka kwenye vyuo lakini ajira halisi ambao wameajiriwa kwa mwaka huu ni 1,382, vijana 422 wameachwa. Ombi langu, nilikuwa naiomba Sekretarieti ya Ajira iwaajiri hawa vijana 422 waliobaki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake nilikuwa naomba, vijana wote waliobaki sasa ambao hawana ajira na wamemaliza vyuo vya kilimo waajiriwe na Serikali ili tuzibe haya mapengo yaliyopo kwa ajili ya maslahi ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hili tu, sasa naomba nirudi. Kwanza, naomba niwaambie kwamba lazima mjue njia kuu ni CCM, sasa sisi hatuwezi kuchepuka kwenda maeneo mengine. Hata hivyo, nataka nisema Chama kilichochoka ni kile kinachofanya juhudi kila mwaka wa uchaguzi kishinde lakini kinashindwa, hicho ndicho kilichochoka. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimwia Gekul na Mheshimiwa Khatib labda kama mna maneno ya kinyumenyume lakini kama mna maneno ya kimbelebele, CCM na Serikali yake iko uwanjani na Wapinzani wako huko wamechepuka wanatafuta jezi na viatu, wanashindwa kuingia uwanjani. Nataka niwaambie kama upinzani ni wa namna hii, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kutawala Tanzania daima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa naangalia, nimeangalia hotuba ya Kiongozi wa Upinzani nikajiuliza, hivi kama Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani ambaye ndiye *cream* ya Upinzani iko hivi, je, ya wale wengine itakuwaje? Vilevile nilikuwa naangalia huyu Mheshimiwa Mbowe ndiye Kiongozi wa Upinzani, amewahi kugombea Urais na ndiye mwenye matumaini ya kugombea Urais tena, kiongozi wa UKAWA, badala ya kujenga hoja za kisera kusaidia Serikali hii iliyoko madarakani izeze kuwatendea mambo mema wananchi, amekuja hapa na hoja ya Katiba na hoja ya madaraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niseme, mimi nilikuwa najiuliza hizi hotuba zinatungiwa wapi, zinatungiwa chumbani au zinatungiwa wapi? Maana kama hotuba ambayo baadaye inakwenda kusomwa mbele ya wapinzani, maana nimemsikia Mheshimiwa Gekul hapa kwamba wananchi wanataka maji, wananchi wanataka barabara, wananchi wanataka afya. Sasa

Mheshimiwa Gekul kwa nini hukumshauri Kiongozi wako wa Kambi ya Upinzani hayo ayaweke badala yake anakwenda kuzungumzia Katiba? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Mheshimiwa Mbowe kwenye hotuba yake amezungumzia sana matumizi mabaya ya Serikali, matumizi mabaya ya vyombo vya habari, nataka nimkumbushe na hasa amelaumu TBC, analaumu magazeti *Daily News* na *Sunday News* na kadhalika. Nataka nimkumbushe, hivi vyombo vyote ukiona CCM inaandikwa, ukiona CCM wakati mwingine labda Televisheni ya Taifa inaonyesha hotuba, tumelipa, CCM imelipa. Hivi ninyi CHADEMA mmewahi kwenda kuomba au kwenda kulipa mkashindwa kuhudumiwa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka niseme, haya matumizi mabaya ni ya Serikali tu? Hivi Mbowe ana usafi gani? Mwaka jana Mheshimiwa Mwigulu alilalamika, alitoa maelezo hapa yaliyokuwa yanaonesha kwamba Mheshimiwa Mbowe alitoka hapa akaenda Dubai, yupo Mheshimiwa mmoja wa jinsia tofauti na Mheshimiwa Mbowe alikuwa Dominica. Yeye akiwa Dominica amelipwa posho na Bunge, hayo matumizi hayo ni mazuri? Mheshimiwa Mbowe akakatisha ziara ya kwake yeye kwenda huko na Wabunge wenzake, akamwambia aje kuvinjari Dubai. Hayo ni matumizi mazuri? Mbona hayo hamyasemi mnasema matumizi mabaya tu ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kawaida yake akishachemsha hapa anatoroka, hata huko aliko ujumbe unamfikia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo huyo Mheshimiwa Mbowe alilidanganya Bunge hapa kwamba hatachukua gari, ilikuwa gari imechakaachakaa hapa, alipoona gari mpya amelichukua kimya kimya bila kutoa maelezo. Sasa ile gari tena katika hali ileile ya matumizi mabaya kaenda nayo mpaka Mombasa imekamatwa kule, inashukiwa kwamba imebeba mabomu. Hayo hamyasemi, mnazungumza tu habari za Chama cha Mapinduzi na Serikali yake. Acheni michepuko rudini kwenye njia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie, nimeona hapa kuna habari ya ndoa sijui ya CHADEMA na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Said Nkuma.

MHE. SAIDI J. NKUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa David Kafulila atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini. Mheshimiwa Kafulila endelea!

MJUMBE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu ambayo kimsingi ni hotuba inayoonesha mwelekeo au tathmini ya nchi katika mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ningependa kuanza na suala la utawala bora katika Serikali hii. Katika Serikali hii kuna matatizo makubwa sana ya Watendaji kunyanyasa raia. Naomba niweke kwenye *record* kabisa kwamba Mkuu wa Wilaya ya Uvinza aliyetoka Chato, ameondolewa Chato akiwa na kesi Mahakama ya Wilaya ya Chato, ana kesi tano, mashtaka 63, ameletwa Wilaya ya Uvinza amesababisha matatizo ya kuchoma nyumba za wakulima wanyonge. Nimepeleka suala hili kwa Waziri Mkuu huu ni mwaka wa pili mpaka leo Serikali inashindwa kuchukua hatua dhidi ya huyu DC. Hivi mnataka muambiwe nini?

MBUNGE FULANI: Wamechoka.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Huyu DC amepoteza uhalali wa kuendelea kuwa mtumishi wa Serikali kama kweli Serikali hii inaheshimu *integrity*, hilo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pamoja na hilo hilo, leo hii Watanzania kwa muda sasa wamekuwa wakisikia kwenye vyombo vya habari na ushahidi unatolewa kwamba TANESCO wakati ina mgogoro na Kampuni ya IPTL walifika mahali wakafungua akaunti inaitwa *Escrow Account* ikawekwa pale Benki Kuu. Tangu mwaka 2004 mpaka sasa Akaunti ile ilikuwa imetimiza takriban dola 122, ikiwa ni utaratibu wa kwamba kesi itakapomalizika na mgogoro utakapomalizika kati ya IPTL na TANESCO pesa ile iweze kugawanywa kulingana na *formula* itakayopatikana baada ya usuluhishi wa Baraza la Usuluhishi la ICSID ambalo ni Baraza la Wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni bahati mbaya sana sekta ya umeme ambayo leo inapigiwa kelele kila kukicha kwamba kuna maeneo mengi yanahitaji umeme ili kujenga uchumi bado pesa yake ya TANESCO imegawanywa kihuni pale Benki Kuu. Jambo hili, naomba liingie kabisa kwenye *record* ya nchi linahusu Benki Kuu yenyewe, linahusu vigogo kwa maana ya Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na linahusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ushahidi upo, hii pesa wamegawanya pale Benki Kuu kinyume cha utaratibu. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, TANESCO wakati ina ina madeni ya takribani bilioni mia nne zinawekwa pale dola 122, anakuja Singasinga wanafanya ufisadi. Anaanzisha kampuni ya PAP inasema inanunua IPTL. IPTL ambayo inanunuliwa iko *under liquidation* Malaysia.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote, pesa ile inatolewa pale kwa maana ya kwamba yalikuwa ni mauzo ambayo yangepaswa kufanyika kwa TANESCO kununua umeme wa IPTL. Kwa utaratibu wa kisheria ilipaswa kodi ilipwe, lakini mpaka Benki Kuu inatoa pesa ile hakuna kodi iliyolipwa. Upo ushahidi kwamba TRA waliandikia Hazina, wakiwataka Hazina pesa hiyo itakapotoka kodi ibaki lakini Hazina haikuweza kuelekeza Benki Kuu waweze kusaidia mchakato wa kupata kodi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemuita Gavana kwa mfano kwenye kikao cha Kamati yetu ya Uchumi, Gavana anakiri kwamba jambo hili kwa namna *pressure* ilivyokuwepo ya kutoa pesa ile mimi kama Gavana sikuwa na namna. Yeye mwenyewe Gavana anakiri kwamba palikuwa na mashinikizo makubwa ya vigogo wa Serikali hii kuhakikisha pesa ile inaondolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Baraza la Usuluhishi la Migogoro ya Uwekezaji Kimataifa (ICSID) walikuwa waamue leo hii kuhusiana na *computation* ya *recalculation* ili kusudi kiasi fulani kiende IPTL kiasi fulani kiende TANESCO. TANESCO wameiandikia barua ICSID wanakataa *recalculation* kwa sababu wanajua pesa ile tayari imekwishakuliwa na wanjanja wachache. Mheshimiwa Waziri Mkuu hili ni jambo ambalo kwa namna yoyote na kwa viwango vyovyote halikubaliki, hii ni zaidi ya EPA. Dola 122,000,000 ni takribani 200,000,000,000 hamuwezi kutafuna pesa hii na jambo hili likaisha, haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Wizara ya Fedha muwajibike, tunataka Benki Kuu iwajibike, tunataka Wizara ya Nishati na Madini iwajibike, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lazima muwajibike. Nashangaa huyu anayejiita Mkurugenzi wa TAKUKURU, watu wana ushahidi wote wa namna gani *deal* imepigwa pale anasubiri nini kwenda Mahakamani? Anasubiri nini? (Makofi)

MJUMBE FULANI: Naye awajibike!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo halitafunikwa lishe hivihivi, tunataka maelezo ya kutosha na hili jambo lazima liondoke na mtu, haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu kwenye hospitali hawana shuka....

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Wanagawana, mtu anasema amechukua shilingi bilioni mia moja ishirini ni hela ya ugolo, kweli? Bei ya umeme inapanda kila kukicha, *ICSID* wanasema mfanye *recalculation* bei ishuke ninyi mnasema hamuhitaji *recalculation* kwa sababu mmekwishalamba hela, haitawezekana hii. Haitawezekana, ni lazima uwajibikaji ufanyike. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la lingine, nchi hii reli ya Kati ndiyo uhai. Hakuna nchi duniani ilianza kujenga barabara kabla ya rel, haipo! Naomba mtu aje hapa, msomi wa viwango vyovyote vile aseme nchi gani wamejenga barabara kabla ya reli. Kwenye uchumi wa usafirishaji, uhai wa barabara ambayo inakwenda sambasamba na reli imara, *maintenance* inachukua ni baada ya miaka kumi. Hata hivyo, kwenye mazingira ambayo reli ni duni kama reli ya Tanzania ukiacha reli ya Malawi, katika Afrika hii ndiyo reli duni ya pili baada ya reli ya Malawi. Sasa unajiliza kwamba tunatumia gharama kubwa ya kufanya *maintance* kila baada ya miaka miwili kwa sababu mzigo mkubwa unapita kwenye barabara ambapo kama tungekuwa na reli imara ingepita huko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nipo darasa la kwanza uwezo wa reli ya kati ulikuwa ni kubeba tani milioni moja na laki nane. Leo hii nikiwa Mbunge reli ya kati inabeba tani chini ya laki nne kwa mwaka. Hamuwezi kujenga uchumi...

MBUNGE FULANI: Wamechoka.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: *Eastern Congo* peke yake inahitaji kupitisha mzigo reli ya kati wa takribani tani milioni tano. Hiyo peke yake ingetoshwa kabisa kuingiza pesa za kigeni katika Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hilo, kuna tatizo la muda mrefu la wafanyakazi kwamba... (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kafulila. Mheshimiwa Roman Selasini atafuatiwa na Mheshimwia Felister Bura!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Waziri Mkuu imezungumza mambo mengi sana lakini nadhani kwa bahati mbaya haikuzungumza kuhusu suala la mazingira. Mimi nafahamu suala la mazingira liko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais lakini nilidhani kwa umuhimu wake Waziri Mkuu angelizungumza kidogo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa sababu watekelezaji ni Wakuu wa Mikoa na wako hapa ili waweze kujua ni nini cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nchi yetu imeingia katika mgogoro mkubwa sana wa mazingira. Tunashuhudia mafuriko katika kila Mkoa na wakati mwingine ukame karibu kila mahali katika nchi yetu na hii ni kwa sababu ya uharibifu wa mazingira ambao nadhani mkakati wa kutosha bado haujafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa sababu ya jitihada zake za kuhimiza upandaji miti katika Mkoa wa Kilimajaro. Hili ni kwa sababu Mkoa wa Kilimanjaro sasa hali ya hewa inabadilika kwa kiasi kikubwa sana, joto limekuwa kubwa na mvua zimekuwa za mashaka kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba hifadhi ya mazingira katika Mkoa ule inahimizwa na vilevile tunahakikisha kwamba mlima wetu unalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ningemuomba sana Mkuu wa Mkoa alegeze baadhi ya masharti ambayo ameweka kwa wananchi kukata miti yao. Nasema hivyo kwa sababu baadhi ya wananchi hasa katika Jimbo langu wanalalamika sana kwamba miti yao iliyokamaa wanakatazwa kuikata kwa sababu mbalimbali na baadhi ya Watendaji wa Serikali katika Wilaya sasa wameamua kazi mojawapo wanayoifanya ni kupambana vijijini kutafuta wazee wanaokata miti yao na hivyo kuongeza rushwa kwa Watendaji hasa Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia pia suala la maji. Hadi sasa katika ahadi ile ya Serikali ya visima kumi vya maji hakuna kisima hata kimoja Rombo ambacho kimeshaanza kuwanufaisha wananchi. Hata hivyo visima ambavyo vimechimbwa viko katika hatua mbalimbali. Kuna visima vitatu ambavyo tenda imetangazwa sasa kwa ajili ya kuanza kutengeneza miundombinu. Vilevile kuna visima vitano ambavyo vilichimbwa na bonde la mto Pangani na sasa hivi tatizo kubwa tulilionalo ni fedha kiasi cha shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya kujenga miundombinu hasa ya umeme ili kuwezesha visima vile vipate kuwanufaisha wananchi. Naomba sana Wizara ya Maji itusaidie kwa sababu Rombo tuna shida kubwa sana ya maji hasa ukanda wa chini ambako hivi visima ndiko vinakochibwa ili wananchi na wenyewe waweze kuona kwamba wanahudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa kuzungumza kuhusu elimu. Wengi wamelalamika hapa kuhusu Wakaguzi. Jimbo la Rombo ni moja kati ya Majimbo ambayo yaliitikia kwa kiasi kikubwa sana wito wa Serikali wa kujenga shule za kata. Tunazo shule 41 karibu shule mbili katika kila Kata. Hata hivyo, Idara ya Ukaguzi imekufa, hakuna kinachofanyika, hawana gari wala vitendea

kazi. Hatuwezi tukazungumza hapa kunyanyua kiwango cha elimu wakati hakuna mkakati wa makusudi unaofanyika kuhakikisha kwamba Wakaguzi wamefanya kazi yao ili Walimu na wenyewe waweze kutimiza wajibu wao na wanafunzi watimize wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tuna tatizo kubwa sana la malalamiko ya Walimu kuhusu malipo yao mbalimbali. Hili ni lalamiko ambalo lipo karibu katika kila Jimbo. Naiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba malalamiko na madai ya Walimu yameshughulikiwa kikamilifu ili waweze kupata moyo na ari ya kuendelea kufanya kazi zao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumza kuhusu ajira kwa vijana. Limezungumzwa na mimi naona ni vizuri pia nilizungumze. Serikali inahimiza vijana kujijiri na vijana wengi wamejijiri katika biashara hii ya bodaboda. Pale Rombo vijana wengi sana karibu katika kila Kata wanavikundi vyao kwa ajili ya bodaboda. Kero iliyopo na ningeomba Serikali itoe tamko, inawezekana vipi pikipiki moja ikaandikiwa *notification* shilingi laki moja na elfu themanini, inawezekana vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa sana kutumia lugha kalikali dhidi ya Watendaji wanaohusika na jambo hili lakini hii ni kero, haya ni malalamiko ya hali ya juu na vijana wanakimbizwa, wakati mwingine vijana wanaanguka, wanavunjika, wanaumia. Hata tunavyoongea sasa hivi, kuna kijana amelazwa pale Huruma Hospital, amevunjika kwa sababu ya kukimbizwa ili akamatwe aandikiwe *notification*. Sasa hili siyo jambo zuri sana, ningeomba lishughulikiwe kikamilifu ili vijana hawa kwa sababu sisi wenyewe tunahimiza wajijiri, basi waweze kujijiri na waweze kupata kipato chao waondokane na kuambiwa ni wazururaji na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika suala la usalama, kule Rombo wananchi wamejitolea kujenga vituo vya Polisi. Wanajenga kituo cha Polisi Mahida, Mengwe, Useri na pale Shimbi. Naiomba Serikali, kwa sababu vituo hivi kwa kiasi kikubwa wananchi wanachangishana na vilevile fedha za Mfuko wa Jimbo zinasaidia katika kuhakikisha vituo hivi vimejengwa ili kuweza kuwasaidia wananchi kuwa katika hali ya usalama hasa kwa sababu Jimbo la Rombo ni la mpakani na tunahitaji sana kuhakikisha kwamba Polisi wetu wako katika vituo ambavyo vinaweza vikahifadhi silaha ili waweze kuwalinda wananchi wetu vizuri. Tunaomba, kwa sababu wananchi wamejitokeza na wamejitolea kuhakikisha kwamba wamefanya kazi hii, basi Serikali ipate kuwasaidia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selasini, ahsante sana. Mheshimiwa Felister Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa na uzima siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa mradi wa Tanzania *Strategic Cities Project*, ambao umefanya mji wa Dodoma kuwa kama Ulaya ndogo kwa barabara zake ambazo zimetengenezwa vizuri sana. Niwaambie wananchi wa Dodoma na hasa kata za Majengo, Uhuru na maeneo mengine kwamba mradi upo, wale wafanyabishara eneo la soko la Majengo, barabara ile ambayo ni mbovu itatengenezwa kwa sababu fedha zipo, baada ya bajeti hii kupita, barabara hizo zitatengenezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali sasa itupe maelezo kwa mauaji makubwa ambayo yalitokea kule Kiteto kwa wakulima wa Wilaya ya Kongwa, Wilaya ya Chamwino na Wilaya ya Chemba. Wananchi waliuawa kinyama sana, wananchi walikopa benki na mashamba yao yakafyekwa, wengine wamekufa na watoto wao. Mahali popote ambapo athari kubwa kama hizi zinapotokea Serikali hufanya tathmini lakini cha ajabu ni kwamba mauaji yaliyotokea kule Kiteto kwa wananchi wale, hakuna tathmini ambayo imezungumzwa na Serikali. Ninaisihi Serikali yetu kwamba tupate tathmini na wale waathirika ambapo wengine wamekufa na watoto wao, Serikali ituambie inawaangalia kwa jicho gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma katika hotuba ya Waziri kwamba ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri zilizoanzishwa, wametengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi. Hata hivyo, Mkuu wetu wa Mkoa ana miaka zaidi ya minne hana ofisi. Kamati ya TAMISEMI walitembelea wakaomba fedha kwa ajili ya kukamilisha ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Nimeangalia katika bajeti ya Waziri wa TAMISEMI, amezungumzia tu ofisi mpya za Wakuu wa Mikoa mipya na Halmashauri mpya zilizoanzishwa. Ninaomba kujua, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma itakamilika lini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia miradi ya maji, tumeongea miaka minne sasa kuhusu mradi wa maji katika Wilaya ya Bahi. Tuliomba shilingi bilioni moja na milioni mia tano lakini mpaka leo wale wananchi wanaokaa pale na watumishi waliohamishiwa Wilaya ya Bahi hawana maji, wanategemea hisani ya *Mission* ambayo ina maji kutoka Manyoni. Ni lini sasa Serikali itawapa wananchi wa Bahi maji safi na salama kwa sababu tunategemea Matoke Mazuri Sasa ambayo hayaji kama huduma kwa jamii hazipo. Ninaiomba Serikali yetu kwamba wananchi wa Bahi sasa wapatiwe maji, shilingi bilioni moja na milioni mia tano, sidhani kama ni tatizo kubwa kwa Serikali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini fedha za miradi zinapochelewa, Serikali inatumia fedha nyingi sana kukamilisha miradi ambayo inachelewa. Mradi wa maji Bahi umechelewa na miradi ya vijiji 10, tuna vijiji viwili tu miradi imekamilika,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kijiji cha Chididimo na Mkonze lakini miradi ya maji Gawaye, Mchemwa, Chigongwe, Michese, Mikoyo na kadhalika wakandarasi wako *site* lakini fedha za kuwalipa wakandarasi, hazipo. Ninaiomba Serikali ifikirie na kuwafikiria wananchi hao wanaoteseka kwa sababu hali ya Mkoa wa Dodoma inajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 31 wa Hotuba ya Waziri, nimeona fedha za huduma za afya zilivyozungumzwa pale lakini hospitali yetu ya Mkoa ilijengwa mwaka 1923, miundombinu imechaka, kuna wodi ya wazazi ilikuwa inajengwa pale, shilingi milioni mia tano, tumeshaomba miaka minne! Jamani, wazazi wanalala watatu, wanne, matokeo yake watoto ndiyo wanaolazwa vitandani, wazazi wanakesha, wanashinda wamekaa, kwa sababu wananchi wameongezeka lakini hospitali iliyojengwa 1923, iko vilevile! Naiomba Serikali sasa ione namna ya kutoa hizo shilingi milioni mia tano ili wazazi wa pale hospitali ya Mkoa ambayo inaitwa hospitali ya rufaa wodi ile ikakamilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa ifike wakati ambapo Serikali izibe mianya ya fedha zinazovuja. Kuna mishahara hewa ambayo imetajwa na CAG katika ripoti yake. Nadhani fedha hizi zingezuiliwa, zingefanya kazi kubwa. Trilioni moja ni fedha nyingi sana, zingeweza kukamilisha mambo mengi. Tunategemea Matokeo Makubwa Sasa katika elimu, Walimu wanadai fedha, tunategemea Matokeo Makubwa Sasa katika mambo ya maji, hakuna fedha, lakini trilioni moja zimelipwa mishahara hewa. Serikali iangalie sasa namna ya kuziba mianya ya fedha ambazo zinavuja bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna ajira kwa watumishi wa kada za chini katika Halmashauri zetu, naipongeza Serikali kwamba wametoa ruksa sasa Halmashauri ziajiri. Hata hivyo, naomba Waraka uende mapema kwa sababu huwa wanatoa taarifa Bungeni lakini Waraka unachelewa! Sasa Waraka uende mapema ili Halmashauri ziweze kuajiri na itakuwa vizuri sasa kuongeza ufanisi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo cha umwagiliaji kule Bahi, ule mradi umesimama.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FELISTER A. BURA: Nakushukuru sana, naunga mkono. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ferister Bura ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nataka niunge mkono hotuba ya Waziri Mkuu lakini yapo mambo ambayo tunahitaji yafanyiwe kazi ili tuweze kwenda haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni miundombinu. Mkoa wa Katavi ni Mkoa ambao hauna barabara za lami. Kuna barabara ya lami kati ya Sumbawanga kwenda Mpanda imekwama mpaka sasa haeleweki ni kwa nini barabara hii haijakamilika. Tuna barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma, mwaka jana ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni nne ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami mpaka sasa hakuna lolote lililofanyika. Naiomba Serikali iweze kuharakisha mchakato ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiunganishi kingine ni barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora kupitia Inyonga, Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele. Bado barabara hii haijawekwa katika mpango wa ujenzi wa kiwango cha lami. Ni Mkoa pekee ambao bado hauna barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye miundombinu vilevile hasa barabara za vijijini, hasa zinazounganisha Wilaya na Mkoa. Tunayo barabara ya Kibo - Mwese, bado ni mbaya inahitaji iongezewe fedha za kutosha ili iweze kujengwa na iwasaidie wananchi wa maeneo hayo. Barabara ya Kalema - Mpanda, nayo inahitaji ipate fedha za kutosha. Kwa ujumla barabara zote za vijijini, hatujapata fedha za kutosha ili ziweze kusaidia wananchi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni bandari. Kuna ujenzi wa bandari ya Kalema ambao una miaka karibu minne. Bandari hii ilipatiwa mkandarasi ambaye hana uwezo, tena kwa mazingira ambayo yanasikitisha sana. Aliyepewa ujenzi wa bandari ile alipewa bandari nne, uwezo wake ni mdogo na alipewa kwa mazingira tu ya *kindugunisation*. Naomba Serikali iangalie na nitahitaji kupata maelezo mazuri kutoka kwa Waziri mhusika ili atoe ufafanuzi wa kuchelewa kwa ujenzi wa bandari ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la ukosefu wa fedha kwenda kwenye Halmashauri za Wilaya na Mkoa kwa ujumla. Mkoa wetu ni mchanga, bado mpya, jitihada za Mkuu wa Mkoa anazozifanya ni kubwa kuhakikisha Mkoa unakwenda lakini bahati mbaya kikwazo kikubwa ni fedha. Fedha ambazo tumepelekewa Mkoa mzima ni karibu asilimia 54 ambazo zimeshindwa kutekeleza miradi mingi ya maendeleo. Naomba katika bajeti hii fedha zielekezwa na ziende kwa wakati ili zikakamilishe miradi ambayo imekaa hasa miradi ya maji, miradi ya elimu ambayo imesimama kwa ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni migogoro ya wananchi na hifadhi. Mkoa wa Katavi asilimia kubwa una mapori makubwa ambayo mengi

yanamilikiwa na Serikali. Bahati nzuri, Serikali ya Mkoa ilitoa wito kwa wawekezaji na kwa wananchi wote waje wawekeze katika Mkoa wa Katavi. Wananchi walio wengi wamekuja Katavi, wamekuja kuwekeza hasa kwenye shughuli za kilimo. Bahati mbaya hawana maeneo ya kufanyia kazi. Karibu kila eneo wanaloligusa, ni mali ya Serikali. Naomba sasa Serikali iangalie upya yale maeneo ambayo yamemilikiwa na Serikali yaweze kugawiwa kwa wananchi ili yaweze kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye huduma za maji, kuna miradi ambayo imekaa ambayo haina fedha za kutosha. Kuna mradi wa Mwese na leo kwenye swali la msingi niliuliza, kuna mradi wa maji wa kijiji cha Majarila, mradi wa Ngomarusambo, mradi wa kijiji cha Igagala, bado miradi hiyo haijapata fedha za kutosha. Niiombe sasa Serikali iweze kupeleka fedha hizo ili iweze kukamilisha miradi hiyo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya kilimo, naiomba Serikali iangalie upya na iache mtindo ambao imeufanya msimu uliopita. Mwaka juzi iliagiza chakula kutoka nje wakati baadhi ya Mikoa kama ya Rukwa, Mbeya na Katavi walikuwa na mazao ambayo hayakuwa na soko. Bahati mbaya wananchi walio wengi hasa wakulima, walipoteza mali zao na wameuza mazao kwa bei ya chini sana. Niiombe Serikali ielekeze nguvu na itenge fedha za kutosha kuhakikisha wananunua mazao ya wakulima ili yaweze kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta hiyohiyo ya kilimo hasa kwenye zao la tumbaku, nilikuwa naomba sana Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuajiri ma-classifier watakaosaidia kuteua zao la tumbaku kwa nchi nzima. Zao hilo bila kuwa na classifier haliwezi kwenda vizuri kwa sababu linahitaji huduma hiyo ya uteuzi wa madaraja mbalimbali. Serikali iajiri classifiers wasiopungua 30 ili yaweze kukidhi katika nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe tena Serikali kwenye sekta ya elimu, hasa malalamiko ya Walimu. Walimu wana madai ya fedha zao za likizo, kupanda vyeo na vitu vinginevyo ambavyo vinaihusu idara hii ya elimu. Naomba Serikali iweze kulipa malimbikizo yao ambayo ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la mawasiliano, ninazo Kata tatu ambazo hazina mawasiliano katika Jimbo la Mpanda Vijijini. Kata hizo ni Kata ya Katuma, Sibwesa na Kabungu, hizo kata zinahitaji zipate mawasiliano. Umekuwa ni wimbo wa mara kwa mara, kila tunapomwambia Waziri anasema atatekeleza. Niiombe sasa katika mwaka huu wa fedha Serikali iweze kupeleka huduma hiyo ya kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye huduma ya afya, tunacho kituo cha muda mrefu ambacho kipo pale mjini Mpanda hakijatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha Chuo cha Uunguzi. Naomba sana eneo hili nalo Serikali ipeleke fedha ili ziweze kuwanufaisha wananchi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Nimekuona Mheshimiwa Machali umesimama.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nasimama kuomba mwongozo wako. Kuna Mheshimiwa Mbunge ambaye nimeona amekamata kitu kama ndoo hivi. Sasa nikajiuliza maswali, humu ndani siku hizi Wabunge tunaingia na ndoo? Suala la usalama ni muhimu sana isije ikatokea watu pengine wana tindikali na kadha wa kadha. Labda ningeomba nipate mwongozo wako, ni lini Wabunge tunaingia na ndoo? Mheshimiwa Mama Kabaka nimeona anapeleka kandoo kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama. Basi watusaidie kuweza kupata ufafanuzi vinginevyo kama tunaruhusiwa kuja na ndoo, basi kila Mheshimiwa Mbunge, labda tupate ufafanuzi, hiyo ndoo ni ya nini ili kutuondoa mashaka humu ndani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mama Kabaka.

MJUMBE FULANI: Hayupo!

NAIBU SPIKA: Hayupo?

MJUMBE FULANI: Hayupo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Ipo kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama pale, amekaweka hivi. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jenista, kuna usalama?

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kumsaidia Mheshimiwa Machali, Mbunge kijana kumwelekeza utaratibu mzuri wa utunzaji wa mazingira. Nadhani kwa uzoefu alionao hana uzoefu wa kujua jinsi anavyoweza kujisaidia kutunza mazingira

yake. Nataka nimwambie tu kwamba utaratibu mzuri tu ambao sisi wengine tunao hapa ndani, hatuna tabia ya kuchafua mazingira tunayokaa, kwa hiyo, hii ni *dustbin* ndogo ya kuhifadha takataka. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu anataka kusikiliza ni nini ninachokieleza, namuomba atulie, kama atataka kuthibitishiwa, unaweza tu baadaye ukamchukua akaja kuthibitisha, lakini ni *dustbin* ndogo tu kwa ajili ya kutunza mazingira ya hapa ndani kwa utaratibu tu mzuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ahsante. Jamani tuko salama, hakuna shida.

Mheshimiwa Godbless Lema, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nikupe pole sana wewe kwamba usiku wa jana tena huko Kiteto wameuawa wakulima wawili na pia pikipiki 11, trekta moja na maduka yamechomwa moto. Hii ni kazi ya Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Martha Umbulla, ana tabia kama ya Ole-Medeye kwa sababu hivi karibuni alifanya mkutano wa wananchi ambapo ukiona Mkuu wa Wilaya amefika mahali anasema wale wageni wakae kushoto na wenyeji wakae kulia, hiyo ni hatari sana kwa nchi. Kwa hiyo, tabia hizi ni kama zilezile za Ole-Medeye. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu hili jambo uliangalie kwa makini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee suala moja tu la machinga. Mheshimiwa Zungu aliongea vizuri sana lakini muda wa dakika saba haukuwa umetosha. Kama menejimenti ya Machinga ikikosekana katika taifa hili, nchi hii inakwenda kuwaka moto. Hivi karibuni katika Jimbo langu kumekuwa na matatizo makubwa sana kati ya Machinga na Mgambo. Ni vyema Serikali ikaelewa kwamba tatizo la Machinga haliwezi kuwa na *quick fix* kwa sasa kwa sababu ni tatizo la kimfumo, tatizo ambalo limesababishwa na kukosekana kwa viwanda, *ranch* na mambo mbalimbali ambayo leo imefanya Watanzania wengi wamekuwa wachuuzi wa biasara barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa tatizo hili, pia ni msingi wa Serikali yenyewe. Serikali ya Tanzania ni Machinga, Serikali ya Tanzania ni ombaomba. Kama asilimia 40 ya bajeti ya nchi hii inategemea wahisani kutoka nje, kama kila kitu tunachotumia madukani asilimia 85 mpaka 90 kinatoka nje, maana yake Serikali yenyewe ni Machinga.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu Arusha limenzishwa kundi lingine la usiku, wale Machinga wanaopata usumbufu mchana, wameamua kuji-organize usiku, wameazisha kundi linaitwa 'kanyaga twende' na hivi karibuni, ni kundi la vijana wengi wanaingia mahali usiku wakiwa 20, 30, wanavunja nyumba, wakikuta chakula wanakula kwanza, wanabaka watu, wanachukua mpaka pete za ndoa! Haya ndiyo matatizo yanayosababishwa na Machinga kusumbuliwa. Ni kweli tunahitaji miji misafi na ni ajenda ya kila mtu mwenye akili timamu lakini ni hatari sana tukiweza kufanikiwa kuondoa Machinga, tukatengeneza Machinga usiku, sina uhakika ni nani kati yetu atakuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naishauri Serikali, pamoja na hitaji la msingi la kuwa na miji bora na miji misafi lakini tatizo la Machinga lisichukuliwe kwa haraka sana, wasiondolewe kwa haraka sana. Amesema hapa Mheshimiwa Zungu kwamba mitaji yao ni midogo, wengine wana mikopo, unatoa mpaka watu wanaofanya biashara ya cherehani barazani? Hawa wakikosa kitu cha kufanya wakasikia njaa na tusiwaone barabarani watakuwa wanafanya kazi usiku. Mfano uliosema ulitokea Arusha, kati ya Alhamisi, Ijumaa Kuu, Jumamosi na Pasaka zaidi ya nyumba 15 – 20 zilikuwa zinavamiwa katika kata moja, kwa sababu jamii hii sasa ambayo iko *desperate*, ambayo haiwezi kufanya kazi inakwenda sasa kufanya shughuli nyingine nyakati za usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *issue* nyingine hapa ya msingi kuhusu Machinga inasababishwa pia na miji yetu. Unaangalia kama *Osterbay* sasa, *Osterbay* zamani ilikuwa ni *residential*, leo unakwenda *Osterbay Dar es Salaam* ama leo unakwenda Uzunguni Arusha ama popote, kila mahali kumekuwa ni Bar, kumekuwa ni maofisi, miji imekosa *organization*, unashindwa kujua Dar es Salaam wapi ni makazi ya watu na wapi ni sehemu ya biashara. Kumekuwa hakuna *proper management* ya miji yetu, *squatter* zinazidi kuongezeka. Mimi nikiwa mdogo au miaka 10-15 nyuma *Osterbay* ilikuwa unakutana na watu wanafanya *jogging* barabarani, sasa hivi *Osterbay* imekuwa kama soko. Hata viongozi wote wenye nyumba *Osterbay* wamegeuza nyumba zao kuwa *bar*, kila mahali kumekuwa na *bar*, miji yetu imekosa *organization*, msikiti nyuma kuna *bar*, ukienda Kanisa nyuma kuna *club*, nchi yenyewe imekuwa na Machinga, nchi yenyewe imekuwa *disorganized*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakwenda hospitalini watu wanalala wawili wawili lakini *emphasis* kubwa imekuwa ni kuondoa wafanyabiashara wadogo barabarani. Sio jambo muhimu wafanyabiashara kubakia barabarani lakini ni muhimu zaidi kwamba matendo haya ya kuwaondoa watu barabarani yanapofanyika kwa ajili ya kupisha usafi wa miji iangalie ubinadamu zaidi kuliko kuangalia usafi wa miji peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilikuwa nataka niongelee habari aliyoongea jana Mheshimiwa Profesa Muhongo. Kwa bahati mbaya sana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Profesa Muhongo jana wakati anatoa takwimu zake za *investment* kwenye gesi, nilikuwa namwonea huruma na pengine nijiridhishe tu kwamba hajawahi kufanya hata biashara ya mapera. *Investment* haihitaji fedha, *investment* inahitaji *plan*. Kuwa na Waziri ama Serikali inayofikiri kwamba hakuna Watanzania wanaoweza wakafanya *investment* ya dola milioni mbili ni kuwa na Serikali yenye viongozi ambao ni *negative thinkers*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, alichokuwa anaongea Profesa Muhongo jana hapa, biashara hiyo inaweza ikafanywa na Watanzania. Wazungu wote wanaokuja nchi hii huwa hawaji na fedha, huwa wanakuja na *laptop* na pesa ya kulala *Movenpic*, wanaandaa *draft*, wanaandaa *plan* na fedha wanachukulia ndani ya benki zetu wanafanya biashara katika nchi yetu, hivyo ndivyo wanavyofanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna biashara inayozidi dola milioni mia moja kwenda mbili ikawa na *partnership* ya watu wawili ama mmoja peke yake, biashara yoyote kubwa inakuwa na *partnership* ya watu wengi. Yeye leo analalamika anasema kwamba Watanzania wanaotaka kufanya biashara ya gesi wanataka kuwa mawakala. Wazungu wanaokuja kufanya biashara ya gesi nao pia ni mawakala wa benki zao kule kwao. Kwa hiyo, kama hutaki Mtanzania kuwa wakala kwa sababu ya faida ya nchi yake, kwa nini unataka Mzungu na Mchina kuwa wakala? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie hili. Kafulila ametoa shutuma kali sana na mimi ningepomba Bunge lako Tukufu na kwa sababu kuna maneno Gavana alisema mwenyewe kwamba ubadhirifu wa karibu shilingi bilioni mia mbili kulikuwa na *pressure* na shinikizo kubwa. Mimi niamini kwamba aliyemteua Gavana ni Rais na kama Gavana anakiri kwamba kulikuwa na shinikizo kubwa la ubadhirifu wa zaidi ya shilingi bilioni mia mbili maana yake ni kwamba Rais anaifahamu *deal* hii vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitake Bunge hili limtake Kafulila sasa kuthibitisha maneno yake aliyoyasema hapa Bungeni ya ubadhirifu wa zaidi ya shilingi bilioni mia mbili ambao unamhusisha Waziri wa Nishati na Madini, unamhusisha Katibu, Gavana pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa sababu hili si jambo dogo, ni wizi wa fedha nyingi sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema nakushukuru sana. Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kasembe.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba Bunge lako Tukufu lichukue hatua ya kuhakikisha kwamba hapa katika eneo la Bunge tunakuwa na Daktari aliyekubuhu katika magonjwa ya akili ili kuhakikisha kwamba wale ambao wanadhaniwa kwamba wamechanganyikiwa kidogo waweze kupimwa na ikithibitika hivyo wazuiwe kuingia Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Godbless Lema, mtoto aliyekulia kwenye *gheto* kwa sababu ya kutelekezwa na wazazi wake, alipata huruma pale Arusha akapata Ubunge. Kama Waarusha wangukuwa wabaguzi ungepataje huo Ubunge wewe? Kila siku akisimama hapa, Ole-Medeye ni mbaguzi, ubaguzi wangu ni upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu hii ni mara ya pili Godbless Lema akisimama katika Bunge hili na kutaja jina langu akisema kwamba mimi ni mbaguzi. Kwanza, alisema kwamba angewasilisha vielelezo. Kama vielelezo vimewasilishwa, naomba Bunge lako lifanyie kazi vielelezo hivyo na uamuzi juu ya suala hili utolewe, hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nampa taarifa Godbless Lema, mwaka 2015 nitagombea Ubunge Jimbo la Arusha ambako ndiko nilikozaliwa. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Kwa sasa naomba tuendelee, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kasembe.

MHE. BALOZI KHAMIS J. S. KAGASHEKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuzungumza katika *item* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitajikita katika suala la Manispaa ya Bukoba. Nadhani hata Mheshimiwa Waziri Mkuu akisikia kwamba nataka kuzungumzia suala la Manispaa ya Bukoba ataelewa kwa nini ninafanya hivyo na katika suala la bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Manispaa ya Bukoba Mjini kwa kweli wana Bukoba ambao wamenituma wamesema ukipata nafasi jambo hili ulizungumzie, wamekuwa katika msiba wa muda mrefu sana, wamekuwa wapweke, wamekuwa ni watoto ambao wametupwa, watoto ambao ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haikuwajali sana. Mgogoro wa Manispaa ya Bukoba umekuwepo tangu mwezi Aprili, 2012. Hivi ninavyozungumza hapa Bungeni, ni mwezi wa Mei, 2014, kwa maana ya kusema kwamba ni zaidi ya miaka miwili mgogoro umekuwepo bila kuwa na suluhisho ama tuseme bila kuwa na uwezo wa kulitatu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu ambao unahusu Manispaa, wala haumhusu Mbunge wala hauhusu chochote umekwenda mpaka hata Chama cha Mapinduzi kiliingia katika mgogoro huu na niseme kwamba kwa kweli natoa shukrani za kipekee kwa niaba ya wana Bukoba Manispaa kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa sababu nasema isingekuwa yeye na isingekuwa Katibu Mkuu wa Chama na Mwenezi wa Chama labda tusingefika hapa tulipofika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba ofisi ya Waziri Mkuu katika suala hili kwa kweli hawakututendea haki hata kidogo. Kwa maana ya kusema kwamba Chama kimeingilia, Chama kimeagiza Ofisi ya Waziri Mkuu kuona kwamba tunapata suluhisho katika suala hili, maendeleo yanakuwepo kwa watu wa Bukoba. Niseme kwamba, baada ya kuamua tukapata *Controller and Auditor General* ambaye alikuja akafanya kazi yake nzuri sana na ripoti yake ilitolewa mwezi Januari mwaka huu. Ripoti hiyo ilikuwa na maagizo na katika utekelezaji wa ripoti hiyo Meya ambaye tulikuwa naye alitamka mbele ya Naibu Waziri ambaye alikuwa anamwakilisha Waziri Mkuu na mbele ya *Controller and Auditor General*, mbele ya Mkuu wa Mkoa na wengine waliokuwepo kwamba amejuzulu na ndivyo ilivyokuwa inaeleweka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya muda akasema hakujiuzulu, amerudi, lakini si hivyo tu, akaweka *Press Conference*, akamtukana *Controller and Auditor General*, akaitukana Serikali na mpaka hivi sasa ninavyozungumza, hiyo ndiyo niseme kwamba inasikitisha juu ya Serikali yetu, juu ya kusimamia mambo, juu ya utekelezaji wa mambo. Mpaka hivi ninavyozungumza katika Bunge lako hakuna kilichofanyika, hakuna! Hata Serikali kusema kwamba wewe ulikwishajiuzulu si Meya pale halijafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 mwezi huu, ipo barua ambayo RAS wa Kagera amemwandikia Katibu Mkuu wa TAMISEMI na katika hiyo kinachosikitisha anasema kwamba, naomba ninukuu barua yake ambayo ni barua namba CAB58/227/01B/7 ya tarehe 30 Aprili, 2014, tunazungumzia siku nane, siku tisa. Katika barua hiyo, nanukuu, anasema uelewa wa ofisi hii ni barua ya Mkuu wa Mkoa kwamba Anatoly Amani ambaye aliandika akisema kwamba ni Meya amejuzulu kutoka katika nafasi yake. Hata hivyo, RAS ambaye ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pale anamwandikia Waziri Mkuu na tunazungumzia Mei, anasema nawasilisha kwako taarifa hii yanayoendelea sasa kuhusu nafasi ya Umeya ili kama kuna maelekezo yoyote ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa yaweze kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika mimi nasema hii kwa kweli ni aibu, kwa sababu jambo hili limefanyiwa kazi, kumekuwepo na Tume, maamuzi yamefanyika, utekelezaji umekuwa taabu. Nasema kwamba leo au wakati tutakapokuwa tunahitimisha bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nitapenda kabisa kabisa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa niaba ya Manispaa ya Bukoba tupate maelezo kama RAS huyu alivyomwandikia Katibu Mkuu wa TAMISEMI. Tunataka tupate maelezo Serikali bado inamtambua huyu ni Meya ama haimtambui kama ni Meya, kwa sababu hatuwezi kuwa katika mgongano ambao hauna manufaa, hakuna maendeleo. Bajeti ambayo inahusu Manispaa ya Bukoba haikuwepo, imekuja imepachikwa katika bajeti ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na kwa miaka miwili kumekuwa hakuna vikao ambavyo vimekuwa vinafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwamba kwa kweli kupitia kwako, Waziri Mkuu atakuwa ananisikiliza ingawaje yuko hapa anaongea, ninayoyazungumza si maneno yangu, ni maneno ambayo ninawakilisha watu wa Manispaa ya Bukoba na niseme kwamba tutaomba tupate majibu. Kwa sababu kwa kweli ni mambo ambayo yana-*frustrate*, ni mambo ambayo yanachosha na hatuwezi kuendelea na suala ambalo ni dogo sana katika taifa letu, suala ambalo linahusu Ofisi ya Meya *for the last two years*. Mimi niseme kwamba *Mr. Prime Minister, this is a shame and I think* ni kitu ambacho kingeweza kufanyiwa kazi, ni kitu ambacho kingeweza kufanyiwa maamuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kabisa kabisa kwamba zile *recommendations* ambazo CAG alizitoa tarehe 17 alipokuja pale Bukoba na ambazo mpaka leo ni mwezi wa tano hakuna ambacho kimetetelezwa, *and yet* mnataka kutuambia kwamba watu wa Bukoba wafurahie, waone kwamba watu wanawajali haiwezekani Mheshimiwa! Hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Kikwete mwenyewe, Rais wa nchi hii amekuwa analizungumzia, maamuzi yakifanywa yatekelezwe na hasa yale ambayo yanahusu watu wengi. Leo watu wa Bukoba nakuambia huwezi ukawaambia kwamba Serikali inawajali wakati miaka miwili imepita hakuna kinachofanyika katika Manispaa, vikao havifanyiki katika Manispaa, maelezo hayatoki katika Manispaa, haiwezekani! TAMISEMI hakuna barua inayokuja. Mimi ninasema kwamba mimi mwenyewe nilikuwa Waziri ndani ya Serikali. Kama haya yanaweza yakanikuta, sasa Mbunge wa kawaida itakuwa namna gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe, kwa kweli hili ni jambo ambalo tunalichukua *very very seriously*. Wale ambao wanaelewa suala hili limekuwa katika Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi kwa muda mrefu na limekuwa linatekelezwa kutokana na msukumo ambao unatokana na Chama cha Mapinduzi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi.

MHE. BALOZI KHAMIS J. S. KAGASHEKI: Kwa hiyo, naomba tupate majibu kabla hatujakubaliana na bajeti hii. (Makofi)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kuhusu watu wanaokaa wanamsemesha Waziri Mkuu wakati mambo mazito yanazungumziwa. Hili nalisema kwa sababu niko kwenye Kamati ya TAMISEMI. Ni kweli bajeti ya Bukoba ilikuja haikujadiliwa kwenye Baraza la Madiwani kwa sababu ya tatizo kubwa walilo nalo, ikaletwa tu kinyemela pale ikajadiliwa juu juu ikapitishwa. Leo Mbunge wa Jimbo hilo anaongea Waziri Mkuu anapiga *story* na watu wengine. Ilemela pia pale tatizo hilo ni kubwa mpaka leo halipatiwi ufumbuzi lakini Waziri Mkuu anaendelea tu kuongea pale. Naomba mwongozo wako kama inaruhusiwa Waziri Mkuu kuendelea kupiga *story* wakati kuna mambo mazito yanazungumziwa. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapigi *story*, ila niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao mnakwenda pale wakati huu wa *session* mumphe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu ili apate nafasi ya kuweza kusikiliza vizuri. Nililiona na nitakachofanya baadaye basi ni kuwaondoa wale watakaokuwa wamefanya hivyo. Kama una jambo ambalo ni *very pressing* basi iwe chini ya dakika moja. Ahsante sana.

T A A R I F A

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa anapewa nani sasa hiyo?

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Hapa Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Haya Mheshimiwa.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kutoa taarifa kwa Mjumbe ambaye alizungumza kabla ya Mjumbe aliyemaliza, Godbless Lema, aliponitaja kwamba Martha Umbulla anafanana na Ole-Medeye kwa kuwatenga wananchi wakati anafanya mikutano.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Godbless Lema kwamba kikao nilichokuwa nahutubia kilikuwa Halmashauri Kuu ya Kijiji cha Kimana ambapo kwenye Halmashauri Kuu ya Kijiji unazungumza na wananchi wa mahali pale peke yao. Kwenye kikao hicho walikuja wananchi wengi kutoka Wilaya ya Kongwa ambalo ni Jimbo lako Mheshimiwa Naibu Spika ambao kusema kweli wamezoea kutuvuruga kila kikao tunachofanya ili tusifanikiwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Godbless Lema aelewe kikao kile ni Halmashauri ya Kijiji cha Kimana, hakikutaka kumjumuisha mwanachi kutoka Wilaya nyingine na kwa hivyo naomba aelewe hivyo na asiendeleo kuvuruga masuala ambayo hayamhusu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana kwa taarifa, nimeivumilia lakini si kwa mujibu wa Kanuni. Kwa kawaida taarifa anapewa mtu palepale anapokuwa bado anaongea na si baada ya kuongea.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla ni kwamba kutokana na mahusiano haya yasiyoeleweka kwenye kijiji hicho anachokisema Mheshimiwa DC, usiku wa kuamkia leo wameuawa watu wawili wa Kongwa haohao.

Nimemwona Mheshimiwa Lukuvi amesimama, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, sikutaka kukatisha hilo unalolisema, ulinipa taarifa usiku, nikamwambia IGP na Serikali imeanza kuchukua hatu. Nilikuwa nataka kuongeza katika hilo ulilotaka kusema.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nilichotaka kuomba, kutokana na mwongozo uliotolewa wa kuzuia kuja hapa imeshasemwa sana. Nataka niombe hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu humu ndani ni Mbunge lakini nafasi yake ni kiongozi wa shughuli za Serikali humu ndani na humu ndani shughuli za Serikali zinaendelea. Sawasawa? Humu ndani kuna pande mbili, kuna Serikali na wengine ambao hawako Serikalini. Kuna *consultation* za muhimu sana lazima ziendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kiongozi wa shughuli za Serikali, maana humu ndani Katiba imemtaja anaingia na kukaa kiti kile kama kiongozi wa shughuli za Serikali humu ndani, si nje. Yaani kiongozi wa shughuli za Serikali kwenye jengo hili si kule nje. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, nakubaliana na ushauri wenu kwamba wale ambao wana maoni ya kawaida ya kiofisi yanayoweza kusubiri waende kule juu, lakini wale wenye maoni ya papo kwa

papo yanayomhusu Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu ndani, vinginevyo uongozi wake wa shughuli za Serikali humu ndani ataufanyia wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuelewane, mimi hapa sasa hivi nikitoka hapa nakwenda kukaa pale, kwa sababu alinituma nje lazima nikampe majibu. Sasa hivi, yaani nikimaliza hapa nakwenda kukaa pale, lazima nimpe majibu ya uendeshaji bora wa shughuli za Serikali humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba tu nieleweke hivyo. Wale waotumia muda vibaya ...

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Waziri wa Nchi, ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kasembe, wajiandae Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Ezekia Wenje.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

T A A R I F A

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa?

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Yes!

NAIBU SPIKA: Jamani tutumie vizuri Kanuni. Taarifa inatolewa wakati mtu anaongea.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama.

NAIBU SPIKA: Basi sikukuona bahati mbaya. Mheshimiwa Kasembe endelea.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu inayohusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kuwapa pole wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi ambao wamekwama kwa zaidi ya siku mbili, wamepata shida sana, kunyeshewa mvua na uhaba wa chakula. Hiyo yote ni kutokana na kutokamilika barabara yetu ya Kibiti - Lindi, ninawapa pole sana. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaambie wananchi wa Mtwara pamoja na Lindi kwamba sisi viongozi wao ambao wametuweka madarakani suala hili tunalisimamia na tunaendelea kuiomba Serikali waweze kukamilisha mapema mahali palipobakia ili adhabu hii tuliyoipata toka enzi za ukoloni iweze kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili suala la barabara, Mheshimiwa Waziri mhusika amelitolea ufafanuzi. Naomba niseme kwamba ufafanuzi aliutoa kazi iliyofanyika juzi na jana ni kwa ajili ya kusaidia tu kwa muda. Tunachoomba sisi watu wa Mtwara na Lindi, kipande kilichobakia kiweze kukamilika kwa sababu barabara hii sasa hivi imeshakuwa ni kero. Kila Mbunge wa Kusini anayesimama tunazungumzia barabara. Sasa hivi barabara toka ianze kujengwa ina zaidi ya miaka sita. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba leo Serikali watuambie, kipande kilichobakia ambacho hakijakamilika tatizo ni nini? Tatizo ni Serikali au mkandarasi? Kwa sababu mkandarasi, yuko *site* lakini kazi inayofanyika hakuna, kazi yake yeye ni kutengeneza *diversion* kila siku na siyo hii barabara ambayo sisi matarajio yetu ni kwamba itakamilika na kutuondolea adha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nichukue nafasi hii nizungumzie suala la ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ambayo inajengwa Mkoani Mtwara. Jana Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba ameuliza swali na akapatiwa majibu lakini katika swali lake alielezea masikitiko yake kwamba Hospitali hii ya Rufaa ni agizo lililokuwa limetolewa toka enzi la Baba wa Taifa, katika utawala wake Awamu ya Kwanza, waliagiza Hospitali ya Rufaa ijengwe katika Mikoa ya Kusini. Leo hii tuko Awamu ya Nne, Hospitali haijaanza kujengwa, taratibu zilizoanza ni za awali. Nataka kujua, Serikali ina mpango gani wa haraka kuharakisha kujenga hiyo Hospitali ya Rufaa na hasa ukizingatia kwamba Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa hivi sasa, hali ya uchumi inakua, ongezeko la watu ni kubwa sana, mahitaji ambayo tunahitaji sisi kupata huduma katika hospitali hii baada ya miaka miwili yatakuwa ni makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali ituangalie sisi watu wa Kusini, isiwe kila mradi unaoanzishwa Kusini unachelewa miaka nenda rudi. Ninataka kujua wakati wa majumuisho, toka enzi za Awamu ya Kwanza hadi sasa ni Hospitali ngapi za Rufaa hapa katikati zimejengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie Mfuko wa Maafa. Suala la Mfuko wa Maafa ni suala muhimu sana. Ninazungumza hili kwa sababu hali ya maafa sasa hivi katika nchi yetu yamekuwa ni matukio ya kila wakati. Ukienda kuangalia katika Mfuko wa Maafa unaambiwa fedha za kutosha hakuna. Mimi mwenyewe ni muathirika mmojawapo niliyepata maafa lakini inasikitisha sana, watu mnapata maafa, zaidi ya mwaka na miezi, hakuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hatua yoyote inayochukuliwa hata ya dharura. Hii inasikitisha! Kwa sisi tunaotoka Mikoa ya Mtwara na Lindi kitu hiki tumeendelea kusikitika na hatuielewi Serikali kwa nini inakaa kimya hadi leo. Ni kweli imeshindwa kutafuta hela ikafidia watu waliopata maafa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni la kusikitisha, maafa hayakutokea kwa watu binafsi tu, Halmashauri zetu zimeathirika kiasi kikubwa sana. Leo hii katika Halmashauri zetu hasa Halmashauri ya Mji wa Masasi, watendaji wanafanya kazi katika mazingira magumu, hakuna usafiri. Watendaji inabidi wakodi bajaj kwenda vijiji ili kutekeleza shughuli za Serikali. Mimi ninaomba, pamoja na bajeti ambayo imepangwa kwa mwaka huu lakini Serikali ingetafuta njia mbadala, njia ya haraka kuweza kutusaidia angalau ofisi za Serikali zikajengwa, wakapatiwa usafiri, tukapewa vitendea kazi ili kazi za Serikali ambazo zinagusa wananchi moja kwa moja ziweze kufanyika kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ambalo kila mwaka ninasimama kuzungumza wakati wa bajeti, ni majengo yaliyokuwa Chuo cha Wasioona ambayo yako katika Wilaya ya Masasi. Inasikitisha, ukifika katika kile Chuo, utaona ni namna gani Serikali yetu hatujali na hatuwezi kuzilinda rasilimali ambazo tunazo. Majengo yale sasa hivi ni miaka mingi, Chuo kiliishakufa, majengo yanakaa, Halmashauri wanaomba yale majengo wakabidhiwe, Serikali inakataa. Leo mimi ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Wizara ya Afya imekuwa ikitenga kila mwaka fedha na fedha ambazo zimekuwa haziendi kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo na wala Chuo hakifufuliwi tena, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ufanye maamuzi magumu ili uweze kubadilisha matumizi ya majengo yale na uweze kukabidhi kwa Halmashauri ya Mji wa Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie suala la umeme. Sisi wananchi wa Mtwara tunasema sasa hivi tunao umeme wa gesi lakini umeme huo wa gesi kwa Masasi ni adhabu kubwa. Imefika wakati tunapata mgawo wa umeme wakati gesi iko Mtwara. Wananchi wanapata umeme siku mbili au mara tatu kwa wiki, siku nyingine zote ni giza, wafanyabishara wanashindwa kufanya biashara zao, watu majumbani vitu vyao vinaharibika, hatupati umeme unaotakiwa. Ninamuomba Waziri anayehusika, kama ni tatizo la fedha, kama ni tatizo la vitendea kazi, wangepanya jitihada wakafanya kazi ya ziada ili kuweza kumaliza service wanazozifanya hivi sasa ili tuweze kupata umeme wa uhakika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalizungumzia hili kwa sababu sasa hivi watu wa REA wako mbioni wanapeleka umeme vijijini. Sasa haitakuwa na maana yoyote, umeme unaenda vijijini lakini umeme wenyewe siyo wa uhakika. Ninaiomba sana Serikali iangalie jambo hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Slika, baada ya kuyasema hayo, nasema ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Ninakushukuru sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, si ulinitaja mimi?

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika mjadala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuunga mkono hoja. Napenda pia kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo inafanya kazi yake ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania, wapenda maendeleo wanapata maendeleo yao.

Naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia na naanza na sekta ya madini. Katika eneo hili, napenda kuongelea kuhusu wachimbaji wadogo wadogo hasa wale wanaopatikana katika Mkoa wa Katavi, eneo linaloitwa Magamba, Ibindi na maeneo ya Kapalamsenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini, ninafikiri sasa inaweza ikawa imepitwa na wakati hasa kuhusiana na leseni zinazotolewa. Nilikuwa naomba, kwa sababu lengo letu ni kuwawezesha hawa wachimbaji wadogo wadogo, kuwapatia mitaji, kuwakopesha vifaa vya kuchimbia na kadhalii, hii sheria ingebidi iangaliwe upya kwa sababu haimlindi sana mchimbaji mdogo mdogo. Kwa nini ninasema hivyo? Inafika mahali leseni yake inapokwisha, kwa mfano, sasa hivi imeongezwa kiwango kutoka Sh.200,000/= mpaka Sh.800,000/, kwa mkulima wa kawaida mimi ninayemfahamu ambaye anasubiri labda achimbe, akachekeche mtoni aone atapata kale kadhababu kiasi gani, kagramu ngapi, ili aweze kwenda kukauza ndiyo aweze kupata hiyo hela alipie na kodi, alipie na lile eneo halafu hapo hapo sheria inamtaka alipe Sh.800,000/= kwa mkupuo, kwa kweli huku ni kumnyanyasa mchimbaji mdogo mdogo. Kwa hiyo, nilikuwa ninapendekeza, kama Sheria hiyo inaweza ikaletwa hapa, ikafanyiwa marekebisho ili tuone tunamsaidiaje yule mchimbaji mdogomdogo, aweze kulipia ile leseni yake kwa awamu. Kwa sababu pale unapoenda kuchimba na kwa sababu hana vifaa vya kisasa, haimaanishi kwamba wakati huohuo atapata ile dhahabu na kuweza kuiuza kwa wakati uleule na wakati huohuo akapata pesa hiyo ya kulipia. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba katika majumuisho niweze kupatiwa majibu mazuri kwa sababu wachimbaji kule wameshachanga hela wanakuja huku kuonana na Waziri Mkuu. Kwa hiyo, naomba kabla hawajachanga tupate majibu mazuri.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba niongelee suala la barabara ambalo kila siku tumekuwa tukilipigia kelele, barabara ya Tabora - Koga – Inyonga – Mpanda ambayo na Mheshimiwa Magufuli aliwaahidi wananchi wa Katavi kwamba angelienda akaitembelea, lakini hajafika. Kwa kweli na mimi sijapendezwa na ahadi yake ambayo hajaitekeleza. Ninapenda Mheshimiwa Magufuli aweze kwenda na kukutana na wananchi wa Katavi, akawaleze kwa nini ile barabara ambayo kila siku tumekuwa tukiipigia kelele na ni toka tumepata uhuru haijawahi kuwekewa lami, wala hatujawahi kuona lami. Mheshimiwa Kakosa katoka kuelezea hayo, nisingependa kurudia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonyesha na imetoa kipaumbele katika sekta ya afya na katika kulinda afya ya mama na mtoto. Katika hili napenda niongelee Kituo cha Afya kilichopo Inyonga ambapo ndipo Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele. Kituo kile ni cha kisasa kabisa. Sielewi ni wapi panapokwama. Nimewahi kuongea na Mheshimiwa Mwanri, akaniambia bado wanataka kwenda kutathmini ama kukagua kitu kama hicho mimi sielewi. Wananchi pale wao wanachotaka ni huduma zifanywe pale. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninamshukuru sana. Jimbo lake lile analipenda sana, wananchi wa Katavi anawapenda sana, amepeleka pale vifaa vya kisasa vimekaa store, vinaharibika bure. Hospitali ile ni nzuri kuliko hata ile ya Wilaya ya Mpanda. Ninashangaa ni kigugumizi gani kilichopo huko kwenye Wizara zenu kwenda kutoa kibali ile Hospitali ikawa ya Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ili hilo jengo liendeleo kuwa zuri na litumike, ili vile vifaa vitumike. Tukimaliza hapa katika majumuisho muwape matumaini wananchi wa Wilaya ya Mlele kwamba ile hospitali sasa inakuwa ni Hospitali ya Wilaya, sioni tatizo, kama ni taratibu zimeshafanywa. Sasa huu Umangi Meza na Umwinyi wa kwenye maafisi yenu huko mbaki nao huko, sisi tunataka utekelezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninapenda niende kwenye suala la kodi maana kuna misamaha ya Kodi lakini mimi naomba niende moja kwa moja kwenye kodi ya VAT. Mimi nilikuwa ninauliza, je, kwani kila bidhaa ni lazima ikatwe kodi asilimia 17? Kama lengo ni kukusanya kodi, kwa nini hawa wanaowekeza mfano kwenye miradi ya gesi ambayo ni miradi mikubwa, tunajua itakuja kutupatia fedha nyingi kodi yao isiwe juu zaidi ili tukampunguzia *National Housing* anayejenga nyumba za wananchi wa kipato cha chini ili akampunguzia bei ya zile nyumba wananchi wale wakaja kuzinunua. Mimi sioni sababu kila bidhaa itozwe asilimia 17 ambayo sidhani kama ina tija ndani yake. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo pia waliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la ajira ambalo tumelisema, ni kwa nini zinacheleweshwa kupelekwa Halmashauri ambapo tumeshapitisha huku na kule wananchi wanalalamika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili la ucheleweshaji wa pesa za maendeleo. Pesa za maendeleo zinazochelewa kwenda, tunakuja tunajadili bajeti hii wakati bajeti ile iliyopita hakuna pesa iliyokwenda. Kwa mfano, tuna visima vya maji Halmashauri ya Nsimbo pesa haijaenda mpaka leo hii ninavyoongea. Tuna kisima Kata ya Kakese, pesa hazijakwenda toka mwaka juzi tunaongelea na maswali ninayo. Kata ya Misunkumilo pale mjini, pesa hazijakwenda toka mwaka juzi. Sasa tunakuwa kwa kweli wakati mwingine unapata hata uvivu kuendelea kuongelea jambo lile lile kila siku. Kwa hiyo, naiomba Serikali, ijaribu kuangalia labda tunakwama wapi na tupange nini ili tuendane na pesa tunayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni hili la kuhusu ruzuku ya pembejeo ya kilimo. Hili suala ni kero, kero. Hakuna mahali utakapokwenda mwananchi ama mkulima aache kulalamika kuhusu pembejeo za kilimo. Sasa mimi naomba nipendekeze, hebu hili jukumu tuachane nalo na hawa Ma-DC na wengineo na tulielekeze kwa Halmashauri, tuwape Wakurugenzi na Vijiji husika kwani vile vijiji husika ndio vinawajua wanaotakiwa kukopeshwa. Kama kuna Vyama vya Ushirika, ama kuna SACCOs, wale ndio wapewe kwa hiyo wakulima waje kulipa kupitia vijiji na Ofisi ya Mkurugenzi, tuone kama linaweza likatusaidia ama vipi. Kwa sababu kupitia utaratibu tunaoutumia imekuwa ni tatizo inaonekana hata baadhi ya viongozi wanahusika, pembejeo hazifiki kwa wakati. Kwa hiyo, kidogo kwa kweli badala ya kumuendeleza mkulima tunamrudisha nyumba. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekia Wenje atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Sbabiby.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba wakati Mheshimiwa Kafulila anachangia, hoja aliyotoa kuhusu kutafunwa kwa fedha zinazokimbilia Sh.200,000,000,000 katika Akaunti ya TANESCO BOT, ni *scandal* kubwa sana kwa taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *scandal* ni kubwa kuliko ile ya EPA, kwa sababu EPA ilikuwa inahusu kutafunwa kwa fedha takriban Sh.155,000,000,000 lakini hii inakimbilia Sh.200,000,000,000. Mheshimiwa Kafulila amesema anao ushahidi na ana uwezo wa kutoa ufafanuzi kuhusu suala hili kwamba Govenor wa BOT alisema kwamba alipata mashinikizo makubwa kutoka kwa vigogo ndani ya Serikali. Sh.200,000,000,000 inao uwezo wa kununua madawati kwenye

shule zote za *primary* na *secondary* katika Taifa hili ambapo wanafunzi wanakaa chini kwa miaka 50 ya uhuru. Tunaomba kwa kashfa hii, Bunge liunde Kamati ya Uchunguzi (*Probe Committee*), Mheshimiwa David Kafulila apewe fursa ya kueleza vizuri, atoe ufafanuzi ili hawa waliotajwa kama Mkurugenzi wa TANESCO, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Nishati na Waziri wa Fedha wapate kujieleza na ili hii *scandal* ijulikane, kwa sababu hii ni kubwa kuliko EPA.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, suala linalotokea Dar es Salaam leo na huko Arusha kuhusu Wamachinga, Wabunge wa Dar es Salaam wamesema, Mbunge wa Arusha naye amesema. Mwanza sasa ni tatizo kubwa. Viwanda vya samaki vilivyokuwa vinaajiri watu Mwanza samaki hakuna tena. Sisi Mwanza hatulimi, kwa hiyo, kitu wanachofanya wananchi ambao hawana fursa kubwa ya kiuchumi wanafanya biashara ndogondogo, ni Mama Ntilie, ni watu wanaouza mbogamboga, ni watu wanaouza nguo jioni pale Mwanza. Leo *stand* kuu ya Nyegezi waliyokuwa wakifanya biashara Wamachinga, wamevunjiwa, maeneo yao usiku, walioacha nguo mle ndani, walioacha biashara zao mle ndani baada ya kuchukua mkopo vyote vimevunjwa tena vinavunjwa usiku wa manane.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hapo tu, mpaka Mafundi Cherehani leo wanatakiwa waondolewe Mwanza. Mnataka hii miji ibaki kwa matajiri tu. Mnataka miji ibakie na akina nani? Kwa sababu hawa ni Watanzania ambao pia wana sehemu na wanastahili kukaa katika hii miji. Kwa miaka mitatu iliyopita, Mwanza tumeendelea kuwa Jiji la kwanza kwa usafi Tanzania pamoja na kwamba Wamachinga walikuwepo pale mjini. Tuliji-*organize* tukasema kwamba tunao uwezo wa kuwaacha na kuwatengea maeneo wafanye biashara lakini mji ukaendelea kuwa msafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii sijui ni Majiji yote wamekaa wamekubaliana sijui kwenye vikao gani hata sielewi kwa sababu matatizo yanayotokea Dar es Salalam, ndiyo hayohayo yanayotokea Arusha, ndiyo hayohayo yanayotokea Mwanza na Mbeya pia lakini hakuna Mtanzania anayependa aitwe Machinga. Hawa watu wanaitwa Machinga kwa sababu hii ni misamiati ambayo Serikali hii ime-*create* hawa watu wanaoitwa Wamachinga baada ya kuuwa viwanda. Zamani Mwanza kwa mfano tulikuwa na MWATEX ilikuwa inaajiri watu 4000 lakini leo MWATEX haipo tena. Kulikuwa na Tanaries ambayo ilikuwa inaajiri watu haipo tena. Kwa hiyo, hata hili kundi la Wamachinga ni kundi lililotengenezwa na mfumo mbovu wa uchumi uliotengenezwa na Serikali hii, ndiyo maana tuna watu wanaoitwa Wamachinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba kwa vile Serikali ipo hapa hakuna haja ya kunyanyasa watu, hakuna haja mpaka sijui Mbunge

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

aende, watu waandamane, kwa nini tufikie huko? Kwa nini watu wavunjiwe vibanda vyao usiku? Mtu ameweka kibanda, amechukua mkopo *PRIDE* au *VICOBA* ameanza biashara ya mitumba mnakwenda mnabomoa kibanda chake usiku mpaka na nguo wanachukua wanakwenda kuuza maeneo mengine, sasa hii siyo kusaidia watu kuondokana na umaskini lakini hii inarudisha watu kwenye umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hili suala la Bodaboda, suala Wamachinga, suala la Mama Ntilie *as long as kadri* tunavyotaka miji iwe misafi lakini bado tunaweza kufanya miji hii ikawa misafi na hawa watu wakaendelea ku-coexist. Leo Mwanza kwa mfano, idadi ya watu wanaopiga watu roba imepungua kwa kiasi kikubwa kwa sababu tulitengeneza fursa ya watu kufanya biashara ndani ya mji. Machinga anauzia mteja anayepita na mtaji wake ni mdogo ukimwambia atoke Mwanza Mjini aende auze Kiloleli atakwenda kuuza mbuzi? Kwa hiyo, tunaomba *as long as* tunataka miji iwe misafi lakini itekelezwe kibinadamu yaani iwe na mazingira ya kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la *wage bill*. Leo duniani kote Serikali nyingi wanajaribu kuangalia ni namna gani wanaweza kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali, posho na mishahara ya hovyohovyoy. Leo unafika Mwanza unakuta ameajiriwa Afisa Nyuki kwamba Waziri Mkuu anakuja Mwanza anatushawishi eti tufuge nyuki, sasa sisi tutafuga nyuki kwenye yale maghorofa? Waziri Mkuu anakuja Mwanza badala ya kutusaidia tufuge samaki anataka tufuge nyuki anatumia magari kama mia kwenda Buhongwa kwenda kuzindua mizinga kama 20 ya nyuki. Anatumia msafara wa magari mia kwenda kuzindua mizinga 10 hadi 20 ya nyuki Buhongwa. Sisi Mwanza tuletenei mikopo kwa Wamachinga, tusaidieni tufuge samaki siyo kufuga nyuki, nyuki hatutafuga Nyerere Road, hatutafuga nyuki Kenyatta Road. Sasa mnatuletea Afisa Nyuki Mwanza Mjini, ukienda Dar es Salaam tena utakuta kuna Afisa Nyuki, Arusha kuna Afisa Nyuki. Mnaajiri watu wengi mno ndiyo maana *expenditure* inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuja Mwanza unakuta kuna Afisa Mifugo, hivi pale Mwanza Mjini sisi Afisa Mifugo anatusaidia nini? Hatufugi *that is the truth!* *Base ya economy* ya Mwanza ni biashara, tuletenei watu waliosoma masuala ya *entrepreneurship* wasaidie Wamachinga wetu namna gani wanaweza wakafanya biashara ikakua badala ya kuuza barabarani siku moja wawe na maduka siyo kutuletea Afisa Mifugo, sisi Mwanza pale Mjini hatufugi. Wanatuletea Afisa Kilimo analipwa na Halmashauri, Afisa Kilimo anatusaidia nini pale Mwanza Mjini? *It is true*, Mwanza Mjini hatuhitaji Afisa Kilimo. Wameletwa pale wamerundikana na wengine wanalipwa humuhumu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kuna mwanafunzi mmoja alisoma Nyegezi ananipigia simu kwamba amepangiwa na Serikali kwenye Wilaya kwenda kuwa Afisa Uvuvi, Wilaya ambayo haina Ziwa wala Mto halafu mnampeleka mtu kwenda kuwa Afisa Uvuvi, anakwenda kufanya nini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Wenje, dakika saba ni chache, Mheshimiwa Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi nataka nizungumzie masuala ya Jimboni kwangu na hasa masuala ya maji. Nimeingia Bungeni kipindi cha pili toka mwaka 2005 mpaka leo na kila mwaka kwenye hotuba ya Wizara ya Maji hunikosi lazima nachangia lakini utekelezaji ni sifuri. Sasa leo nimeamua kungea na kiongozi wa Wizara zote ambaye ni Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka toka niingie Bungeni haijawahi kutokea hata Waziri mmoja aliyeteuliwa katika Serikali hii au Naibu wake katika Wizara ya Maji ambaye hajawahi kufika Gairo, wote wamefika Gairo. Kila mwaka mradi wa Gairo uko 80% mpaka 84% hauishi. Sasa mimi sielewi, hili tatizo liko wapi? Gairo leo imekuwa Wilaya, tunashukuru kwa kutupa Wilaya lakini maji hakuna ndoo ni Sh.1000. Mimi kama Mbunge nimejitahidi hata kwa pesa zangu binafsi kuchimba visima lakini Serikali hakuna lolote. Kila Waziri anayekuja pale ni hadithi na maneno mengi hakuna chochote kinachoendelea na mipango mingi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa Mheshimiwa Makalla kateuliwa ameshafika Gairo na Wataalam zaidi ya 20 au 30 lakini mipango hakuna. Ukimuuliza Waziri na Naibu Waziri kila mtu ana mipango yake. Sasa leo nataka niongee na wewe Waziri Mkuu bado wewe hujafika Gairo sasa zamu yako na wewe uje kuwaambia watu wa Gairo mradi wa maji uko wapi? Maana wote wameshafika bado wewe kiongozi wao uje pale. Mimi siungi mkono hoja ya Waziri yeyote ambayo utekelezaji wake hautekelezeki, haiwezekani! Naunga mkono nini sasa? Waziri Mkuu ndiye kiongozi wa Mawaziri, sasa kama hakuna maji Gairo nakaa hapa naunga mkono ya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo imefikia hatua hata wale wanaonyemeleanyemelea Ubunge Gairo, unajua kuna watu wengine hawaelewi, duniani hawapo akili zao na Mbinguni bado hawajafika, wapowapo tu kwenye Majimbo! Kwa hiyo, akidanganywa hivi naye anachukua hivyo. Sasa kuna watu wanajua kabisa kwamba Mbunge ndiye anayechukua zile fedha za mradi anakaa nazo mfukoni kwa hiyo yeye kala. Mimi ni mfanyabiashara, juzijuzi nimenunua mabasi mapya wamesema

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

umeona, kutumia fedha zetu za maji! Wanafikia hatua mpaka wanasema kwamba Mbunge labda yeye ndiye anapewa pesa halafu anakula zile fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko kiongozi mwingine wa chama tena Chama changu cha Mapinduzi anakaa kila msiba, anasema Mbunge kala Sh.500,000,000, Mbunge kala Sh.600,000,000. Sasa mimi hili kwa kweli haliwezekani halafu nakaa hapa naunga hoja mkono, naunga hoja gani mkono? Haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sizungumzii habari ya TAMISEMI kwani TAMISEMI najua kuko safi lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu kama wewe binafsi mimi sikuungi mkono kabisa, kuna kitu kingine ambacho nitakuja huko mbele. Kuna mradi wa vijiji vya Chakwale, Kibedya, Leshata, Idibo, Iyogwe bado mpaka leo kila tukija hapa toka mwaka 2005, tukija hapa ni hadithi tu, mara imeingilia huku imetokea huku, hakuna!

Mheshimiwa Naibu Spika, Gairo imekuwa Wilaya, nashukuru TAMISEMI kwa kunipa Wilaya na kunipa Walimu wa kutosha lakini kila siku tunazungumzia habari ya Kituo cha Afya cha Gairo kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya, limejengwa jengo la *operation* huu mwaka wa nne. Ukiangalia kutoka Morogoro mpaka Dar es Salaam kuna kilomita 200, kuna hospitali maalum kwa ajili ya kushughulikia majeruhi ya Tumbi Kibaha.

Kutoka Morogoro kuja hadi Dodoma kuna kilomita 262 ambapo katikati yao ni Gairo. Tumeomba siku zote pale, *accidents* nyingi zinatokea, pawe na huduma muhimu kama za Tumbi kwa ajili ya watu wanaopata *accidents*, *accidents* kila siku zinatokea kipande cha Gairo, Dumila na Kibaigwa lakini hakuna. Sasa mpaka aje kiongozi aje afyatuke kiuno pale ndiyo mje muone kama pana umuhimu pale Gairo kuwa na hospitali ya haraka? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna hata *ambulance* kila siku ya Mungu, sasa gari la Mbunge ndiyo limekuwa *ambulance* mara ipeleke watu Dodoma mara ipeleke sijui wapi, jamani tunachoka! Haiwezekani kitu kama hicho, tunaomba tupate *ambulance* na jengo la *operation* lianze kazi.

Mheshimiwa Lema pamoja na Naibu Spika walizungumzia habari ya Kiteto. Ile Gairo jinsi ilivyo, ukishaanza kuingia Gairo mkono wa kushoto ni kilomita tisa tu unaingia Wilaya ya Kiteto. Kata nzima ya Dongo watu wanayolima katika Wilaya ya Kiteto ni watu wa Gairo. Nilizungumza mimi katika *Radio Free* kwamba Serikali msipoangalia watu watauana na kweli watu waliuana kutokana na ubaguzi katika Mbuga ya Murutangosi. Mnasema ile ni hifadhi mnawafukuza wakulima mnawaacha wafugaji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifika pale lakini ulikwenda moja kwa moja kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, walewale waliosababisha majanga yale hawawezi kukupa vitu vya muhimu au sababu ya kwa nini watu walikufa pale. Walichokuambia basi, ukaenda kwa wananchi ukawapa pole ukaondoka, hukutaka kusikiliza, suala liko Mahakamani, suala lipo Mahakamani watu wanazidi kufa. Leo hii alichozungumza Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Naibu Spika ni kweli, wamekufa watu wawili jana usiku, trekta moja limechomwa moto, pikipiki kumi na moja zimechomwa moto na maduka vilevile. Watu wa Gairo, Kilindi, Kongwa wote wanalima pale kwa sababu ni maeneo ambayo yanapakana, lakini hakuna hicho, kisingizio ni kwamba wakulima wakubwa, wanachoma dizeli msitu, kwa nini msiwafukuze hao wakulima wakubwa mkawaacha wakulima wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi jamani siyo mfanyabiashara tu bali ni mkulima mkubwa na ni mfugaji mkubwa. Nina shamba eneo la Kiteto, shamba langu safari hii ilibidi nisilime niwaachie wananchi wadogowadogo tu walime. Sasa tumekaa tu tunasingizia Mahakama, tunasingizia hiki, twendeni tukagawe yale maeneo lakini kila siku hii ni hifadhi, hii ni hifadhi, hifadhi zenyewe zipi? Hizo hifadhi tulizonazo majangili wanaingia kila siku mnashindwa kuzilinda bado tena tunaanzisha hifadhi nyingine. Gaweni kwa wakulima wajue eneo lao ni lipi na wafugaji wajue eneo lao ni lipi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana!

MHE. AHMED M. SHABIBY: Ahsante sana lakini nilikuwa bado kidogo!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana! Dakika nilizonazo Mheshimiwa *Innocent* jaribu kuzitumia kama utaweza, tumia kama dakika tano tu hivi!

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi vilevile kwa kunipa nafasi. Nami nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri japo ndugu yangu hapa anasema yeye haungi mkono hoja lakini mimi nasema naunga mkono hoja kwa sababu ili tuweze kukamilisha haya ni lazima tuunge mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusiwe sehemu ya kulalamika bali tuwe sehemu ya kutafuta suluhisho na majibu katika kuisaidia Serikali. Katika hili niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tusijitoe kwani sisi ni sehemu ya Wizara ya TAMISEMI katika Halmashauri zetu. Tuna wajibu wa kusimamia vyanzo vya mapato, tuna wajibu wa kusimamia watendaji na kuhakikisha kwamba fedha zinazopelekwa kupitia bajeti ambazo tutapitisha zinafanya yale ambayo Serikali inataka kufanya. Naomba katika hili tumsaidie Waziri Mkuu katika kutunga Katiba ili tumpatie meno sasa awe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

msimamizi mkuu na mwajibishaji wa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende katika ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini Mvuha. Mheshimiwa Waziri Mkuu toka mwaka 2009/2010, Halmashauri ya Morogoro Vijijini ilitakiwa kujenga Makao Makuu yake Mvuha, tumepata Sh.500,000,000 tu. Kila mwaka katika bajeti nimekuwa nikizungumza, mmetuambia tuombe maombi maalum lakini hakuna chochote. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba wakati una-*wind up* mtuambie nini hatma ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini katika Kata ya Mvuha. Tumeshuhudia kila siku ufunguzi wa Wilaya mpya, ufunguzi wa Mikoa mipya lakini sisi Morogoro Vijijini hatuna chochote kinachoendelea, nataka majibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndugu yangu Shabiby amekuja jukumu la maji na mimi nakupa jukumu ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwenye Halmshauri ya Morogoro Vijijini ni kero. Hivi ninavyokwambia wananchi mafuriko yamewazungukia, tunashindwa kwenda popote tunasubiri fidia lakini hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuja juzi Ndugu yangu Makalla kama Naibu Waziri wa Maji, nimekutana na Kaka yangu Maghembe na nimesema katika bajeti zote lakini hakuna kinachoendelea. Ninakuomba uje wewe sasa ili utupe suluhisho la kudumu nini kinachoendelea katika ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili Dar es Salaam wapate hayo maji lakini wananchi wa Kata ya Selembala na Mkulazi wapate haki yao stahiki ili waweze kwenda kujitafutia maendeleo kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi pale tumesimamisha ujenzi wa Zahanati, ujenzi wa nyumba za Walimu, tumesimamisha ujenzi wa barabara, Makanisa, Misikiti na kadha wa kadha. Tunachoomba tunataka tupate fidia yetu ili wananchi wakaanze maisha mapya huko na kupisha ujenzi wa hilo Bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba liende sambamba, mafuriko ya mwaka huu yameonyesha picha kwamba kuna hatari kubwa inayokuja kwa wananchi wa Kata nzima ya Selembala lakini kwa wananchi wa kijiji cha Manyunyu na kijiji cha Kidunda. Tunaomba, kama tuna dhamira ya kuendelea na mradi huu Kata nzima ya Selembala, Kijiji cha Kidunda chote kiingizwe katika mpango wa kupewa fidia ili maafa yasije kuwa makubwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Toka tarehe 12 mwezi ulioisha mpaka leo ninavyozungumza maji yametanda vijiji vyote. Leo hii maji yanakwenda katika utaratibu wake hali hii iko hivi, je, itakapotufikia tumejenga bwawa maji yakirudi nyuma ni kielelezo tosha kwamba na tuna uhakika hata hizi mvua tunazozungumza upo uwezekano maji haya yatafika, tutakuja kuleta maafa makubwa kwa wananchi na Serikali itakuja kuingia katika kipindi kigumu.

Naomba muangalie hilo, watu wa DAWASA njooni kwa sasa mpime upya na muangalie hali halisi ya nini kinachotakiwa kufanyika katika ujenzi wa bwawa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni katika suala zima la upimaji wa ardhi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya kitabu cha bajeti ukurasa wa 46-48 mmezungumzia kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji na hili ndiyo ambalo sasa hivi ndugu Shabiby katoka kulizungumza.

Pamoja na jitihada za dhati za Waziri Mkuu katika kupima vijiji, kuanisha mipaka na mambo mengine, sasa hivi migogoro walau kidogo imetulia kwa sababu nyasi ni nyingi na maji ni mengi lakini tunaamini kipindi cha ukame kutakuwa na migogoro mikubwa. Jamani, haya mapori ya akiba yanafanya kazi gani? Tupunguze maporo ya akiba tupime ardhi tukawagawiwe wananchi walime na wafugaji wafuge kwa kujinafasi ili wajilettee uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili niombe na Bunge letu Tukufu tuliunda Kamati kwa ajili ya kwenda kuangalia vyanzo vya migogoro ya wakulima na wafugaji, naamini kazi imekamilika. Tupewe taarifa nini kilichotokea, tunaishauri nini Serikali ili kuweza kutatua moja kwa moja migogoro hii ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho ambalo napenda kulizungumza ni kwenye suala la mafuriko. Mkoa wetu wa Morogoro umekumbwa na mafuriko makubwa sana, niwape pole wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro kwa adha ambayo imetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais na kwa kwako wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Ujenzi na Mawaziri wengine lakini Mkuu wetu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya lakini hata sisi Wabunge kwa jitihada ambazo tumefanya.

Barabara zimekatika, madaraja yamekatika na hata uharibifu wa mazao na kadhalika. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali, tunahitaji kusaidiwa chakula, tunahitaji kusaidiwa mbegu kwa sababu bado kuna mabonde hata mafuriko yakiondoka tukipanda tunatarajia kupata.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

NAIBU SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Silinde halafu Mheshimiwa Keissy kwa kifupi.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) dhidi ya Kanuni ya 48(3)(a) kuhusu jambo la dharura linaloweza kutokea wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa mbele yako leo ni tarehe 8 na ninayasema haya kwa sababu Walimu katika Jimbo langu la Momba pamoja na Mkoa mzima wa Mbeya na maeneo mengi mbalimbali na wafanyakazi katika taasisi nyingine, wamelalamika kwamba hawajalipwa mishahara yao na wanajiandaa kufanya migomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na hali hii kuwa mbaya kwa sababu ni wiki mbili tangu tarehe 25 ndiyo mishahara ya Serikali inatakiwa itoke, leo ni wiki mbili sasa Walimu hawajalipwa pamoja na wafanyakazi wengine katika sekta nyingine. Tunataka sasa Serikali na ninajua utaturuhusu katika mwongozo wako, Serikali itoe kauli ni kwa nini hawajawalipa wafanyakazi ambao wanaishi katika mazingira magumu mpaka kufikia siku ya leo ya tarehe 8?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Keissy!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kumpa taarifa mzungumza aliyetoka kuzungumza sasa hivi kusema kwamba Wabunge tunakwenda kinyume na Serikali na Serikali tuisaidie kwani iko sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yeye kama anaongea azungumzie Jimbo lake, labda Jimbo lake liko peponi, atuachie sisi Majimbo yetu yako motoni tuzungumze tunavyoweza kwani wametutuma watu wetu. Nashangaa Mbunge

anazungumza kuisifu Serikali baadaye anaanza kuomba, kuna hiki na hiki halafu anamvunga Shabiby anayedai maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Bunge tumetumwa na wapiga kura wetu, hatukutumwa na Mawaziri au Serikali. Kama wewe Mbunge una neema kwako basi zungumzia neema yako tuache sisi watu wetu wako motoni wanateketea tukose kutoa hoja hapa, tumetumwa na wapiga kura hatukuja kwa njia yoyote hapa. (Makofi)

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa yake kwa sababu nilichokuwa nazungumza ni kwamba ni wajibu wetu kuisimamia Serikali katika Halmashauri zetu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri wa Fedha umesimama.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka tu kutoa taarifa kwa Mheshimiwa ambaye amesimama kuhusiana na suala zima la mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa mishahara kuanzia tarehe 24 Aprili, sasa kama hizo fedha zitakuwa hazijafika ni katika mtiririko huu wa kibenki. Suala la Walimu ni kwa sababu tumeajiri Walimu wapya na Wizara ya Elimu haikutaka ku-*incur* madeni kwa sababu ukianza kulipa mishahara kabla ya kuwatia Walimu wapya kwenye *payroll* ina maana utakapowalipa uwalipe na madai kwa hiyo Serikali itaendelea kulimbikiza madai.

Kwa hiyo, kama kuna tatizo limetokea basi ni kwa mtiririko huo wa kibenki zimechelewa lakini fedha zote za mishahara tumetoa tarehe 24/4/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala jioni. Mimi kwa nafasi yangu ya Naibu Spika, sina dakika saba za kuchangia lakini kama ningekuwa nazo dakika saba moto ungeweka lakini itoshe tu kusema kwamba watu wa Kongwa wamekuwa wakiuawa sana Kiteto na majibu mnayasikia, ni ubaguzi, ubaguzi, ubaguzi! (Makofi)

Kama Rwanda, kama Burundi, ni ubaguzi wa kilabila tu siyo mapambano ya wakulima na wafugaji, ni ubaguzi tu! Hatuwezi kwenda na ubaguzi, ni aibu kubwa sana kwa viongozi wanaosimamia ubaguzi unaosababisha mauaji haya, *this thing has to stop!*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Leo mimi sikulala usiku kucha, unasikia bunduki, wananchi wananipigia simu bunduki zinalia, watu wanauawa, Tanzania! Halafu anasimama kiongozi hapa anaongea, unaongea kitu gani? (Makofi)

Naahirisha kikao mpaka saa kumi alasiri!

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala. Sasa ninamwita Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Namelok Sokoine!

MWONGOZO WA MWENYEKITI

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, kulingana na maelezo aliyoyatoa mmoja wa Wajumbe wa Kamati yangu, Mheshimiwa David Zacharia Kafulila leo asubuhi.

Maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Kafulila kuhusiana na *Escrow Account*, ya kwamba, Gavana wa Benki Kuu alipokuja mbele ya Kamati alikiri kwamba, kulikuwa na *pressure* kubwa ya malipo hayo kutoka Serikalini. Naomba kusema kwamba, maelezo hayo siyo sahihi na kauli hiyo ilipotolewa kwa kuwa tayari nilikuwa nimealika kikao cha Kamati yangu, nilienda kukaa na Kamati kabla sijakanusha kauli hii, kujiridhisha kama katika Wajumbe wangu au Wajumbe wa Sekretarieti kuna mtu aliyesikia kauli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukujulisha kwamba, Kamati ambayo inajumuisha Wajumbe wa kutoka vyama mbalimbali inakanusha kwamba, Gavana wa Benki Kuu hakusema jambo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni tarehe 30, Gavana wa Benki Kuu alipokuja mbele ya Kamati kwa ajili ya kuendesha semina na kuelezea majukumu ya utekelezaji wa Taasisi hiyo ya Benki Kuu. Mjadala ulipokuwa

unaendelea, lilijitokeza suala la *Escrow Account*, ambapo Gavana wa Benki Kuu alieleza kuwa katika jambo lile yeye alikuwa mtunzaji tu wa fedha. Kwa hiyo, zilipokuja zile taratibu ambazo zinamwelekeza kutoa malipo, yeye hakuwa na kipingamizi cha malipo hayo na alithibitisha kwamba kwa upande wake yeye amejitahidi kuzingatia taratibu zote za kuhakikisha kwamba, upande wake kama mlipaji taratibu zimefuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara ikamwelekeza kwa sababu ya jambo hili kuleta utata wa zile dola milioni 122 kulipwa kwa PAP wakati kesi ya msingi au malalamiko kati ya IPTL pamoja na TANESCO hayajafika mwisho. Kamati imemwagiza Waziri wa Fedha aje mbele ya Kamati aieleze licha ya hatua zilizochukuliwa za ukaguzi unaofanywa na CAG, lakini Kamati imemwagiza Waziri wa Fedha aje mbele ya Kamati aieleze kama malipo yale yalifuata taratibu na kanuni zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa utaratibu wa kawaida, namfahamu Mheshimiwa David Kafulila, Mjumbe wa Kamati yangu ya Uchumi, Viwanda na Biashara, kijana mwenye uwezo mkubwa na uadilifu wake, aiondoe hii kauli. Hoja yake ni ya msingi tu, Mbunge kutaka kujua uhalali wa fedha za Watanzania zilivyotumika ni sahihi kabisa, lakini kitendo cha kusema kwamba, Gavana wa Benki Kuu alikiri mbele ya Kamati, hayo maneno ayaondoe. (Makofi)

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mpina, mwongozo wangu nitautolea majibu yake muda siyo mrefu sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba hii.

Kwanza kabisa, nipongeze tu kwamba, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imetoa taswira na mwelekeo wa namna ambavyo bajeti itatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka huu; hivyo, napongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Kwa sisi Wananchi wa Mkoa wa Singida, nilikuwa nikiongea na Wazee fulani ambao umri wao umeshakwenda, mzee mmoja akaniambia kwa kinyumbani naomba nizungumze, akasema; *“Inanizalia uogale kutili.”* Kwa maana ya kwamba, mboga sasa zimechanua lakini chakula hakuna. Nikamuuliza maana yake; akaniambia mwanangu mambo sasa hivi yameshakuwa mazuri, lakini sisi umri ndiyo unakwenda, kwa hiyo, ninyi vijana ndiyo mnaosherehekea mambo mazuri ambayo yameletwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana mzee yule kwa kuyaona, lakini naomba na yeye basi amalizie muda wake na uzee wake kwa mambo haya mazuri ili aweze kuneemeka kwenye uzee wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu upande wa utawala bora, nataka nisisitize suala la amani katika nchi yetu. Nimepata wasiwasi sana katika maeneo ya kutuhumu Vyombo vya Ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa salama, tumekuwa tukilindwa kwa amani kwenye mipaka na maeneo yote na Vyombo vya Usalama. Ni kweli kuna matatizo madogo madogo ya uhalifu na hayo yamekuwa yakishughulikiwa. Nilichokuwa nataka kuomba ni kwamba, Vyombo vyetu vya Usalama viongezewe vitendea kazi hasa usafiri kwa askari wetu, nyumba na makazi bora. Naomba waboreshewe kwa sababu kazi wanayaoifanya wanastahili pongezi na ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba tena kushukuru na kupongeza kwamba, maendeleo ambayo yamekuja katika Mkoa wa Singida hususan kwenye upande sasa wa umeme, nguzo katika Wilaya ya Iramba zimeshatandazwa kwenye vijiji karibu 43; hivyo, ninaomba hiyo kasi iongezeke. Ukienda Mkalama umeme umeshabakia kilomita 11 kufika Makao Makuu ya Wilaya. Ninaomba kasi hiyo iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia utaratibu wa maji katika mji wa Ndukuti ambako ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ile. Kwa upande wa barabara kuunganisha Kata na Tarafa, naomba tupatiwe kifungu kwa sababu hiyo ni Wilaya mpya. Ninaomba sana Wilaya mpya ziangaliwe. Ukienda pale Mkalama kwa kweli DC wetu na Watendaji wengine, hawana mahali pa kufanyia kazi. Wamepanga tu na hii haipendezi. Tunalo Shirika letu la Nyumba, naomba tulitumie liweze kutuletea ofisi na nyumba nzuri za wafanyakazi ili mambo yaweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la ukamilishwaji pia wa Barabara na Daraja la Mto Sibiti. Barabara ile si kwa ajili ya Wananchi wa Mkalama na Singida peke yake, ile ni kwa ajili ya watu wa Meatu, kuanzia Bunda kule kwa Babu au Wajukuu zangu, watapita ile barabara, hawatazunguka kupitia Mwanza. Kwa hiyo, naomba uharakishwaji wa ujenzi wa barabara ile pamoja na Daraja la Mto Sibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, naomba sasa nije upande wa fani ambayo ninayo. Nimekuwa nikipigania sana suala la Wasanii. Hapa ninaomba niwaeleze kwamba, tulikuwa tumedai *stickers* kwa ajili ya kulinda kazi za Wasanii, lakini *stickers* hizi ambazo TRA wanatoa, kwanza, kuna ukiritimba mkubwa sana mpaka msanii kupata kibali cha kuzipata.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza; namna ya kuweza kufikia TRA, unapitia milolongo karibu mitano na kote unapita unalipa na *stickers* zile ziko Dar es Salaam peke yake. Ukienda Kasulu, Mbeya, Mtwara, Bukoba, wote wanatakiwa waende Dar es Salaam, Msanii gani anayeweza kumudu adha kubwa kama hiyo? Naomba jambo hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke angalizo; *stickers* tulizotaka siyo za ninyi TRA kukusanya mapato peke yake ni *stickers* za kulinda kazi za Wasanii. *Stickers* hizi tayari zilikuwa zimeanzishiwa mchakato na Sheria ya COSOTA. COSOTA walitakiwa wao ndiyo watoe *stickers* za kulinda haki na kazi za Msanii. TRA walitakiwa wawe wakala, lakini sasa hivi TRA ni kukusanya tu lakini siyo kulinda. Walisema wataingia mitaani kukamata zile kazi za Wasanii, watakamata na kazi zilizo halali kwa sababu wao wanataka kodi. Ninaomba wasitishie jambo hilo, wakae mezani na COSOTA ili waone ni namna gani wanaweza wakakusanya mapato, lakini bado wakalinda kazi za Msanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kengele ni ya kwanza, naomba nimalizie dakika zangu mbili zilizosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze watu wa TCRA, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya sasa hivi kwa Mkongo wa Taifa, mambo yanaenda vizuri. Bado nilikuwa naiomba TCRA, Wizara itusaidie kusimamia Vyombo vya Habari kwa kazi za Wasanii wanazotumia ambazo hawalipi mrabaha. Tafadhali naiomba Serikali isimamie jambo hili. Nafahamu TCRA wana uwezo mkubwa wa kuvibana vyombo hivi. Hata TBC, Televisheni ya Taifa, hamtulipi kazi zetu! Unatumia muziki unasema labda zilipendwa au redio, ukimaliza unasema kipindi hiki kimedhaminiwa sijui na watu gani, unalipwa. Kwa nini *percent* ile isiende kwa wale wenye kazi zao? Naomba sana TBC waoneshe mfano ili na wengine waweze kufuata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida sasa hivi kuna madini mengi sana, lakini naomba wale wachimbaji wadogo ambao tayari walishakamata maeneo yao, tafadhali Serikali isiende kuwabugudhi, kwa sababu kulikuwa na utaratibu uliowekwa lakini bado Serikali ilianza kuchakachua na kutaka kuwapa wachimbaji wakubwa. Hivyo, nilikuwa naomba sana maeneo ya Wachimbaji Wadogo yabaki kuwa ya Wachimbaji Wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mrema, ajiandae Mheshimiwa Amina Amour, na Mheshimiwa Iddi Azzan.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue nafasi hii nichangie yale yanayohusu Jimbo langu la Vunjo. Kwanza, nataka niseme kuwa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya Halmashauri ya Moshi ambayo ina Majimbo mawili; Moshi Vijijini na Vunjo, katika mwaka 2013/2014, nimeambiwa na Mkurugenzi jana fedha ambazo zilizotengwa ni kama shilingi bilioni 2.2 lakini mpaka jana fedha ambazo amepata ni shilingi 370,000,700, ni sawa sawa na asilimia 16.4.

Sasa kama ni asilimia 16.4 ya fedha zote, ambazo ni shilingi bilioni 2.2 na kufikia mwisho wa mwezi ujao, tarehe 30 Juni, sina hakika kama fedha nyingine zote zitafika. Kwa hiyo, hilo ni la kwanza nililotaka niseme kwamba, lazima Bunge lijiulize matatizo yako wapi? Najua matatizo yako kwenye ukusanyaji wa fedha na tunakusanya kulingana na uchumi wetu ulivyo, sasa kile kinachokusanywa hakifiki mahali kilipokusudiwa, aidha kinaibiwa au kinapelekwa mahali pengine.

Kwa hiyo, nilitaka niseme hilo la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu hututendei haki watu wa Moshi Vijijini na Vunjo, kwa sababu fedha zilizotengwa, shilingi bilioni 2.2 zimefika shilingi milioni 370 peke yake. Sasa maendeleo yatapatikana namna gani? Hilo ni kwanza ambalo nilitaka niliseme na nimtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu aniambie hizo tofauti kama zitapatikana kati ya sasa na Juni 30 au tufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo limetuathiri sana. Kwa mfano, kwa upande wa barabara ambazo nilipewa za lami Marangu – Mtoni – Kilema Sokoni ni kilomita tano tu, lakini barabara hiyo inajengwa kuanzia mwaka 2011 na ilitakiwa iishe mwaka 2013 mpaka leo ndiyo wanaendelea, sina hakika kama itakamilika mwaka huu au watangojea mpaka mwaka ujao, mwaka wa uchaguzi. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisaidie, hiyo barabara ya kilomita tano itakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, barabara nyingine ya lami ni Kawawa – Luoni – Kiruwa Vunjo Magharibi, kilomita 10, nayo inasuasua tangu mwaka 2011 mpaka mwaka 2013 ambapo ilitakiwa niwe nimekabidhiwa barabara ile. Sasa nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aniambie nitafanyaje? Tatizo kubwa nililoliona, nilikuwa namuuliza Mkurugenzi, fedha za *road fund* ambazo zimekwishafika kwenye barabara hizo kufikia jana,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

akaniambia ni asilimia 50. Tena afadhali hizo ni nyingi kidogo. Asilimia 50 nyingine itapatikana lini? Hilo ni la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ninavyoona fedha hizi zinazokwenda huko pengine zinaibiwa njiani. Shahidi yangu ni Mheshimiwa Waziri Mwanri, leo kwenye swali langu la Soko la Mwika nimemuuliza. Nimemshukuru barabara ile kutokana na TAMISEMI tulitengewa shilingi milioni 300, lakini anajua Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi alikuja hapa na Madiwani wake wanataka ku-divert zile fedha nikamililia itakuwaje fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya Barabara ya Uchira mpaka kwa Raria kupitia Kisomachi, ambayo inatesa watu kwa miaka mingi, leo fedha zimepatikana zinataka kupelekwa mahali pengine! Kwa kweli ninamsifu sana, alitumia nguvu zake na kweli fedha zile nimeona kwenye gazeti la juzi wame-*float tender* kwamba barabara ile itajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni Mradi wa Maji. Serikali iliji-*commit* kwamba, kwa mwaka 2013/2014 Vijiji vya Vunjo ambavyo vingepata maji ni Mawanjeni, Matala, Kilimo Makuyuni, Makame Juu na Makame Chini; lakini nilipokuwa naonea na Mkurugenzi ananiambia hata shilingi mia moja hazijafika. Sasa mimi nitawaambia nini watu wa hivyo vijiji wakati bajeti ilisomwa hapa na Waziri akaji-*commit*? Mambo kama hayo ndiyo ynatufanya tunagombana na Serikali bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Ushirika kule Kilimanjaro. Mimi niliona yale matatizo ya Ushirika nikaandika kitabu hiki hapa, nikamwandikia Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika hiki hapa, kumweleza matatizo makubwa ya *KNCU* na nakala kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais. Laiti kitabu change kingesomwa na kuchukuliwa hatua, huu mgogoro mkubwa ambao sasa hivi uko Kilimanjaro usingekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wenyewe ni nini? Mmesikia *KNCU* wameita Halmashauri yao wanayojua wala siyo Vyama vya Msingi, Wanachama wa Vyama vya Msingi, wanataka kuuza rasilimali za wanachama wa kahawa. Wamekwenda kuvamia Shamba la Garagua lenye eka 3,400, wanaliweka rehani na mashamba hayo yalikuwa ni ya Serikali tuliyokabidhiwa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira kama hayo, nimemwandikia Mheshimiwa Rais, nimemwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Kilimo na Mrajisi, tunafanyaje! Wamekwenda mpaka *TCCO* kule wameuza zile nyumba tatu pale. Hawa watu wanaouza nimeomba iundewe tume iangalie hiyo hasara ya shilingi bilioni nne tunazoambiwa tulipe za *CRDB* zimetokana na nini; nani amekula hizo fedha? Sheria ya Ushirika mwaka jana mlisema mtu yeyote atakayeleta hasara atakamatwa, atatiwa adabu,

atapelekwa mahakamani, atashtakiwa, atafilisiwa! Mbona hao watu ambao wanakula mali za Ushirika kule Kilimanjaro kule KNCU wanatia hasara na wapo nani anawalinda? Sasa mambo kama hayo ndiyo yanatufanya sisi tugombane na ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni pale Meresini Himo, kuna shamba lililokuwa la Serikali, mmeenda kugawa lile eneo. Wanakijiji wa Himo wameomba eneo la kujenga shule ya sekondari, mahakama na nyumba za waganga, wamenyimwa wamepewa watu binafsi. Sasa leo wanafanya safari ya kuja Dodoma kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumwona Waziri wa Kilimo, ni vitu gani tunafanya! Kwa nini hamchukui hatua tunapopata matatizo huku mnatuachia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Njiapanda, tajiri amejenga kiwanda kwenye makazi ya watu, nimeandika kitabu kiko hapa, Mawaziri wote wanacho, chukueni hatua hamtaki, sasa mnataka sisi tufanyeje? Mbona mnakuwa hivyo jamani, mnakuwa kichoi! Kule kwetu kichoi ni mtu asiyesikia kitu. Kwa hiyo, hii kazi inakuwa ni ngumu, sisi tuko tayari kushirikiana na ninyi, tuko tayari kuwaunga mkono tusaidiane. Ule ushirika ambao umeuza rasilimali za watu, nataka kujua ni hatua gani zitachukuliwa. Kama hamchukui hatua na mimi najua cha kufanya.

Pili, najua lile Shamba la Meresini, kama haliwezi kugawiwa tukajenga shule, mnaenda kuwapa watu matajiri kujenga redio badala ya shule, ni mambo gani hayo! Kama kile kiwanda kimejengwa kwenye makazi ya watu, watu wanalalamika tukiwaambia hamsikii, naomba mtujengee heshima. Najua Mheshimiwa Waziri Mkuu ni msikivu, utanisaidia kuchukua hatua nisivunjiwe heshima.

Bada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mrema, nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Amina Amour, ajiandae Mheshimiwa Idd Azzan.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mpaka mwezi Machi fedha za maendeleo ni asilimia 50 tu zilizotolewa na kutokana na hilo maendeleo hayafanyiki, Miradi mingi imesimama, Miradi mingi imeshatolewa fedha nusu na nyingine hazijapatikana mpaka leo. Sasa naiuliza Serikali; kwa nini wana-*budget* fedha nyingi kwenye maendeleo halafu wanashindwa kutimiza kuzipeleka? Je, hizi fedha zilizobaki ambazo tangu mwezi Machi mpaka leo bado hazijaenda; zitakwenda kabla bajeti inayokuja?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la tatu nawauliza; Kwa kuwa fedha nyingi za Miradi ya Maendeleo zinatokana na Wafadhili; kwa nini Wafadhili mpaka hivi sasa hawajatoa hizo fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitazungumzia kuhusu kilimo. Kilimo ni kichocheo cha uchumi Duniani na hapa Tanzania ni hivyo hivyo, lakini fedha zinazokwenda kwenye kilimo ni kidogo na haziendi kwa wakati. Mpaka hivi sasa nimesimama hapa ni asilimia 71 tu ndiyo iliyokwenda kwenye Sekta ya Kilimo kwa fedha za kigeni na asilimia 50 kwa fedha za ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na haya, kilimo kinasuasua na kilimo ni msimu; kama utakawia kupeleka fedha, mazao hayatapatikana na wata-stop kulima. Ukipeleka kwa wakati unaoutaka wakulima hawatapata mazao wanayotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Sekta ya Uvuvi. Kwenye ukurasa namba 37 nimesoma hapa Kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kimezungumzia uvuvi wa kwenye mabwawa. Ninakumbuka Kamati ya Mheshimiwa Chenge ilitoa mapendekezo yake kuwa uvuvi ufanyike kwenye Bahari Kuu na hapa kwenye kitabu sijaona. Sasa ninamuuliza Waziri, kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu umefikia wapi au yale mapendekezo wameyatupa hawana haja nayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunataka *Big Results Now (BRN)*, lakini mpaka hivi leo vipaumbele ni vingi na kila mwaka tunatoa ushauri kwa nini hatuweki vipaumbele vikawa viwili ambavyo tunaweza kuvitimize kwa wakati halafu tena tukaja na vipaumbele vingine. Tunakusanya vipaumbele kama sita, kila kimoja tunakifikisha nusu nusu. Kwa hivi tunavyokwenda itakuwa kazi bure, kila mwaka tutapanga bajeti, lakini yale tunayotaka kufanya hatutoyatimize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali moja nataka kuliuliza; kuna haja gani ya kila mwaka kuzidisha bajeti, maana kama mwaka jana ilikuwa trilioni 18, mwaka huu trilioni 19; sasa kuna haja gani ya kuzidisha hii bajeti ambapo haitekelezwi? Kwa nini hatubakii na ile ile ya mwaka jana tukaendelea nayo ikawa ndiyo ya mwaka huu, tukaweza kutekeleza. Huu mfumo tunaokwenda kusema kila mwaka ni lazima tuongeze bajeti ambapo tunashindwa kutekeleza hautufikishi. Matokeo yake hizi fedha za bajeti hii itabidi zilipwe kwa bajeti iliyopita na ile Miradi ambayo tumeipanga tufanye kwa mwaka huu hatutaweza kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru kwa kuokoa muda. Sasa ninamwita Mheshimiwa Iddi Azzan, ajiandae Mheshimiwa Mbassa!

MHE. IDDI MOHAMED AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Niseme tu, nchi yoyote ambayo iko huru inatumia aina zote za nguvu za hali na mali kuhakikisha uhuru ule unalindwa.

Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Amiri Jeshi Mkuu pamoja na Mkuu wa Majeshi, kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati tukisherehekea miaka 50 ya Muungano. *(Makofi)*

Yale waliyoyaonesha pale ndiyo ambayo Watanzania tulitarajia kuyaona, kwa sababu baada ya Vita vya Kagera tulidhani labda tumelegalega. Kwa kilichooneshwa juzi kwenye Sherehe za Muungano inaonesha kwamba tuko imara, Serikali iko imara kulinda mipaka yake, lakini iko imara kuwalinda Watanzania. Hongereni sana Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tumekumbwa na maafa, wenzangu wameyasema na mimi naomba nirudie tena kwa msisitizo mkubwa sana. Tunayo matatizo ya msongamano ambayo yanajulikana miaka yote, lakini kwa mvua zinazoendelea kunyesha Dar es Salaam hivi sasa ni maafa. Wenzetu mmezoea maafa yakitokea huko mtakusanyana kwenda kutoa misaada ya chakula, sisi chakula hamtupatii, lakini hatukitaki; tunachotaka ni msaaada juu ya miundombinu ambayo imeharibika kwa kiasi kikubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua tuna msongamano, lakini mvua hizi zimesababisha miundombinu kuharibika kwa kiasi kikubwa mno, kiasi kwamba sasa Dar es Salaam imekuwa ni mahali ambapo tuseme ni janga ambalo liko pale. Kwa hiyo, tuombe na Halmashauri ziliomba, Mheshimiwa Mtemvu jana alisema na mimi narudia, Halmashauri ziliomba Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, mtusaidie kuona tunaondokaje pale tulipo hivi sasa Dar es Salaam. Tuliomba fedha kwa ajili ya miundombinu, bahati nzuri zinaonekana zipo za Ilala 4.5 billion, lakini kuna bilioni 8 ambazo ziliombwa na Kinondoni na takribani bilioni 5 ambazo ziliombwa na Temeke hazikuonekana. Kwa hiyo, inawezekana Ofisi ya Waziri Mkuu fedha hizi mnaweza msizitoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hali ilivyo Dar es salaam, tunaomba sana mtusaidie ili tuweze kuweka miundombinu yetu vizuri kwa sababu hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ujenzi unaoendelea hivi sasa wa Mabasi yaendayo haraka (*DARTS*). Ni mpango mzuri, ni ujenzi mzuri, napongeza sana hatua ambazo zimechukuliwa mpaka sasa, kazi inakwenda vizuri na tuko kwenye hatua za mwisho mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa ujenzi ule wa barabara ya mabasi yaendayo haraka mwisho wa siku nao utakuwa janga, kwa sababu kabla ya

hapo Barabara ya Morogoro ilikuwa na mifereji iliyo wazi ya kuondoa maji ya mvua. Ujenzi huu tangu umeanza na hivi sasa unaelekea mwisho mwisho, mifereji ile imefukiwa kabisa, kwa hiyo, maji ya mvua yote badala ya kwenda kwenye mifereji kuondoka, yanakwenda kwenye nyumba za watu na kuleta mafuriko. Kwa hiyo, tunaomba kabla hajaondoka mkandarasi huyu, mifereji ile ambayo ilikuwa ipo awali, irudishwe itengenezwe vizuri ili maji ya mvua yasiwasumbue Wananchi wa Dar es Salaam. Hili lipo sana kuanzia maeneo ya Mwembechai mpaka Jangwani, lakini inawezekana pia tangu ulipoanza Mradi huu, tatizo hili lipo kwa maana ya Kimara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine wenzangu wamelizungumzia ni juu ya unyanyaswaji wa waendesha pikipiki (bodaboda). Pamoja na amri ambazo zimetolewa, kuzuiwa kwenda mjini, lakini kuna vibali vya shilingi 180,000, vya shilingi 90,000, ukitoa hizo fedha unapata nafasi ya kwenda mjini, kitu ambacho tunaona pia ni uonevu. Kikubwa ambacho kinasikitisha ni jinsi *SUMATRA* wanavyowanyanyasa waendesha bodaboda hawa. Imefika mahali kuonekana waendesha bodaboda hawa basi wote ni wahuni tu, kumbe ni watu ambao wana familia zao, wanafanya kazi kwa ajili ya kupata riziki kama ambavyo na sisi wengine tunafanya kazi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa bodaboda anakwenda kuomba leseni *SUMATRA* analipa shilingi 68,000 leseni ile ni kwa mwaka, lakini anapewa leseni ya miezi miwili au mitatu na ikiisha arudi tena akatoe tena shilingi 68,000 apewe leseni nyingine ya miezi miwili au mitatu. Huu ni unyanyasaji, naomba hili liondolewe, kama ada ya shilingi 68,000 ni kwa mwaka basi walipe wapewe leseni ya mwaka mzima, lakini si kuwapa ya miezi miwili halafu waje walipe tena muwape ya miezi miwili, ni kuwaonea. Badala ya kulipa shilingi 68,000 sasa wanalipa zaidi kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uonevu na tunaomba hili likomeshwe, kwa sababu tulipitisha sheria hii kwa nia ya kuwasaidia wao kupata riziki na pia kusaidia na wengine kupata usafiri. Kwa hiyo, naomba sana tatizo hili tuliondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia, wenzangu walizungumza hapa asubuhi kuhusu TAKUKURU. Kwa namna yoyote ilivyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana TAKUKURU kwa kazi nzuri wanayoifanya. Sisi Watanzania tuko wengi sana, lakini askari ama kikosi cha TAKUKURU ni watu wachache, hawawezi kukidhi kila mahali, inatakiwa na sisi pia tuwe ni askari wa TAKUKURU, kwa maana ya kutoa taarifa pale ambapo tunaona kuna rushwa inafanyika ama inataka kufanyika. Nashangaa sana, kiongozi kuja kulalamika Bungeni badala ya kwenda kutoa taarifa kwa rushwa ambazo ameziona. Kwa hiyo, niipongeze sana TAKUKURU, kazi nzuri wanafanya, tuendeleo kuwaunga mkono, tuwaongeze bajeti yao wapate vitendea kazi ili kukomesha tatizo la rushwa

hapa nchini. Tatizo hili haliwezi kuisha kwa kutegemea TAKUKURU peke yake, ni lazima wote tusaaidiane ili kuondokana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa sana suala la msongamano Dar es Salaam; hali siyo nzuri, foleni zimekuwa kubwa na hata bodaboda zinazofanya kazi Dar es Salaam, kama unataka zisifanye kazi Dar es Salaam, kama unataka zisiingie Dar es Salaam, basi boresha miundombinu. Tengeneza barabara, nani atapanda bodaboda kama mjini unaweza ukaenda tu kwa mara moja! Leo inafika mahali unapanda bodaboda na begi kichwani ili uwahi *Airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba suala la miundombinu Dar es Salaam limekuwa ni kero na bahati nzuri asubuhi ulisema hapa, tunapoomba Dar es Salaam wengine mnaona kama tunapendelewa, lakini mjue karibu asilimia 80 ya Pato la Taifa linatoka Dar es Salaam. Kwa hiyo, sisi kujengewa si vibaya, lakini mjue na ninyi mlioko humu ndani makazi yenu yote karibu yako Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunapoomba kuboreshewa miundombinu Dar es Salaam, tunawaomba na ninyi pia msipate tabu mnapokuja Dar es Salaam au mnapokuwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba barabara ambazo zimeainishwa na zile ambazo tumezipigia kelele siku nyingi hazijapangiwa fedha mwaka huu, tuhakikishe zinapatiwa hizo fedha barabara hizo zitengenezwe ili kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu sana kwa hali ilivyo hivi sasa Dar es Salaam, mahali pa kwenda nusu saa au dakika 10 unatumia muda mrefu. Tunapoteza muda mwingi wa kufanya kazi na tunapoteza fedha nyingi kwa maana ya mafuta mengi yanatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Azzan. Mheshimiwa Mbassa, ajiandae Mheshimiwa Paresso!

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia katika hotuba hii muhimu iliyo mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea yaliyoko Jimboni kwangu. Naomba nianze na ule ukurasa wa 35 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akiongelea kuhusu Vyama vya Ushirika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Ushirika ndiyo ilikuwa nguzo muhimu kwa mkulima, vilikuwa mkombozi wa mkulima na ndiyo vilivyokuwa vinajenga uchumi wa mkulima, lakini leo hii vyote vimekufa havijulikani viko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kuna Waraka umetungwa kwa ajili ya kuwazuia Viongozi wa Kisiasa wasiwe Wajumbe au wasiwe Viongozi, mimi naunga mkono. Vyama hivi viko wapi? Napenda kujua kilichokuwa Chama cha Ushirika *Biharamulo Co-operative Union* kiko wapi? Mali zake ziko wapi? Hali ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Wilaya hii ilipomegwa kukawa na Wilaya ya Chato, chama hiki kimekufa hakijulikani kiko wapi. Kwa hiyo, naomba katika majumuisho tupate jibu Wanabiharamulo kwamba Chama hiki kiko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 44 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongea juu ya Hifadhi ya Mapori ya Akiba. Mimi pale Wilayani kwangu lipo Pori la Kimisi na Pori la Burigi, ni Mapori ya Hifadhi ya Akiba. Mapori haya yanatumiwa ndivyo sivyo, askari wa wanyamapori wanayatumia mapori haya kwa ajili ya kuendeleza unyanyasaji dhidi ya wafugaji. Aliyeona juzi taarifa tarehe 5 Mei, 2014, zaidi ya ng'ombe 170 wameshikiliwa na hawa askari wa wanyamapori ambao nilishawataja hapa, ng'ombe wale wamekufa. Zaidi ya ndama 115 wamekufa, kisa wamekutwa kwenye Pori lile la Akiba na askari wakaamua kuwazuia wale ng'ombe wamekufa baada ya wale wafugaji kutokutoa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoamini, watu wote ndani ya Serikali hii tunaishi au tunalindwa na sheria, taratibu na kanuni; hivi kuna wafanyakazi gani ambao wako juu ya sheria?

Tarehe 20 Desemba, 2013 niliongelea suala hili hapa, nikawataja watu hawa ambao walikuwa wanaendesha vita hii ya kuwanyanyasa wafugaji, wa kwanza akiwa Jonathan Musiba, wa pili Frederick Kobelo. Watu hawa ndiyo wameendeleza jambo lile pamoja na kauli kutolewa hapa Bungeni kwamba operesheni ile isitishwe, wao waliendeleza. Leo hii nashukuru kwamba, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na Mama Anna Tibaijuka wameshuhudia. Sasa tunataka kujua ni nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikubaliki na hii haitatusaidia; mfugaji ni Mwananchi, mfugaji ni Mtanzania, mfugaji ana haki, hebu haki zake zilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 46 ameongelea migogoro ya ardhi. Tumekuwa tukiongelea mara nyingi hapa migogoro ya ardhi iliyoko majimboni kwetu. Nimeeleza mgogoro

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa ardhi uliopo katika Jimbo langu la Biharamulo, Kata ya Kaniha, Kijiji cha Kaniha na Kijiji cha Mpago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wamewekewa bango mwezi wa 12 na TFS wahame, wahamie wapi, hawajaonyeshwa sehemu ya kuhamia, hawajawekewa miundombinu? Leo hii cha kushangaza wale wale waliowaambia wahame ndiyo wanaenda kule kuwataka watoe mchango kwa ajili ya mwenge, watachanga nini! Wachangie nini wakati wameambiwa wahame, wameambiwa wasilime na wesiendeleze maeneo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuja kutoa majumuisho atuambie hao watu wanaoambiwa wahame wahamie wapi? Tuna Serikali ngapi inayotenga Mapori ya Hifadhi na inayotenga Vijiji ambavyo Serikali ile ile inavisajili lakini Wananchi wanaambiwa wahame! Tunaomba tupate jibu, vinginevyo yatakuwa siyo maisha bora kwa kila Mtanzania ila ni maisha ya adha kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la Mkoa wa Kagera kuhusu usafiri. Tuliahidiwa meli kubwa katika Ziwa Victoria. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naona kuna utaratibu wa kukarabati wa meli nyingi tu na nyingine ambazo ziko nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutumia gharama kubwa ya kukarabati hizi meli, kwa nini isipatikane meli iliyoahidiwa na tukaona inasaidiaje kuendeleza uchumi wa Wanakagera? Tunaomba meli hii ipatikane na isaidie katika usafiri au kupunguza gharama za Wananchi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee makazi na nyumba za askari wetu na hiki ni Kituo cha Polisi Biharamulo. Nyumba zile zimechakaa. Jengo lile limechakaa kiasi kwamba halifai. Mtumishi yeyote anapokuwa amepewa kazi anahitaji afanye kazi ile katika mazingira mazuri. Jengo lile ni la miaka nenda rudi, limeshatoboka juu linavuja, kiasi kwamba inakuwa ni aibu kutamka hapa kwamba kituo kile hawana hata sehemu ya kujihifadhi kwa maana ya choo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha. Tunaomba tupate jibu Wizara hii inalifikiriaje jengo hili, inafikiriaje nyumba za askari ambao sasa wamevunjiwa heshima wanaishi mitaani kwa kupanga. Leo hii tunapowaweka askari wetu mitaani wakaenda kupanga heshima ya kazi haipo. Haiwezekani ukasema mtu huyu atakuwa mwadilifu wakati unaona maisha yake yalivyo. Hiyo ndiyo nafasi ya kuanza kuwahonga na sisi tunasema kwamba rushwa imekithiri nchi hii, lakini ni sababu ya askari hawa kutokuwatendea haki.

Niongelee suala zima la vijana maarufu bodaboda. Vijana hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, hata mimi pale Wilayani kwangu

wapo, inafika mahala kila saa inakuwa ni kukimbizana na polisi. Askari wengine siyo wa Usalama Barabarani lakini wakimwona tu inakuwa ni tabu, wengi wamevunjika miguu, wengi wamepata tabu. Tumejaribu kufanya kikao na OCD walau kuona tunawasaidiaje, lakini bado wengine wanazidi kulalamika juu ya suala hili.

Ninaomba tupate utaratibu mzuri wa kuwasaidia na kuwatambua vijana hawa kwamba hii ni ajira yao rasmi na ndiyo inayowapatia kipato. Wakikosa ajira hii wataingia msituni watakuwa vibaka, tutaanza kulaumu tena kwamba vijana wetu wamekuwa vibaka. Hebu tuwasaidie kwa hili dogo ambalo wanaliweza liweze kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea hali ya barabara zetu. Barabara nyingi zinatengewa fedha zinajengwa lakini zinajengwa kwa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutegemei barabara ijengwe bila kuwekewa mitaro, madaraja ya kutosha au makaravati pale ambapo kunahitaji tutegemei barabara hii idumu. Barabara nyingi zinatengenezwa, lakini zinatengenezwa kwa kipindi ambacho tunakwenda kwenye Vikao vya RCC na Road Board, kabla ya hapo barabara hizi hazitengenezwi. Nawaomba Wakandarasi wanaopewa barabara hizi, watengeneze kwa uimara na wasimamiwe vizuri. Inawezekana tatizo ni usimamiaji, nawaomba wale wote wanaopewa dhamana ya kufanya kazi hii wasimamie vizuri ili tuweze kupata barabara ambazo zitatuvusha kwa kipindi kitufaacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kugongewa kengele, ninakushukuru ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ninashukuru sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Mbilinyi ajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, ninaunga mkono Hotuba iliyosomwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni.

Ninachukua nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, toka ilipoanza kuongozwa na CHADEMA imekuwa ikipata Hati Safi za Mahesabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 1998 na 1999 kulikuwa na dhana ya ugatuuji wa madaraka kupeleka Serikali za Mitaa na kupeleka mamlaka makubwa Serikali za Mitaa kwa sababu ndiko watu waliko. Dhana hii imebaki

kimaandishi na kwa maneno tu si kwa vitendo. Asilimia 30 ya *National Budget* ndiyo inapelekwa Serikali za Mitaa, fedha nyingi zinabaki Serikali Kuu lakini Serikali Kuu yenyewe haina watu, watu wako *Local Government*. Sasa tunasema hapa kila siku, mkiambiwa hamsikii mnaona CHADEMA wanasema lakini ni kweli hamsikii kwa sababu hamyatendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupeleka fedha za maendeleo Serikali za Mitaa inaonekana kama ni hisani, hakuna umuhimu unaofanywa na hii Serikali ya CCM inayojiita sikivu kupeleka fedha ambako Wananchi wako, ambako Wananchi wanataka kuona Miradi ya Maendeleo katika maeneo yao.

Niongelee suala la uharibifu wa mazao unaofanywa na wanayamapori. Wilaya ya Karatu inapakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Wananchi walio jirani katika maeneo hayo katika Kata za Rotya, Mbulumbulu na Ganako, wanapata usumbufu mkubwa wa wanyama wanaotoka Hifadhi ya Ngorongoro wanaharibu mazao. Tumelisema mara nyingi hapa Bungeni, tunaambiwa Wananchi watapata fidia. Wananchi hawapati fidia kwa wakati, hawapati fidia ya uhalisia kutokana na mazao yaliyoharibika, kila siku tunaahidiwa, mkiambiwa hamsikii mnatuona sisi sijui tukoje, lakini tunawaambia hamsikii na mmeshindwa, Wananchi wanapata adha hiyo.

Niongelee suala la barabara; kulikuwa kuna ahadi ilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura amekuja Karatu aliahidi tutatengenezewa Barabara ya Njia Panda - Mang'ola - Lalago kwa kiwango cha lami. Kila siku tunaambiwa uchambuzi, usanifu, mchakato unaendelea, leo tunamaliza kipindi cha Mheshimiwa Rais na hakuna kinachofanyika, ni maneno ya mchakato, ni maneno ya usanifu na mambo mengine ambayo tumezoea kuyasikia. Hatuoni hasa kinachoweza kufanyika kwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais.

Barabara hii ni muhimu kwa sababu Wananchi walio katika Tarafa ya Yasi wanazalisha vitunguu maji kwa wingi sana. Vitunguu vinasafirishwa nje ya nchi, vinaenda mpaka nchi za Uarabuni, Nairobi, Sudani, kote vinasafirishwa lakini hakuna miundombinu ya kutosha; huyu Mwananchi atasafirisha vipi mazao yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tusikie haya maneno yanaisha na utekelezaji wa hii ahadi inafayika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Daraja la Kirurumu ambalo lipo mpakani mwa Wilaya ya Monduli na Wilaya ya Karatu. Daraja hili ndiyo barabara kuu ya kuelekea Ngorongoro, kila mara wakati wa masika linasombwa na maji. Watalii wanaenda Ngorongoro hawapiti daraja linakuwa na usumbufu. Panatokea utengenezaji wa muda kulitengeneza lakini tatizo liko palepale; tunataka kujua

njia hii ni njia kuu ya Wazungu kwenda Ngorongoro, kwenda Serengeti, Wazungu hao ndiyo wanaotuletea mapato ya nchi lakini usafiri wa uhakika kwa sababu daraja linakatika! Tunataka kujua ni lini daraja hili litapatiwa *solution* ya kudumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ardhi. Wilaya ya Karatu sehemu yake ya ardhi inamilikiwa na Wazungu, inaitwa Mashamba ya Mikataba. Wazungu hawa wanamiliki ardhi hizi kwa umiliki wa miaka 99, ni muda mrefu. Walikuwapo toka ukoloni. Hawa Wazungu wanaomiliki mashamba haya wengi wao wanazalisha zao la kahawa na wapo Wananchi ambao wameajiriwa maeneo yale. Wazungu hawa wamekuwa wakimiliki maeneo makubwa ka *lease* ya miaka 99, lakini kuna maeneo ambayo hawajayaendeleza hawataki kuyaachia.

Wananchi hawana hata pa kuzikwa, hawana maeneo ya kujenga, lakini wameendelea kuyamiliki; ni kwa nini Serikali hamlioni hili? Ni kwa nini hamwoni umuhimu wa kuwanyang'anya; kama mtu anamiliki ardhi kwa miaka 99 na baadhi ya maeneo yake hayaendelezi ameyaacha ilhali Wananchi wanakosa hata makaburi ya kuzikwa? Hii siyo haki, tunataka Serikali muingilie kati kwa kushirikiana na Halamshauri, Wazungu ambao wameacha maeneo yale mapori hawayaendelezi wanyang'anywe Wananchi waweze kugawiwa.

Nizungumzie suala la afya. Halmashauri ya Wilaya ya Karatu inayoongozwa na CHADEMA, imejenga Chuo cha Afya Karatu pale kwa nguvu za Wananchi, wadau mbalimbali na fedha za Halmshauri, lengo likiwa ni kuzalisha wataalamu, manesi na madaktari. Jitihada hizi zimefanywa kwa kujenga madarasa manne lakini bado kuna upungufu mwingine, tunaomba kujua Serikali ni lini na ninyi mtaweka nguvu yenu kwa sababu hawa watakozalishwa hapa hawatasaidia Karatu tu watasaidia Mkoa mzima wa Arusha kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la ukosefu wa dawa. Ukosefu wa dawa siyo kwa Karatu katika Zahanati zetu, Vituo vya Afya na Hospitali, ni nchi nzima na sababu mnajua hamuwezi kuikwepa. MSD inaidai Serikali shilingi bilioni 89. Kazi ya MSD, Bohari Kuu ya Dawa ni kununua dawa, vifaa tiba na vitenganishi ili isambaze nchi nzima. Hawana cha kufanya kwa sababu wanawadai. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii ni *serious* sana; MSD inaidai Serikali bilioni 89, inashindwa kuagiza dawa, Wananchi hawana dawa halafu ninyi mnasema maisha bora yako wapi?

Mnasema ni sikivu usikivu wenu uko wapi? Hamna hata huruma na afya za Watanzania, Wananchi wanakosa dawa kwa sababu kuna madeni. Mbona hamwachi kusafiri mkalipa MSD? Kwa nini msipunguze safari siku moja mkaacha na haya magari yenu msiweke mafuta makaamua kujinyima mkalipa hili deni la

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MSD Wananchi wapate dawa? Hamna usikivu wowote na lazima tuwaambie na tutaendelea kuwauliza ni lini mtalipa deni la MSD lililofikia bilioni 89?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la masilahi ya Madiwani. Wabunge tukiwa hapa wasaidizi wetu wakubwa ni Madiwani katika maeneo yetu. Madiwani ndiyo wanaofanya kazi, Madiwani ndiyo wanaosikiliza kero za Wananchi kila siku. Diwani anaamka nyumbani kwake asubuhi anakuta foleni ya Wananchi weanamweleza matatizo mbalimbali lakini hakuna umuhimu wowote wanaopewa; masilahi yao yako duni, hawapati mafunzo, hawapati ziara za kujifunza wapo tu. Wabunge na Maadiwani hatuna tofauti, wote tuna jukumu la kusaidia Wananchi lakini kwa nini ikifika suala la masilahi tunawatenga Madiwani na nyinyi hamsikii? Ni rai yangu kwa Madiwani wengi ambao ni wa CCM mwone Serikali yenu inavyowafanya, oneni jinsi ambavyo hampati hata mafunzo, hampati hata *capacity building* mnazotakiwa kupata ambazo zilikuwepo wakati huo. Hii inasikitisha, ninaomba suala la Madiwani lizingatiwe. (Makofi)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Mbilinyi, ajiandae Mheshimiwa Aeshi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimi pia ninaomba nichukue fursa hii kuungana na Mheshimiwa Wenje na wengine, kuhusiana na suala la Wamachinga. Takribani wiki mbili zilizopita hata Mbeya wamevunja vibanda vya Wamachinga maeneo ya Mwanjelwa na maeneo ya Kabwe. Tatizo ni kwamba, wanavunja usiku na ukiuliza mamlaka husika zinasema Mheshimiwa tulikubaliana nao. Sasa kama ulikubaliana nao kwa nini uende saa nane usiku kuvunja vibanda vyao na mle ndani wameweka vocha zao, kuna stock za biashara zao na wengine hawaendi na hela nyumbani wanaweka mle kwa sababu ndiyo ofisi zao?

Ninajjuliza sana kwa nini Serikali inaenda kuvunja vibanda vya Wananchi usiku maeneo ya biashara au ni dhamira ya wale wanaovunja kutaka kupora zile hela zilizomo mle na bidhaa zingine?

Niwape pole Walimu wa Mkoa wa Mbeya, japokuwa jibu limetoka lakini bado ninapokea *message* kutoka kwao, ninawaambia waendeleo kuwa wavumilivu tuangalie mpaka kesho hali itakuwa vipi. Wanasema mpaka sasa hivi bado hawajapata mishahara. Wanauliza fedha zimekwenda wapi au fedha zote zimemalizika kwenye Sherehe ya Muungano! Ninawaambia vumilieni. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili bajeti hii lakini kama nilivyosema bajeti ya mwaka jana, kila siku tunajadili vitu vilevile kwa sababu fedha hakuna. Tumetoka kwenye Kamati, kuna baadhi ya Wizara wanasimama wanakwambia

wamelipa mishahara tu, Wizara haijafanya maendeleo, wamepata hela ya kulipa mishahara tu. Utashangaa Katibu Mkuu au Waziri anasimama anasema ninashukuru safari hii tumeongezewa tumekuwa na bilioni 30. Enhe mwaka jana mliidhinishiwa shilingi ngapi; bilioni 20. Mlipata kiasi gani; bilioni sabu au bilioni nane.

Sasa ni kwa nini tunakaa kujadili bajeti tusiendeleo na bajeti ya mwaka jana kwa sababu haijafika hata nusu? Tungeendeleo na bajeti ya mwaka jana. Tuna tatizo Serikali Kuu la kukusanya fedha, Halmashauri ndiyo usiseme. Halmashauri yangu ya Jiji la Mbeya imetajwa kama Halmashauri zilizoshindwa kukusanya mapato; ni kweli, lakini inakuwaje Mkoa ambao ni kati ya wachangiaji wakubwa wa Pato la Taifa *and best* wanashindwa kukusanya mapato katika Jiji lake? Hapa jibu tunalopata ni nini; *leadership*.

Nilisema mwaka jana kwamba, Jiji la Mbeya halina Meya; Meya hana upeo, Meya mbabe, Meya haitishi vikao, Meya anatumia fedha kwenda kutembea China na vitu kama hivyo. Meya hawazi nini kinatakiwa kifanyike katika kuboresha ukusanyaji wa mapato kwenye Jiji la Mbeya ambalo liko kwenye Mkoa ambao uko katika *top of the list* kwenye kuchangia Pato la Taifa hili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu siku moja tulishawahi kukutana kwenye korido wakati ule wa mtiti wa Wamachinga ukaniuliza vipi Mbeya kumetulia; nikakwambia kumetulia. Ukaniulioza hakuna tatizo lolote; nikakuambia lipo. Ukaniuliza nani? Nikakwambia tatizo ni Meya; ukasema eeh, yakapita. Mbeya tuna tatizo la Meya na ndiyo maana hakuna *leadership* na ndiyo maana mpaka leo hii, mimi ninaingia kuwa Mbunge mpaka ninamaliza huu ni mwaka wa nne, Soko maarufu la Mwanjelwa ambalo ndiyo lingekuwa chanzo kikuu cha mapato katika Halmshauri ya Jiji la Mbeya, mpaka leo limelala. Limelala siyo kwamba fedha hakuna, fedha zimetolewa mkopo CRDB bilioni kumi na tatu zikaenda. Wanasema sijui mkandarasi kakimbia na hela, sijui kaenda kujenga nyumba ya Waziri Mkuu Dodoma, kachukua hela za Mbeya.

Haya mambo wanasema kwenye vikao. Unauliza sasa tunafanyaje? Wanasema tumtengue na tukimtengua inabidi tuongeze bilioni tatu zingine; tunakopa tena bilioni tatu, bilioni kumi na sita mpaka leo hii Soko la Mwanjelwa halijaanza kazi na wala halina dalili ya kuanza kazi halafu tunasema kwamba kwa nini Mbeya mapato hakuna.

Mapato hakuna kwa sababu hakuna *leadership* kwenye Halmashauri ya Jiji la Mbeya. Meya amekaa tu sasa hivi kupambana na Dada yangu Mary Mwanjelwa, anaangalia atamdhiti vipi kwenye kura za maoni! Mbeya hamchomoi kwenye kura za maoni mwaka 2015 tumeshaziba! Suala la Mbeya lilishaisha, sasa Meya anaacha kufanya kazi kama Meya, anaanza kugombana

na Wabunge wenzake wa CCM kwa ajili ya kura za maoni za mwakani!
(Makofi)

Tuondolee mtu huyu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Uliniuliza na nikakwambia huyu ndiyo tatizo la maendeleo la Jiji la Mbeya. Tunafanya kazi, watu wanafanya shughuli zao wanatulia, yeye akikaa akiwaza kura za maoni za CCM, anaibuka na vitu vya ajabu anataka kuhatarisha amani ambayo imetulia Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii japokuwa wanasema hawatajwi lakini mimi ninajua wale wa vyeo vya juu wanatajwa; nimpongeze sana Mzee Salmin. Mheshimiwa Waziri Mkuu unamjua, sitamtaja kwa cheo, lakini yule Mzee ndiyo anayesababisha amani ya Mbeya kwa kushirikiana na watu wote sisi bila ya kumsikiliza Meya Kapunga, ambaye anatuyumbisha kila saa katika Jiji la Mbeya.

Jiji la Mbeya linakuwaje halina mapato jamani? Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa Mawaziri wote wako chini yako. Sasa hebu angalia barabara zetu, kila siku tunakaa hapa tunajisifu barabara kilomita ngapi! Mheshimiwa Magufuli anapiga siasa kwenye hela za Wananchi, hela zetu, anasema kwamba kutoka Mtwara mpaka Bukoba sasa hivi unaweza kwenda kwa Bajaji. Ninamwambia hivi, sasa hivi hata GX100 au VITZ hutoboi, hupiti katika Brabara zake, kwa sababu zote zimeumuka.

Vilevile asisingizie mvua, hii ni kabla ya mvua, barabara zote zimeumuka. Barabara inajengwa baada ya miezi minane inaumuka, kila siku watu tunataka kupata ajali, siyo Mikumi barabara mpaka kwenye mizani. Sasa mizani zinaanzishwa za nini? Unasema huko kwingine kuna tatizo; kwenye mizani pale Morogoro ile barabara yote imeumuka imeyumba au tatizo ni udongo wa Tanzania labda haufai kwa barabara za lami? Kwa nini ni barabara zote za Tanzania? Kuna siku nilikuwa nje ya nchi na Wabunge wa CCM, marafiki zangu, tukaangalia barabara wote tukasifia; nikawaambia jamani mkamwambie Magufuli aje kuangalia huku au anakuja haangalii?

Mimi ninajiliza; huu ujenzi wa sasa hivi ukoje angalia Barabara ya Makambako – Songea, BAFOBIT walijenga ile Kampuni ya Uingereza; mbona mpaka leo haiumuki? Mpaka leo tunapita Makambako kwenda Songea Barabara imetulia, halafu leo mnasema Magufuli sijui nani anafaa kuwa Rais! Hafai kuwa Rais ajaye, anafaa kuwa mfungwa ajaye kwa sababu fedha za Wananchi utamuuliza akija hapa atakwambia fedha zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa sehemu zilizoumuka, sehemu zilizoharibika. Fedha zimetengwa vipi? (Kicheko)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hizo fedha zingepona si zingeweza kujenga zahanati, kununua madawati na kadhalika? Sasa kwa namna hii hatuwezi kwenda. Hiyo Miradi yenyewe ya Barabara angalia ilivyokuwa na manung'uniko, kuanzia Mbeya, Kampuni ya SAIKO China sijui nini inayojenga mpaka STRABERG, tunaangalia kwenye TV kila siku Dar es Salaam ni malalamiko. Hawa wafanyakazi vibarua wazawa ni kwa nini wanapata tabu sana na haya makampuni wakati haya makampuni yanapata faida kubwa? Kila siku ni migomo, STRABERG Dar es Salaam wale wanaojenga hiyo *Rapid Road*, mnazungumzia usafiri utakuwa wa haraka, foleni zitaondoka; foleni zitaondoka kuna watu wana njaa pale hawalipwi?

Sasa hii inakuwa vipi? Mimi nashauri hivi; haya Makampuni ya kigeni ambayo yanakuja kufanya kazi hapa, sehemu ya makubaliano ya mkataba iwe ni masilahi yenye malipo kwa vibarua wazawa wanaofanya ile kazi. Wewe unamlipa mtu shilingi 3000 kwa siku au shilingi 4000 kwa siku! Ujenzi wa barabara unakamilika, Mchina anaondoka, Mzungu anaondoka, wote wanaondoka, yule aliyekuwa anashika sepetu hajanunua hata TV, hajanunua hata kiti au stuli. Kipindi chote barabara inajengwa anapata hela ya kula tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, muda hautoshi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mbilinyi. Ninamwita Mheshimiwa Aeshi, ajiandae Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, ninaomba niunge mkono Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pili nimpongeze kwa bajeti nzuri. Tatu, nataka niongelee kuhusu kilimo kwa sababu sisi ni wadau wakubwa sana wa kilimo hususan Jimbo langu la Sumbawanga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA, ninaamini kabisa imefanya vitu vikubwa na vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo tumeendelea, kwa kweli tumepiga hatua, tumeweza kutoka kwenye tani laki nne mpaka tani milioni moja na laki nne. Kaulimbiu ninafikiri sasa imefikia kwenyewe. *(Makofi)*

Nikuombe tu kwenye suala kilimo hili tuwasaidie hawa wakulima wadogo wadogo kwa kuongeza matrekta, kuongeza pembejeo, kuongeza mbegu na mbolea. Tumekuwa waathirika wakubwa ukizingatia kwamba, katika *Big Five*, Mkoa wa Rukwa nao umo, lakini ninasikitika sana katika matrekta yote yaliyoletwa na SUMA JKT au makampuni mengine, tulipata matrekta matano tu. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naongelea kilimo, nigependa sana kuzungumzia mashamba yaliyochukuliwa na wawekezaji. Huu ni wizi mkubwa! Wamechukua maeneo makubwa sana, inasikitisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Malocha aliongea jana na mimi namuunga mkono leo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais alishatoa maagizo na mimi naamini kabisa kauli ya Rais ni maagizo tosha. Sasa nilitaka kujua, Waziri wa Ardhi aliyepewa jukumu hili na Mheshimiwa Rais mbele ya Wabunge waliokuwepo kwenye kikao hicho mpaka leo haijatekelezwa. Sasa nilitaka kujua hii kauli ya Rais nani anatakiwa aitekeleze? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua tu hatima ya hawa walioathirika na shamba hili, tumekuwa tunawadanganya kila siku; kila tukienda tunapeleka ripoti kwamba tumeanza kulishughulikia. Alipokuja Katibu Mkuu akaahidi na yeye kwamba shamba hili litarudi. Sasa nataka kujua kama hili shamba ni hadithi turudi kwa Wananchi tukawaambie jamani haiwezekani kuliko kuwa na matumaini kila siku ambayo hayapo. Kwa hiyo, naomba sana, shamba hili ni kero kubwa. (Makofi)

Hatuzungumzii shamba moja, Sumbawanga kuna mashamba mawili makubwa ni sawasawa na Wilaya mbili, leo hii wanamiliki watu wachache na sasa hivi mlikuwa mnapiga kelele za Wafugaji na Wakulima. Kwa nini msichukue mashamba haya? Mtu mwenye ng'ombe elfu moja wagaiwe eneo la ng'ombe elfu moja na maeneo yanayobaki wapewe hawa Wafugaji wadogo wadogo tutapunguza kero hii. (Makofi)

Leo hii nasikia Mbunge mwingine analalamika anataka mbuga za wanyama zipunguzwe au Hifadhi ya Taifa ipunguzwe; mashamba yapo makubwa sana wanashika watu wachache hebu chukueni. Mheshimiwa Waziri Mkuu, chukueni hatua ngumu tunyang'anye mashamba haya ambayo hayajaendelezwa. Ni aibu kubwa, ukifika Sumbawanga kila eneo limezungukwa na watu wawili tu, wakulima wangu hawana pa kulima, watoto wanashindwa kuwasomesha, matokeo yake wamekuwa vibarua na bahati mbaya wakikatiza kutafuta *shortcut* wanafungwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nina wafungwa 50, wamefungwa kwa sababu ya kukatiza tu kutafuta *shortcut* kwenda kwenye maeneo mengine hususan kufuata hospitali. Nikuombe tu Mheshimiwa Waziri, ninaamini kabisa wewe ndiye Waziri Mkuu, umewasimamia Mawaziri wote, hii kauli ya Rais naomba uifuatilie sana. Tunaomba uwarudishie shamba hawa Wananchi. Ninasema hivyo kwa sababu Tanzania nzima, mashamba yote makubwa wamechukua watu wachache, wameenda kukopea kwenye mabenki, matokeo yake yameachwa mapori tu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee uwanja wa ndege. Uwanja ule mpaka leo tuna hadithi tu, bajeti imepita, wale ambao wanatakiwa kulipwa fidia mpaka leo. Nyumba zinapanda gharama kubwa, leo hii watakuja kupewa fidia za mwaka juzi, hawawezi kujenga tena nyumba. Kwa hiyo, anapokuja Waziri wa Uchukuzi aje atupe jibu hili amefikia hatua gani?

Jambo la nne nilitaka niongelee *NFRA*. Watu wamefilisika, *transportation* wamefilisika, mpaka leo mwezi wa nane, wa tisa, hawajalipwa hata shilingi; wanadaiwa kwenye mabenzi na kila kona mpaka kuna wengine wamenyang'anywa magari na kisa ni *NFRA* haijawalipa. Tukimuuliza Waziri wa Kilimo anasema pesa imetoka, lakini mpaka dakika hii naingia Bungeni, hakuna msafirishaji hata mmoja aliyelipwa hata shilingi moja. Mnaturudisha nyuma, tunapenda kufanya biashara na Serikali, matokeo yake Serikali inawarudisha nyuma wafanyabiashara wetu, hatutaweza kuendelea. Nitamwomba Waziri wa Kilimo akija hapa atupe majibu tusamehe, tuendeleo kudai au tujue tumedhulumiwa moja kwa moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea Manispaa yangu ya Sumbawanga Mjini. Naomba nimshukuru sana aliyekuwa Waziri wa Fedha, Marehemu Mheshimiwa Mgimwa, nilimwomba shilingi milioni 250 kwa ajili ya kununua magari ya taka, alinipatia fedha zile. Fedha zile zimeenda kwenye Manispaa yangu zimechakachuliwa! Sasa naomba nitumie Bunge hili kutuma salamu zangu kule Sumbawanga Mjini kwamba, magari yaliyonunuliwa hatutaweza kuyapokea.

Magari tuliyoomba sisi matokeo yake tumezidishiwa *invoice* zile imesoma milioni 90 badala ya kusoma milioni 55. Kwa hiyo, tumeibiwa milioni 70. Naomba niseme kabisa, Mheshimiwa Waziri (TAMISEMI), nilikupa dondoo hizi, kuna kijana mmoja anaitwa Sadick, Afisa Manunuzi, yupo pale na Bodi ya Manunuzi yote imekula rushwa. Ninaomba Mheshimiwa Ghasia, lichukue hili na likiwa lina ukweli na ushahidi ninao, tia ndani wote, kwa sababu wamekula rushwa, hakuna gari la kichina linalouzwa milioni 90, hakuna gari la tani 13 linouzwa kwa milioni 85! Nimekwenda maduka yote, milioni 55 mpaka 58 pamoja na VAT. Kwa hiyo, tumechakachuliwa takribani milioni 70; huu ni wizi wa ajabu. (*Makofi*)

Naomba kama wananisikia, magari hayo na ninawaambia Wananchi wangu, hatutaweza kuyapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza, ushuru wa *NFRA* kutulipa Manispaa zetu pamoja na Nkasi, Kalambo, Kwela na Mkoa mzima wa Rukwa. Tumekuwa wazalishaji wakubwa sana lakini mpaka leo hatujalipwa.

La mwisho, nimwombe Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tumekuwa wakusanyaji wakubwa wa mazao, tumekuwa walimaji wakubwa wa

mazao, lakini wasafirishaji mwaka huu wametoka Dar es Salaam kuja kusafirisha mazao; ni aibu kubwa. Matokeo yake sisi tunalipa kodi ndani ya Mkoa Rukwa, wanaotoka Dar es Salaam hawaji kulipa kodi kule. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wapate nafasi ya kusafirisha mazao yanayokusanywa na NFRA. (Makofi)

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuamini, *keep it up*, tupo pamoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mchuchuli!

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa salama kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinanishangaza kidogo kinanifurahisha, naona Wabunge wakisimama hapa wanasifia vifaru, wanasifia magari ya kijeshi; kwanza magari yenyewe ya kizamani! Halafu vifaa vyenyewe vya mikopo hatujalipa. Nchi hii inadaiwa takribani trilioni 21, madeni ya ndani na nje, sasa tunajisifia vifaru wakati tuna Deni la Taifa kila siku linakua; tunajisifia ili iwe ni nini? Vifaa vya kizamani vile wasijisifie tunadaiwa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie kidogo kuhusu TAMISEMI. Leo tunapitisha Bajeti ya TAMISEMI kwa ajili ya Halmashauri zetu. Tunapitisha leo takribani trilioni 4.2 ambazo zinakwenda kwenye Serikali zetu za Mitaa. Katika trilioni nne tunategemea trilioni tatu tutatumia kama matumizi ya kawaida na fedha shilingi bilioni 682 zitakwenda kwenye Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka niwajulishe Wananchi kwamba, wajue hapa tunapitisha pesa kwa ajili ya mishahara na OC. Kwa hiyo, wasishangae wakiona Miradi ya Maendeleo haiendi, tunapitisha pesa na pesa nyingi inakwenda kwenye mishahara na OC, siyo za Miradi ya Maendeleo. Ndiyo maana unakuta pesa za mishahara na OC zitakuwa trilioni tatu, lakini pesa za Miradi ya Maendeleo zitakuwa takribani bilioni 600 tu. Kwa hiyo, wasishangae kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Taarifa ya CAG inaonesha kwamba, Mwaka wa Fedha 2012/2013 tulipitisha pesa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, lakini mpaka tunafunga mwaka sasa ipo wazi kabisa inaonesha takribani asilimia 38 ya pesa ya maendeleo hazijaenda kwenye Miradi yetu ya Maendeleo. Sasa tunashabikia tu lakini hiyo ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CAG anatuonesha pesa takribani asilimia 36 zimekwenda hazijatumika. Kwa nini hazijatumika? Imekuwa ni kawaida kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Serikali kila siku ikifika mwisho, bado mwezi au bado wiki tatu tunafunga bajeti ya mwaka ndiyo pesa zinakwenda kule. Sasa tunategemea ile miradi tuliyoipanga tuitekeleze kwa mwaka husika itatekelezwa vipi?

Hii ni makusudi kwa sababu huwezi kupeleka pesa kwenye Halmashauri mwisho wa mwaka wa fedha, bado mwezi, bado wiki mbili! Tunajua kuna Sheria za Manunuzi, kuna mchakati mrefu wa Sheria za Manunuzi, sasa tunapopeleka fedha mwishoni tunategemea zitatumika lini? Kwa hiyo, hawafanyi kwa bahati mbaya, wanataka zilale mwakani ziende tena, kwa hiyo, tumezoea kutumia viporo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Aeshi alikuwa anasema hapa kidogo sijui kule yamenunuliwa magari, yamechakachuliwa! Nakumbuka katika ile Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2010, mwaka jana hapa tulifanya marekebisho katika kifungu cha 60(4) kwamba, sasa zile *Tender Board* kwenye Halmashauri zetu zinavyofanyika mwishoni pale Kamati za Fedha watie baraka zao kwa kuangalia wale wazabuni ambao wana-award zile *tender* kwa ajili ya kutekeleza miradi yetu.

Katika pitapita yangu kwenye safari zangu za Kamati nimegundua sehemu nyingi bado haijatekelezeka. Sasa nataka nijue TAMISEMI nini ni kikwazo? Kwa nini mpaka sasa baada ya timu ya kufanya zabuni ikipitisha kwenye Halmashauri haiendi kwenye Kamati ya Fedha ili Waheshimiwa Madiwani watie Baraka zao waone katika haewa yupi anaweza kufanya vizuri katika Miradi yetu na yupi hawezi kufanya vizuri? (*Makofi*)

Suala hili limekuwa na kigagaziko, tulitarajia ianze kutumika mwaka jana Desemba lakini mpaka sasa haijaanza kutumika. Kwenye manunuzi ndiyo kunatuharibu kidogo katika Halmashauri zetu, kwa hiyo, mimi nawaomba sana tuangalie vizuri Sheria ya Manunuzi na hasa hii tuliyoirekebisha humu ndani, kile kifungu cha 60(4) ili sasa Waheshimiwa Madiwani kupitia Kamati ya Fedha, waweze kutia baraka na kazi ziende vizuri kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongelea kuhusu suala la makusanyo ya mapato kwa kutumia Mawakala. Bado kuna changamoto kubwa sana katika Halmashauri zetu hasa katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CAG anatueleza kwamba takribani shilingi bilioni 6.7 Mwaka wa Fedha 2012/2013 zimeshindwa kukusanywa kwa kutumia Mawakala. Sasa mimi nawaomba TAMISEMI, kwa sababu ninyi ndiyo walezi wa Halmashauri zetu, tuliangalie hili kwa jicho la karibu sana. Kwa sababu kama tunapoteza trilioni 6.7 zingeweza kuleta manufaa makubwa sana katika Miradi yetu ya Maendeleo hasa katika Halmashauri zetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Lipo tatizo saa zingine unakuta pesa zinakusanywa lakini haziwi *banked*; kwa mfano, CAG anatuambia kuna takribani milioni 500 zimekusanywa hazijawa *banked*. Sawa mimi najua sisi Madiwani tunahusika moja kwa moja katika Halmashauri zetu, lakini TAMISEMI kama walezi wetu kidogo mtuungezee nguvu hasa katika suala la mapato, haiwezekani watu wanashindwa kukusanya vizuri. Kwa hiyo, mimi naomba kidogo mtusaidie hapa kama walezi ili tupandishe mapato tuweze kujisaidia vizuri kule chini.

Mimi naona mfano hata katika Halmashauri yangu ya Rufiji, unaweza kumuweka Wakala leo mnapata naye labda shilingi milioni 300, akikaa wiki tatu atakwambia haikusanyiki. Kwa hiyo, kidogo kuna matatizo. Tupeni mwongozo tuone tunaendaje tuweze kukusanya zaidi kwa ajili ya Miradi yetu ya Maendeleo hasa kwa kutumia *own source* zetu. Mwenyekiti wa TAMISEMI kasema hapa, tunatarajia labda tuifanye asilimia 60 ya mapato ya ndani iende kwenye Miradi ya Maendeleo kwenye Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutakusanya vizuri sidhani kama tunaweza kupata zile asilimia 60 ambazo tunazitarajia. Kwa hiyo, tuliangalie vizuri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 52, aliongelea suala la Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa. Akaelezea pesa ambazo zimekusanywa katika mwaka wa fedha uliopita na sehemu ambazo wamewekeza. Mimi naomba nishauri kidogo hapa; hizi pesa tunazikusanya katika Mfuko wa Serikali za Mitaa, tujitahidi ziwanufaishe katika Halmashauri zetu kwa sababu ndiyo wachangiaji. Halmashauri ndiyo inachangia pesa kwenye Mfuko huu wa Serikali za Mitaa, lakini wao wamekuwa hawanufaiki moja kwa moja. Tunajenga haya maghorofa ambayo tunayapangisha, sijui vitega uchumi, lakini te, wale Wanachama ambao wanaingiza pesa kwenye ule Mfuko wananufaika vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaweza tukatumia hizi fedha za Mfuko wa Pensheni za Serikali ya Mitaa labda katika Halmashauri ambao zina matatizo ya nyumba, tukawasaidia hata kukopesha nao wakajenga nyumba kwa ajili ya watumishi ili na wao waweze kunufaika moja kwa moja na huu Mfuko. Tusiweke tu maghorofa Dodoma, Dar es Salaam, lakini wale wanaochangia kutoka katika Halmashauri husika hawanufaiki nazo. Kwa hiyo, naomba hili tuliangalie ili sasa watu ambao wanachangia kwenye Halmashauri zetu katika ule Mfuko waweze kunufaika na hizi pesa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika *speech* yake ukurasa wa 28 aliongelea hapa, kwamba, kuna pesa takribani bilioni tano zimekwenda kwenye Mfuko wa Wanawake. Mimi ninataka niulize wanawake gani? Maana imekuwa kawaida katika Bunge hili kusema pesa zimeenda

kwenye Mfuko wa Wanawake au Vijana lakini ukienda kule kabisa kwenye *ground*, huoni pesa iliyoenda! Halmashauri ngapi zimepelekewa pesa za Mfuko wa Wanawake katika Mwaka wa Fedha 2012/2013?

Mimi nimetembea na Kamati yangu ya LAAC, Halmashauri nyingi hazijapata hizi fedha za Mfuko wa wanawake. Sasa hizi bilioni tano kapewa nani? Tumezoea hapa, pesa za JK zimeliwa, Mfuko wa Wanawake ukienda anapewa mtu ambaye wala hahusiki. Kigezo gani kinatumika kugawa fedha hizi? Tunataka tujue hizi bilioni tano zimekwenda kwenye Halmashauri ngapi Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpaka leo unatuletea takwimu nzuri hapa? Watu wanafurahia Mfuko wa Wanawake; wengine hata hawajui Mfuko wa Wanawake umemnufaisha nani!

Kwa hiyo, mimi nataka nijue Halmashauri ngapi zimepata pesa hizi bilioni tano kwa sababu kila Halmashauri unapata milioni nane? Mimi nilizoziona kwa hesabu zangu hata Halmashauri mia hazijafika kupata hizi pesa, nani kapata milioni tano? Mimi naomba nepate jibu kamili kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, ajiandae Mheshimiwa Mwanjelwa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Taarifa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Taarifa!

T A A R I F A

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyemaliza kuongea hivi sasa alizungumzia vifaa vya jeshi kwamba ni vibovu, chakavu na tumepewa kwa mikopo. Niseme tu kwa mujibu wa Sheria za Manunuzi za nchi hii, hatuwezi kununua ama Serikali haiwezi kununua kifaa chochote kibovu ama kilichotumika. Vifaa vile ni vipya vilivyonunuliwa kuanzia baada ya Vita vya Kagera, mpaka hivi sasa vinafanya kazi vizuri na hatujakopa na kama tumekopa tutalipa. Kukopa si ajabu, kwa sababu ukiaminika utakopeshwa, ndiyo maana hata yeye amekopeshwa gari na Bunge na mpaka leo hajamaliza kulipa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchuchuli, taarifa hiyo.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeikataa kwa sababu mpaka mwanangu anadaiwa katika Deni la Taifa. *(Kicheko)*

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Silinde kaa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Tulibadilisha sheria akumbuke.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o,
Mheshimiwa Mwanjelwa ajiandae.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Naanza kwa kusema kwamba, hakuna nchi yoyote Duniani hapa ambayo haikopi na kama haikopi ina maana hakuna maendeleo. Mtanzania yeyote anatakiwa aisifie nchi yake na kutoa kasoro siyo kila kitu ni kasoro. *(Makofi)*

Naanza kwa kusema naipongeza Serikali yangu, ambayo inafanya kazi nzuri hasa katika barabara. Napoongeza ujenzi wa Barabara ya Iringa - Dodoma na barabara hiyo tumeitumia hata kutafuta kura Kalenga, ndiyo tuliyokuwa tunapita Wabunge arobani tukitokea hapa. Leo tunasema hakuna chochote kilichofanyika tumechoka, tupo macho na tutasimama imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema kwamba, tunashukuru kwa barabara ambazo zinaendelea kujengwa, lakini bado tungependa kuona Barabara ya Iringa mpaka *Ruaha National Park* inajengwa kwa kiwango cha lami ili tuweze kupata watalii. Watalii wengi hawawezi kuja kwa sababu hatuna miund mbinu mizuri, barabara yetu haijajengwa kwa kiwango cha lami. Naomba Waziri wa Ujenzi atakapokuja atueleze barabara hiyo itakamilika lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuhusiana na barabara hiyo, nizungumzie kwamba tunahitaji barabara ziwe nzuri. Mkoa wa Iringa ndiyo wenye *National Parks* kubwa hapa nchini, lakini ndiyo tunapata watalii wachache kwa sababu ya miundombinu. Vilevile tuna utalii wa utamaduni, naomba pia Waziri wa Maliasili akija atueleze kwa sababu utalii wa utamaduni pia unaingiza fedha. Mkoa wa Iringa tuna makabila ambayo yana historia kubwa, tungependa utumike pia utalii wa utamaduni ili tuweze kuingiza kipato. Wahehe, Wabena, wana mila nzuri sana na Wakinga ambazo zinaweza kutumika kama kivutio cha utalii kwa mila zetu ikiwemo pia na vyakula vyetu vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie maji. Tatizo la maji ni sugu hapa nchini kwa Mikoa yote. Akina mama wanateseka usiku kucha, wengine hata ndoa zao zimevunjika kwa sababu ya kuamka usiku wanashinda

kisimani. Tatizo la maji lazima litafutiwe ufumbuzi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kuna vijiji ambavyo vililingizwa katika *Big Results Now*. Vijiji hivi vilisaini mkataba, Halmashauri ilisaini mkataba kwa ajili ya Vijiji vya Indingudu, Alizanga, Kikombo, Isupiro, Lumuli na Itengulinyi na tulisaini kwa gharama ya bilioni tano, lakini mpaka sasa hivi ni shilingi milioni 900 tu zimeshatolewa. Sasa hivi huo Mradi umeshasimama, karibu wafadhili wanajitoa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuomba, tupewe hizo fedha ili tuendeleo kuwapatia Wananchi maji, kwa sababu wakijitoa itakuwa gharama kubwa sana kuweza kupata Mradi. Yawezekana pia ikawa gharama kwa Halmashauri kulipa kwa sababu ni mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni maji mjini. Bodi ya Maji Safi na Maji Taka Manispaa ya Iringa (*IRUWASA*), imekopwa fedha nyingi sana na Taasisi za Serikali, kiasi kwamba, sasa inakuwa tatizo kulipia gharama za umeme na madawa. Tuna hofu tunaweza kushtukia tunaanza kukosa maji. Tunaomba Serikali ilipe madeni ya Magereza na Polisi kwa sababu imeachiwa Polisi Mikoa ilipe, haina uwezo wa kulipa. Tunaomba Hazina ichukue hayo madeni ilipe. Hii nadhani siyo kwa Halmashauri yangu tu na Halmashauri zingine pia madeni ni makubwa. Sasa sisi karibu tutakosa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwatie moyo Wananchi wa Manispaa ya Iringa kwamba, kinu chetu karibu kitaanza kusaga kama alivyoeleza Naibu Waziri wa Kilimo. Karibu tani elfu kumi za nafaka zitasagwa kwa majaribio katika kinu chetu na nina hakika tutapata ajira hapo mjini. Naomba isije ikawa ni majaribio na tukaacha kusaga, tunaomba kinu kisage na Wananchi wetu waweze kuuza mahindi yao kwa soko zuri ili tuweze kuinua uchumi wa Watanzania na hususan Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hali ya UKIMWI katika Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa; Kamati yetu imezungumzia tatizo lilivyo na tukaomba mikakati iwekwe lakini hakuna mkakati wowote licha ya jitihada ambazo tumepongeza mikoa hii. Watumishi wa Afya hawapo kwenye vituo vya afya na zahanati. Wananchi wamejitolea wamejenga zahanati, lakini watumishi ni wachache. Hivi kweli huduma zitategemaa kwenye mikoa yenye matatizo makubwa namna hii? Mikoa hii miwili ina mwingiliano mkubwa wa kibiashara, Wananchi ni wengi sana wanaoingia kwa ajili ya biashara, barabara kuu inapita pale. Mikoa hii miwili inatakiwa iwekewe mikakati mahususi, tunarudia kusema na tunaomba turudie kusema hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mufindi hususani Wodi ya Wazazi, Wodi hii imeshajengwa imekamilika, tunaomba Serikali itusaidie kuweka vifaa ili akina mama wajawazito waweze kujifungua kwa usalama, kwa sababu

wanalala wawili wawili kwenye wodi ndogo, wodi kubwa imejengwa vifaa vinatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira ni tatizo kubwa sana na wenzangu asubuhi wameongea. Sasa hivi kuna majiko yanayotumia kuni kidogo na mkaa kidogo ya Taasisi na yale ya Wananchi. Tunaomba Serikali ipunguze kodi kwenye haya majiko kama tulivyopunguza kwenye vifaa vya umeme jua ili Wananchi wengi waweze kutumia na waweze kupunguza gharama ya matumizi ya mkaa na kuni na hatimaye tutakuwa tumepunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la lishe, ninapongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya ili kuondokana na utapiamlo hapa nchini. Ninashangazwa kuona Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha SUA, wanaochukua fani ya *Home Economics and Nutrition* wamekataliwa kupewa mikopo, wamepewa mikopo wale wanaochukua fani ya kilimo, wameambiwa fani ya lishe siyo muhimu haipo kwenye *Big Results Now*. *Big Results Now* zipi ambazo haziangalii afya? Hakuna *big results* bila kuwa na lishe bora. Mwaka huu wameingia wanafunzi wachache kwa sababu ya kukosa ufadhili, Waziri Mkuu suala hili naomba uliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, ajiandae Mheshimiwa Kitandula.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Jehova kwa kunifanya hivi nilivyo. Vilevile ninaipongeza Hotuba ya Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI pamoja na Kamati zote ambazo zimewasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapa pole ndugu zangu wa Kyela, kwa mafuriko makubwa ambayo yamewapata na mimi ninasema tupo pamoja na tunaendelea kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita moja kwa moja kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Halmashauri zetu, Manispaa na Majiji ndiyo injini ya maendeleo ya Taifa letu kwa Mfumo wa Serikali yetu. Kitu cha ajabu na cha kushangaza sana, kwenye Serikali za Mitaa ambako ndiko kwenye Halmashauri zetu, ndiko ambako kumejaa udhaifu, mianya ya rushwa, *ten percent* zimezidi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

ukusanyaji mapato, utolewaji wa *tender* mbalimbali, *procurement*, kwa kweli hauko *transparency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Kama mfumo ni mbovu tufanye maamuzi magumu, tubadilishe kuliko kuendelea kulalamika kila siku, hii inakuwa haileti tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, kule kwangu Mbeya kuna suala zima la barabara. Ninazungumzia barabara ile ya *by pass* ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anaifahamu, Dkt. Magufuli anaifahamu, barabara ya kutoka Uyole hadi Mbalizi *by pass* na hili jambo kwenye bajeti ya mwaka jana nililizungumza kwa uchungu sana. Nikatolea mfano wangu mimi mwenyewe nilipopata ajali pale lwambi mwaka juzi. Haya magari makubwa tunayoyasema kwamba yapite kwenye ile barabara ya zamani kutoka Uyole hadi Mbalizi kwa ajili ya kupunguza foleni ajali na kadhalika, lakini hili jambo pamoja na kwamba tumelizungumza sana mpaka kwenye vikao vyetu vya *Road Board* mara nyingi sana halijapata tija. Wizara ya Ujenzi patachimbika hili jambo lisipokuja na tija, tunahitaji maelezo kwa kina na Mheshimiwa Waziri Mkuu akisimama hapa atuambie lina *kick off when*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, wadogo zangu wameongea; Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Sugu, mimi naendelea kupata meseji Watumishi wa Halmashauri, Walimu Mkoa mzima wa Mbeya hawajapata mishahara yao mpaka dakika hii. Hivi mnategemea wataishije Walimu hawa wa Mkoa wa Mbeya? (Makofi)

Waziri wa Fedha ninashukuru sana rafiki yangu pale amesimama amesema mishahara imetoka Hazina tangu tarehe 24 Aprili, lakini meseji bado zinaendelea kumiminika kwamba mishahara yao hawajaipata. Kwa hiyo utaratibu maalum ufanyike ili hili jambo liweze kutafutiwa ufumbuzi. Mimi naomba niwaambie ndugu zangu wa Mbeya hususan Walimu, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshasema pesa zimeshatolewa Hazina, naomba mvumilie mwezi huu maana yake huu ni mwezi wa pili sasa, mishahara yenu itafika naomba tuwe na subira kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri na Majiji, tumesikia sana kwenye Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI hapa akizungumzia juu ya ukusanyaji wa mapato. Ninaomba kuishauri Serikali kitu kidogo; zile Halmashauri ambazo hazijafanya vizuri kitafutwe chanzo ni kwa nini hazijafanya vizuri. Halmashauri hizi zipewe adhabu, tusilalamike tu kwamba hazijafanya vizuri, kitafutwe chanzo ni kwa nini. Tukishapata chanzo pia tuweze kuwapa adhabu waadhibiwe. Vilevile Halmashauri ambazo zimefanya vizuri zipewe *incentives*, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na Mbunge wa Chunya, Jimbo la Mkwajuni Songwe, Wilaya ya Chunya ama Halmashauri ya Chunya imefanya vizuri imepata Hati Safi. Sasa watu kama hao wapewe *incentives* tusiwaangalie tu ili Halmashauri zingine ziweze kuiga mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia, *initially* mwaka huu unapaswa kuwa ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa Serikali za Mitaa. Mchakato wa Katiba unaendelea, ni kweli tutarudi hapa kwenye Bunge la Katiba. Kuna kitu kinaitwa *Referendum*, kuna kitu kinaitwa kuboresha Daftari la Wapiga Kura, ningeomba Waziri Mkuu atakaposimama hapa ku-*wind up* atuambie huu uchaguzi Mkuu wa Serikali za Mitaa mwaka huu utafanyika ama hautafanyika. Wananchi wanataka kujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilichangie, ninaipongeza Serikali yangu, kule Mbeya tumepewa Uwanja wa Kimataifa wa Songwe. Ndege mbalimbali zimeanza kufanya kazi pale na hii ni kweli itaongeza biashara na utalii. Naomba sana tuwekewe angalau *traffic lights* na hili nilishalizungumza mara nyingi, pamoja na *round about* pale eneo la Mafiat, kwa sababu Jiji pia linapanuka kutokana na ndege mbalimbali ambazo zinatua pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa kugongewa kengele, lakini naomba haya niliyozungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, akisimama hapa tafadhali sana atulettee majibu ambayo yatakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninaunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Sara Msafiri ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuiunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naiunga mkono kwa sababu inanipa matumaini kwamba, mambo yaliyoanza kutekelezwa katika Wilaya yangu yatakamilika na hata yale mengine ambayo tunayatarajia katika bajeti hii yatafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa Miradi ya Maji ya vijiji kumi, ambayo yote katika Wilaya yangu inatekelezwa. Ninaishukuru sana Serikali kwa sababu tatizo la maji lilikuwa kubwa mno. Mradi katika Kijiji cha Kiluluduga, Mradi katika Kijiji cha Doda, Bwagamacho, Mbuta, Bamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mwarongo, Parungu Kasera, Mapatano, yote hii ipo katika hatua za utekelezaji. Mradi mmoja uliobakia wa Mwakijembe mkandarasi yupo kwenye eneo lile, lakini umesimama tu kwa sababu ya mvua zinazoendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, tunaomba fedha zile zitolewe kwa wakati ili wakandarasi wale wasivunjike moyo waweze kukamilisha Miradi ile kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiishukuru Serikali katika eneo hilo, naiomba Serikali ikumbuke vilevile kwamba, tuna changamoto kubwa ya maji katika Mji wetu Mkuu wa Wilaya, Mji wa Kasera. Mji ule hauna maji, tulianzisha Mradi wa muda mfupi wa dharura, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, alitupa shilingi milioni mia mbili ambazo tumeweza kutekeleza Mradi ule. Rai yangu kwa Serikali yangu, Mradi ule wa chanzo cha Kinyatu uwekewe fedha katika mwaka huu wa fedha unaokuja ili maji yaweze kupatikana katika Mji wetu ule na Mji uweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana *National Housing*, kwa kutujengea nyumba katika Mji wetu ule mpya, lakini wamefanya kazi katika mazingira magumu sana. Jambo la kufurahisha ni kwamba, nyumba zote zimekamilika na zimekuwa *over subscribed*. Mahitaji bado ni makubwa na yapo mashirika mengi yaliyoonesha nia ya kuja kutujengea Mji wa Kasera. Naomba mtukamilishie suala la maji ili kazi yetu iweze kuwa nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye eneo la ardhi. Wilaya ya Mkinga ni miongoni mwa Wilaya zenye tatizo la migogoro ya ardhi. Nimefarijika niliposikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba ninukuu ukurasa ule wa 48 anasema: "Katika mwaka 2014/15 Serikali itatoa kipaumbele katika Sekta ya Ardhi hasa kushughulikia maeneo yanayolenga kutatua migogoro ya ardhi kama vile upimaji wa mipaka ya vijiji, kutoa hati miliki na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limenipa faraja kwa sababu Wilaya ya Mkinga tuna tatizo la migogoro ya ardhi, ambalo tumekuwa tukiliripoti kwa muda mrefu. Tangu mwaka 2007, Uongozi wa Halmashauri umekuwa ukiwasiliana na Wizara husika ili wanaohodhi ardhi kule, wenye mashamba ambayo hayafanyiwi kazi, hati zile ziweze kufutwa na Wananchi waweze kupatiwa ardhi, lakini hilo halijafanyika. Nilipoingia Bungeni hii ilikuwa ni ajenda yangu kubwa, nimefuatilia kwa karibu, lakini jambo hili bado haijatekelezwa. Hofu yangu ni kwamba, jambo hili lisipochukuliwa kwa umuhimu mkubwa, linaweza kutuletea matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali tulipojenga leo Makao yetu Makuu ya Wilaya ni eneo lenye mgogoro. Shamba la Kilulu ambalo lina ukubwa wa heka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

2696 lina mgogoro wa umiliki, lakini hapa ndipo mahali ambapo tumeweka Makao yetu Makuu ya Wilaya, tunaomba jambo hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba la Moa lenye ukubwa wa ekari 15,739 linamilikiwa na mtu binafsi, lakini ndani ya shamba hilo tuna vijiji vinne ambavyo vina usajili. Jambo hili limepelekwa kwa Wizara husika tangu mwaka 2007 na mimi nimeliandikia, nimelizungumzia, hakuna utekelezaji. Shamba la Mwele ambalo lipo katika eneo la Mji Mdogo wa Maramba, Wananchi wana tatizo kubwa la ardhi, shamba lile lina hekta 964, halitumiki. Kwa miaka minne, mitano, iliyopita shamba lile halitumiki, Wananchi wanaliangalia, wana tatizo la ardhi; tushukuru Mungu tu kwamba Wananchi wale wamekuwa wastaarabu, hawakuvamia shamba lile. Tunapeleka meseji gani kwa shamba ambalo limekaa *idle*, Wananchi wana shida ya ardhi na sisi tunashindwa kufanya maamuzi ya kuwapa ardhi ile? Nadhani hii siyo sahihi, tufanye maamuzi tuwaondolee adha Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wangu wa Mwakijembe, eneo ambalo lipo katika mpaka na Kenya, tuna tatizo pale; Wananchi wa Kijiji cha Mkota kitongoji cha Kimuni wapo kabla ya uhuru katika eneo lile, leo hii wanaambiwa waondoke kwenye eneo lile kwa sababu ni eneo tengefu. Hii siyo sahihi hata kidogo. Tumeleza juu ya jambo hili, hakuna utekelezaji, tunaomba Serikali ilifanyie kazi jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka nitoe elimu kidogo kwa wale wenzetu wanaoshangaa maonesho ya kivita, jambo hili linafanyika ulimwenguni kote.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa ninamwita Mheshimiwa Sara Msafiri, ajiandae Mheshimiwa Kibona na Mheshimiwa Nassari.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa kudhibiti mfumko wa bei kutoka asilimia 9.8 mwaka 2013 mpaka asilimia 6.1 mwaka 2014. Ninasema hivyo kwa sababu imesaidia sana kupunguza kupanda kwa bei za bidhaa za nafaka hasa mchele na mahindi, ambacho ni chakula

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kikubwa cha Watanzania. Kwa hiyo, napenda kutoa pongezi kubwa sana kwa Serikali ya Chama cha Mpinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa pongezi kwa ukuaji wa uchumi, tumetoka asilimia 6.4 mwaka 2011 mpaka asilimia 7.0. Haya ni mafanikio makubwa, tumeweza kuishinda nchi ya Kenya, nchi ya Uganda na nchi nyingine za Afrika. Kwa hiyo, tunasema kwamba, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Hata kama wapo wanaosema kwamba Serikali haifanyi jambo lolote, lakini wapo watu ambao wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kuwa hii nchi inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, Sekta ambazo zimechangia sana ukuaji uchumi ni zile sekta za huduma tu; huduma za kibenki, huduma za mawasiliano, viwanda na ujenzi. Sekta ambayo inachukua Watanzania wengi, Sekta ya Kilimo, ambayo ina wakulima asilimia kama 80 ya Watanzania, Sekta hii inakua lakini siyo kwa kasi ile ambayo Watanzania wanaitarajia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Serikali yangu sikivu, ifanye tathmini upya, asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo. Wakulima wanalima sana, ukipita maeneo ya kilimo, ukienda Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine, wakulima wanalima na wanavuna sana. *(Makofi)*

Changamoto zilizopo lazima Serikali ijipange upya ikae kimkakati kwenye suala la uwekezaji na uwezeshaji. Wakulima wanakopwa mazao yao na Serikali, wakulima wanakopwa mazao yao na Vyama vya Ushirika. Wakulima wanakopwa mazao yao na Sekta Binafsi ambazo zinaingia kwenye biashara ndogo ndogo na kuwadanganya. Vilevile kuna Sheria kandamizi, kwa mfano, Wilaya ya Mvomero, kuna kiwanda cha sukari pale. Tuna kiwanda kimoja tu.

Wale wakulima wa Mvomero wamelima miwa mingi tu, lakini kile kiwanda hakina uwezo wa kununua miwa yote. Wananchi wanapotaka kujenga kiwanda kingine, wakienda kwenye Wizara ya Uwezeshaji, wanaambiwa Sheria hairuhusu kujenga kiwanda kingine. Kwa hiyo, unakuta miwa ile inaharibika, Wananchi wamechukua mikopo mikubwa benki, wanadaiwa na wanafilisiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nasema kwamba, yapo mambo mengine ambayo hayahitaji fedha, ni suala la maamuzi tu. Kama ni Sheria zinasema kilomita 40 kuwe na kiwanda kingine, wakulima wamelima kilimo chenye tija, wanazalisha zaidi. Sasa kwa nini tuendelee kuwa na kiwanda kimoja kinachowanyonya wakulima, wanashindwa kuuza miwa yao kwa faida, wawasomeshe watoto wao shule nzuri, wajiunge na huduma za afya, ili kasi ya maendeleo ikue. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kabisa kwamba, kwenye Sekta ya Kilimo kuna haja ya kuangalia njia nyingine ya kuisaidia hii Sekta. Tusijikite tu kwenye masuala ya fedha, lakini kuna masuala tunasema ni ya *management*, tukae tuangalie tufanye hayo mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwakopa sana wakulima nafaka. Sawa, tunasema wanaweka vyakula kwenye maghala, lakini muwalipe basi. Sasa Wananchi wanaandamana, wanadai hela, wanaidai Serikali; tunawarudisha nyuma Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye migogoro ya wakulima na wafugaji. Wabunge wenzangu wameongea sana mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie tatizo kubwa hatujawa na matumizi bora ya ardhi. Tutakuwa tunakamatana uchawi kila siku; mwenye tatizo mkulima, mwenye tatizo ni mfugaji, mwenye tatizo sijui kiongozi gani; kama ardhi yetu haitapimwa tukawa na matumizi bora ya ardhi, kila siku tutaendelea kuwa na migogoro. *(Makofi)*

Wakulima wanauwana na wafugaji, maandamano wamefanya, wamewafukuza mpaka viongozi, wanaoenda kwenye mikutano yao hawawataki. Kule Mvemero walishamfukuza mpaka Mkuu wa Wilaya. Kule Mvemero walishafunga mpaka barabara wanamtaka Mkuu wa Mkoa, lakini atafanya nini kama ardhi haitapimwa? Lazima tukae tutoe sasa matumizi ya ardhi, eneo gani la wakulima, eneo gani Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niombe sana Serikali yangu, tukae tuamue na mimi nasema kwamba, tulikosea sana wakati wa kuweka Vipaumbele vya Taifa, kuacha suala la ardhi kutokuwa kipaumbele cha nchi. Kwa sababu shughuli yoyote ya uwekezaji lazima ihitaji ardhi. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba, lazima suala la ardhi sasa liingie kwenye kipaumbele. Nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 46 na 47, inaonesha juhudi kidogo za kutaka kupima ardhi, lakini kasi ile haitoshi. Kupima viwanja 5,000 tu na kuwa na mpango wa kupima maeneo laki moja tu kwa nchi hii, ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tutenge hela, mtuambie inahitajika kiasi gani cha fedha kupima ardhi ya Watanzania ili tujue sasa kama Mkoa wa Morogoro ni ghala la chakula, watu walime au wafuge. Kwa sababu huwezi ukalima hapa heka 80, halafu jirani yako ana mifugo 7,000 hana kwa kulishia malisho, mtagombana tu! *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi niombe sana, kuna Miradi mingine tunaiona ya TASAF ya kuwezesha kaya maskini kuwajengea uwezo kidogo kupata hela na kuanzisha

miradi midogo midogo. Hawa wafugaji hawana kaya, hawana makazi, wanahamama tu, basi tuiombe Serikali sasa ije na mpango mpya wa kuzisaidia jamii ambazo zina rasilimali lakini hazina uwezo wa kukaa na kubuni Miradi na kuwa na eneo moja la kujiendeleza. Kwa hiyo, unakuta kwenye maeneo kwa mfano ya Kishapu na Meatu kule Shinyanga, mtu mmoja ana mifugo 7,000. Serikali kwenye Wilaya ya Meatu kila mwaka inatoa mahindi siyo chini ya milioni 500 kuwasaidia zile familia, lakini wana mifugo huko wamekaa nayo 3,000 mpaka 5,000. *(Makofi)*

Hawa wanatakiwa waelimishwe tu ufugaji bora wa kisasa, wajengewe majosho, wafuge kisasa. Kuhama hama wanakuja Morogoro, inaleta migogoro isiyokuwa na msingi. Kwa hiyo, mimi niombe kabisa Serikali ihakikishe ardhi inakuwa kipaumbele cha kwanza kwenye eneo lolote la uwekezaji. Kwa hiyo, lazima ardhi yote ipimwe na kila mtu aamue sasa kama anaenda kulima aende sehemu ya kilimo, kama anaenda kufuga aende eneo la wafugaji. Tukiwaacha Wananchi wenyewe hivi watakuwa wanagombana, migogoro itakuwa mingi na maafa yatakuwa mengi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana suala la ardhi lipewe kipaumbele cha kutosha. Mwisho kabisa, pesa zinazotengwa kwa vijana hazitoshi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kibona!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa sababu ya muda mfupi, kumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kwa jinsi anavyoendelea kulifanya Jiji la Mbeya kuwa safi. *(Makofi)*

Nampongeza na namshukuru Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Sote tumetoka Dar es Salaam tumeona mabadiliko makubwa. Tumpongeze kwa kazi nzuri aliyofanya, aendeleo hivyo, sisi wageni tunapofika pale, kwa kweli tupate nafasi ya kupita na magari yetu katika Jiji la Dar es Salaam. Hongera sana Mheshimiwa Sadick. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze machache kuhusu Ileje. Ileje kuna maafa, kama alivyosema Waziri wa Ujenzi, Wilaya ya Ileje tuna maafa. Barabara kutoka Keikei kwenda Luswisi kwenda Lubanda –Sange - Katengele mpaka Kalembo Ibungu, imefungwa kwa sababu milima imeteremka imekaa barabarani, hatuna mawasiliano. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, nawashukuru kwa kulifahamu hilo, naomba ahadi kwamba Serikali italishughulikia mara moja iweze kutimia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafa yale yamesababisha wakazi wa maeneo ya Luswisi sasa hivi wameshindwa kukaa kwenye nyumba zao, nyumba zimepata ufa na wengine wamehama majumbani mwao wametafutiwa mahali pengine kwa kukaa; ni maafa kama yalivyokuwa kule Dar es Saalam na Kyela na sehemu zingine. Naomba Serikali ilichukue hilo, wahusika wote walisikie, hatua zichukuliwe tuwasaidie ndugu zetu wa pale Ileje. *(Makofi)*

Naomba kutoa pongezi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Mwaka jana nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi juu ya barabara ya kutoka Mpemba kwenda Isongole akaniahidi mwaka huu lazima kuna jambo litafanyika. Nasubiri kauli ya Waziri na ninaamini atakuwa mwaminifu, Barabara ya Mpemba – Isongole itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kama sehemu ya shukrani. Maeneo ya Ibaba na Malangali hawana mawasiliano ya simu. Nashukuru kwenye Mpango wa Wizara tumepata mnara pale Ibaba, tumepata mnara pale Malangali. Ahsante sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu maji. Kweli kama wasemaji wengine walivyosema, Serikali imejitahidi sana kutekeleza Miradi ya Vijiji Kumi, lakini kuna tatizo la hawa Washauri wa Miradi *(Consultancy)*. Hawa watu nilikuwa nafikiri niishauri Serikali; hivi hawa Washauri wao kozi hizi wanasoma wapi? Hatuwezi kuwatumia Wataalam wetu katika Halmashauri zetu wakasimamia hii Miradi? Mara nyingi pesa nyingi zimepotea na Miradi haijakamilika, hatuwezi kuwabana wale Washauri wa Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iliangalie upya jambo hili. Pesa nyingi wanalipwa Washauri, lakini Miradi haikamiliki, Miradi inakuwa katika viwango hafifu. Naomba tushirikiane katika hili, Waheshimiwa Wabunge tuangalie ni namna gani Miradi yetu inaweza kukamilika katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze tena Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Wilaya ya Ileje tumelia sana juu ya Hospitali moja ya Isoko, kwa miaka mingi haijawahi kupata gari la kubeba wagonjwa *(ambulance)*. Tunashukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweza kufanya mambo makubwa, sasa hivi tuna gari la kubeba wagonjwa pale Hospitali ya Isoko. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia kwa ajili ya Miradi. Mradi wa umeme kupitia REA; wengi walifikiri ni utani, wengi walibeza, lakini nashukuru Chama cha Mapinduzi lani yake inatekelezwa kule Ileje. Maeneo ambayo hatukuwa na umeme sasa Wataalam wamefika wamefanya survey; ni imani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

yangu kwamba, ifikapo mwakani na sisi tutapata umeme kama watu wa maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi; Hospitali yangu ya Wilaya ya pale Itumba haina X-Ray wala haina *Ultra Sound*. Mimi naomba Waziri anayehusika, naomba mamlaka zinazohusika zilichukue hili. Ndugu zangu pale wapiga kura wangu wanatoka Itumba kwenda Isoko, umbali wa kilomita 68, wanatoka pale kwenda Vwawa, umbali wa kilomita 67; kwa kweli ni mateso. Mtu anapata *fracture*, mtu anapata tatizo la kifua, wanataka kujua ni kitu gani, ni lazima abebwe, ni lazima ndugu zake wamsindikize Isoko, wamsindikize Vwawa. Kwa umbali niliousema, ni matatizo, ni mateso kwa ndugu zangu pale. Naomba tafadhali wahusika walichukue ili wapiga kura wangu, Wananchi wetu, Watanzania wenzetu, katika Wilaya ya Ileje iliyoko pembezoni, ambayo kwa muda mrefu imekuwa *disadvantaged* sasa wapate nuru hiyo ya kutibiwa pale magonjwa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Vijiji: Wilaya ya Ileye tuna Kata 18, Kata tisa zina Watendaji na Kata tisa hazina Watendaji. Pia kwenye vijiji, tuna vijiji 71, vijiji 10 havina Watendaji. Tunaomba, kama ombi maalum, mtusaidie mamlaka zinazohusika tupate Watendaji ili hawa watu ambao wamekaa kule kwa ajili ya kusukuma maendeleo waweze kupatikana na wasimamie maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mishahara au posho kwa ajili ya Watendaji wa Vijiji: Wengi wamelizungumza hili na mimi niungane nao, haingii akilini kizazi hiki mtu anafanya kazi anaamshwa usiku, anawa-*attend* watu shida zao mbalimbali, lakini hapati posho! Muda huo umepita. *(Makofi)*

Ninaomba sasa, sitaki kuingia kwenye malumbano kwamba Serikali sijui, sherehe sijui, lakini tunaweza kuji-*adjust* tukawalipa hawa watu japo kwa kiasi kidogo. Unaweza ukapiga, hata sisi hapa Wabunge, hebu siku moja, nakumbuka siku moja Mheshimiwa Mwandosya alisema kuna maafa kule Dar es Salaam tuchange, aah ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kibona.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Naunga mkono Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa asilimia mia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassari, ajiandae Mheshimiwa Juma Ngwali!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa fursa, japo kwa dakika chache nizungumze machache niliyotumwa na Wananchi wangu wa Jimbo la Arumeru Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na barabara. Tumekuwa tunapitisha Bajeti kwenye Halmashauri zetu, Bajeti hizi zinapitishwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na tunakuja Bungeni tuna-approve budget ya Serikali nzima. Kwenye Mfuko wa Barabara, kwa Halmashauri yangu ya Meru; kwa mfano, ukiangalia kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Halmashauri ya Meru fedha ilizopokea kwenye Road Fund kama Mfuko wa Barabara ilikuwa ni pungufu ya asilimia 40.

Mwaka wa Fedha 2013/2014, ambao ndiyo huu tunaoumalizia, mpaka tunapozungumza leo tarehe 8 Mei, bado siku chache kumaliza mwaka wa fedha, tumepokea asilimia 50 peke yake kwenye Miradi ya Barabara. Kwa bahati mbaya zaidi, barabara zimeharibika kweli, mvua zimenyesha barabara zimedi kuwa mbovu. Ukienda leo hii barabara inayotokea Sans kwenda Akeri mpaka Kwarisamu haipitiki. Barabara ya Sans - Yakeri - Nkwanduu haipitiki. Barabara ya Kikatiti kwenda Makiba haipitiki.

Barabara ya Mkwaranga kwenda Kilinga ni mbovu. Barabara ya Kibaoni kupita King'ori kwenda Legoruki mpaka Ngarinanyuki na Arusha National Park haipitiki. Barabara ya Tengeru kushuka Nambala haipitiki. Barabara kwa mfano kama hii ya kutoka Sans kwenda mpaka Akeri, mara ya mwisho ilitengenezwa wakati alipotutoka aliyekuwa Mbunge wetu, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mungu amlaze pema Peponi. Ndipo ikatengezwa kwa sababu Mheshimiwa Rais alikuwa anakuja kwenye msiba na Mawaziri na ninyi Wabunge mlikuwa mnakuja.

Sasa mimi nataka niulize leo hii; hivi hizi barabara hazitengenezwi mnataka na mimi Mbunge mwingine nife ndiyo itengenezwe mpite kuja kunizika? (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia aibu mno kuona mpaka tunafikia hatua ya kiongozi kuondoka, yaani mtu akishaondoka ndiyo thamani yake inaonekana, lakini tukiwa tuko hai thamani haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kilichonishangaza ni kwamba, ukiangalia Halmashari jirani, ambazo zinaongozwa na Wabunge kutoka Chama cha Mapinduzi, baadhi yao fedha zinakwenda vizuri lakini kwetu haziji. Kwa mfano, Halmashauri ya Arusha DC kwa Mheshimiwa Medeye, pesa ya development peke yake ambayo ni nje ya bajeti kwa mwaka 2012/2013 walipata milioni 800, Arumeru Mashariki kwa maana ya Halmashauri ya Meru hatukupata kitu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa fedha za *emergency* walipata shilingi milioni 600. Sisi tuliomba shilingi milioni 300 na tuliomba mapema zaidi kwa Mkurugenzi wa Barabara wa TAMISEMI, lakini bado hatukupata hata shilingi. Kwa mwaka huu wa fedha tulioko sasa hivi vilevile hatujapata hata shilingi, wenzetu wameomba milioni 400 wameshapelekewa karibu milioni 300.

Sasa mimi nataka kujua; hivi tatizo ni kwa sababu Mbunge ni wa Upinzani au tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo ndiyo tatizo mtuambie tu mapema kwa sababu tumeomba Ubunge tuwe neema na baraka kwa watu, tusiwe laana na matatizo kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kwenye suala la maji. Nilipiga kelele hapa mwaka jana wakati wa Bajeti na nashukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Dkt. Mahenge alikuja. Miradi ile ya Maji ya Benki ya Dunia ilikuwa imesimama ikaanza kwenye Vijiji vya Majengo, Kikuletwa, Patanumbe, King'ori, Ishupu, Amburei, Mwaivaro, kule Migandini, Maroroni mpaka Relini na Mbuguni na maeneo mengine, yenye thamani ya shilingi bilioni 7.9. Hivi sasa Miradi hii imesimama tena na wanadai wale Wakandarasi hawajalipwa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kujua ni kwa nini tunawahadaa Wananchi mwaka jana tumewaambia watakunywa maji ifikapo tarehe 26 Desemba lakini mpaka leo hii tunaelekea mwezi Juni maji hayajanywewa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala ambalo lilizungumzwa hapa mapema leo asubuhi na Mheshimiwa David Kafulila aliliongelea vizuri kweli. Kuna wizi wa fedha umetokea kwenye hii *Escrow Account* na kuna watu wanalichukulia hili suala *for granted!* Jamani shilingi bilioni 200, pesa za walipa kodi wa Taifa hili siyo ndogo hata kidogo. Fedha ni zaidi ya zile za EPA. Hii ni EPA mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu walifungwa kwa sababu ya EPA na nitashangaa kweli kama hili suala litapita; kuna watu wanasema ni upepo utapita, nitashangaa kama upepo huu utapita utawaacha baadhi ya watu kwenye nyadhifa zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wametajwa huku, kuna Ofisi kwa maana ya Ofisi: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lazima ituambie; Ofisi ya Waziri wa Nishati na Madini lazima ituambie hapa; Katibu Mkuu wa Nishati na Madini lazima atuambie; Hazina lazima watuambie, Benki Kuu (BoT) lazima watuambie; CEO wa TANESCO lazima atuambie; na watu wanajaribu kufunika haya mambo lakini kuna mambo ya msingi ya kuhojiwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza jambo rahisi tu nitauliza; kwamba, hawa watu wa *VIP* walivyouza *share* zao 30% na hawa wa *Mechmar* walipouza 70% ya *share* kwa hawa watu wanaoitwa *PAP*, hivi hata *Capital Gain Tax* haijaonekana. Mtatwambia kwamba, jambo hili ni la salama? Hata *Capital Gain Tax*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile hizi fedha zilikuwa ni fedha za umeme ambazo ziko *subjected to VAT*; hebu tunaomba kujua inakuwaje hata *VAT* haijaonekana? Serikali inakosa fedha, halafu tunanyanya Wamachinga, tunachukua ushuru kwa akinamama wanaouza ndizi kwenye soko, ndizi moja sh 300/= au 400/=, hata kabla ya kuuza pale Tengeru wakati hujui kama atauza au hatauza, lakini mabilioni ya pesa shilingi bilioni 200 hapa zinapotea halafu kuna watu wanakaa kimya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali itoe Kauli na Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa atwambie vizuri kwa sababu, yeye ndiye mkubwa wa Mawaziri wake. Kwamba, kabla ya Hotuba hii kuhitimishwa pengine Serikali itoe ufafanuzi na kama si leo basi ni kesho, aje Waziri wa Nishati na Madini au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, azungumze mbele ya Bunge hili. Atwambie hizi fedha zaidi ya shilingi bilioni 200 zilizopotea kwenye *Escrow Account* zimekwenda kwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nyaraka tumeona. Juzi nilikuwa nasoma gazeti la *The Citizen*, Mwandishi akamuuliza huyu mtu wa *VIP*, alipombana sana akamwambia mbona unanibana mimi, kwa nini huibani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo inajua dola zaidi ya milioni tatu zilipokwenda? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kuna watu wamepewa rushwa. Kuna watu wamekula pesa, halafu hili Bunge limekuwa ni la kuonea watu. Miaka iliyopita hapa kuna watu walishika mshiko huku ndani, kuna watu wamelazimishwa kujiuzulu, kwa ajili ya fedha kwenye kashfa kadha wa kadha, lakini zinapokuja kashfa zinazogusa baadhi ya watu, wao wanaonekana ni *exceptional*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote niliowataja hapa ni Wateule wa Mheshimiwa Rais na ningetegemea Mheshimiwa Rais Kikwete ajitokeze na asimame atake hili suala litolewe ufafanuzi mbele ya umma, ili tuwaondolee Watanzania kuondoa mashaka pamoja na yeye. Kama suala hili halitatolewa ufafanuzi na Ikulu tutakuwa na mashaka pengine hata Ikulu inafahamu na inahusika kwenye kashfa hii ya upotevu wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 200. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia hapo sitaki nikupotezee muda, lakini naomba Serikali ije itoe Kauli kuhusu upotevu wa hizi fedha, bilioni 200 za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante.
(Makofi)

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini kwanza pia nimshukuru Comrade Majaliwa pamoja na Mheshimiwa Amos Makala, kwa kuingiza *input* kidogo katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 Desemba, 2013, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa pesa za Mfuko wa Kuchochea wa Maendeleo ya Jimbo, lakini kwa bahati mbaya kabisa bila aibu, bila fedheha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikaamua kupora, kunyang'anya na kuiba fedha hizo. Ziko tetesi kwamba, fedha hizo zimeibiwa na wajanja wachache, baadhi ya fedha hizo zilitumika katika kujenga majumba ya kifahari na pia zinatumiwa katika kuhonga kwa kutafuta, kwa kusaka Urais wa Zanzibar mwaka 2015.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachusika wakubwa wa wizi huo ni bwana mkubwa mmoja, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Zanzibar, Hamis Mussa na Waziri katika Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Abood, wakisaidiwa na mzoefu katika shughuli hizo, Dkt. Khalid, Katibu Mkuu Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais. Ni aibu kubwa sana, namshangaa sana jamaa yangu Rais Shein kuchukua timu hii Mohamed Abood, kumchukua Dkt. Khalid, akamchukua na Khamis Mussa akawaweka pamoja, Zanzibar ni lazima itaangamia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna tetesi kuna miradi mikubwa ambayo inakuja na naomba kwamba, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atwambie ni miradi mingapi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imepelekwa Zanzibar kwa miaka 10 nyuma iliyopita, ili tuweze kujua tuifuatilie kwa sababu, wajanja hawa wanapiga pesa nyingi katika miradi hii inayopelekwa Zanzibar. Uko ushahidi kabisa kwamba, fedha hizi zinamalizika katika Ofisi ya chinjachinja ya Makamu wa Pili wa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya MIVAF; miradi ya MIVAF ni miradi mikubwa ya kuboresha miundombinu ya kifedha vijijini na kuongeza thamani ya mazao ambayo mpaka sasa wajanja hawa wanainyemelea. Mheshimiwa Lukuvi nafikiri ni lazima akimbie, simwoni; Mheshimiwa Lukuvi alituletea barua ya tarehe 2 Desemba, kututaka Wabunge tusimamie miradi hii mikubwa ya MIVAF. Kwa upande wa Wilaya yangu naomba niitaje miradi hiyo itatekelezwa katika maeneo gani? (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Chakechake, miradi hiyo itatekelezwa katika Jimbo la Ziwani, langu mimi mwenyewe, Jimbo la Chonga la Mheshimiwa Haroub, Jimbo la Chakechake la Mheshimiwa Mussa Haji na Jimbo la Wawi la Mheshimiwa Hamad Rashid. Miradi hiyo itatekelezwa kama ifuatavyo na nasema hivyo ili fedha hizi zisije zikaingia kwa Khamis Mussa, Mohamed Abood Mgunya, pamoja na Dkt. Khalid. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilomita 25.5 za Gombani – Nang’ambwa, barabara ya Kianga kilomita 5, Vikunguni – Mzambaru Boko kilomita 4, Mfikiwa – Pujini kilomita 5, Dodeani – Langoni – Makaani kilomita 5.6, Mchanga wa Kwale – Kichuwani kilomita 2.5, Chanjamjawiri – Matale kilomita 4.5 na uboreshaji wa Soko la Chakechake la Tibirinzi. Yako maneno makubwa sana katika miradi hii inayopelekwa Zanzibar; wakati tunachangia katika Bunge la Katiba, tulitaka Serikali Tatu, maana yake ilikuwa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotolewa na Hazina ya Jamhuri ya Muungano zinapokwenda Zanzibar zikiingia katika Hazina ya Zanzibar Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali wa Jamhuri ya Muungano hana mamlaka tena ya kuzikagua tena fedha ambazo kazitoa mwenyewe. Hilo ni ombwe kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni gumu sana kwa Wabunge, fedha ambazo Mbunge sio Mjumbe wa Halmashauri wala sio Mjumbe wa Mabaraza ya Miji, sasa fedha zozote zile zinazoingia Mbunge hana uwezo wa kuzifuatilia kwa sababu, hawezi kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wajanja wale watatu wanatumia njia hii, upenyo huu, kwa sababu Wabunge hawaelewi miradi, basi wanapiga hela vibaya sana, wanatafuna hela vibaya sana, matajiri wa kutupwa. Zanzibar iko masikini, wao ni matajiri wa kutupwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata TAKUKURU haina mamlaka ya kufanya kazi Zanzibar, hivyo wale wajanja wanapiga hela, matatizo ya Muungano yanaongezeka na nyie mpo mnakaaka tu, hamsemi lolote mnawaogopa. Sijui mnachowaogopa nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu muundo wa Serikali Mbili unawanufaisha baadhi ya watu. Namshukuru sana Mheshimiwa Masele Mabumba kwa kunipa Taarifa za huu msako wa Urais na nikipata nafasi nitazitoa kwa upana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo siungi mkono hoja na niishie hapo. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tauhida! Ajjandae Mheshimiwa Neema.

Taarifa!

TAARIFA

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa Taarifa mzungumzaji. Mambo ya ujenzi sio ya Muungano, hayahusiki kabisa na Muungano. Ujenzi ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar huko huko, lakini Mfuko wa Jimbo ni halali azungumze, lakini mambo ya kilomita mbili za barabara, kilomita 20 barabara, si mambo ya Muungano; hatuhusiki na Muungano wa Ujenzi.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba tu kutoa Taarifa kuhusiana na fedha za Mfuko wa Jimbo ambazo asubuhi zilizungumzwa na mimi kama Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nadhani limenigusa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha zipo hazijatafunwa. Fedha zipo na wiki ijayo fedha zitaingizwa katika *Account* za Waheshimiwa Wabunge za Majimbo. Kwa hiyo, nadhani hiyo *notion* kwamba, fedha zimetafunwa na sidhani kama itakuwa ni *trend* nzuri kuanza kutaja majina ya watu ambao hawawezi kufika hapa kuelezea, nadhani sio vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimezifuatilia kwa uhakika kabisa hizi fedha zitaingia. Maelezo mengine yatawasilishwa na Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *auditing* kuhusiana na miradi. Kweli Mkaguzi Mkuu wa SMT hawezi kukagua, lakini amekasimu madaraka yake kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale Zanzibar na anafanya hiyo kazi anakagua. Kwa hiyo, hiyo ndio Taarifa tu ambayo nilikuwa nataka kumpa Mheshimiwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngwali, Taarifa unaipokea?

MHE. JUMA AHMED NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya MIVAF ni miradi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Keissy nafikiri hasomi kile kitabu akaona, la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Taarifa ya pili ya Mheshimiwa Waziri, nafikiri Waziri anataka kuingia katika hilo kundi la kutafuna hizo hela. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tauhida!

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Nianze kwanza kwa masikitiko kabisa wakati tunachangia tunataja majina ya watu ambao hawana uwezo wa kuingia hapa kujitetea, lakini hili hatulishangai siye na hatulishangai kwa sababu, maumivu makali ya Wapinzani waliokuweco Zanzibar ni suala zima la Mapinduzi. Hiki kinachozungumzwa hapa Mheshimiwa Mohamed Abood ni Kiongozi aliyesimamia Mnara wa Kumbukumbu ya Mapinduzi; ndicho ambacho kinasumbua na ndio kinachopigiwa kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zaidi kupitia Mheshimiwa Mohamed Abood kwa kusimamia kuweka Kumbukumbu ya Mnara wa Mapinduzi ndani ya Zanzibar. Huu utakuwa ni kumbukumbu mpaka kwa vizazi kuona mnara ule uko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lilizungumzwa suala la mikopo kwamba, tumekopa tumenunua vifaru, lakini kule kwetu Zanzibar kuna eneo moja hupati mke kama hukuwa mtu ambaye unakopa, kuna hadithi ndogo tu nitawapa; kuna mtu mmoja alikwenda kuposa, alipofika pale akaulizwa baba una madeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema nashukuru sijawahi kukopa toka utotoni mwangu. Akaambiwa hatuna uwezo wa kukupa mke kwa sababu, tukikupa mke utamlaza na njaa siku utakayoishiwa hutaweza kwenda kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niipongeze Serikali ya Tanzania kwa kukopa. Naamini ndani ya mikopo hiyo ni waaminifu ndio maana wakawa wanakopeshwa, maana wanalipa. Mwanaume aliyekuwa mwanaume lazima akope, akikopa huwa anaweka kwamba, anaaminika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa Taarifa hiyo fupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha kwamba, mradi huu kuna mwongaji mmoja kaka yangu yuko pale, alizungumza kwamba, fedha hizi zilitokana na Mfuko wa Jimbo; sio kweli kaka yangu, vizuri ile Serikali sasa hivi tunashirikiana, CCM na CUF iliyokuweco Zanzibar. Mpate wakati muwaulize Mawaziri wenu fedha zilizojenga mnara Zanzibar zimetoka wapi? Ili mpewe majibu, mzungumze Bungeni kuwaambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizojenga mnara Zanzibar zimetoka katika Mfuko wa ZSSF. Huo ni mradi wao ambao wanahakikisha watakusanya mapato kurudisha hizo fedha za Mfuko wa ZSSF. Kwa kuwa, masuala mengi

haya yanayohusika kuzungumzwa ni Baraza la Wawakilishi, wako watu watayazungumza na wao watapata majibu yao maana wanafuatilia Bunge toka asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu tulipofikia niwapongeze Mawaziri, mabadiliko yako kupitia Mawaziri na kazi wanafanya. Watu wazuri au binadamu wazuri mnapowaambia wanasikia na sisi tunaosema ukifika wakati kuwaambia kwamba, mnaofanya vizuri sasa, tuwaambie kwamba, mnaofanya vizuri Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinachonisikitisha ni kwamba, Watendaji huko nje wanataka kukaa nyuma ya migongo yenu kuwatendea vibaya Watanzania, ili muwajibishwe ninyi, lakini tunawaambia sasa tunageuka na mfumo tutakaokwenda nao, tutakwenda nao wao jino kwa jino mpaka tunahakikisha wanamalizika Watendaji wote waliokuwa hawaitendei haki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili na nusu iliyopita nilikuwemo ndani ya Kamati ya LAAC na sasa hivi naendelea kuwoko ndani ya Kamati ya LAAC ambapo kwa masikitiko makubwa sana kitu ambacho kinaniumiza moyo wangu, Wahandisi na wengine ambao wamo ndani ya Halmashauri hawaitendei haki Tanzania hata kidogo. Hawa watu imefika wakati wanatafuna pesa hata haya hawaoni, hata vibaya hawaoni kwa vitu wanavyowatendea Watanzania, lakini sisi tukiwa kama vijana sasa hivi wakati wa kukaa kimya kuyaona hayo, tunayaona kwenye Kamati kwa kuwa, tunakuja hapa tunawawajibisha Mawaziri, umeshakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nikiwa kama kijana, tutasimama majukwaani, kama Wilaya au Halmashauri au Mkoa, kila aliye na madhambi yake sasa tutayafichua, tumechoka. Leo anasimama Mwenyekiti wetu wa Kamati alizungumza mradi wa milioni 500 uliokuwoko Arusha, mradi wa maji, ni kitu cha kusikitisha na cha aibu, leo Mtanzania unaoishi na Watanzania wenzio wanaolipa kodi asubuhi, mchana na jioni, mnakwenda kutafuna milioni 500?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale wako Arusha kwa Wamasai. Leo Mmasai amebeba mtoto mgongoni, anabeba dumu la maji kichwani kwa sababu ya ufisadi wa mtu mmoja au mafisadi wawili, tumechoka, vijana wa CCM hatutakaa kimya tena. Viongozi wetu kwa hili mtatusamehe na mtatustahamilia, tumekuwa muda mwingi tunautumia kuwawajibisha Mawaziri, sasa hivi hatutakaa kimya tena kila tutakapokwenda kuna vijana wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakishukuru Chama cha Mapinduzi kiko vizuri na kimejipanga vizuri. Tuko tangu Mikoa, Matawi na Mashina, tutawaambia vijana wenzetu nani wanaofanya ufisadi huu?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji vijana wenzetu mnatutia aibu. Kuna watu wako rika sawa na sisi, tunadhani kwamba, vijana tunapiga kelele wapewe nafasi. Tunasikitika na tunaona aibu kumkuta Mhandisi kijana anatafuna fedha hata huruma hana kama mama yake ndio anayekwenda kuchota maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye masuala ya majengo; tunapokwenda kukagua majengo, unasikitika kumkuta Mtanzania ana lisimamia jengo la Hospitali kuna chumba kimoja, unauliza hili lingine ni *hall* au ni nini? Unafika wewe, mimi sina sifa ya uhandisi, unamuuliza unavyodhani mwanamke atajifungulia wapi? Unavyodhani sindano mtu atapigiwa wapi? Anabaki anakuangalia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoka, Waziri Mkuu sasa tumechoka, inabidi sasa na sisi tuanze huko kuwaambia huyu ndiye anayehusika, huyu ndiye anayekuharibieni Halmashauri yenu. Mheshimiwa Waziri, kama mlivyo na mikakati yenu mnavyoendelea kufanya kazi, naombeni zidisheni *speed*; hawa sasa wamekuwa wanakaa nyuma ya migongo yenu, waondosheni, wanafika wakati wanaifanyia vibaya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifika wakati siku moja nilijiuliza; hivi kweli hawa wanaoajiriwa katika Halmashauri ni Watanzania halisi? Maana nashindwa kuelewa, kweli kama Mtanzania Mzalendo utafanya vitu vya ajabu kiasi hiki? Hata uchungu huna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kitu siwezi kuamini. Naiomba Idara ya Kazi, Ajira, ishughulikie suala hili na ilishughulikie kwa undani kabisa kwa sababu, Tanzania tuna wahamiaji wengi wanaingia. Kweli hawa watu tunaowaajiri ni Watanzania? Kwa nini hawana huruma na Tanzania yetu? Kwa nini hawawaonei huruma wazee wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye masuala mazima ya 5% ya vijana na wanawake, huko ni kilio kikubwa na tena kinatia aibu. Mawaziri mnaohusika na Wizara hii nakuombeni kati ya kazi sote mnazozipa kipaumbele na hii ipeni kipaumbele; fedha za Mfuko ule zinatafunwa kuliko mchwa aliyeingia katika mti mkavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu moja tu, nimekaa katika Kamati hii sasa hivi miaka mitatu na nusu, lakini siku moja tu ambayo nilikwenda Tanga ndio angalau tulipouliza fedha hizi ziko wapi? Tukajibiwa kwamba, zimetumika kutengeneza mradi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiache kumsifia ni Mheshimiwa DC Subira Mgalu, ndio hiyo Halmashauri yake. Nikapata moyo hivi kweli kama tungekuwa tunakwenda angalau basi 5% zile hazikwenda kwa vijana kwa...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Tauhida kwa mchango wako. Nakushukuru sana.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Hotuba ya Mheshimiwa Waziri...
(Makofi)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Neema Mgaya, ajiandae Mheshimiwa Bukwimba.

MHE. NEEMA H. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Moja kwa moja katika mchango wangu ningependa kwanza kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutambua umuhimu wa kujenga na kupanua barabara ambazo zinaingia katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Waziri Mkuu katika bajeti ya mwaka 2014/2015, kutenga fedha za kuweza kujenga barabara ambazo zipo pembezoni, barabara za michepuko (*feeder roads*) kuzijenga katika kiwango cha lami ili ziweze kusaidia kuondoa msongamano wa magari. Vile vile bado naikumbusha Serikali kuna baadhi ya barabara ambazo zipo pembezoni kama barabara ya Mbezi Mwisho inayopita Segerea na kutokea Banana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni vizuri nayo ingewekwa katika mpango wa kujengwa katika kiwango cha lami, kwani itasaidia wale wakazi wa Gongolamboto, *Airport* ambao wanapita kwenda Mikoani wakapita *shortcut* hiyo, lakini vile vile wakazi wa Kibamba, Mbezi wakatamia barabara hiyo kwa ajili ya kwenda *Airport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine ambayo inatoka Kibaha, *TAMCO* inapitia Vikawe kutokea Baobab. Barabara hii pia naiomba Serikali iweke katika mpango wa kujengwa katika kiwango cha lami kwani itasaidia wale wakazi wote wa kutoka Bunju, Mbweni na wa Bagamoyo ambao wanakwenda Mikoani baada ya kuzunguka kwa kupitia Ubungo, watapita *shortcut* ile kwa ajili ya kwenda Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende katika Mkoa mpya wa Njombe. Sisi wana Njombe, Mkoa wetu ni mpya, lakini tunasikitika hatuna hata barabara moja ambayo ipo katika kiwango cha lami, ni barabara moja tu

ambayo inatoka Makambako kwenda Ruvuma ndiyo ambayo tunaweza tukahesabia kwamba iko kwenye kiwango cha lami ambayo imejengwa tangu miaka ya 1980.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Njombe – Makete, tunashukuru hii ilikuwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba ijengwe sasa katika kiwango cha lami, lakini barabara hii imetengewa shilingi bilioni 2.7 wakati barabara hii ina urefu wa kilomita mia moja na tisa. Kwa kusema kweli fedha hizi ni ndogo ukizingatia na urefu wa barabara hii na inahitajika kujengwa katika kiwango cha lami. Hivyo, tunaiomba Serikali ituongeze fedha ili kuweza kujenga barabara hii ya Njombe - Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Njombe Makete ina umuhimu mkubwa; kwanza inaunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya, lakini vile vile barabara hii inapita katika Mbuga ya Kitulo. Mbuga ya Kitulo ina *special species* kwamba, ina maajabu ambayo yako tofauti na mbuga nyingine. Mbuga hii ina maua mazuri ya kupendeza ambayo hayapatikani katika mbuga yoyote hapa Tanzania hivyo kwa kujengwa barabara hii katika kiwango cha lami itavutia watalii kuja kwa wingi katika Mkoa wetu wa Njombe, Makete kwenda kuona Mbuga hii ya Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile katika Mbuga hii ya Kitulo tuna shamba la ng'ombe, tunavuna maziwa mengi sana katika shamba hili. Sasa hivi maziwa yanashindwa kusafirishwa kwa sababu barabara hii imekuwa mbovu sana ukizingatia maeneo ya Isonje, Makete sasa hivi barabara hii haipitiki. Hivyo basi, tunaiomba Serikali ituongeze fedha ili tuweze kujenga haraka barabara hii ya Makete – Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tena tuna barabara ya Njombe – Mdandu – Iyayi. Barabara hii ya Njombe – Mdandu – Iyayi inapita Makao Makuu ya Wilaya ya Wanging'ombe, Wilaya hii ni mpya, Wilaya hii ina wafanyabiashara wengi, wanashindwa kusafirisha mazao yao, wengi wanasafirisha mazao yao kwenda Mbeya kwa ajili ya kwenda Dar es Salaam. Naomba pia izingatiwe barabara hii ili iweze kujengwa katika kiwango cha lami. Vile vile bado tunazidi kuomba barabara ya Itoni – Ludewa – Manda. Hii nayo ina umuhimu wake, tunaomba pia mtujengee katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la maji. Mwaka 1976, UNICEF ilianzisha mradi mkubwa wa maji ambao uliweza kuhudumia vijiji arobaini katika Wilaya ya Wanging'ombe. Lakini cha kusikitisha kwamba mradi huu hadi sasa una takribani miaka thelathini na nane, mradi huu umechakaa, miundombinu yake imechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilituahidi kwamba mwaka 2010 ingeweza kukarabati mradi huu wa maji, lakini mpaka leo ninavyozungumza hapa Serikali haijafanya kazi hiyo ya kukarabati mradi huo wa maji na ukizingatia kwamba mradi huu wa maji kama utakarabatiwa na kupanuliwa vizuri utasaidia Vijiji vya Kata ya Saja lakini vile vile itasaidia Vijiji vya Kata ya Kijombe kuweza kupata maji kwani vijiji hivi vya Kata ya Saja na Kijombe vina tatizo kubwa sana la maji. Naiomba Serikali iangalie kwa ukaribu zaidi katika kukarabati mradi huu wa maji ili iweze kusaidia Kata za Saja na Kijombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijawatendea haki vijana wenzangu kama sitazungumzia suala la ajira. Suala la ajira linazidi kuwa kubwa, siku hadi siku, vijana wana matatizo ya ajira. Napenda kuishauri Serikali iendelee kupanua wigo wa kuweza kutumia Wakandarasi wa ndani katika sekta tofauti. Kwa kutumia Wakandarasi wa ndani katika sekta tofauti itasaidia wale vijana wanaomaliza vyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. NEEMA H. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi ya Waziri Mkuu ni muhimu sana kwa sababu inashughulika na maisha ya wananchi katika Halmashauri zetu hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa jinsi ambavyo alisikiliza kilio cha wananchi katika Jimbo la Busanda, barabara ambayo ilikuwa haipitiki kwa kipindi kirefu, aliweza kutoa fedha na sasa hivi barabara inatengenezwa iko katika hali nzuri na wananchi wamenituma niweze kufikisha salamu hizi za shukrani kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara ni changamoto kubwa sana hasa katika mwaka huu. Karibu kila sehemu kutokana na kunyesha kwa mvua kumetokea kuharibika kwa barabara zilizo nyingi hasa za vijijini. Nitumie pia fursa hii kuomba Ofisi ya TAMISEMI iweze kutusaidia hasa katika Halmashauri zetu fedha za Halmashauri hazitoshi kukarabati barabara hasa kipindi hiki ambapo kuna mafuriko, kuna mvua nyingi, barabara nyingi zimekatika, hazipitiki kwa mfano, kule Butundwe kuna Kijiji kinaitwa Kasamwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho Kijiji cha Kasamwa barabara yake haipitiki yaani wakati wa mvua wananchi wale wamekuwa kama wapo kisiwani, hawawezi kwenda huku na kule. Kwa hiyo, niombe tu kupitia bajeti hii, mniangalie sana hasa wananchi wa Kasamwa ambapo kiukweli wapo kisiwani, Halmashauri hawana uwezo wa kuweza kuitengeneza barabara hii ya kutoka Chemamba kwenda Kasamwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tulipeleka maombi yetu ya kuweza kupandisha hadhi baadhi ya barabara, kwa mfano, kuna barabara ya kutoka Katoro, Busanda, Nyakamwaga, Kamena kwenda Mwingiro ambayo ni barabara inayunganisha Wilaya ya Geita na Wilaya mpya ya Nyang'wale. Niombe sasa Serikali iweze kuipandisha hadhi barabara hii ili wananchi waendeleo kupata huduma iliyo bora zaidi na kuweza kufanya shughuli zao vizuri kuliko hivi sasa barabara hizi zinashindwa kuhudumiwa na Halmashauri kwa sababu ya bajeti ambazo hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya madini. Sitawatendea haki wananchi wa Geita na Jimbo la Busanda kwa ujumla nisipozungumzia suala la madini. Zaidi ya 70% ya uchumi wa Geita, unategemea shughuli za madini. Katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 45 na 46 nimeangalia sana nimeona wananchi wa Geita wametengewa hasa katika Kijiji cha Isamilo na Lwenge ni mjini Geita, lakini katika Wilaya ya Geita vijijini ambapo ni Jimbo la Busanda hasa katika maeneo ya Lwamgasa, Nyarugusu, kwa kweli sijaona wananchi wakitengewa maeneo ya kuchimba madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba sana Serikali, ni kipindi kirefu sasa karibu kila bajeti ya kila mwaka huwa nazungumzia suala hili. Kwa hiyo, niombe safari hii mnisikie hasa hasa Wizara inayohusika Wizara ya Nishati na Madini tumebadilisha Sheria ya mwaka 2010, tumeweka vipengele vizuri kabisa ambavyo tukiweza kuvifanyia kazi nina uhakika wananchi wetu wataweza kunufaika zaidi kwa rasilimali ambazo Mungu ametujalia. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Serikali iweze kuangalia wachimbaji wadogo hasa walioko vijijini ili waweze kunufaika zaidi na rasilimali za Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika suala la mitaji, ni kweli kwamba Serikali imeamua kupitishia fedha kwenye Benki ta TIB Mwanza. Niombe Serikali iweke kwa sababu Benki kama Benki zinakopesha kwa masharti magumu sana na wachimbaji wadogo walio wengi hawana uwezo huo wa kuwekeza dhamana kubwa kubwa. Kwa hiyo, mara nyingi wanaoweza kukopa ni wale wachimbaji wakubwa na wala siyo wadogo wadogo kama ambavyo dhamira ya Serikali ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa Serikali iweke utaratibu mzuri ili wachimbaji wadogo wadogo ambao hawana uwezo na ambao ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

vijana kuweza kupatiwa mitaji, kwa sababu bila mitaji haiwezekani kuweza kunufaika. Kule Igunga tumeona vijana ambao wamewezeshwa, Serikali imewapatia fedha, imewapatia mtaji, tunaona jinsi ambavyo vijana wanaendelea vyema. Kwa hiyo, niombe hata katika sekta hii ya madini tuwawezeshe vijana wetu, tuwape mitaji ili waweze kuchimba, waweze kufanya vitu vyao kwa uhakika na waweze kuinua pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia katika suala la Walimu. Katika Bunge tulilokuwa nalo Bunge maalum nilizungumzia kidogo sana kuhusiana na suala la Walimu. Walinialika katika kikao chao cha Walimu takribani mia tatu katika Wilaya ya Geita, walizungumzia masuala yao makubwa madeni, niombe Serikali ilipe madeni yao, wanadai milioni tisini na nane katika Wilaya ya Geita. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Wizara ya Elimu, TAMISEMI tuhakikishe tunalipa madeni ya Walimu, lakini vile vile tuboreshe utendaji wa kazi, tuboreshe mazingira ya kazi ili Walimu wetu waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la ajira kwa vijana wetu. Kuna Wizara ya Kilimo ambayo imeajiri watu wachache sana. Kuna baadhi ya wahitimu hawajapata ajira kiasi kwamba wengine wamekata tamaa, wengine wanataka kujinyonga, kwa hiyo, niombe Serikali iajiri wote waliomaliza kilimo wote waajiriwe tusibakize hata mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la umeme. Umeme ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo yetu. Niombe Wizara ya Nishati na Madini katika suala la usambazaji wa umeme waongeze kasi, wananchi tunahitaji umeme; Kata mbalimbali, shule za Sekondari Kamena, Rwamgasa tunahitaji umeme, shule ya Sekondari Katoro tunahitaji umeme. Kwa hiyo, niombe Serikali iongeze kasi ya usambazaji wa umeme. Najua tayari kuna baadhi ya vijiji viko kwenye mpango, lakini niombe sasa Serikali iweze kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ni suala la maji. Kuhusu maji kwanza kabisa niishukuru Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, jinsi ambavyo pamoja na kwamba nimehamishwa kwenye ile Kamati, lakini wameendelea kunisaidia hasa katika kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika Wilaya ya Geita kwa ujumla. Kuna mradi mkubwa sana wa Maji Geita Mjini, naomba Serikali ihakikishe maji yanapatikana, wananchi wa Geita wanahangaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Mradi wa Maji Nyakagomba; ule Mradi wa Vijiji Kumi, naomba Serikali ihakikishe inatekeleza mradi huu. Pia kuna Mradi wa Chankorongo wa kuvuta maji Ziwa Victoria, naomba Serikali ihakikishe wananchi wawe wanapata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mapema leo mchana Mheshimiwa Kafulila alitoa tuhuma kwa Gavana wa Benki kwenye Kamati alisema kuwa alifanya malipo ambayo alifanya kwa shinikizo na baadaye Mheshimiwa Mpina akaomba mwongozo na kusema maneno aliyosema Kafulila hayakuwa ya kweli amemwomba ayafute. Wakati Mheshimiwa Mpina anajibu tuhuma hizi Mheshimiwa Kafulila alikuwa hayupo. Nimewasiliana na Mheshimiwa Kafulila yuko tayari sasa kusimama na kutoa maelezo yake. Hoja ilikuwa ni ufute tu maneno yako.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumza kuhusiana na ufasadi mkubwa wa takribani bilioni mia mbili ambazo ni zaidi ya ufasadi wa EPA nilirejea kauli ya Gavana wa Benki Kuu akiwa kwenye Kamati yetu ambapo nilimbana kwa maswali, Gavana wa Benki Kuu akafika mahali akaiambia Kamati Mheshimiwa Kafulila mengine mnanionea, nilijitahidi kufanya kwa kadiri nilivyoweza, lakini *pressure* iliyokuwepo ilikuwa ni kubwa kuhusu jambo hili.

Alifika mbali kabisa Gavana akasema kwamba, pesa hii ilikuwa itoke mwezi wa Tisa mwaka jana, lakini pesa hii kutoka mwezi wa Kumi na Moja mwaka jana ilikuwa ni kwa sababu ya juhudi za Benki Kuu kuhakikisha kwamba fedha hii anachukua kila hatua ili kusudi jambo hili lisije kumfia katika mikono yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huo ndiyo ukweli ambao ulijitokeza na ndiyo maana jambo kubwa kama hili linahitaji kwa kweli iundwe Kamati Teule ya Bunge ili kusudi mambo yote ambayo yanahusu jambo hili yaweze kufahamika. Ambacho nimekizungumza leo ni kama asilimia kumi tu ya ambacho nakijua kuhusu jambo hili.

Kwa hiyo, naomba kuisitiza kwamba jambo hili Benki Kuu walitoa fedha ile ya *Escrow Account* moja ya sababu ikiwa ni *pressure* kubwa ya ufuatiliaji kutoka kona mbalimbali za wadau wanaohusika kwa maana ya Serikali na *IPTL* kutaka fedha hii itoke ndiyo maana hatuwezi kuyamaliza hapa kuna kila sababu ya Bunge hili kama linataka kulinda heshima yake iundwe Kamati Teule ili kusudi mbivu na mbichi zipatikane. Hii sinema ya *IPTL* ya tangu mwaka 1995 mpaka leo inabadilishwa *sterling*, wanabadilisha rangi tu, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa heshima kabisa ya Bunge hili, naomba tusizungumze mambo vipande vipande wala nusu nusu, niombe iundwe Kamati Teule ya Bunge ili kusudi mbivu na mbichi zipatikane kuhusu jambo hili kwa sababu nchi hii ni maskini sana kuibiwa kiasi hiki cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii risala tumeisikia tangu mchana, maelezo ya Mheshimiwa Kafulila tumeyasikia tangu mchana, haiingii akilini Gavana wa Serikali kusema maneno haya na hawezi kusema, kwa sababu, bahati mbaya hawezi kuwepo hapa kujitetea, lakini sisi tumemuuliza hajawahi kusema maneno hayo, lakini ninachotaka kusema ni kwamba, mkubwa wake, Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali atafafanua kesho wakati ana *wind-up* jambo hili kwa sababu limezungumzwa kupitia kivuli cha hotuba ya Waziri Mkuu, hana sababu ya kuleta maneno ya Tume Teule ya mtu ambaye amesema mtaani huko.

WABUNGE FULANI: No! no!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Hii ni hotuba, kwa sababu amesema chini ya kiti cha Mwenyekiti ambaye Mwenyekiti mwenyewe amekataa.

WABUNGE FULANI: Aaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mwenyekiti wa Kamati hapo alipokuwa anasema amekataa. Sasa kwa sababu Mwenyekiti ameizungumza kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwenye bajeti yake na ndiye kiongozi wa shughuli za Serikali ataitolea maelezo kesho. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lukuvi. Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na ratiba yetu tuna muda mchache sana kabla Mawaziri hawajaanza...

MHE. HALIMA J. MDEE: Huku Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Wasira kwa dakika tano tu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mwenyekiti, mwongozo wako.

MWENYEKITI: Subiri kwanza Halima.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika tano naweza kusema mambo machache sana, lakini nataka niseme, kwamba, mfumo wetu wa demokrasia tena ya Vyama Vingi unatutaka tuwe tunatoa mambo katika Bunge hili ambayo yanafanana na hadhi ya Bunge lenyewe na ambayo yanazingatia kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimesikiliza hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Katika ukurasa namba nane amesema mambo ambayo si ya kweli. Anasema kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, haijawahi kutokea kwa Mkuu wa Nchi na Amir Mjeshi Mkuu kuchochea Jeshi lake kufanya mapinduzi ya kijeshi. Haya maneno ya ajabu sana. Sisi wote tulikuwepo hapa wakati Rais anazungumza na Bunge la Katiba na Watanzania kwa mamilioni walikuwa wanamwanguka na kumsikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais hakuchochea Jeshi, alichosema Rais na namnukuu, kwamba mfumo unaopendekezwa na kwa sababu kuna mashaka juu ya uwezekano wa kuwa na fedha za kuweza kumudu uendeshaji wake na kwa sababu mfumo huo ndiyo utakuwa unasimamia ulinzi na usalama wa Taifa, uwezekano wa kuwa na Serikali imara ambayo haina fedha, unaweza ukaathiri ulinzi na usalama wa nchi yetu. Haya yalisemwa na Rais na alikuwa na haki ya kuyasema kwa sababu kuongoza ni kuonesha njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno ya namna hiyo, haya yaliyoandikwa hayastahili kusemwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa sababu katika mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi, Kiongozi wa Upinzani ana heshima yake na Chama chake kinatazamiwa kuwa Chama mbadala, kama hiki ndiyo mbadala, yaani nchi hii haina mbadala. *(Makofi)*

Maana chama mbadala hakiwezi kusema maneno haya Bungeni na maneno ya uwongo, nimepewa dakika tano sisikilizi kitu cha mtu, ukae chini kwanza mambo ya kuingie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema na narudia, wakati anaeleza, sababu za kutoka, alisema walitoka Bungeni kwa sababu ya ubaguzi, matusi, kubadilisha rasimu na kadhalika. Haya maneno hayana nguvu ya kutosha mtu serious kutoka Bungeni. *(Makofi)*

Maana matusi yalianzwa na wao wenyewe, Jussa na Mheshimiwa Lissu na walitukana mpaka wakamtukana Julius Nyerere ambaye hayuko Bungeni na yuko kaburini, nani anasema aliyetukana zaidi kuliko mwingine. Leo nilikuwa namsikiliza yule kijana pale anasoma mambo ya lugha anasema Nyerere alisema, Nyerere gani aliyesema na mlisema ni mwongo katika Bunge lililopita. *(Makofi)*

Bunge hili lazima lilinde heshima yake, lilinde heshima ya historia na lilinde heshima ya watu ambao wametufikisha hapa. Hatuwezi kuvumilia lugha ya namna hii katika Bunge hili. Tunajua mlitoka bila sababu, mkitaka kurudi mnaweza mkarudi bila sababu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kukaa hapa watu wazima tukawa tunashangilia vitu ambavyo havipo, lazima tu-respect historia, tu-respect mchango wa watu wengi wanaotoa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, nimesimama hapa kusema, Rais wetu alikuwa na haki ya kutoa uongozi wa Taifa hili na kuelekeza ili Watanzania wanapojadili Katiba wawe wanajua athari inayoweza ikapatikana katika maamuzi ambayo wangepanya. Kwa hiyo, alikuwa *right* na alikuwa na haki ya kusema na vilevile waliotoka walikuwa na haki ya kutoka bila sababu na wana haki ya kurudi bila sababu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. (Makofi)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7), lakini kwanza niseme alichozungumza mzee wangu hapa aliyetangulia ni porojo tu za kujibu, lakini kinajulikana Rais alisema nini. (Makofi)

Pili, yametolewa majibu hapa na Mheshimiwa Lukuvi na kueleza kwamba kilichosemwa na Kafulila ni maneno ya mtaani na kwamba Waziri Mkuu kwa kuwa ndiyo mtoa hoja atajibu hoja. Jukumu la Bunge ni kuisimamia Serikali na kama tunaona Serikali inatumia fedha kinyume na utaratibu, Serikali inafanya ubadhirifu ni jukumu la Bunge kuisimamia Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kafulila amefanya rejea ya kikao cha Kamati vikao vya Kamati vinaendeshwa kwa *Hansard*, kuna kumbukumbu za kila kinachozungumzwa, majibu ambayo anatoa Mwenyekiti wa Kamati ni mategemeo na matarajio kama ambavyo majibu yanatolewa na wana CCM wengi wakati wanajua ukweli halisi ni nini? (Makofi)

Tokea asubuhi tumeomba, kama kweli hamtuthibitishii, kwa sababu mkisema anajibu Waziri Mkuu, tafsiri yake ni kwamba hizi pesa kweli mmeiba, lakini kama hizi fedha hizijaibwa, ikiundwa Kamati ya Bunge, Kamati Teule, yenye jukumu la kufanya uchunguzi, itajulikana mbivu na mbichi ziko wapi, itajulikana kama Gavana alisema uongo kwa sababu ataitwa, itajulikana kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipata chake kwa sababu ataitwa, atajulikana kama Waziri wa Nishati na Madini alipata chake kwa sababu ataitwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu kwako, Kafulila kasema asubuhi, jamani nipeni muda nithibitishie, mnakimbia nini, kama hamjui ukweli mnakimbia nini, anasema hapa vijana kwamba wataita jeshi la vijana kukamata watu wa Halmashauri wanaoiba, wezi wamo humu humu tuanze kukamatana humu humu. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozi, wangu kwako, Kamati Teule kwa utaratibu tuchunguze hela za Escrow zimeenda wapi, otherwise fedha zimeibiwa humu ndani. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee nikisimama, wewe unakaa, ndiyo utaratibu wa kibunge. Majibu kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu yatatolewa kesho na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe mkuu wa Serikali na kama hamkuridhika au kama mtu ana hoja nyingine, taratibu za Kibunge zinafahamika, ndiyo mwongozo wangu huo. Lingine na tuvumiliane.

Waheshimiwa sasa namwita Mheshimiwa Majaliwa, dakika 15; akimaliza Mheshimiwa Mwanri, dakika 15; Mheshimiwa Hawa Ghasia dakika 20 na Mheshimiwa Lukuvi atamalizia kwa dakika 15. Mheshimiwa Majaliwa!

MJUMBE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: *We are out of time, sorry.*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendeleee na mipango yake mizuri kwa wananchi wake. Naomba changamoto zifuatazo zifanyiwe kazi:-

Tunaomba Mbagala sasa ipewe Jimbo la Uchaguzi, idadi ya watu iliyopo sasa ni 586,272. Kutokana na wingi huu wa watu, naiomba Serikali yangu sikivu ione umuhimu wa kupata Jimbo la Uchaguzi sambamba na Jimbo pia tupate Wilaya ya Kigamboni kwani idadi ya watu takribani 800,000, vigezo tumefikia na michakato tayari, naomba Serikali yangu ifanye maamuzi magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la wizi wa ardhi ambao wananchi wetu wanatapeliwa na wafanyabiashara ambao wao hawana mtaji wanatumia ardhi ya wananchi wetu kama mitaji yao kwa kisingizio cha kupata faida ya kuwa na hati miliki.

Halmashauri ya Temeke inashirikiana na Ardhi Plan. Mradi huu una matatizo makubwa kiasi cha kutugawa Madiwani na wengine kudhalilishwa pale tunapotaka kuuliza taratibu za mradi huu unakosa nafasi kwa kunyimwa kwa makusudi usiweze kuhoji sababu hazieleweki. Binafsi mradi huu unanitia mashaka makubwa sana. KDA ndio wasimamizi wa eneo je, wameruhusu haya yafanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mipango mingi ya maendeleo yote yamewezekana kwa usimamizi madhubuti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na utendaji makini wa Waheshimiwa Mawaziri wanaosimamia sekta zilizoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ustawishaji Makao Makuu, kazi nyingi zilizofanywa na CDA zimeboresha sana ustawi wa Mji wa Dodoma. Wananchi wa Dodoma wanashukuru sana kwa kazi za kuendeleza miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maombi ya kata Mpya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilikwishaleta maombi ya kugawa kata mpya tisa (9) kwa ajili ya kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Ombi letu ni kupatiwa majibu ya maombi hayo kwa kutukubalia kupata kata hizo mpya. Kata zinazohusika kugawanywa ni:-

Manchali, Buigiri, Msamalo, Dabalo na Haneti, mchakato wa kuzipitisha Kata hizo kwenye vikao vyote vya Wilaya na Mkoa ulikwishakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pia naomba sana katika mapendekezo tuliyoleta ya kugawa Kata na Vijiji, Wilaya ya Uyui yasaidiwe kupata ruhusa ya kugawa.

Tarehe 8 Januari, 2013, Mheshimiwa Rais aliahidi kuigawa Wilaya ya Uyui. Mchakato mzima tumekamilisha na kikao cha RCC kimeridhia, naomba sana ahadi ya Rais itekelezwe ili wananchi waendeleo kuwa na imani na Serikali ya CCM ili uchaguzi mwakani uende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu zilizokuwa zinajengwa kwa kiwango cha lami Tabora – Puge, Puge – Nzega, Tabora – Nyahua – Ifigi, Tabora – Ndoni, Ndoni – Urambo zote zimesimama, naomba Serikali ilipe madeni ya Wakandarasi ili kazi iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana maji tunayoyategemea kutoka Shinyanga mradi uanze kutekelezwa kwa sababu Wilaya nne zitanufaika na mradi huo, Wilaya hizo ni Nzega, Igunga, Uyui na Tabora mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajali hapa nchini linamaliza maisha ya Watanzania wengi sana. Kila mwaka ajali zinaongezeka, vifo vinaongezekana na majeruhi wanaongezeka. Watu 8,153

kupoteza maisha kwa ajali za gari tu kwa miaka miwili 2012 na 2013, ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali ichukue hatua za haraka kwenye ajali hizi za barabarani. Vyanzo vya ajali hizi vinafahamika na viko wazi kwa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali iliongeza faini za adhabu za madereva wanaotenda makosa barabarani kwa lengo la kupunguza ajali, je, hili limepunguza ajali? Mbona zinaongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa Serikali ambao ni askari *traffic* barabarani hawafanyi kazi yao kikamilifu, magari mabovu yanapita mbele yao wao wanachukua fedha kwa madereva, magari yanaendeshwa *speed* kubwa wakikamatwa wanatoa rushwa kwa *Traffic* wanaachiliwa, wanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari yanayosababisha ajali hawapewi adhabu kubwa za kutoa fundisho kwa wamiliki na madereva ili waheshimu sheria. Serikali ichukue hatua madhubuti kupunguza ajali hizi zinazomaliza maisha ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madereva wengi wa pikipiki hawana mafunzo yoyote na sheria za barabarani hawazifuati, pamoja na lengo zuri la Serikali kuruhusu pikipiki kubeba abiria ili kusaidia ajira kwa vijana na kutoa usafiri maeneo ya vijijini. Kwa hali hii ni lazima Serikali itazame nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa TAMISEMI mwaka jana 2012/2013, Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya jumla ya sh. 362,206,000,000/= . Katika makusanyo walikusanya sh. 117,292,888,960.91, sawa na asilimia 38.4 ya malengo. Hotuba ya mwaka huu takwimu zimebadilika za mwaka jana. Makadirio yalikuwa bilioni 324.4, makusanyo yakawa shilingi bilioni 240.9, sawa na asilimia 73.4 kwa mwaka huo 2012/2013, kati ya takwimu hizi zipi ni za uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya Taifa. Zoezi hili linakwenda taratibu sana sana kwa miaka miwili sasa utambuzi umefanyika kwa Mikoa miwili tu *that is* Dar es Salaam na Zanzibar na kwa watumishi wa umma na vyombo vya Usalama ambao kwa ujumla ni asilimia ndogo sana ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu aeleze Bunge kwa *speed* hii itachukua muda wa miaka mingapi kwa Watanzania wote kupata vitambulisho vya Taifa? Je kwa *speed* hii gharama hazitaongezeka na hiyo fedha iliyotengwa kutotosha kukamilisha kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali imetoa sh. billion 9.5 kwa wajasiriamali, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana bilioni 1.22 na mfumo wa maendeleo shilingi bilioni 5.44 kwa wanawake 500,000 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri Mkuu anahitimisha hoja aeleze Bunge hizo fedha za makundi hayo zimekwenda katika Mikoa mingapi na ipi na pia katika Wilaya ipi na idadi gani ya walengwa walionufaika na fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Serikali yamekuwa yanaongezeka sana na hayo kusababisha fedha nyingi kwenda matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kukosa fedha. Hatuwezi kuondoa umaskini kwa Watanzania kwa kuendelea kutenga fedha kiduchu kwenye miradi ya maendeleo ambayo iko kule vijijini na ndio inatoa huduma. Mheshimiwa Waziri Mkuu aeleze Bunge ni mikakati gani ameweka kupunguza matumizi ya Serikali?

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Uchaguzi hivi sasa inakabiliwa na mambo matatu makubwa, jambo la kwanza Tume inapaswa kuboresha daftari la wapiga kura. La pili kujitayarisha kwa ajili ya kura za maoni kwa Katiba mpya itakayopendekezwa na la tatu ni uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zote hizo zinahitaji fedha nyingi ili Tume iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Uchaguzi mwaka jana ilihitaji shilingi bilioni 371 kwa ajili ya kuboresha daftari la kufunga kura na kura za maoni. Licha Tume kuelewa mahitaji yake, lakini jambo la kusikitisha bajeti ya mwaka jana 2013/2014 iliomba iidhinishwe Sh. 5,531,727,000/=. Ninachotaka kuelewa kwa nini Tume iliomba fedha hizo ilielewa kuwa mahitaji yake ni shilingi bilioni 371.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la kushangaza zaidi Tume iliidhinishwa Sh. 5,531,727,000/=. lakini mpaka Machi, 2014, Tume imepatiwa sh. 15,727,017,991.96. Ninachotaka kuelewa idhini ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge ziliidhinishwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziada ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge sikubaliani kuambiwa kuwa yalikuwa matumizi ya dharura kwani mahitaji ya Tume yalikuwa shilingi bilioni 371 kama wangepewa kima hicho basi tatizo hilo lisingetokea.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume kwa mwaka wa fedha 2014/2015, inahitaji sh. 761,462,903,911/=, lakini fedha iliyoombwa na Tume kwa kipindi hicho ni sh. 7,071,305,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo ni kweli malengo yaliyokusudiwa na Tume kwa kipindi cha 2014/2015 ya kuboresha daftari la wapiga kura mara mbili, kuendesha kura ya maoni na kuendesha Uchaguzi Mkuu wa 2015? Kama fedha hiyo itapatikana matumizi ya fedha kwa kiwango hicho yatakuwa yameidhinishwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayoombwa na Tume kwa mwaka 2024/2015 ni sh. 7,071,305,000/= na ni kwa sababu gani Tume haikuomba fedha kwa mujibu wa mahitaji yake ambayo ni ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Serikali ituambie kwa nini iwe na utaratibu huo ambao unaonekana kuwa bajeti ya 2013/2014 na 2014/2015 wa kuweka mazingira ya kuweza kutumia kinyume na fedha zinazoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa urahisi wa kuwasilisha nimeona nitume dondoo kutoa hoja zangu kwa ufupi. Kutokupatikana au kucheleweshwa fedha za miradi ya maendeleo. Kwa miaka mitatu sasa Serikali miradi mingi imekosa fedha au inaletwa fedha chini ya asilimia 30. Jambo hili limewakwaza wananchi kumaliza miradi yao na kuwa na viporo kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri iwapo fedha za miradi zimeonekana hazikupatikana mapema mradi huu uangaliwe upya (*the development project be reviewed*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora, nini nafasi ya Wakuu wa Wilaya katika kazi ya kila siku? Wakuu hao wanawaingilia kazi Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwenye shughuli zao hata mpaka kudai fedha za usafiri kama Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgongano wa maslahi katika uendeshaji wa Halmashauri, nashauri Sheria ya Maadili ya Viongozi isimamie fika kwani Madiwani wengi wanafanya biashara na Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zabuni za ushuru wa kuegesha magari mijini (*Car park levy*) na *Parking fees*; kwa kuwa huu umekuwa kadhia kubwa kwa watumia magari, nashauri kazi hii ifanywe na Halmashauri zenyewe na

Jeshi la Polisi. Kwa jinsi mambo yalivyo sasa fedha nyingi za Halmashauri zinaibiwa na magari ya watu yanafungwa minyororo bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kurudisha mamlaka ya kuajiri kada ya chini ya wafanyakazi wa Halmashauri kwenye Halmashauri.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muungano, ukurasa wa 13 nipongeze Serikali kwa kusherehekea miaka 50 ya Muungano. Pili, kwa kipindi kirefu Serikali zetu mbili zimekuwa zikifanya juhudi za kurekebisha kero za Muungano na kwa taarifa tu kero nyingi zimeweza kutatuliwa, lakini hata wananchi wengi hawaelewi kero hizo zilizopata ufumbuzi. Hivyo, naishauri Serikali ikaandae utaratibu maalum wa kuwaelimisha wananchi hao, kupitia vyombo vya habari, mikutano ya hadhara, makongamano na vitabu maalum. Naamini wananchi wakielimishwa kwa utaratibu huo wataweza kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Bunge, nalipongeza Bunge langu kwa kuweza kufanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa, pamoja na kuwathamini Wabunge. Hata hivyo, kuna suala la siku nyingi la ujenzi wa ofisi za Wabunge, suala hili kwa kweli linahitaji msukumo binafsi baina ya watu husika na Mbunge mhusika wa Jimbo, kwa kushirikiana kwa pamoja kwa hatua za awali za kupatikana kwa viwanja ambapo Mbunge ataweza kutoa mchango mkubwa wa upatikanaji wa kiwanja na baada ya hapo utaratibu wa ujenzi utaweza kuanza. Naomba niarifu kwamba wananchi wanapata shida za kuonana na Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho vya Taifa, ukurasa wa 18; naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya kuwapatia vitambulisho wananchi wake. Hata hivyo, nashauri utaratibu huo ukarahisishwa na kukamilika kwa haraka. Hata hivyo, napenda kuishauri Serikali kutoa upendeleo wa pekee kuwapa vitambulisho vya Taifa kwa wanafunzi wanaopewa mikopo ya elimu, kwani kumekuwepo na matatizo ndani ya Wizara ya Elimu ya kuwafuatilia wale waliopewa mikopo na hawalipi, hivyo wakipewa vitambulisho hivyo, Serikali itaweza kuwafuatilia kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF). Naipongeza Serikali kwa adhima yake nzuri ya kuwawezesha wananchi katika Mfuko huo. Hata hivyo, lengo na adhima hii ya Serikali inaingia dosari pale watendaji wanapovuruga kwa makusudi wakati wananchi wanapotaka huduma yaani usumbufu unakuwa mkubwa sana. Hivyo nashauri Serikali kulisimamia suala hili kwa ukamilifu na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala Bandari, ukurasa wa 58. Ni muda mrefu Serikali imekuwa ikieleza kwamba itajenga gati namba 13 na 14, lakini cha kushangaza katika mipango ya Serikali katika bajeti ya 2014/2015 hakuna maelezo na hata Serikali ilipowasilisha mpango kule Dar es Salaam haikuelezwa kuwa gati hizo zitajengwa. Hivyo, naomba kuuliza ni lini Serikali itaanza kujenga gati Namba 13 na 14?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya tabianchi tumeshuhudia maeneo mengi ya nchi yakiwemo Jiji la Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya na kadhalika yakikumbwa na mafuriko ya mara kwa mara. Mafuriko hayo yanasababisha uharibifu wa miundombinu, ikiwemo reli, barabara, makazi, madaraja, mashamba na kugharimu maisha ya watu na mali zao. Athari nyingine za mafuriko ni pamoja na njaa, milipuko ya magonjwa, gharama za kuhamisha na kutunza waathirika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri; mafuriko yanayoleta maafa yote hayo yanaweza kudhibitiwa kwa kujenga mabwawa makubwa ya umwagiliaji na kudhibiti mafuriko (*Irrigation and Flood Control Dams*). Mabwawa hayo yakisanifiwa kwa ufasaha na kujengwa vizuri yanaweza kusaidia kutoa majibu ya changamoto zifuatazo:-

- (1) Maji yanaweza kutumika kwa kuzalisha chakula.
- (2) Maji ya mabwawa yanaweza kutumika kuzalisha malisho ya mifugo kwa kumwagilia “pastures” na kutoa maji ya kunywesha mifugo.
- (3) Namba mbili ikitekelezwa tutaweza kuchangia kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji.
- (4) Maji ya mabwawa yanaweza kutumika kwa matumizi mengine kama vile kuzalisha umeme na matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sasa sekta zinazohusika kuanza kubuni mradi mkubwa wenye mtizamo wa pamoja unaolenga kupunguza maafa wakati huo huo ukitatua changamoto nyingine. Aidha, mradi huo utaleta dhana ya kuzuia maafa kuliko kutibu madhara ya maafa.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zilizotolewa na ofisi hizi kuhusu bajeti zao za 2014/2015. Aidha, nakumbushia juu ya kilio cha wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kuhusu kuigawa Wilaya Manyoni na kuwa na Wilaya mpya ya Itigi ili kusogeza huduma kwa wananchi wa Jimbo hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio hiki kinazidi kupanda kadri tunavyoelekea uchaguzi Mkuu 2015. Natambua mchakato wa mapendekezo ya Wilaya mpya ya Itigi umefanyika na tayari mapendekezo hayo yamewasilishwa ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na mapendekezo ya Vijiji na Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua suala hili litafikishwa lini kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa uamuzi wake ili Wilaya ya Manyoni yenye ukubwa wa kilomita za mraba 18,000 na hususan baada ya Jimbo hili kufikia idadi ya wananchi wanaozidi lakini moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii ili nichangie katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nauuelekeza kwenye viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda ni chachu ya maendeleo kiuchumi, lakini hatuwezi kuzungumzia viwanda vikubwa na tukasahau viwanda vidogovidogo chini ya *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepiga kelele kuiomba Serikali kuboresha na kuisaidia *SIDO* kwa juhudi zote, lakini juhudi hazionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa Mikoa mipya nchini na Mkoa ambao umejaliwa kwa uzalishaji mali kwa shughuli za kilimo na ufugaji, lakini wananchi wengi wa Mkoa wa Katavi bado wanafanya biashara za mbegu za mazao. Kwa maana kwamba mfano, wanapanda karanga, wanavuna karanga na wanauza karanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko siyo rahisi kumuinua mkulima anayetaka kupata faida ya mazao yake. Mkulima anapashwa kupata faida katika kuuza mazao yake tena mara mbili. Akilima karanga avune karanga na auze mafuta. Pia makapi auze kwa mfugaji wa mifugo ili apate faida mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo naiomba Serikali kama ina nia ya dhati ya kumkomboa mwananchi masikini, *i-support* na kuisaidia *SIDO* nchini ili *SIDO* iwakomboe wananchi wafanyabiashara wadogo wadogo, hasa vijana waliomaliza darasa la saba na kushindwa kuendelea na *Secondary School*, pia waliomaliza kidato cha nne na kushindwa kuendelea na elimu ya juu ambao ni wengi hawana ajira na kubaki mitaani kwa shughuli za biashara ndogondogo na kuitwa majina ya wahuni vibaka nakadhalika. Hii *SIDO* ikiimarishwa kwa

kusaidiwa na Serikali itawakomboa sana makundi haya kwa mafunzo na mikopo midogo midogo, pia wanawake nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la UKIMWI nchini. Suala la UKIMWI ni suala pana sana nchini. Pamoja na Serikali kupambana na UKIMWI kwa kuhakikisha tunafikia sifuri tatu kwa maana ya (a) vifo sifuri, (b) maambukizi sifuri na (c) unyanyapaa sifuri, lakini hatuwezi kufikia hatua hiyo kama (a) hatutokuwa tayari kutoa elimu majukwaani (b) hatutokuwa tayari kuwazungukia wananchi hasa vijijini kutoa elimu ambako elimu haiwafikii sana (c) kuzuia unywaji pombe asubuhi au saa za kazi na badala yake *Bar* za pombe zifunguliwe jioni (d) nyumba za kulala wageni zipewe sheria ya kutoruhusu nyumba hizo kuwa sehemu ya kufanyia biashara ya ngono kama ilivyo sasa hivi chumba kimoja kinaweza kukodisha wateja wa biashara ya ngono hata mara saba kwa siku, wanaingia hawa na wanatoka hivyo hivyo, hii ni hatari, Serikali iweke sheria kali na tunaweza kufanikiwa kupambana na janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imechukua hatua zipi kwa *Guest House* zinazofanya kukodisha biashara za ngono holela wakiwemo wanafunzi? Naomba nipatiwe majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mpango wa MMES II. Mpango huu ambao ni mahususi kuziwezesha shule zetu kujiendesha katika maeneo ya utawala wa ununuzi wa vitabu na shughuli za mitihani bado kuna changamoto kubwa sana katika matumizi ya fedha hizo na nidhamu katika utoaji wake, wakati lengo la mpango huu ni kutoa sh. 25,000/= kwa kila mwanafunzi. Kumekuwa na ufujaji mkubwa sana wa fedha hizi kuanzia Hazina Kuu, kwenye Halmashauri zetu na kwenye shule zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfano mzuri ni utafiti uliofanywa na Haki Elimu mwaka 2012 unaoonesha kwamba, kwa mwaka huo Serikali ilipokea fedha zote toka Benki ya Dunia na hivyo kutoa sh. 25,000/= toka Hazina kwenda kwenye Halmashauri, lakini cha kushangaza fedha hizo zilianza kudokolewa hapo hapo Hazina na mpaka kufika shuleni zilifika sh. 11,000/= tu. Je fedha hizo zilipotelea wapi? Nani huwa anadokoia fedha hizi kila mwaka? Je, hatua gani zimeshachukuliwa kwa wafujaji wa fedha hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali itoe majibu ya kina juu ya hilo! Mfano mahususi wa fedha hizi za MMES II, ni katika Halmashauri mpya ya Ikungi, Singida. Halmashauri hii ina jumla ya sekondari 32 na jumla ya wanafunzi 8571. Bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2013/2014 ni sh. 153,000,000/=, badala ya sh. 214,275,000/= ambayo ndiyo stahili ya kila mwanafunzi kupata 25,000/=, lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

mpaka leo hii zimetolewa sh. 79,000,000/= tu, kwa maana hiyo ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kupata sh. 9,217/= tu.

Swali, kama fedha hizi (25,000/=) nusu yake inatakiwa kununua vitabu vya sayansi na hisabati na nusu nyingine ni kwa ajili ya utawala wa shule na kulipia mitihani, hii sh. 9,217/= itafanya kazi gani ili shule ziweze kufanya kazi yake sawasawa? Kwa hali hii si ni kumpa mzazi mzigo mkubwa wa michango isiyokoma na Serikali kutumia hata hizo fedha za wafadhali? Naomba majibu ya uhakika ni kwa namna gani Halmashauri ya Ikungi itafanya kazi yake sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, matatizo ya Halmashauri mpya pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha Halmashauri mpya ili kusogeza huduma kwa wananchi, Halmashauri hizi zimekuwa kama yatima kwa kukosa huduma, mfano, katika Halmashauri ya Ikungi, kabla ya kugawanywa ofisi zake zilikuwa Singida Mjini, lakini baada ya kugawanya Halmashauri ya Ikungi ilibidi ipewe agizo la kuhamia Ikungi haraka iwezekanavyo, hii imesababishia Halmashauri hii kupanga ofisi kwa sh. 1,500,000/= kwa mwezi kabla ya kujenga ofisi zake.

Ukiangalia kwa jinsi mtiririko wa fedha ulivyo ni shida kubwa kwa Halmashauri hii kupanga ofisi na wakati huo huo ijenge ofisi yake, pamoja na kwamba kiwanja tayari kipo. Tatizo lingine ni uhaba wa nyumba za watumishi na kikubwa zaidi ni kutolipwa mafao kwa watumishi waliohamia Wilaya hii mpya ya Ikungi mpaka leo hii. Ni kwa nini haki hii ya mafao bado haijatekelezwa mpaka sasa? Je, tatizo ni nini? Naomba nipewe jibu la uhakika kwamba ni lini watumishi hawa watalipwa stahiki yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ajira kwa Walimu wapya; kumekuwa na malalamiko makubwa toka kwa wanafunzi waliohitimu Vyuo vya Ualimu kutokupata ajira mpaka sasa ili hali tuna upungufu mkubwa sana wa Walimu nchi nzima. Tatizo ni nini kwa Walimu hawa kutokupata ajira? Napenda kukumbusha tena, kulikuwa na pendekezo la kuanzisha chombo kimoja au Tume ya kusimamia matatizo ya Walimu kote nchini.

Cha kushangaza tunasikia mchakato unaendelea, huu mchakato utamalizika lini? Kwa kutokuwa na chombo kimoja cha kusimamia Walimu ni kuchelewesha haki ya Walimu na kutowatendea haki kama walivyo watumishi wengine, maana ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *change* ya rada, fedha hizi zilipangiwa kazi ya kununua vitabu kwa shule zote za Tanzania, basi kwa nini mpaka sasa bado kuna upungufu wa kutosha wa vitabu nchini kote? Je, mpaka sasa ni vitabu vingapi vimenunuliwa kwa fedha hizi ni shule ngapi na kwa majina zimefaidika

kwa change ya fedha hizi? Kama siyo fedha hizo zimefanya kazi gani? Naomba majibu ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SAID A. ARFI: Mshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na Serikali kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu, lakini kumekuwepo na mtawanyo mbaya wa Walimu waliopo kati ya shule za mjini na vijijini na kuendelea kuwa na pengo kubwa la upungufu wa Walimu vijijini, ni vyema sasa yakatolewa maelekezo mahususi ya eneo hilo. Aidha, pamoja na Bunge kuidhinisha na kupitisha fedha za matumizi na maendeleo katika ofisi yako, inasikitisha fedha hizo hazipelekwi katika Halmashauri nyingi hasa za maendeleo, hivyo miradi mingi kutokamilika na kuongezeka kwa gharama za mradi. Ni vyema na inapendeza kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha ili maana ya kuwepo na mpango wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali uwe na uhalisia badala ya kuwa na tarakimu tu lakini hakuna fedha inayopelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya umwagiliaji Wilaya ya Mpanda kutopelekwa fedha na kukamilika kwa miradi hiyo kupunguza umaskini wa wananchi na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kwa maoni yangu miradi ambayo ina uhakika wa uzalishaji ningepewa kipaumbele hususan miradi iliyopo katika Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mpanda - Tabora na Mpanda - Kigoma ni muhimu katika kutekeleza azma ya Serikali kuunganisha Mikoa kwa barabara za lami. Barabara hizi zinaunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Kigoma, fedha inayotengwa ni kidogo mno, ni vyema Serikali ikaangalia eneo hili hata kukopea ili kuzijenga kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kuhusu Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ina wataalam 35 nao wanahitaji kujengewa uwezo ili waweze kukabiliana na changamoto zilizopo. Tume hii ya Mipango ambayo ndiyo tegemeo letu la kutukwamua kiuchumi, utendaji wake unazorota kutokana na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina. Katika kipindi cha mwaka uliopita Tume ya Mipango imepata asilimia 42% katika fedha walizopangiwa, hili ni tatizo litatuliwe ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ina shida ya watumishi wengi sana hasa kwenye utafiti. Naishauri Serikali iweze kuiwezesha Tume ya Mipango ili ikwamue nchi yetu kwenye uchumi.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maslahi ya Walimu lipewe kipaumbele kwa kuondokana na madeni ambayo Serikali inadaiwa kwa muda mrefu. Serikali iangalie upya kuwapatia Walimu *Teaching Allowance* kama motisha jambo ambalo huko nyuma lilikuwepo na wao wapo radhi sana endapo watapatiwa motisha hiyo itaondoa manung'uniko ya kuona wanasahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la Walimu wanaostaafu kutolipwa nauli za kurudi makwao kwani hiyo ni stahiki yao, *PSPF* wanafanya vizuri kwa kuwapatia cheki zao bila usumbufu wala kuchelewa, sasa suala la nauli ni vema likawa linaandaliwa mapema, kwani wanaostaafu wanafahamika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa shule za Sekondari ambazo zinachukua wanafunzi wenye ulemavu wa macho na ulemavu wa ngozi (*Albino*). Nashauri Serikali shule hizi zenye vitengo vya walemavu, bajeti za hao wenye ulemavu zitolewe zote ili kuwasaidia kuwawezesha kufanikisha mahitaji yao hususan upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia hivyo kutawatia moyo Walimu wanaowafundisha wanafunzi hao.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kusimamia na kuhimiza maendeleo ya wananchi. Pili, natoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Rombo kwa hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali katika sekta za afya, elimu na maji katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ya Waziri Mkuu imejikita katika mambo mengi, naomba kusema kwamba naiunga mkono na nampongeza pamoja na Waziri, Manaibu Waziri na watendaji wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mipango mingi na miradi mingi ya maendeleo inaathirika kutokana na ukosefu wa fedha. Kutokana na hayo nashauri kwamba:-

- (1) Serikali iweke mkakati wa nguvu wa kukusanya mapato yake.
- (2) Kuzuia mianya mingi ya upotevu wa mapato, hasa tozo mbalimbali.
- (3) Kubuni vyanzo vipya vya mapato.
- (4) Kupunguza matumizi ya Serikali hasa yale yanayotokana na matumizi yasiyofaa ya magari.

(5) Kuiangalia upya Sheria ya Manunuzi ambayo inatumika vibaya na watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo mapato ya Serikali yanaweza kuongezeka na kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hotuba ya Waziri Mkuu ni mtambuka, nilitegemea sana iguse hifadhi ya mazingira. Hivi sasa maafa hasa yatokanayo na mafuriko na ukame yamezidi sana. Haya yanatokana na uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miti ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili halitaangaliwa nchi iko hatarini kugeuka jangwa na Serikali kutumia fedha nyingi nje ya bajeti kwa ajili ya maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Maji kwa msukumo wake katika kuwapatia wananchi wa Rombo maji. Hivi sasa visima vitano vimechimbwa na Mamlaka ya Bonde la Pangani, lakini Halmashauri inahitaji sh. 300,000,000/= kwa ajili ya kujenga miundombinu hasa ya umeme. Visima vitano tenda zimetolewa lakini hata hivyo upatikanaji wa fedha ni wa kusuasua sana. Tunaiomba Serikali kutoa fedha na hasa hizo za ujenzi wa miundombinu ili tufaidike na ahadi hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu bado Walimu wana malalamiko kuhusu madai na haki zao. Hali kadhalika Idara ya Ukaguzi imekufa kwa sababu ya ukosefu wa vitendea kazi, tunaomba tupatiwe gari kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama hivi sasa wananchi wamejitolea kujenga Vituo vya Polisi katika Kata ya Mahida, Mengwe, Kirongo Chini na Shimbi. Tunaimba Serikali kuwatia wananchi moyo kwa kutoa fedha ili kumalizia vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahimiza sana vijana kujiajiri wengi wamejinunulia pikipiki zao, lakini vijana hawa wanakamatwa kiholela na kutozwa faini kubwa, wengine wanapigwa sana na kuumizwa. Hali hii tumeshailalamikia katika Mamlaka za Wilaya na za Kipolisi, lakini bado hatua hazichukuliwi. Tunaiomba Serikali kutoa tamko la kukomesha unyanyasaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wananchi wa Rombo tunalalamika kwa kutoona faida ya Mlima Kilimanjaro ambao uko katika Wilaya yetu. Imekuwa jambo la kawaida wananchi kukimbizwa kuzima moto, lakini wanaofaidi ni wengine. Tunaiomba Wizara iweke utaratibu wa wazi wa namna Halmashauri

ya Rombo na zile ambazo zinauzunguka mlima zitakavyofaidika na mapato ya Mlima Kilimanjaro.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa limekuwa upatikanaji wa fedha hasa za maendeleo ndio bado iko nyuma sana kimakusanyo ukilinganisha na nchi za jirani, hivyo kushindwa kujitegemea kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili nyuma nilitoa wazo kupanua ukusanyaji na kuwahusisha hata wafanyabiashara ndogondogo. Siyo siri Wamachinga wengi mali wanazouza ni za wafanyabiashara wakubwa na wanawatumia wao kukwepa kodi. Dar es Salaam kuna Wamachinga takribani laki moja, leseni ya sh. 200/= kwa siku ni sawa na milioni 20 kwa siku, milioni 600 kwa mwezi na bilioni 7.2 kwa mwaka.

Pili bado hakuna mpango madhubuti wa kuhakikisha wenye nyumba wote wanalipa *Property tax*. Niliwahi kutoa wazo la kuwahusisha Wenyeviti wa Mitaa kuhakikisha wanakagua nyumba zote, lakini pia nilitoa wazo la kutoa hata asilimia moja kwa Mitaa kwa maendeleo yao. Hii ingekuwa ni chachu ya kuongeza makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengi sana ya ardhi kwenye Manispaa nyingi baina ya wakulima na wafugaji, wakulima na wawekezaji, lakini pia wananchi na Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa kadhaa zimekuwa zikinyang'anya ardhi za watu kwa kuwarubuni na kuwatisha kuwa wamebadilisha matumizi, hivyo wanapaswa kuuza/kutoa kupimwe uwanja, lakini wananchi wanalipwa fedha ndogo sana na kuwatumbukiza kwenye dimbwi la umaskini na wanaoneemeka ni viongozi na wafanyabiashara. Ni kwa nini Serikali isiwaelimisha wananchi juu ya hali yao badala ya kuwaacha wakitapeliwa na kudhulumwa ardhi yao na viongozi wa Manispaa. Hili ni tatizo katika sehemu nyingi; Temeke/Kigamboni, Bagamoyo, Ikwiriri na kwingine kwingi tena wakati mwingine walisingizia eti Jeshi wanataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua za mwaka huu zimeleta maafa makubwa sana Dar es Salaam na zimeharibu miundombinu ya barabara na kurudisha msongamano kuliko ulivyokuwa. Je, Serikali ina mpango gani? Inajiandaa vipi kurekebisha hali hii kwa sababu Dar es Saalam inategemewa sana na nchi katika biashara mbalimbali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake na vijana bado wanahangaika na mitaji na kuboresha biashara zao ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo kwa Manispaa nyingi hasa zenye makusanyo makubwa kutoa ile asilimia tano, tano kwa vijana na wanawake. Ni kwa nini Serikali isibadili utaratibu ili hiyo asilimia tano tano ipelekwe kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ili basi kuhakikisha fedha zinatolewa. Hii kama ilivyo VETA inaweza ikasaidia zaidi kuliko hali ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa matunda wakati wa msimu, hii ni pamoja na nyanya, machungwa, mananasi, embe na kadhalika. Ni mpango gani Serikali itawasaidia wakulima hasa akinamama na vijana wanaolima mbogamboga na matunda watajikwamua. Sasa hivi sehemu kubwa inatupwa kwa kuharibika hasa sehemu zile wanazolima sana, ikiwa pamoja na Dodoma, Shinyanga, Arusha, Mbeya, Pwani, Dar es Salaam, hasa Kigamboni, Ukonga, Segerea na maeneo mengi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaondoa hasara kubwa wanayopata wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na nasisitiza kufanyiwa kazi masuala yanayotolewa mawazo na sisi Wabunge.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ya kuhimiza maendeleo ya watu wake. Naomba kuchangia maeneo mawili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi naipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kupima na kumilikisha ardhi kisheria. Hii itasaidia sana kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Watanzania sasa hivi ni zaidi ya milioni 45, ni wakati muafaka sasa hivi kuweka mikakati ya makusudi kuhakikisha ardhi yetu itabeba watu milioni 45 ya sasa na watu zaidi ya hao baada ya miaka 10 ijayo na kadhalika. Hivi sasa kuna jambo kubwa linalotisha na kusikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa ardhi maeneo ya wafugaji umeibua Ukabila kitu ambacho ni cha hatari katika nchi yetu na ambayo ilikuwa imefutwa na waasisi wetu. Wafugaji wanahitaji ardhi ya malisho, ambayo imelimwa yote na wakulima. Huko Mbulu, Yaeda Chini vita vimezuka baina ya Wadatoga na Wairaq. Wadatoga ni wafugaji na Wairaq ni wakulima, haijawahi kutokea watu hawa kugombana, sasa hivi wanauana shauri ya kugombania maeneo (Wadatoga (Barbaig) hawahami tena maana hawana

pa kuhamia. Huku Kiteto Wamasai wanapambana na Wagogo, Warangi, Wakaguru na Wakamba na kadhalika, watu wanauana kila kukicha shauri ya kugombea ardhi. Kule Sunya Wakamba wamechoma nyumba 42 za Wairaq ili kuwafukuza wabakie Wakamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatishia amani ya nchi yetu na kurudisha Ukabila, Serikali itoe kipaumbele katika kuwapimia ardhi jamii za wafugaji ili sheria ichukuliwe kwa watakaokiuka. Marekebisho ya sheria za kumiliki ardhi pia ufanyike haraka. Bajeti ya kupima mipaka ya vijiji hadi vijiji, Wilaya na Wilaya na kadhalika kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotueleza wafugaji hawawezi kuhamahama tena kama zamani kwa kuwa hawana pa kuhamia, kila ardhi ina mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa kisiasa kutochochea wananchi wavunje sheria tutumie nafasi zetu kuwaelimisha wananchi wetu badala ya kuwachochea. Ni budi wananchi tunaowaongoza wakaelewa sheria, kanuni na taratibu za kumiliki ardhi na kuheshimu mipaka ya kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Afya tunao vijana wetu wanaosomea Udaktari Bingwa katika hospitali zetu za rufaa KCMC, Muhimbili, Bugando na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu na tukizingatia kuwa ni Madaktari wetu tunaowajenga wawe Mabingwa. Ukweli ukitaka kumpata Bingwa lazima umjengee uwezo na msingi mzuri. Vijana hawa wanalalamikia kutolipwa sh. 10,000/= wanayopaswa kulipwa kwa siku, yapata miezi tisa sasa. Wako *frustrated* kupita kiasi, wanashindwa kuacha masomo kwa kuwa watakosa kazi, lakini hawafanyi vizuri masomo yao shauri ya kutolipwa fedha hizo. Wanashindwa kujikimu na hata kulipia *Thesis/Dissertation* zao kwa kutolipwa fedha hizo. Naiomba Serikali kupitia bajeti ya Wizara ya Afya ifanye hima kuwalipa fedha zao hao vijana kuepuka migomo isiyo ya lazima. Naomba kauli ya Waziri Mkuu katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kituo cha Afya Dongobesh, Wilaya ya Mbulu. Kituo hiki cha Afya Dongobesh ni cha muda mrefu sana na kinahudumia watu wengi sana, lakini bila upanuzi wala huduma zingine za lazima. Kilio cha wananchi wa Dongobesh katika bajeti ya mwaka huu, ni kuomba Serikali ipanue kituo hiki, ikiwezekana kuwa hospitali, lakini muhimu sana ijengwe chumba cha kuhifadhi maiti (mochwali).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bajeti hii iwe *realistic*, tuzingatie kilio cha wananchi na hapa ni wananchi wa Dongobesh, Wilaya ya Mbulu. Upanuzi wa

kituo na ujenzi wa mochwali. Naomba kauli ya Waziri wa Afya katika haya niliyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri mpya ya Igalula tumeleta maombi ya kugawanywa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui (Tabora) kuwa Wilaya mbili baadaye za Igalula na Uyui kwani vigezo vinatimia. Kugatua madaraka kwa wananchi kutawezekana tukianza na Halmashauri mbili na hatimaye Wilaya. Tunamwomba Waziri Mkuu utaratibu ukamilike haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Afya; Wilaya ya Uyui haina Hospitali ya Wilaya halikadhalika Jimbo la Igalula halina hata kituo cha Afya katika Kata zote kumi. Hali ni tete Serikali ituone tupate hospitali ya Wilaya na vituo kumi vya Afya kati ya Vijiji sitini, zahanati ziko 16 tu, kati ya hizo uhaba wa Wauguzi ni mkubwa sana. Wauguzi (A.M.A) sita na Manesi wanne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji na umwagiliaji; pia mabwawa, majosho, visima tisa vijiji 60. Tatizo la maji ni kubwa yaliyo safi na salama. Visima virefu Kata za Tura, Kizengi, Goweko na Nsololo vinahitajika, visima vya kati Kata za Miyenze, Kigawa, Igalula na Lutende pia Miswaki na Loya. Mabwawa Goweko, Loya, Miswaki na Nsololo kwa kunywa mifugo na umwagiliaji mashamba ni muhimu sana na baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora posho za watendaji wa Vijiji na Vitongoji ni muhimu kwa utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu; nimeahidiwa maabara na TAMISEMI kwa sekondari za Goweko (2013/2014) na Tura (2013/2014), naomba maabara zijengwe 2014/2015 nimeona kwenye *extract* kwamba kuna pesa za maendeleo ya Elimu ya Sekondari *subvote* 8091 *line terms* 4390 na 6277 Ukurasa 231 *Volume IV* pesa kwa kila Sekondari sh. 80,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu DART mfumo wa usafiri Chanya (*Multimodel*) kwa kutatua msongamano Jiji la Dar es Salaam:-

(a) Barabara za pete (*Ring roads*).

(b) Barabara Lishe (*Feeder Roads*).

(c) *Trans* pamoja na mabasi yaendayo kasi DART katika barabara ile ile ila yatumie umeme kuhifadhi usafiri wa hewa (*Air Quality*) Dar es Salaam.

(d) *Fast Rail* – Treni za kasi, Sea Buses (mabasi ya baharini) Posta – Tegeta – Bunju – Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara zifanye mipango/usanifu (*planning na Design*) pamoja:-

(a) Uchukuzi.

(b) Ujuzi.

(c) TAMISEMI.

(d) Mipango ili hata *flyovers* zipangwe pamoja na mahitaji ya Wizara zote kwa miaka 40 hadi 50 hatimaye 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge ni la bajeti na si la Katiba, hivyo Mheshimiwa Mbowe hakuwa na mahali kusema alivyosema hapa Bungeni kwa dakika 53 ya saa ya saa moja.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi hotuba hii muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu. Ningependa nianze na suala la afya. Afya ni jambo muhimu sana kwa wananchi na nchi inaweza kuendelea kama wananchi wake watakuwa na afya njema, lakini liko tatizo kubwa sana kwenye vituo vyetu vya Afya na zahanati kutokuwa na huduma nzuri zikiwemo dawa, vifaa vya kutolea huduma. Pia liko tatizo la watumishi katika vituo hivyo na hii inasababisha wananchi wetu kukosa huduma nzuri za afya. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili lifanyiwe kazi kwa haraka ili tuweze kunusuru wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro, upo ujenzi unaendelea katika Mkoa wetu kwa muda mrefu sasa na hii inasababisha gharama za ujenzi kuendelea kuwa kubwa sasa ningependa kujua ujenzi wa chumba cha upasuaji na wodi ya wazazi umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nimekuwa naliuliza kila mwaka, najua Mkuu wa Mkoa wetu amekuwa akijitahidi sana, lakini fedha zinazohitajika ni nyingi sisi kama Mkoa hatutaziweza hasa ukizingatia bajeti zinazotolewa kwenye Mikoa yetu hazifiki kwa wakati na hazifiki zote kama zilivyopitishwa na Bunge letu. Nimwombe Waziri Mkuu afuatilie suala hili kwa umuhimu mkubwa maana akinamama wajawazito wanapata shida sana na hata wengine wameshapoteza maisha kwa kukosekana kwa chumba cha upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hayo machache katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

MHE. RACHEL MASHISHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuchangia kuhusu huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu. Ni kweli kabisa Serikali imeweza kuanzisha makazi 17 kwa ajili huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa makazi haya yamekuwa duni sana fedha hazifiki kwa wakati pamoja na madawa, hivyo kuihatarisha afya za wazee hao na makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, makazi yaliyopo Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga kwanza majengo yake tayari yamechoka sana wazee wale na wengi wao wana ugonjwa wa Ukoma wamekuwa wakipata shida sana yakiwemo madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa Ukoma ni tishio sana katika makazi hayo, kama Serikali inachelewesha pesa pamoja na madawa ni dhahiri wazee hao na walemavu hao wanateseka sana, lakini pia chakula ni cha shida mpaka inafikia hatua ya wazee kutoka katika makazi yao na kwenda kuombaomba mjini, kitu ambacho hakileti picha nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ihakikishe makazi haya yako katika hali nzuri, lakini fedha ziwe zinafika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ni kila kitu katika kusukuma gurudumu la maendeleo, nchi yoyote haiwezi kuendelea kama wananchi wake wanakosa madawa na huduma za afya, katika maeneo yao. Tatizo hili limekuwa sugu sana na imekuwa kama mazoea kuwa akienda hospitali au zahanati unaambulia *panadol* au *paracetamol*, zingine unaambiwa kanunue nje ya hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali/zahanati hazina Waganga/Wauguzi pamoja na madawa kweli? Basi ni bora madawa yakapatikana kwa wingi hata Wauguzi wawe kidogo ni sawa maana Wauguzi wakiwa wengi dawa hakuna, nini maana yake? Yote tisa kumi hospitali ya Mkoa inakosa hata mashine ya kupimia BP. Mwezi uliopita nilikwenda hospitali ya Mkoa Dodoma ku-check *pressure* usiku saa mbili niliambiwa hakuna *BP machine*! Nilistaajabu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ya kusikitisha sana, ni kila mwaka sasa pesa zimekuwa hazitoshi, hazitoshi, hazitoshi ni lini sasa zitatoshwa ili kunusuru maisha ya Watanzania walio wengi ambao ni maskini na kutupwa?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji Mijini pamoja na Mamlaka za Maji safi na usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa kutoa huduma kwa wakazi wake kwa wastani wa asilimia 80, bado kuna changamoto kubwa sana. Mfano, Mamlaka ya Maji – KASHWASA Serikali imetumia pesa nyingi sana katika mradi ule, lakini unaendeshwa kwa hasara kwa sababu bado watumiaji ni wachache sana kulingana na mradi wenyewe, hivi kuna ugumu gani wa kusambaza maji katika Mikoa ya Simiyu na Tabora pamoja na maeneo bomba linapopita ili wananchi wafaidi, lakini pia mradi uweze kujiendesha bila kuongeza gharama za mara kwa mara kwa Mamlaka za Maji Safi za SHUWASA (Shinyanga) pamoja na Mamlaka ya Maji Safi ya Kahama ambapo mwisho wa siku mtumiaji wa mwisho ndio anaumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka maji maeneo ya karibu yaliyobakia ili wananchi waweze kunufaika na mradi huo wa kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna matatizo ya ardhi katika maeneo mengi ya nchi yetu hususani baina ya wafugaji na wakulima, kimsingi ni tatizo sugu sasa na bado tunaona au kusikia vifo vikiendelea kwa ajili ya migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali itenge maeneo hasa ya wafugaji kwa asilimia kubwa ndio wamekuwa wakihamama na hivyo kusababisha migogoro. Naomba waangaliwe wafugaji hawa na wasidharauliwe kwani kumekuwa na matamshi yakisemwa kuwa “Wafugaji wamekonda kama mifugo yao” huu ni udhalilishwaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo makuu matano:-

Kwanza kabisa ni masikitiko juu ya Serikali kutokuwa na dhamira ya dhati na maendeleo ya nchi yetu. Tumeendelea kushuhudia fedha za maendeleo zikiwa ndogo sana hata theluthi moja ya bajeti nzima haifiki na mbaya zaidi hizi fedha hazitolewi kwa wakati na mpaka tunamaliza mwaka wa fedha hata nusu ya fedha zilizotengwa hazipelekwi. Cha ajabu fedha matumizi (*Public expenditure*) ni kubwa sana *almost 70%* na hizi fedha za matumizi zinatolewa kadri zinavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fedheha hasa tunaposhuhudia jinsi akinamama wanavyokuja na watoto hasa wakati wa kujifungua kutokana na sababu nyingi kama uhaba wa vituo vya afya/*dispensary* huko vijijini ambako barabara ni mbovu, kuja kuchukuliwa hadi hospitali ya Wilaya aweza poteza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

maisha. Pia hospital zetu za Wilaya hazina *theatre*/au zina *theatre* ambazo hazina vifaa mbadala/hazina *standby generator*, hazina vitanda/mashuka wagonjwa wanalala chini, wanabanana hata wanne kitandani. Haya vililetwa vibajaji vya miguu mitatu kama *ambulance* ambavyo ni *wastage of resources because sio applicable*. Huu ni mwanya mwingine wa kula fedha za umma kwa ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juu ya suala zima la kuwalipa fidia Watanzania ambao wanatakiwa kupisha maeneo yao kwa ajili ya matumizi mengine. Tumeshuhudia adha kubwa na kuwarudisha nyuma kimaendeleo wananchi hawa tumekuwa tukihangaika na kushuhudia hata mauaji, mfano, suala la watu wa *resolute* tangu 2007 wahama kuacha shughuli zao za maendeleo kuomba ardhi ili waachiwe JWTZ. Hadi leo hii wale wananchi hawajalipwa fidia wamerudishwa nyuma kimaendeleo hadi leo hii. Hivi kweli tunawatendea haki wananchi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kule *North Mara* kuna wananchi wamefanyiwa tathmini hadi leo hii ni zaidi ya miaka miwili hawajalipwa huu ni unyanyasaji na hawa wananchi wanaathirika na vumbi la shughuli za migodi na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni juu ya mauaji ya raia yanayofanywa na Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Mara na hasa Wilaya ya Tarime. Tumeendelea kusikia angalau wananchi wawili wakiuawa kila wiki katika mgodi wa *North Mara*, hii haivumiliki kama ni mualifu apelekwe Mahakamani, imefika wakati tutakataa udhalimu huu. Serikali iliahidi kutatua tatizo la ajira katika maeneo yale kwa kuanzisha maeneo ya kuchimba kwa wananchi wanaozunguka maeneo yale. Waliahidi hayo Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Wassira, Mheshimiwa Ngeleja baada ya mauaji ya wananchi watano, lakini wameacha kutimiza ahadi zao kama kawaida ya Serikali hii kuwalaghai wananchi wa Tanzania, wangukuwa wanauawa wanenu/ndugu zenu msingekaa kimya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juu ya maji jamani, ni kweli hizi *report* alizopewa Mheshimiwa Waziri Mkuu zinaakisi ukweli na je, amezipitia na kujiridhisha kabla ya kutusomea sisi? Maana wakati anazungumzia kuhusu suluhisho la maji vijijini ni uongo mtupu. Eti sasa ni mwanadamu kutembea chini ya mita 400 kutafuta maji? Jamani jamani vijiji gani hivyo vya Tanzania Zanzibar labda lakini kama ni Tanganyika ni dhahiri ni uongo mtupu. Vijijini kwetu tunatembea zaidi ya kilomita mbili mpaka saba kutafuta maji tunaamka usiku tunarudi mchana au jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoa zinavunjika sana, Serikali imechoka sana, ukija mjini maji ndio janga la Taifa kabisa mfano Jiji la Dar es Salaam maji ni

kitendawili, maji hayatoki kabisa watu wananunua maji maisha yanakuwa magumu zaidi kwa Watanzania maskini. Ni aibu sana kila siku *story* za utatuji wa maji Mheshimiwa Mnyika alileta hoja yake juu ya maji ikazimwa kuwa wanasuluhisha matatizo yote kumbe ni uongo mtupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge juu ya *operation* tokomeza. Tunataka kujua waathirika wamelipwa fedha zao?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu, Mizengo Pinda kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2014/2015 haijawezesha hatua za haraka na stahili kuhusu masuala niliyochangia wakati wa mjadala wa ofisi tajwa mwaka 2011, 2012, na 2013. Hivyo sioni sababu ya kurudia maelezo kwa kirefu ambavyo Ofisi ya Waziri Mkuu inayofahamu na inaweza kuyarejea katika *Hansards*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu stahili yasipotolewa kwa angalau nusu (50%) ya orodha hii yasipotolewa, nitaondoa shilingi katika mshahara wa Waziri Mkuu au nikikosa nafasi nitalazimika kuanzisha mchakato wa kuwasilisha hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi matatizo ya maji Jimboni Ubungo, hasa upande wa maeneo yanayohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu, sababu za matatizo yaliyodumu kwa miezi mitatu mfululizo katika maeneo ambayo yalikuwa yanapata mgawo, sababu za kuchelewa kwa ujenzi wa bomba toka Mlandizi mpaka Kimara wakati ambapo mkopo kutoka India na kwa nini ujenzi usigawanywe na kuharakishwa kama inavyofanyika katika bomba la gesi. Pia mgogoro wa maji Goba na lini mtandao wa mabomba ya Wachina utanza kutoa maji katika maeneo ya pembezoni ya Malamba mawili, King'ongo, Bonyokwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha mabasi Ubungo itolewe kauli ya kusitisha utoaji wa kiingilio cha sh. 200/= sawa na zaidi ya milioni tano kwa siku wakati ndani hakuna huduma muhimu na miundombinu ni mibovu kama ilivyoelezwa katika Hotuba ya msemaji wa Upinzani (TAMISEMI). Aidha, kauli itolewe ya kusitisha utaratibu wa *gate pass* kwa Mawakala wa mabasi ambao umekuwa chanzo cha uvunjaji wa haki za binadamu, kukosesha ajira wanawake na vijana na ufisadi Mahakama ya Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa miundombinu baada ya maafa ya mafuriko hasa Kata ya Msigari (Msingwa) ambayo mawasiliano yuamekatika, Makuburi (Makola) ambapo mawasiliano yamekatika Goba (Kulangwa) ambapo mawasiliano yamekatika, barabara ya Sinza mpaka Tandale na

maeneo mengine ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu tayari inayo barua. Mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wa Manispaa ya Kinondoni. Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya ujenzi watafanikisha matengenezo lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ijengwe, agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam la kuzuia bodaboda kuingia katikati ya Jiji kwa kuwa lina athari kwenye fursa za ajira na usafiri nafuu. Nguvu ielekezwe kuboresha usafiri husika kwa kutoa mafunzo na kuweka utaratibu wa udhibiti na si kupiga marufuku.

MHE. SILYESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa Kibaha Mjini, naishukuru Serikali yetu kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri bado kuna matatizo na upungufu mkubwa sana katika sekta za huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kibaha Mjini kuna tatizo kubwa na sugu la huduma za afya, kituo cha Afya cha Mkoani hakina majengo ya kutosha kiasi cha kufanya wafanyakazi viongozi kukosa ofisi, wodi ya kuzalia ni ndogo, haitoshi na wagonjwa wengi hulazimika kulala chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Mkoa ya Tumbi iko katika kitendawili kikubwa kinachostahili kuteguliwa na Serikali sasa. Kwanza, jengo jipya limesimama kwa takribani miaka mitatu sasa na kufanya jengo la awamu ya kwanza kushindwa kutumika na kuwa nyumba ya popo kama jengo la awamu ya pili halijakamilika basi awamu ya kwanza haiwezi kutumika maana miundombinu yake inaingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hii ambayo imeshapewa hadhi ya rufaa ina majokofu mabovu ya kuhifadhi maiti, mashuka machakavu na hakika bado huduma zake kutokana na ufinyu wa vifaa haiendani kabisa na hadhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ya Mheshimiwa Rais Kibaha mwaka jana aliahidi kutatua matatizo ya hospitali ya Tumbi na kituo cha Afya kwa Mkoani, lakini hadi leo bado utekelezaji haujafanyika. Namwomba Waziri Mkuu kwa makusudi kabisa atusaidie matatizo hayo yatatuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali kutekeleza mradi wa maji Vijiji 10, bado changamoto kubwa ni upatikanaji katika mabomba makubwa yatoayo maji Mto Ruvu hadi Dar es Salaam. Kuna ahadi ya mradi wa bomba kubwa la maji toka Mto Ruvu hadi Kimara ambalo litatupatia maji

ya kutosha, bado mradi huu unasuasua na hatujui utatekelezwa na kukamilika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu uhakikishe kuwa mradi huu unakamilika na majawabu ya maji yapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Kibaha, tunalo tatizo kubwa upande wa Mahakama ya mwanzo. Karne hii bado Mahakama ya mwanzo maili moja ni ya tope na ipo katika eneo la barabara, naomba Mahakama ijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gereza la Mkuza limezidiwa sana, wakati uwezo wake ni mahabusu 70, sasa linaweka hadi mahabusu na wafungwa 180, karibu mara tatu ya uwezo wake. Serikali ifanye mpango wa kupunguza idadi ya wafungwa magerezani na hasa mahabusu kwa kuharakisha kesi zao na kutoa adhabu stahili nje ya Gereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za mji wa Kibaha zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais bado ni kiasi kidogo kimejengwa, kati ya kilomita 10 za barabara za lami, hadi sasa ni takribani kilomita mbili na nusu tu zimejengwa naomba ofisi yako itusaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. ABDUSALAAM SELEMANI AMER: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua fursa hii kuunga mkono Hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutupa dira na mwelekeo mzuri wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naelekea kwenye Wizara ya TAMISEMI. Pamoja na juhudi ya Serikali kupeleka pesa za Miradi kwa Halmashauri zote nchini ili zitumike ipasavyo na kwa Miradi iliyotengwa, Miradi mingi hasa ya Afya, Elimu na Barabara, huwa inahujumiwa kwa njia moja au nyingine. Upande wa afya, madawa hayafiki kwa wakati mwafaka na elimu pia kuhusu ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu kwa Halmashari zetu haitolewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Ofisi ya TAMISEMI ifuatilie Miradi ya Ujenzi wa Barabara kwa karibu sana, kwani ni Miradi inayogharimu pesa nyingi sana za walipa kodi. Ningeomba itumwe Timu ya Wataalamu wakaangalie Miradi ya Barabara inavyohujumiwa na baadhi ya Wakandarasi ambao siyo waaminifu katika kutekeleza Miradi hiyo katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linaloikabili Halmashauri yetu ya Kilosa ni Kampuni zinazopewa Miradi ya Maji katika Vijiji Kumi. Kuna kampuni

zinazopewa *tender* ya kusambaza maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 800. Kampuni hii haina uwezo kwani mkataba umesainiwa mwezi wa Januari na akakabidhi mwezi wa Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni hii haina uwezo wa kutekeleza Miradi hii ya thamani kubwa. Mkandarasi huyo, mashine ya kufyatulia matofali anaikodi, tena ni moja tu. Sementi anasomba kwa pikipiki (bodaboda), mifuko mitano kila siku. Sasa hivi uwezo wa kuendelea hakuna, kasimama anasubiri *down payment*. Naomba mzifuatilie kampuni zote zinazopewa Miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ni maombi ya daraja ambalo tuliomba siku nyingi sana. Daraja hili ni Kero sana kwa Wananchi wa maeneo husika. Daraja la Mto Ruhemba ni kilio kikubwa kwa maeneo hayo. Kijiji hiki kina wakulima wakubwa wa miwa Bonde la Ruhemba na ndiyo tegemeo la kampuni ya sukari katika uzalishaji wa sukari. Chonde chonde, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliangalie kwa jicho la huruma daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba nichangie kwa kukumbusha mambo muhimu kuhusiana na Jimbo langu, ambayo kwa muda sasa nayasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ilione suala la posho za Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Viongozi hawa ni muhimu sana, naomba walipwe posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanja na fidia kwa Wananchi wa Kijiji cha Sokoine; nilieleza hapa bajeti ya mwaka 2011/2012 kuhusu tatizo la Halmashauri kutokuwapa kipaumbele cha kuwapatia viwanja Wananchi Wakazi. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu au Waziri wa Ardhi atoe tamko. Aidha, sasa imefika miaka minane, Wananchi hawajapata fidia na thamani imebadilika. Naomba TAMISEMI ilifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ni ndogo sana; hivyo, kufanya ujenzi kusuasua. Naiomba Serikali iongeze fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali Teule ya Bwangala, haipatiwi fedha. Mwaka uliopita haikupata fedha. Baada ya kuwa Teule, Hospitali iliomba watumishi walipwe mishahara na Serikali ili kupunguza gharama za uendeshaji. Kutokutoa fedha za madawa na mishahara kwa watumishi, kunapelekea gharama za matibabu kuwa juu na kuwashinda Wananchi na hata Sera ya

Wajawazito, Watoto chini ya Miaka Mitano, Walemavu na Wazee kutopata matibabu. Mwaka jana niliandika barua kwa Waziri wa Afya na nakala kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ombi langu Hospitali hii itengewe fedha za madawa na watumishi walipwe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya Bajeti ya nchi inapaswa kuelekezwa katika maendeleo ya jamii zaidi ya ilivyo sasa. Bajeti ya maendeleo ni ndogo sana, Serikali iangalie upya mwenendo wa bajeti yetu ili Wananchi waelewe kuwa Serikali yao inawahudumia basi bajeti ya maendeleo iongezwe hadi kufikia asilimia 40 ya bajeti nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikiwa, nashauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuwapa elimu wasimamizi wa fedha za Serikali. Hapa naelekeza moja kwa moja kwa watendaji wa vijiji kama wasimamizi wa miradi kule vijijini, Waheshimiwa Madiwani wapate elimu ya kutosha kuhusu fedha. Wao ndiyo wasimamizi wakuu wa fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ubadhirifu wa fedha hizi kwa sababu ya uelewa mdogo wa Madiwani walio wengi katika Halmashauri zetu. Madiwani wapate fursa za kila wakati kuhusu wajibu wao kama wasimamizi wakuu wa fedha za Serikali katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri Serikali ihakikishe skimu za umwagiliaji kule Mang'ole, Tarafa ya Eyari, inakamilishwa ipasavyo na kutatua migogoro inayoikabili sasa. Hatua za makusudi zichukuliwe haraka ili kunusuru kilimo cha umwagiliaji wa mazao ya biashara na chakula katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanja cha Ndege Manyara; naomba Serikali ione sababu ya kukiimarisha kiwanja hiki hasa katika hali ya utalii Kanda ya Kaskazini. Uwanja huu unatumiwa sana na watalii. Naomba Serikali iweke lami (*running ways*) za Kiwanja cha Ndege Manyara. Hii itaongeza sana mapato ya Serikali (utalii).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Kirurumu mpakani mwa Wilaya ya Karatu na Monduli, limekuwa tatizo kila mwaka. Naomba Serikali iweke mpango wa kudumu wa daraja hilo ambalo hutumiwa na watalii na watu wengi katika Ukanda wa Kaskazini. Mkondo wa asili wa maji uangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iipe Mamlaka ya Mji Mdogo wa Karatu, hadhi ya kuwa Halmashauri Kamili kwani vigezo kamili vyote vinavyotakiwa tayari vimetimia na maombi yalishakubaliwa na RCC. Naomba TAMISEMI ikubali Karatu iwe Halmashauri ya Mji wa Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya kuwa na Zahahati kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata, Karatu tumefanya vizuri sana, changamoto kubwa ni wataalam (Watumishi wa Afya). Ili kukabiliana na hilo, tumeanzisha Chuo cha Afya Karatu (Waganga na Wauguzi), lengo likiwa kukidhi Wataalamu hao. Naomba Serikali itupatie walimu kwa ajili ya chuo chetu, Madaktari Wakufunzi na Wauguzi Wakufunzi Karatu na pia itusaidie ruzuku kwa maendeleo ya chuo chetu.

MHE. HERBERT J. MTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Hotuba ya kina iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), juu ya mwelekeo wa kazi Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Mawaziri wake, wamekuwa wakitembelea Wilayani na kukagua na kushauri juu ya Miradi ya Maendeleo inayoendelea katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Muheza, nampongeza sana Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa ushauri wake juu ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mhamba, uwekaji zege eneo la mlimani Barabara ya Magoroto na uboreshaji wa eneo la soko la mitumba Muheza Mjini. Kubwa zaidi, maombi yake kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji juu ya utekelezaji wa Ahadi za Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, juu ya Mradi wa Maji kutoka Mto Zigi ili kuondoa tatizo sugu la maji Mji wa Muheza. Mheshimiwa Naibu Waziri, katika barua yake aliambatanisha pia nakala ya upembuzi yakinifu juu ya Mradi huo wa Maji wa Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi, 2014, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alifika ziarani Muheza na katika mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Mpira Muheza, alisema Mradi wa Maji wa Mto Ziggi kwa Mji wa Muheza utaingizwa katika Mpango wa Utekelezaji 2014/2015. Kwa msingi huo, nimemwandikia Mheshimiwa Waziri wa Maji juu ya kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais. Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo msimamizi Mkuu wa shughuli za Wizara Bungeni, namwomba anisaidie kufuatilia utekelezaji wa Mradi huo na kunijulisha hatua zilozifikiwa hadi tarehe 8 Mei, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kufahamishwa ni nini kinachelewesha Mji Mdogo wa Muheza kuwa Mji na kupata Halmashauri ya Mji wa Muheza. Kimsingi, vigezo vikuu vimekamilika na maombi ya Baraza la Madiwani yaliwasilishwa na kukubaliwa na Baraza na Mandeleo ya Mkoa

(RCC), tangu 2013/2014. Pamoja na yote hayo, Muheza (Mji Mdogo), ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Muheza. Tunashauri Wilaya ya Muheza ipewe hadhi ya kuwa Mji wa Muheza na Halmashauri ya Mji. Jedwali Na. 1 katika Kitabu cha Hotuba ya maelezo ya Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mwaka wa Fedha 2014/2015, ukurasa wa 12, inaonesha makusanyo ya mapato ya ndani kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kati ya 2011/2012 hadi 2013/2014, imeongezeka kwa asilimia 110.95. Mbona zipo Wilaya nyingine zina Halmashauri za Mji zaidi ya moja wakati Wilaya ya Muheza, Mji Mkuu wa Wilaya bado siyo Mji wala haina Halmashauri ya Mji? Tutaendelea hivyo mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia tena niliyoshauri mwaka 2004/2005 na mwaka 2007/2008 kuhusu uwezo anaopewa Mwenyekiti wa Halmashauri (Diwani). Kimsingi, Mwenyekiti ni Diwani wa Kata moja miongoni mwa Kata nyingi za Jimbo, mfano Muheza ni Kata 33. Kwa mfumo uliopo, Mwenyekiti anapata mamlaka makubwa na kufanya maamuzi makubwa hata kuliko Mbunge wa Jimbo wa Kata zote 33. Mapendekezo ya kupanga ratiba za Vikao vya Mabaraza ya Madiwani utazame mwenendo wa Vikao vya Bunge ili kuwapa Wabunge nafasi ya kushiriki kikamilifu katika vikao hivyo, vyenye maamuzi makubwa na hata mpango wa bajeti za Wilaya, maagizo hayo hayatekelezwi kabisa! Huu ni udhaifu katika usimamizi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI inayosimamia Halmashauri pia lazima isimamie mfumo wa Serikali au Wizara zingine katika kutoa vibali vya uvunaji wa misitu na vibali na leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini. Vibali vingi na leseni vinatolewa bila Wilaya husika kushirikishwa na leseni za utafutaji na uchimbaji wa madini kutolewa na kazi kufanyika katika maeneo ya vyanzo vya maji na kuharibu mazingira. Mfano, Muheza, leseni ya utafutaji na uchimbaji wa madini imetolewa na kazi zinaendelea kufanyika eneo la mlimani katika chanzo cha mradi wa maji wa Ubembe -Kwemhosi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Mombe na Halmashauri ya Mji wa Tunduma, kuna uhaba mkubwa sana wa maji; asilimia 90 ya Wananchi hawapati maji safi na salama. Umbali ni mkubwa. Katika Kata 14 zilizopo Jimboni, hakuna Kata hata moja yenye uhakika au inayopata maji walau asilimia 50. Hivyo, naomba majibu kutoka kwa Serikali ni kwa nini kwa miaka 53 ya Uhuru wa Tanganyika Wananchi hawapati maji safi na salama. Upi ni mkakati wa muda mfupi kusaidia Wananchi wangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Halmashauri ya Momba tuliomba barabara zetu zipandishwe hadhi, ambazo ni kutoka Ntungwa – Chilulumo – Mkulwe – Kamsamba Km51.1; Kakozi – Kapelo –

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Namchinka – Ilonga KM 50.6; na Chole – Songwe (Halmashauri ya Wilaya Chunya) Km 24.4.

Huu ni mwaka wa tatu tangu tumeleta maombi hayo na hakuna majibu yoyote ya kupandishwa hadhi barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya msongamano wa magari katika Mpaka wa Tunduma mpaka leo bado ni mbaya. Tuliomba Wizara ya Ujenzi kupitia RCC, mambo matatu yakamilike ili tupunguze msongamano:-

(1) Kutengeneza “Dual Carriage Way.”

(2) Kuanzisha bandari ya nchi kavu.

(3) Kuruhusu watu wa Forodha (*Customs*) na TRA kufanya kazi saa 24 kwa siku saba.

Pamoja na mapendekezo hayo, bado Serikali mpaka sasa haijachukua uamuzi wa kuyafanyia kazi. Naomba majibu ya maswali haya ya kushindwa kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Halmashauri ya Wilaya ya Momba ipo nyuma sana katika elimu hususan kukosa walimu wa kutosha, hakuna vitabu, hakuna maabara na maktaba mashuleni, nyumba za walimu, upungufu wa madawati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Halmashauri ya Momba ni kuwa na Hospitali ya Wilaya. Hii ilikuwa ni Ahadi ya Mheshimiwa Rais. Hivi Ahadi za Rais zinakamilika baada ya muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayosimamia masuala ya maafa na UKIMWI. Naomba nipatiwe majibu hizi fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba ni kwa nini hazifiki? Mfano, mwaka huu wa 2014, maafa yaliyotokana na mvua ni makubwa na hivyo Halmashauri ya Wilaya imeshindwa kukabiliana nayo, kutokana na fedha hizo kutokufika. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Halmashauri ya Momba ilipangiwa zaidi ya Shilingi milioni 500, Fedha za Mfuko wa Barabara, lakini mpaka sasa tumepata chini ya milioni 50. Je, ni kwa nini fedha zinazopangwa hazifiki kabisa? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyotegwa ipo kisiasa zaidi kuliko mahesabu, kwa maana kwamba, fedha haziendi au kupelekwa zilikopangwa; hivyo, baadhi ya Miradi kukaa mwaka mzima wa fedha bila kupatiwa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iache kutengeneza bajeti kisiasa na badala yake bajeti ikipitishwa ipelekwe ilikopangiwa ili nchi yetu ijengeke kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara umekua kutoka asilimia 4.9 mwaka jana hadi 5.5 kwa mwaka huu huku uchumi wa Tanzania ukikua kwa asilimia 7, lakini Wananchi wake wakiendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Ukuaji wa Uchumi wa Fedha Katika Ukanda wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kama ilivyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (*IFM*), kwa kushirikiana na Taasisi ya Tafiti za Kupunguza Umaskini (*REPOA*), ni kwamba, licha ya uchumi huo kukua lakini haujaweza kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania, kasi ya ukopaji imeongezeka kutoka asilimia 28 ya Pato la Taifa kwa mwaka huu. Ili kuondokana na umaskini lazima kuwepo na Sera ambazo zitaweza kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Sera hizo ni pamoja na kuhakikisha Sekta ya Kilimo inakua zaidi, kuongezeka idadi ya viwanda vitakavyoongeza ajira kwa Wananchi, kuwekeza katika ukuaji na upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa Wananchi pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara badala ya kubomoa bomoa bila ya kuwawekea wafanyabiashara utaratibu unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi waliostaafu wanaishi kwa tabu sana, hawapati matibabu kama inavyotakiwa na akiba yao ya uzeeni kwa wengi waliokuwa Watumishi wa Serikali kwa maisha ya leo ni ndogo sana. Kiwango cha chini ni Shilingi 40,000, maisha yamepanda na isitoshe hawapewi kila mwezi. Nashauri wastaafu wapewe malipo yao ya pensheni kila mwezi na malipo yao yasifanyike kila baada ya miezi mitatu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya askari wa barabarani kutekeleza majukumu yao yanayowahusu, askari wa usalama wa barabarani, kinachoendelea ni kukusanya makosa 60 kwa mwezi, askari asipopoleka au asipopata makosa 60 anaondolewa kwenye kikosi cha barabarani kwa kushindwa kukusanya Shilingi 1,800,000 kwa mwezi. Je, askari wa barabarani

wamekuwa TRA? Hali hiyo ifuatiliwe na utaratibu huo wa kubambikiza madereva makosa ili kutimiza lengo la makosa 60 kwa mwezi uachwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia njia ya maandishi, nichangie Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, jinsi wanavyoitikia wito kufuatia maafa yaliyowapata Wananchi wa Bulembu – Muleba Kaskazini. Ushauri kwa Serikali ni kuwepo mafunzo kwa Watendaji kuanzia ngazi ya vitongoji na vijiji, juu ya kuyakabili maafa mbalimbali. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na ongezeko la Wananchi wa makazi, ni busara Watendaji wetu hata na Wananchi waongezewe uelewa juu ya majanga au maafa ya aina mbalimbali ambayo sasa yanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuishauri Serikali juu ya usimamiaji na ufuatiliaji wa Miradi. Hii ikiwa Wizara kinara, inao wajibu wa kuhakikisha kuwa kila Mradi unaopelekwa katika ngazi ya utekelezaji, unakamilishwa kwa tija ya hali ya juu. Kwa fedha kidogo ambayo Serikali inaipata kwa shida, ni busara matumizi yake yawe na ufanisi. Halmashauri za Wilaya ikiwemo Wilaya ya Muleba, utekelezaji wa Miradi hasa ya Maji uko chini ya kiwango kinachotakiwa. Kuna haja ya mamlaka kusimamia Miradi na kuchukua hatua pale inapobainika kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee Miradi ya Barabara katika Wilaya ya Muleba. Ubainishaji wa Barabara za Halmashauri kwa Wilaya hii una upungufu mkubwa, yapo maeneo ya Kata na Vijiji hayaunganishwi na Barabara za Halmashauri kama inavyotakiwa. Hali hii inasababisha Wananchi kubeba mzigo mzito wa kutengeneza barabara ambazo kimsingi ni jukumu la Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Wananchi wa Muleba Kaskazini kushiriki kutengeneza barabara, kimsingi ni jukumu la Serikali kutokana na uzito wake kigharama. Nachukua fursa hii kuiomba tena Ofisi ya Waziri Mkuu, itusaidie kugharamia ujenzi wa Daraja la Kishala. Serikali imeshatoa Shilingi milioni 400 na kazi ya awali imefanyika. Naomba Serikali iende hatua moja mbele kwa kutengeneza daraja. Endapo tutaweza kutengeneza daraja, kazi ya barabara zinazounganisha zitafuatia awamu kwa awamu zikiboreshwa kwani kwa viwango vya kupitika hizo *ring roads* wataweza kujitolea na kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuishauri Serikali kuamua kwa haraka kufanya mabadiliko ya maboresho kwenye Sekta ya Elimu. Ipo haja

Tanzania kama Taifa, kuamua kuwekeza kwenye elimu ya mafundi mchundo. Hii ni elimu ya mafundi stadi au ni elimu ambayo mhitimu anaweza kuingia sokoni au kwenye maisha na kuanza kujitegemea. Mataifa yanayofanya vizuri China na hao Tigers wa Asia, mafanikio yao yametokana na uwekezaji katika elimu stadi. Yapo makosa yaliyobadili Vyuo vya Kati kama IFM, Mzumbe na Dar Tech kwa kutaja baadhi na kuwa Vyuo Vikuu. Tunahitaji kuwa na vyuo kama hivi kwa lengo maalumu la awali lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie Jimbo la Muleba Kaskazini kuondoa kero kuu mbili; moja, mgogoro wa Kata ya Rutoro na Ranchi ya Narco. Wananchi wameendelea kuishi kwa shida na mashaka makubwa. Tunaomba Serikali ifanye maamuzi. Pili, migogoro kati ya Jeshi la Wananchi wa Kambi ya Kaboya na Wananchi wa Kata za Mayondwe, Muhutwe na Izingo. Tarehe 25 Julai, 2013, Mheshimiwa Rais wakati wa Siku ya Mashujaa Kaboya, aliamuru mgogoro huu upatiwe ufumbuzi. Naomba na kushauri Ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie kuona mamlaka husika zinaondoa kero hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia maoni yangu juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia juu ya kero ya maji katika Mkoa wa Singida kama ilivyo katika maeneo mengi nchini. Mkoa wa Singida hasa vijijini, tatizo ni kubwa zaidi ukizingatia hali ya nchi ya ukame ya Mkoa huu. Wananchi wa Singida Vijijini hawana maji, wanategemea maji ya vidimbwi ambavyo navyo hukauka wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Wizara ya Maji wa Vijiji Kumi kila Halmashauri kwa mwaka wa fedha unaoisha haukutekelezwa! Ukosefu wa maji safi ni janga kubwa kwa Taifa na Serikali haitakiwi kulifanyia mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la nchi hii wala siyo ukosefu wa fedha bali ni ukusanyaji hafifu wa mapato, Serikali kuwa wavivu wa kufikiria na kufanyia utekelezaji vyanzo vipya vya mapato, matumizi makubwa na yasiyo ya tija ya fedha za umma mfano maadhimisho ya sherehe mbalimbali na mbaya zaidi ni rushwa iliyokithiri katika karibu kila eneo la utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ununuzi wa Umma imekuwa ndiyo ikihalalisha wizi na ubadhirifu wa fedha za umma kisheria. Serikali itaileta lini Sheria hii Bungeni ili irekebishwe?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo wa Zao la Alizeti katika Mkoa wa Singida wanahitaji kuwezesha ili walime kwa ufanisi zaidi. Wanahitaji Soko la mafuta ya alizeti ili wapate uhakika wa kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumetokea ajali mbaya katika Kijiji cha Utaho, Wananchi wengi wamepoteza maisha. Pamoja na barabara hii kuanza kuchochea maendeleo katika maeneo mengi inakopita, imeleta pia janga kubwa la ajali za mara kwa mara na kuchukua maisha ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia TANROADS wanatakiwa kuweka matuta ya kupunguza mwendo katika eneo lenye makazi ambako magari hupita kwa mwendo wa kasi bila kujali wapita kwa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam umekuwa ni aibu kubwa kwa nchi! Wageni wanaosafiri kwa ndege huenda uwanja wa ndege kwa usafiri wa bodaboda wakiwa na mabegi yao vichwani kwani bila hivyo hawawezi kuwahi ndege! Hii ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wananchi ni nyingi sana lakini kwa sasa haya yanatosha na nahitaji Serikali ifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Bajeti ya Ofisi yake, TAMISEMI na Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimestuka na kushangaa kidogo na ningependa kupata ufufanuzi kuhusu Mradi wa DMTP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa napongeza sana utekelezaji wa Mradi huu muhimu, mimi nikiwa Mbunge katika Jiji la Dar es Salaam, ambaye nimeshiriki kama mdau katika kubuni vipaumbele, nakumbuka sana kwamba, katika vikao vyote vya Wadau vya Wataalam wa TAMISEMI na Wataalam wa Benki ya Dunia, ilikubalika kwamba, kutakuwa na miradi saba katika Mpango huu wa DMTP. Moja kati ya Miradi hiyo ni barabara za lami za mitaa zitakazoweza kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Barabara hizi za kupunguza msongamano zikaainishwa na Wananchi husika kushirikishwa na tathmini ya fidia ikafanywa. Ieleweke kwamba, maana ya barabara za kupunguza msongamano ni zile zinazoweza barabara hizo kuunganishwa na barabara zote kuu za Kibaki, Bagamoyo, Morogoro, Mandela, Nyerere/Pugu na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mshangao na mstuko wangu katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), ukurasa wa 23 na 62, Mheshimiwa Waziri ameelezea Mradi wa *DMTP* wa barabara za lami na mitaa, kama vile ni barabara za mitaa zinazounganisha barabara ya *DART* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa barabara ya *DART* ni barabara ya Morogoro pekee, hizi barabara za *DMTP* zitakuwa zile zinazounganisha na barabara ya Morogoro tu kwenye Wilaya ya Kinondoni na kidogo katikati ya Jiji. Ina maana kwamba, barabara zote zinazopunguza msongamano kwenye Majimbo ya Segerea, Ukonga, Temeke na Kigamboni hazitaguswa tena, lakini hizi barabara zinaunganisha kwenye Barabara Kuu za Mandela, Nyerere/Pugu na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halikubaliki, kwa sasa uondoaji wa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam hautafanikiwa kwa kujenga tu barabara zinazounganisha na Barabara ya Morogoro (*DART*) bila kushughulikia barabara za pembezoni (*ring roads*) zinazounganisha, siyo na *Morogoro Road (DART)* tu, bali pia zile zinazounganisha kwenye barabara zingine kuu zikiwemo Mandela, Nyerere/Pugu na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tatizo ni ufinyu wa fedha toka Benki ya Dunia, wadau wote wangeitwa, wakiwemo Wabunge, ili kuchagua upya barabara za kipaumbele zitakazosaidia kupunguza msongamano kwenye Majimbo yote ya Dar es Salaam na siyo Wataalam kuamua peke yao barabara zinazounganisha *DART* tu kwenye Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2014 inayolenga kuondoa migogoro na migongano ya kimasilahi kati ya Viongozi wa Chama na Serikali imeanza kutekelezwa; ni vyema Waraka huo ukasambazwa kwa Wananchi hususan Wanaushirika na Afisa Ushirika ili iweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Maendeleo ya Viwanda: katika eneo la mkakati wa Wilaya moja, bidhaa moja kutokana na malighafi zilizopo kwenye Wilaya husika. Ushauri, ni vyema pia utafiti wa kina ukafanyika ili kuwe na ushirikiano wa kutosha kati ya mpango huo na Wananchi wa Wilaya husika hasa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini: Katika hili ni suala linalohusu wachimbaji wadogo wadogo kuhusu leseni zao hasa muda unapokwisha, kwa kiasi kinachotakiwa kulipa. Je, Serikali haioni sasa ni vyema ikaletwa sheria hiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwa marekebisho hasa yanayohusu wachimbaji wadogowadogo ili waweze kulipia leseni hizo kwa awamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Tabora – Koga – Inyonga – Mpanda ni lini itaanza kuwekewa lami na inatarajiwa kwisha lini?

Je, ni lini ajira za kawaida zitarudishwa kwenye Halmashauri?

Je, kwa nini kunakuwa na ucheleweshwaji wa fedha za maendeleo na je, tatizo hili Serikali imejipangaje kulitatua?

Serikali ina mpango gani wa kumaliza kesi zinazohusiana na TANAPA na pia ni kwa nini kesi hizi zimekuwa hazisikilizwi kabisa ama zinachukua muda mrefu?

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nianze na suala la Vyama vya Ushirika. Vyama hivi vilikuwa ndiyo nguzo pekee ya kumsaidia mkulima, ndiyo ulikuwa msingi wa maendeleo ya mkulima na ndiyo msingi mkuu wa soko la mazao yake. Leo hii Ushirika huu umekufa; naomba kujua hali ya Chama cha Ushirika cha Biharamulo (*Biharamulo Co-operative Union*); Chama hiki kipo wapi? Mali za Chama hiki cha Ushirika zipo wapi? Mashamba na magari yako wapi? Bodi ya Ushirika huu ipo wapi?

Naomba nipate jibu juu ya Chama hiki cha Ushirika hususan mara baada ya Wilaya ya Chato kumegwa toka Wilaya kongwe ya Biharamulo.

Pili, kuhusu suala la Pori la Hifadhi la Kimisi na Burigi. Leo hii askari wa wanyamapori wanatumia pori hili kama sehemu ya kuendeshea mkakati wa kuendeleza unyanyasaji wa wafugaji. Katika Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira (Kamati ya Lembeli), tulielekeza kwa upana sana. Sasa hivi yale yote tuliyoadili ndani ya Bunge bado kuna watu wapo juu ya sheria. Nchi hii tunaongozwa na sheria, taratibu na kanuni, watuhumiwa katika sakata hili bado wapo kazini wakiendeleza hujuma hizo.

Katika Pori la Kimisi, zaidi ya ng'ombe 170 wamekamatwa na kuuwawa, ndama zaidi ya 115 nao wamekufa; tunataka mfugaji huyo ajikomboe vipi kiuchumi? Walitajwa wafanyakazi wafuatao kuhusika na zoezi hili la kunyanyasa wafugaji; Jonathn Msiba, Fredrick Kobero, Hilary Ramadhani na Nathan Ally na Aaron Lyimo toka KDU Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watumishi hawa wasiofuata maadili ya kazi wachukuliwe hutua za kiutumishi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhusu migogoro ya ardhi; suala hili Serikali haitoi majibu ya wazi kwa Wananchi, kumekuwa na migogoro hii kwa muda mrefu. Kuna mgogoro wa ardhi katika Kata ya Kahihamu, Kijiji cha Karuta na Mpago. Vijiji hivi vimesajiliwa rasmi, lakini bado mwaka jana *TFS* wamewawekea mabango Wananchi hawa wahame. Je, wahame waende wapi? Mbaya zaidi, hakuna Wataalam waliofika kulifanyia kazi suala hili. Naomba kupewa majibu suala hili limefanyiwaje kazi? Vilevile naomba nipate majibu kwa Wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuhusu Daftari la Wakazi wa Vijiji na Vitongoji. Uboreshaji wa Daftari hili ufanyike kwa uwazi na ukweli. Leo hii kuna baadhi ya Wananchi wamekataliwa kuandikishwa kisa hawana maelewano mazuri na Wenyekiti wa Serikali ya Vijiji na Vitongoji. Ieleweke kuwa, suala hili ni haki ya msingi ya Mwananchi; hivyo, Wananchi wapewe utaratibu unaoeleweka na kila mtu apate haki ya kujiandikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la rushwa limekithiri sana, leo hii haki ya mtu kupata haki yake imeporwa. Ukienda Mahakamani bila ya rushwa haki haipo, ajali barabarani zimekuwa nyingi sababu ya rushwa. Taarifa ya CAG inaonesha jinsi watu wanavyochota pesa ndani ya Halmashauri mbalimbali. Chombo hiki cha TAKUKURU kifanye kazi yake, la sivyo Taifa hili linaangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Ahsante.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwenye maeneo yanayohusika. Kwanza kabisa, napenda kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Longido, kutoa pongezi kwa mifugo waliyopewa Wananchi. Napenda kueleza kuwa, Wilaya ya Longido ni kame sana, kwa hiyo, tatizo la maji ni kubwa sana. Wizara ya Maji ijitahidi kuwapa kipaumbele Wilaya hii kutokana na hali mbaya ya ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya elimu kwenye maeneo ya Halmashauri ya Longido ni duni kutokana na ukosefu wa walimu pamoja na vifaa vya kufundishia na kusomea havipatikani. Hali ya Watumishi kwenye Halmashauri ya Longido wengi wao wamekuwa wakitumia fedha za Halmashauri bila kuchukuliwa hatua, ndiyo maana Miradi yote ya Longido ipo chini ya kiwango na mingine haikamiliki. Naomba Ofisi ya TAMISEMI iangalie kwa karibu fedha ambazo zimepelekwa Halmashauri ya Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa Watendaji kwenye maeneo ya Vijiji na Kata, hakuna Watendaji ambao wameteteleza Miradi inayoendelea

kwenye maeneo yote ya vijiji. Hatuwasaidii kuwa na Miradi mizuri kama hakuna wasimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wengi ambao hawana kazi huku hatuna wafanyakazi. Msimamizi wa Miradi vijijini ni Mtendaji wa Kijiji na mlinzi wa amani kijijini, lakini huyo mtumishi hayupo, Mtendaji wa Kata ndiyo msimamizi wa Miradi kwenye Kata na mlinzi wa amani kwenye Kata na huyu hayupo. Je, ni nani atakuwa msimamizi wa Miradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iruhusu Halmashauri iajiri Watumishi wa Kata na Vijiji. Kwa muda mrefu Halmashauri zote waliomba kibali cha kuajiri watumishi lakini hawakupata. Kama Watendaji hawa hawataajiriwa shughuli za maendeleo hazitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro mkubwa wa mpaka wa Wilaya ya Arumeru na iliyokuwa Wilaya ya Monduli ya zamani, ambayo kwa sasa ni Wilaya ya Monduli na Longido. Tunaomba Wataalam wabainishe mipaka kwani ilikuwepo na mpaka leo inajulikana lakini Wananchi wa upande mmoja hawataki kuheshimu mipaka, jambo ambalo linasababisha vita na mpaka sasa Wananchi wengi wako hospitalini na mapigano bado yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vitambulisho vya Taifa; Longido ni Wilaya iliyoko mpakani mwa Kenya, Wananchi wanapata usumbufu sana kutokana na kutokuwa na vitambulisho wanapokuwa mpakani. Hawana kitambulisho kinachomwonesha kwamba, ni Mtanzania huku wenzao wa upande mwingine wa Kenya wana vitambulisho vyao. Watanzania wengi wanakamatwa kwa vile hawana vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwamba, mgogoro wa wakulima na wafugaji inawezekana kabisa kusuluhisha jambo hili kwa kupima maeneo na kuheshimu maeneo yaliyopimwa. Uadui umekuwa mkubwa sana kwa Wananchi ambao ni ndugu. Imefika wakati Serikali ichukue uamuzi mgumu kutatua mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuwa, kwa kuwa mapori ambayo hayana wanyama tena hata digidigi, lakini wanapelekwa maaskari kulinda na kukamata mifugo kwenye mapori ambayo hakuna wanyama, mapori hayo wapewe wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Longido haina Hospitali ya Wilaya kwa muda mrefu. Halmashauri imepitishwa kwenye bajeti kwa mfululizo wa miaka mitatu, bado Wilaya wanatumia Kituo cha Afya kuwa Hospitali ya Wilaya. Wagonjwa wanasafirishwa kila mara kupelekwa Hospitali ya Mkoa na Hospitali za Serikali na za binafsi. Serikali iweke bajeti ya kujenga Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi. Nashukuru sana kwa jitihada za Serikali katika kuona umuhimu wa kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbarali haina Hospitali ya Wilaya, badala yake Kituo kilichokuwa cha Afya cha Rujewa ndicho kinachotumika kama Hospitali ya Wilaya. Mchakato wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ulianza toka 2011, hadi sasa jengo hilo halijapewa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa awali ili iweze kufunguliwa na kutoa Huduma ya Wagonjwa ambao wanakosa huduma kwa maradhi mbalimbali yanayowakabili pamoja na akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita, yaani Bajeti ya Mwaka wa Fedha hazijapelekwa ambazo zilipangwa kusaidia Hospitali hii walau ifunguliwe. Tunaleta maombi ili tusaidiwe, tunaomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu ni kubwa. Kata za Ipwani na Mawindi hazijawahi kupata maji ya bomba toka nchi hii ipate Uhuru. Bajeti ya mwaka 2013/2014, tunaishukuru Serikali kwa kupitisha Mradi wa Maji kutoka Njombe kwenda Mbarali. Ombi langu, fedha zitolewe ili kazi ya Mradi huu muhimu ianze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbarali ni eneo muhimu sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Tuna Mradi wa Maji wa Mwendamtitu, naishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga *Intake* na 123 kuondoa mgogoro uliokuwepo kati ya Wananchi na Mwekezaji wa *Mbarali Rice Farms Estate*. Ombi langu, naomba Serikali itoe fedha ili kukamilisha Mradi huu muhimu kwa Taifa letu na Wakulima wa Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Lwanyo Kijiji cha Igurusi limejengwa ili kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka mzima. Kwa bahati mbaya, halijakamilika na kuna sehemu linavuja, ipo hatari ya kubomoka; hivyo, naomba Serikali itoe fedha za kukamilisha ujenzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Bwawa la Igurusi, upo ujenzi wa Bwawa la Madibira, naomba lipewe fedha kwani linategemewa kumwagilia hekta 3600 ili kuongeza Pato la Taifa na uchumi wa Wananchi kwa ujumla. Tunaomba fedha zilizopangwa kwa kazi hii zitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Wilaya ya Mbarali ni wabunifu wa kutengeneza miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji. Yapo maeneo ambayo

Wananchi wanalima kwa miundombinu dhaifu. Tunaomba Wananchi hawa waruhusiwe kuwapata wawekezaji wazawa ambao wataingia nao mikataba kwa ajili ya kuboresha miundombuni ya kumwagiliaji. Maeneo hayo ni Munazi, Kijiji cha Manavala, ambacho kipo Kata ya Songwe Imalilo, Mwashikamile, Yala na Luhanga, ambavyo vyote vipo Kata ya Luhanga. Yapo maeneo pia ya Mpunga Mmoja, Kata ya Itamboleo na Chimala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadhirifu katika Halmashauri zote ni mkubwa mno hasa fedha za Miradi ya Maendeleo. Mbarali ni miongoni mwa Wilaya iliyopata tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hatua ambazo zilichukuliwa na Waziri wa TAMISEMI kwa kuwataja wabadhirifu ndani ya Bunge lako Tukufu na Wananchi wa Mbarali walitegemea hatua zitakazochukuliwa wataziona. Kwa bahati mbaya hatua zimechukuliwa kwa Watendaji wa Kata wawili tu, Maafisa wengine waliotajwa ni DT tu na Afisa Mipango Msaidizi, wengine waliotajwa hadi leo wapo kazini. Wananchi wanataka kujua ni lini hawa wengine nao watachukuliwa hatua za kuonekana kama hawa ambao nimewataja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo na huduma za Jamii linahitaji jitihada kubwa ili kuboresha zaidi. Wilaya ya Mbarali, vijiji vingi vimejitolea kujenga Zahanati na Vituo vya Afya lakini havijaanza kufanya kazi. Shule za msingi nyingi bado zinahitaji msaada wa Serikali, Shule za Sekondari za Kata za Kidato cha Kwanza hadi cha sita. Wananchi wamejitahidi kujitolea kujenga, lakini jitihada za Serikali ziongezeke ili kuona shughuli za Wananchi zinaungwa mkono vizuri kuondoa dhana ya kuona shule za kata hazina ubora wa kutosha. Naishauri Serikali iongeze nguvu kuboresha miundombinu ya huduma za jamii ili kusiwe na shule za wanyonge ambao ndiyo Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kumaliza mgogoro wa mpaka wa Hifadhi mpya ya Ruaha na Wananchi wa Mbarali, kwa kuunda Tume Maalum ya kwenda Mbarali kurekebisha mgogoro wa mpaka. Naomba Tume hiyo ndogo ifanye kazi hiyo muhimu kwa muda mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la msingi la ujenzi wa Barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga. Barabara hii ni Ahadi ya Mheshimiwa Rais, imekuwa ikipewa ahadi toka enzi za Mheshimiwa Edmund Mjengwa, lakini hadi leo bado. Mara ya mwisho ilisadikika kuwa barabara hii ingepewa fedha za MCC; mpango huu umeishia wapi? Naomba nipewe majibu kwa niaba ya Wananchi wa Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa katika utekelezaji wa Miradi ni kutokana na Miradi yenye makadirio makubwa kwenye manunuzi (*Quotations*); kwa mfano, saruji bei yake katika soko ni shilingi 20,000, lakini Serikali itanunua kwa 30,000. Hali hii hufanya gharama za Miradi kupanda na wakati mwingine kutokamilika. Miradi hutumia pesa nyingi bila ya umuhimu huo; kwa mfano, pesa za Miradi miwili hutumika katika Mradi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Manunuzi, nayo huchangia ucheleweshaji wa *tender* kutokana na kuwa na mlolongo mkubwa; kwa mfano, kutangaza *tender* na hatua zake hivyo kuchukua muda mrefu mpaka Mradi kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya bado hazitolewi ipasavyo na pia mazingira ya baadhi ya Hospitali zetu hayaridhishi na badala yake huchangia kueneza maradhi. Bado hakuna huduma nzuri katika Vituo vya Afya na pia upatikanaji wa dawa na pia huduma za bure kwa watoto na wazee zina mlolongo mrefu sana kiasi cha kufikia kutwa nzima mpaka siku mbili mgonjwa bado hajapata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usumbufu kwa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ni mkubwa si tu ka upande wa huduma nafuu bali hata kama wagonjwa wa kulipia utakuta huduma ni jengo lingine, kulipia ni jengo lingine, wakati jengo alilotoka kuna sehemu ya kulipa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kuwa, utaratibu huu ni wa usumbufu sana, bora malipo yafanyike kwenye jengo husika, wazee na watoto wapewe huduma bure na kwa wakati bila usumbufu. Usimamizi wa utoaji huduma hospitalini uboreshwe na usafi uzingatiwe. Kuwe na utaratibu mzuri wa kuwezesha upatikanaji wa dawa kiurahisi bila ya urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*), imebaki kuwa kama simulizi tu katika jamii kwani ni Miradi mingi ambayo mpaka sasa haijakamilika na mingine kukwama kabisa kutokana na kufeli kwa utekelezaji wake, kwa kutopatiwa pesa kwa wakati. Ucheleweshaji huo wa fedha hupelekea kutokufanikiwa kwa Miradi hii na kuonekana Serikali kuahidi vitu visivyotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kuwa, bora Miradi iwe michache ambayo itapatiwa pesa kwa wakati kuliko kuweka orodha kubwa ya Miradi isiyotekelezeka na kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa za Miradi mbalimbali katika Wizara tofauti tofauti zitoke kwa wakati kuepusha usumbufu na kukwama kwa Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado suala la elimu linaendelea kuwa chini ya kiwango kutokana na wanafunzi wengi wanaofeli katika mitihani yao na kutokana na ukosefu wa walimu mashuleni. Walimu wanaopangwa katika shule za vijijini huacha kwenda kwa kukosa posho zinazokidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya kufundishia kama madawati, maabara na vitabu, vikiboreshwa itapelekea matokeo mazuri kwa wanafunzi na pia walimu nao watafanya kazi zao katika mazingira mazuri na kuzingatia malipo yao na motisha.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge Maalum la Katiba limetamkwa katika kifungu kinachoelezea hali ya siasa, ukurasa 4, kifungu 6 – 7; hivyo, si kosa kwa Mjumbe yeyote wa Bunge hili kuzungumzia suala linalohusu Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amewasihi Wanasiasa na Wananchi wote kwa ujumla kutoa ushirikiano mkubwa wakati wa maandalizi ya Katiba mpya hadi kufikia kura za maoni na kuomba pia kwamba tushindane kwa nguvu ya hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza tunashindana vipi kwa nguvu za hoja wakati wengine wameshakwenda kinyume na hoja husika ambayo ililetwa na Tume ya Warioba na wamekuja na hoja za nguvu, za mabavu na kukiuka maoni ya Wananchi juu ya madai ya Serikali tatu walizodai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli za baadhi ya Viongozi ndizo ambazo zinaonesha Zanzibar kama nchi iliyoungana na Tanganyika mwaka 1964, baada ya Muungano huo Zanzibar imegeuzwa kuwa Koloni la Tanganyika na vipo viashiria vingi ambavyo vinaonesha hivyo; mfano, kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Kikwete wakati akilizindua Bunge Maalum ya kusema kwamba, iwapo Rasimu ya Serikali Tatu itapita, Jeshi litachukua nchi. Jambo ambalo limemfanya yeye mwenyewe kwenda kinyume na Rasimu aliyoileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli iliyotolewa Kanisani mwezi uliopita na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu, aliposema asilimia 95 ya Wazanzibari ni Waarabu, tukiwaachia wataunda Serikali ya Kiislamu; nani kamwambia kama siyo nia ya kuwagawa Wazanzibari na wenzao wa Tanganyika kwa misingi ya dini? Hii si nia ya kuendela kuifanya Zanzibar kuwa ni Koloni la Tanganyika? Kauli ya kusema kuwa Zanzibar hatuwezi kuiachia hata siku moja inamaanisha nini kama si uthibitisho wa kulifanya Koloni la Tanganyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Waziri Mkuu kusema Zanzibar si nchi ni uthibitisho tosha wa Zanzibar kufanywa Koloni la Tanganyika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Rais wa Zanzibar kuteuliwa Dodoma bila ya ridhaa ya Wazanzibari ni njia na uthibitisho wa kutosha juu ya kuonesha kuwa Zanzibar ni Koloni la Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khamis Kigwangalla kusema kuwa Serikali ya Zanzibar ni *Local Government* ni uthibitisho tosha wa kuifanya Zanzibar ni koloni la Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kuwataka Zanzibar wafanye mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ni kuonesha dhahiri kwamba, Zanzibar ni Koloni la Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli usiopingika kwamba, fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo zinasemekana kwamba zimeingizwa kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar toka Desemba mwaka jana, lakini mpaka leo hazijatufikia kwa upande wa Majimbo ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar uwezo wa kuzitumia fedha hizi za Mfuko wa Jimbo iliupata wapi kama si wizi au ujambazi wa fedha za umma ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, Wabunge wa Zanzibar tumeanza kukosa imani na ofisi hii juu ya kupokea fedha hizi za Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo; kuna haja ya Sheria hii kufanyiwa marekebisho ili Mfuko huu uweze kufika kwa walengwa mapema kinyume na tabia hii ambayo inapelekea kudumaza maendeleo ya Wananchi.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na wenzangu kuunga mkono Hotuba hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wilaya zilizo nyuma na pembezoni zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ruaha – Ifakara, muda wote imesahauliwa. Tangu miaka ya 1960 mpaka hii leo, Barabara hii ni ya muda, hata madaraja yake ni ya muda. Huu ni mwaka wangu wa tisa Bungeni, kila mwaka nakumbusha kuomba barabara ya lami lakini mpaka leo hii barabara hii bado haipitiki wakati wa masika. Barabara ni mbaya sana, ikitengenezwa ni kifusi tu na kokoto ambazo wakati wa mvua zote zinazolewa. Sasa tunaomba huruma. Kwa nini mnapoteza pesa? Heri kuweka lami kipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja lakini cha kushangaza Kilombero imesahauliwa. Sasa hivi hata usafiri wa kwenda Kivukoni – Mahenge haipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la Mji wa Ifakara ni maji. Mji umekua, una vyo, mashule, taasisi mbalimbali, na wakazi wa mji huu wameongezeka mara 1000 lakini miundombinu ya maji ni ya mwaka 1970. Maji ni tatizo, tunaomba mwaka huu Wananchi wapatiwe maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa Kilombero ni mgogoro kati ya wafugaji na wakulima. Wananchi wa Kilombero asilimia 90 ni wakulima. Ahadi ni nyingi, lakini mpaka leo wafugaji wanatamba na kusumbua wakulima. Sisi ni wakulima tukalime wapi? Tunaomba Barabara ya Ruaha – Ifakara. Mji wa Ifakara upatiwe maji. Vilevile migogoro ya wafugaji na wakulima Kilombero iishe; asilimia 90 ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, akumbuke na kuiangalia kwa huruma Wilaya ya Kilombero.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya miaka mitano Hospitali yetu ya Mkoa ya Mawenzi, chumba cha upasuaji hakifanyi kazi na *Maternity Ward* bado haijakamilika sababu tu ya uzembe wa Mkandarasi. Hii inakuwa usumbufu kwa Wakazi wa Kilimanjaro kwani upasuaji mdogo inabidi ufanyike KCMC na kupelekea kuongeza msongamano katika Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate majibu kutoka kwa Serikali ni lini majengo yale yatakamilika ili kuokoa maisha ya watu wanaopata hata ajali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya KCMC ambayo Serikali ina ushirikiano nayo, kwa sasa hivi imeshuka viwango sana, wagonjwa wanalala chini, hakuna vitanda vya kutosha, pia kuna baadhi ya vipimo ni vibovu kwa muda mrefu; mfano, *CT Scan* ni mbovu kwa zaidi ya miaka miwili. Vipimo kama vya ku-*check cholesterol* inabidi wagonjwa waende kwenye vituo vya watu binafsi kupimwa na ni Hospitali ya Rufaa. Je, Serikali ina mikakati gani ya kulinusuru hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha Bunge la Bajeti mwaka jana, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kutupa bajeti mwaka huu kwa ajili ya kununulia vitanda, magodoro na mashuka kwa ajili ya Hospitali Teule ya ST. Joseph iliyopo Soweto Manispaa ya Moshi. Hospitali ile ndiyo imekuwa mkombozi wa Wakazi wa Moshi na Mkoa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utalii iliingiza Pato la Taifa zaidi ya 1.5 billion kwa kipindi cha mwaka uliopita na kati ya fedha hizo Mlima Kilimanjaro imechangia zaidi ya bilioni 20. Cha kusikitisha mpaka sasa Halmashuri zinazozunguka mlima ule bado hazijafaidika na mapato yatoakanayo na mlima ule. Mfano, Halmashauri ya Moshi Vijijini katika maeneo ya Mahoma, Kikasara, Tela, Sambarai, licha ya kuishi chini ya Mlima huu hawapatii maji kabisa. Je, kwa kupitia mapato haya Serikali inaweza kutupa fedha na kuwapatia maji ili waweze kufaidika na mapato ya mlima huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Operesheni Tokomeza, Bunge lako Tukufu lilipitisha azimio la kumfukuza Mkurugenzi wa Wanyama, Prof. Songoro, huyu ndiye aliyedanganya ya kwamba, yule mwanamke aliyeuwawa alifariki kwa Ugonjwa wa Kiharusi wakati mwili wa mama yule ulikutwa na matobo ya risasi. Mpaka hivi sasa katika vyombo vya habari bado Tembo wanauwawa na imeundwa Tume ya kuendelea kuchunguza. Je, uchunguzi huu utakuwa huru wakati kati ya anayechunguzwa bado yupo kazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumrudisha huyu kazini; Serikali inatueleza nini kuhusu Mawaziri waliojiuzulu? Itabidi Serikali iwatolee maelezo na wao au warudishwe? Kwa kumrudisha Mkurugenzi huyu siyo kudharau Azimio la Bunge na ni matusi makubwa kwa wale walioathirika? Ni kigezo gani kilichotumika kumrudisha Mkurugenzi huyu kazini? Naomba majibu.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naanza kwa kunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pili, nitoe shukrani kwa TAMISEMI kwa kuifanya Halmashauri ya Misungwi itulie, kwa kuleta wafanyakazi wapya, wanaoheshimu sheria, kanuni na taratibu. Vilevile kwa kuwaelimisha Madiwani na kudhibiti wizi uliokuwa umekithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena ombi langu kwa Wizara juu ya kurundikana kwa wahasibu 28 wakati wanaohitajika si zaidi ya kumi. Watumishi wengi namna hii wanasababisha yale ya zamani. Ikumbukwe kwamba, wengi wa wahasibu hawa ni wale walioisababishia Halmashauri hasara. Naomba suala hili lipewe uzito unaostahili.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ni kiungo muhimu kati ya Wizara za Kisekta na Asasi mbalimbali za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mbunge wa Kilwa Kusini, napenda kutoa maoni yangu kuhusu kero za Jimbo langu na ninaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu iyashughulikia ipasavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka 53 ya Uhuru, Kata ya Pande na Lihimalyao hawajapata maji safi na salama. Kwa kweli Serikali imejitahidi sana kuwashughulikia Wananchi wa Kata ya Pande na Lihimalyao, visima vyote vinavyochimbwa maji yanakuwa si safi na salama. Kwa hiyo, naiomba ofisi yako iwashughulikie Wananchi wa Kata ya Pande na Lihimalyao kwa kuchimbiwa malambo; kwa kweli utawasaidia Wananchi hawa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2010, Mheshimiwa Rais Kikwete aliahidi kujenga Barabara ya Singino – Kivinje, yenye urefu wa km 4.5. Barabara muhimu inayoelekea Hospitali ya Wilaya. Serikali ilifanya jitihada zikatengwa shilingi 350,000,000 kwa ajili ya kuanza kilomita moja katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 lakini mpaka leo hakuna matengenezo ya hiyo kilomita moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijulishwe katika majumuisho ya Waziri Mkuu, awafahamishe Wananchi wa Kilwa ni lini barabara hiyo iliyoahidiwa na Mheshimiwa Rais itamalizika? Natambua kuwa ahadi ya Rais ni muhimu kutekelezwa ili ionekane kuwa Rais wetu ni mwadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Kilwa ina matatizo makubwa ya maji. Je, huoni sasa ni wakati wa Hospitali ya Wilaya ya Kilwa kupatiwa maji ya uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa chakula cha njaa Wilaya ya Kilwa. Tunashukuru na kupongeza lakini tumepata changamoto kubwa kwa kutokufika chakula hiki kwa wakati. Kutokana na kutokuwa na barabara za uhakika vijijini hususani Kata za Pande, Mikoma, Lihimalyao, Likawage na Kikole, kwa heshima na taadhima tunaomba barabara hizo za Makao Makuu ya Kata ya Pande, Lihimalyao, Likawage na Kikole zishughulikiwe.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, ambayo inalenga kuendeleza kuleta maendeleo na kubadilisha maisha ya Wananchi hasa wa vijijini kwa kuboresha huduma mbalimbali muhimu za kijamii na kiuchumi kama vile miundombinu, afya, barabara, elimu, maji safi na salama, utawala bora, usawa katika kutoa na kupata huduma. Msisitizo katika Sera ya KILIMO KWANZA na mipango mingine mingi ya kuharakisha maendeleo kwa Wananchi yanakuja kwa haraka na kuwafikia kwa wakati.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii ya mwaka wa fedha 2014/2015 ya ofisi ya Waziri Mkuu, kama itatekelezwa ilivyokusudiwa nina hakika kabisa kwa kiasi kikubwa itabadili maisha ya walio wengi ambao hali zao kimaisha na kimaendeleo ni duni na pia itapunguza Umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuzungumzia suala la wakulima nchini kwetu kwani hata kwenye mchango wangu wa Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana nilizungumzia. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi za kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kulingana na Mipango inayotekelezwa chini ya Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA na Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa.

Katika mwaka 2013/2014, Serikali imesambaza jumla ya vocha za ruzuku 2,796,300, zenye thamani ya Shilingi Bilioni 83 kwa ajili ya mbolea na mbegu bora za mpunga na mahindi kwa Kaya 932,100. Pia, Serikali ilitoa ruzuku ya dawa za korosho kiasi cha lita 158,845 na Tani 620 zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.5.

Vilevile, ruzuku ilitolewa kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora za pamba tani 4,0000 zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.8, miche ya kahawa 350,000 yenye thamani ya Shilingi milioni 100 na miche ya chai 1,850,000 yenye thamani ya shilingi milioni 300. Hiyo yote inatokana na Serikali kuwa na nia nzuri kwa wakulima kwani inatambua umuhimu wao katika nchi na hata ukizungumzia dunia kiujumla, wakulima huthaminiwa sana kutokana na mchango wao mkubwa katika Taifa.

Kutokana na kuboreshwa Sekta ya Kilimo, Serikali ilikuja na Mkakati wa KILIMO KWANZA, lakini mpaka hivi leo haukufanya vizuri kwani wakulima hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo. Ingependeza Serikali ianzishe Mkakati wa ELIMU KWANZA kwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima, kwa kuwa wakulima hawa wanaokusudiwa katika KILIMO KWANZA hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo. Tukija na Mkakati wa ELIMU KWANZA itasaidia wakulima kupata elimu kuhusu kilimo bora. Kufanya hivyo, itasaidia pia kuwapeleka wataalam wetu vijijini na kutoa mafunzo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niikumbushe tu Serikali, tuna wataalam wengi wa fani mbalimbali hapa chini, lakini tuna tatizo moja la kutowatumia ipasavyo na wamekuwa hawatumi fani zao ipasavyo ili kuisaidia nchi katika maendeleo. Ningeomba Serikali iwapeleke hawa wataalam sehemu husika za fani zao na si kukaa maofisini mijini ambako kilimo hakifanyiki. Hapa naongelea zaidi wataalam katika fani za mifugo na mabwana shamba, yaani kilimo, kwani

itasaidia sana kuinua wakulima na wafugaji na kuboresha sekta hizo na kuinua uchumi wa nchi na kipato cha wakulima na wafugaji.

Vivyo hivyo, napenda kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kuendelea kushirikisha Washirika wa Maendeleo kuchangia Programu ya Kuendeleza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT*). Miongoni mwa malengo ya Programu hiyo ni kuwaunganisha wakulima wadogo na mnyororo wa thamani wa kibiashara na Makampuni makubwa ya ndani na nje ya nchi. Ili kufikia lengo hilo, pia Serikali imeanzisha Mfuko Chochezi wa Uendelezaji wa Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT Catalytic Trust Fund*).

Mfuko huo utatoa mitaji itakayogharamia hatua za awali za Miradi inayotoa tija ya haraka ambayo imebainishwa kwenye Mpango Mkakati wa Uwekezaji. Vilevile, Mfuko huo utahamasisha biashara inayolenga kumwinua mkulima mdogo kwa kumuunganisha na mnyororo wa thamani na kampuni kubwa kupitia madirisha makuu mawili.

Dirisha la kwanza ni *Matching Grant Fund* linalolenga kuwezesha kampuni kubwa zilizoanzisha biashara ya kilimo nchini, kuimarisha minyororo ya thamani inayowahusisha wakulima wadogo zaidi au kuanzisha kilimo cha mkataba kati ya wakulima wakubwa na wakulima wadogo. Dirisha la pili ni *Social Venture Capital Fund*, linalolenga kuziwezesha biashara changa na za kati kwenye Sekta ya Kilimo au kuwezesha Kilimo cha Mkataba kati ya wakulima wakubwa na wakulima wadogo. Tayari Bodi ya Mfuko imeteuliwa na Mtendaji Mkuu wa Mfuko ameajiriwa, hatua hiyo ni nzuri na kubwa, wala si ya kubeza kwani wakulima wetu sasa watafaidika na kuona manufaa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali zetu hapa nchini kama tunavyojua zina matatizo mengi sana, matatizo hayo ni changamoto kwa Serikali. Tumekuwa tukiona jinsi wagonjwa wanavyopata shida wanapokuwa hospitalini. Pia kumekuwepo na matatizo upande wa upatikanaji wa madawa. Tatizo la uhaba wa madawa ni kubwa sana katika Hospitali zetu nchini na hii inapelekea watu kupoteza maisha kwa kukosa dawa kwa wakati. Kujumla, hali si nzuri katika Sekta ya Afya na kwa kutambua hilo, napenda kuiomba Serikali itilie mkazo wa kutatua tatizo hili na kuboresha Hospitali zetu. Kuna tatizo pia la upungufu wa Madaktari Bingwa nchini na hasa mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kwa mara nyingine tena, ipeleke Madaktari Bingwa katika Hospitali zote ambazo zina upungufu wa wataalam hao, kufanya hivyo kutasaidia kupunguza usumbufu wa wagonjwa kusafiri kuja Dar es Salaam kuonana na hao madaktari, pia kuna baadhi ya vipimo vinapatikana Dar es Salaam, ila Serikali ikiweza kusambaza vipimo hivyo kote nchini, itawapunguzia wagonjwa hawa kusafiri umbali mrefu kwenda Dar es Salaam kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuzungumzia hali ya Jimboni kwangu Kibaha Vijijini. Suala hili nilisema katika Bunge lililopita na napenda kulisema tena. Tunatambua kila Kata inastahili kuwa na Kituo cha Afya, lakini kule Jimboni kwangu ni Kata chache tu ambazo zina Vituo vya Afya, naomba jambo jili liangaliwe vizuri na kwa mapana yake na umuhimu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mlandizi tuna Kituo cha Afya ambacho kinapokea wagonjwa wengi wanaopata matatizo mbalimbali. Tuliomba Kituo hiki kipandishwe hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya, kwa kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Cha kusikitisha, mpaka sasa kituo hiki hakijapandishwa hadhi na sababu zilizotolewa ni kwamba, hakijakamilisha vigezo. Tunajiuliza ni vigezo gani vya msingi ambavyo havijakamilika ili kituo hiki kipandishwe hadhi na kuweza kuwasaidia Wananchi wetu? Asilimia 80 ya vigezo vyote vimekamilika. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa huruma yake atusaidie Kituo hiki cha Afya kipandishwe hadhi na kuwa Hospitali, kwani hiki ni kilio cha muda mrefu. Wakazi wa Kibaha Vijijini wanastahili kubadilishiwa Kituo hicho cha Afya na kuwa Hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Kituo hiki cha Afya Mlandizi kutokupandishwa hadhi na kuwa Hospitali, Wananchi wanapata tabu pale wanapotakiwa kupata huduma za ziada na kutakiwa kusafiri kwenda Hospitali ya Tumbi. Wananchi hao hutakiwa kuchangia ama kutoa fedha ya mafuta ili yatumike kwenye gari la kubebea wagonjwa kwa ajili ya kupelekwa Hospitali ya Tumbi. Je, sheria inaruhusu kuwachangisha Wananchi hela ya mafuta? Kama siyo sheria naomba jambo hili lisitishwe mara moja kwani limekuwa ni kero kubwa na adha kwa Wananchi ndiyo maana naendelea kulisema hapa Bungeni. Tunaomba Serikali iliangalie hili kwa ukubwa wake na kutekeleza ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais ya kuipandisha hadhi hiki na kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuzungumzia mgogoro wa ardhi uliopo kati ya mwekezaji na wanakijiji wa Kijiji cha Kipangege na Kitongoji cha Kifuru, Kata ya Soga, mgogoro huu unahusu lililokuwa shamba la mkonge ambalo mwekezaji ni Mohamed Enterprises Ltd.; naomba Serikali iuangalie mgogoro huu na kuutafutia ufumbuzi kwani wanakijiji wanataka kuhamishwa katika maeneo yao na kumpisha mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuwa na migogoro ya mipaka nchini kote, nalo hili pia limejitokeza Jimbo la Kibaha Vijijini, limekuwa ni tatizo kubwa kati ya Kijiji na Kijiji, Wilaya na Wilaya na kati ya Kata ya Kwala na Kata ya Ruvu, Kata ya Dutumi na Kitomondo na Kata ya Mama; kwa hiyo, inaleta matatizo makubwa. Naomba Serikali ichukue hatua madhubuti kutatua matatizo haya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna migogoro ya wafugaji na wakulima Kata ya Gwata, Magindu, Kwala, Dutumi na Kata ya Ruvu. Wafugaji wametengewa sehemu maalum ya malisho, lakini wamekuwa wakivamia maeneo ya wakulima na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazao na kusababisha migogoro kuanza. Vilevile migogoro hii imefika hadi mahakamani ili hatua za kisheria ziendeleo na kuchukuliwa, lakini wakulima wamekuwa wakizidiwa nguvu katika kupata haki yao. Tunaomba Serikali iingilie kati matatizo haya ili kuepusha vurugu za wenyewe kwa wenyewe baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa katika mfumo wa elimu, kwa mfumo huu ambao tunao hivi sasa, hakika tunahitaji kuubadilisha ama kuuboresha ili tuendane na wakati kama yalivyo Mataifa mengine ili na sisi tupate maendeleo kwa haraka kupitia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Jimbo la Kibaha Vijijini tuna matatizo mengi sana kwenye Sekta ya Elimu, tuna upungufu wa walimu, madawati, maabara, kwa ajili ya mazoezi ya vitendo katika shule zetu. Pia vitabu vimekuwa haba kwa wanafunzi wetu na hata vikiwepo basi kitabu kimoja hutumiwa na watoto zaidi ya watano. Vilevile tumekuwa na upungufu wa matundu ya vyoo kwenye shule zetu. Napenda kuiomba Serikali ilianganalie hili na kulitafutia utatuzi wa haraka, kwani kuboreshwa kwa elimu yetu na mazingira ya watoto wetu wanayosomea, kutasaidia kuwajenga vizuri watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali ianganalie upya swala la ajira kwa vijana, kwani mpaka sasa idadi ya vijana wasiokuwa na ajira inazidi siku hadi siku. Vijana wanaomaliza vyuo vikuu kila mwaka ni wengi na wanaobahatika kupata ajira ni wachache mno, ukiangalia kwa wastani huo, utagundua kuwa tatizo ni kubwa sana. Naiomba Serikali iweke utaratibu wa kuwajengea elimu ya ujasiriamali vijana hawa tokea wakiwa vyuoni, ili kuwafanya pale wamalizapo elimu zao kujijaji wenyewe na si kusubiria ajira Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia nyingi za kuwawezesha hawa vijana waliomaliza vyuo na kufaulu vizuri. Nashauri ungewekwa utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo midogo midogo kutoka kwenye mabenki yetu ili waanzishe miradi midogo midogo, kwa njia nyingine watakuwa wamejajiri wenyewe. Suala zima la uzoefu katika matangazo ya ajira, naomba lianganaliwe upya katika sekta zote hasa sekta binafsi kwani limekuwa likiwanyima fursa vijana wetu waliomaliza elimu zao za vyuo vikuu. Hivi kwa mfano kila mwajiri akisema anahitaji ajiri mtu mwenye uzoefu; hawa watoto wetu wanaomaliza elimu zao vyuoni nani atawaajiri? Naomba ikiwezekana Serikali itunge sheria kuwabana sekta binafsi kutoa ajira kwa haki na usawa kwa vijana wetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni tatizo pia linaloikabili nchi yetu. Napenda pia kuipongeza Serikali kwa kujitahidi kuboresha miundombinu yetu, ila kuna ukiukwaji wa sheria ambao hufanywa na madereva wachache ambao hupitisha magari yenye uzito mkubwa katika baadhi ya barabara ambazo zimeainisha uzito unaotakiwa. Ifahamike kuwa, Serikali imetumia na inatumia kiasi kikubwa cha fedha kuzitengeneza barabara zetu, naomba usimamizi wa sheria uzingatiwe na adhabu kali zitolewe kwa wale wote watakaobainika kuvunja sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mabunge yaliyopita nilizungumzia Sekta hii ya Barabara hususan ujenzi wa Barabara ya Makofia - Mlandizi hadi Mzenga ambao Mheshimiwa Rais aliahidi zitajengwa. Nilipouliza katika swali langu la msingi katika Bunge lililopita, nilijibiwa kuwa walikuwa wanafanya upembuzi yakinifu, lakini baada ya mimi mwenyewe kufanya uchunguzi wangu wa kina niligundua kuwa, hakukufanyika upembuzi yakinifu na hakuna fedha zozote zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake amesema ile barabara itajengwa kuanzia Bagamoyo mpaka Mlandizi, ikizingatiwa Bandari ya Bagamoyo inayojengwa itafanya hiyo barabara kutumika kwenda bandari ya nchi kavu Mzenga ambako kuna Kituo cha Reli ya Tazara. Pia hakuna uhakika kama itajengwa kutoka Mlandizi mpaka Mzenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kongowe – Soga – Kisarawe pia zingepandishwa hadhi kuwa Barabara za Mkoa. Vilevile Barabara za Vigwaza - Kwala na Dutumi hadi Kisarawe, zipandishwe hadhi kuwa Barabara za Mkoa. Hata hivyo, Barabara za Chalinze – Gwata – Magindu – Lukenge hadi Morogoro Vijijini, barabara hizi zimeunganisha Wilaya tatu, zikiwa katika kiwango cha lami, tutakuwa tumefikia lile lengo la kuunganisha Wilaya hadi Wilaya na kuwafanya Wananchi wa Wilaya hizo kufanya shughuli zao za kibiashara kwa uraisi. Naomba Bajeti ya mwaka huu itilie mkazo katika hili kwani umuhimu wa barabara hizo ni mkubwa sana kiuchumi na kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alituhidi kujenga soko la kisasa Mlandizi na kiwanda cha kusindika matunda, lakini mpaka leo hakuna utekelezaji wa aina yoyote. Tunaomba maelezo kutoka kwa Waziri wa Viwanda na Biashara atakapoleta bajeti yake hapa Bungeni atuambie hizi ahadi za Mheshimiwa Rais zinatekelezeka lini, kwani Wananchi wa Kibaha Vijijini bado wanaendelea kupata harasa kwa kukosa mahali pa kusindikia mazao yao kipindi chote hiki. Pia kuna Mradi wa Machinjio ya Kisasa uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, Mradi huo haufanyi kazi yoyote ikizingatiwa kodi za Wananchi ndizo zilizotumika kufanikisha Mradi huo,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

lakini mpaka hivi sasa umeachwa bila kufanya kazi yoyote ilhali Wananchi walihamasishwa na kuhamasika, wakanunua ng'ombe wa kiasasa ili waanze ufugaji, lakini hivi leo wanapata hasara kutokana na Mradi huo kutokufanya kazi na pia kupoteza ajira. Mradi huo ungeanza kufanya kazi, ungetoa ajira kwa vijana na kusaidia tatizo la ajira kwa kiasi kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha Vijijini linakabiliwa na tatizo kubwa la maji kwa Wananchi wake. Jambo hili nimekuwa nikilisema sana humu Bungeni na pia kumwambia Mheshimiwa Waziri, ingawa Wananchi hawa ndiyo walenzi wakuu wa chanzo cha maji kinachotoka Ruvu kuelekea Dar es Salaam, lakini Wananchi hao wana matatizo makubwa ya maji. Naomba Wizara husika iwaangalie Wananchi hawa kwa jicho la huruma ili na wao waondokane na adha hii ya maji. Vilevile Miradi mingi inasuasua; kwa mfano, Mradi wa Ngeta ambao unatakiwa upeleke maji katika Vijiji vya Kikongo, Mwanabwito na Soga na Kipangege. Pia kuna tatizo la muda mrefu la upatikanaji wa maji Kata ya Boko Mnemela, Vijiji vya Boko Kati, Mpiji na Mkalambati. Tunaomba maelezo ya Miradi hii kwa Wizara husika na ikibidi utekelezaji wake uanze ili Wananchi hawa waondokane na shida ya kutokupata maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kutatua tatizo na kupeleka umeme Kata ya Ruvu. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi hii ulishaanza kwa Waziri wa Nishati na Madini kufanya ziara katika Jimbo na akaona ukubwa wa tatizo. Napenda kujua ni hatua zipi zimefikiwa na nini kinaendelea katika utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu kwani kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka na kuinua uchumi wa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kituo cha Polisi Mlandizi tumekuwa na tatizo la Gari la Polisi na hivyo kufanya shughuli nyingi za kiutendaji kusuasua. Napenda kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa kunihakikishia kuwa pindi watakapopata fedha, basi Kituo cha Polisi Mlandizi kitapewa kipaumbelele katika kupatiwa gari. Napenda kuiomba Serikali, katika bajeti ya mwaka huu tupatiwe gari ili shughuli za kiusalama ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha Wananchi wanapata huduma muhimu ambazo zilikuwa zinafuatwa nje ya nchi kwa Mheshimiwa Rais kufungua kituo cha upasuaji wa moyo pale Hospitali ya Muhimbili. Napenda kuishauri Serikali kama alivyozungumza Mheshimiwa Rais kuwa, kituo kile kiwe kinatoa huduma bila ubaguzi na si watu waliokuwa na fedha tu, kufanya hivyo kutasaidia Wananchi wote kupata huduma kwa usawa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kugusia kidogo kuhusu uwekezaji. Napendekeza Sera na Sheria ya Uwekezaji iwekwe bayana na kumnufaisha Mwananchi. Sheria hiyo iboreshwe kwa kuzingatia masilahi ya Taifa na Wananchi wake. Mwekezaji yeyote wa nje ni lazima awe mbia na Mwananchi na hasa katika masuala ya madini. Hapa kwenye Sekta ya Madini tumekuwa tunapata matatizo mengi kutokana na mikataba tunayoingia kutokusimamiwa vizuri na kutokutunufaisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sheria ya Madini iboreshwe ili tufaidike na madini yetu na tukue kiuchumi, kwani tuna madini mengi sana na mengine huwezi kuyapata nchi yoyote ile isipokuwa hapa kwetu Tanzania, kwa kuzingatia hilo kulikuwa hakuna sababu ya umaskini kuendelea kutokandamiza bali tungekuwa tunafaidika na rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wawekezaji katika Sekta ya Madini wamekuwa hawatekelezi yale yote waliyoahidi kuyafanya kwa jamii iliyowazunguka na hivyo kuwajengea Wananchi imani potofu kuona kuwa Serikali yao haifai kwa kuingia mikataba na wawekezaji kama hao. Naomba wawekezaji wa aina hii wachukuliwe hatua kali za kisheria. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa kurekebisha Sheria ya Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la foleni Jijini Dar es Salaam linazidi kuwa fishio na hivi sasa limeanza kutokea katika miji mingine kama Arusha na Mwanza ingawa katika miji hiyo hali haijafikia katika kiwango kama cha Dar es Salaam. Hivi sasa Dar es Salaam kuna huu Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi, napenda kwanza kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia kwa Mradi huo, lakini kama tujuavyo, changamoto huwa hazikosekani, kwani kampuni ambayo inafanya Mradi huo imekuwa ikisuasua na kuleta hofu Mradi kutokamilika kwa wakati. Siku za hivi karibuni wafanyakazi wa kampuni hiyo waligoma kutokana na madai yao na hivyo kupelekea shughuli kusimama kwa takribani zaidi ya siku tatu.

Napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara husika, iweke utaratibu wa mkandarasi kufanya kazi usiku ili mchana kupisha magari mengine kupita bila kusuasua, kwani kwa hivi sasa kumekuwa na msongamano mkali pale mkandarasi anafunga njia moja ama nyingine, foleni huwa kubwa sana na kufanya safari moja kutumia saa zaidi ya tatu mpaka nne. Tukifanya hivyo, itasaidia kwani muda wa usiku watumiaji wa barabara wanakuwa wachache ukilinganisha na mchana. Pia napenda kushauri upande wa mikoani kuchukua tahadhari mapema kwa kuboresha miundombinu ili kuepuka hali ambayo inaikumba miji mingine kwa matatizo ya foleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashauri watu wa mipango miji kuweka mipagilio mizuri na inayovutia katika miji inayokua hivi sasa ili kuleta mandhari nzuri. Kwa kufanya hivyo, itasaidia watoa huduma kupanga kutoa huduma kutokana na miji hiyo ilivyopangwa vizuri na itarahisisha pia kufikika kwa haraka kwenye matukio kama ya moto, kwani tumejionea wenyewe mara nyingi pindi litokeapo janga la moto, ufikaji wa gari la zima moto unakua mgumu na pindi linapofika, hufika kwa kuchelewa na lawama kupelekwa moja kwa moja Jeshi la Zima Moto, lakini tukiwa na miji iliyopangika itasaidia sana kupunguza adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kwamba, matumizi ya fedha za kigeni yanaathiri sana uchumi wetu na watu wetu pia. Naomba Serikali itilie mkazo na kusimamia hilo na kukataza biashara ndani ya nchi zifanyike kwa fedha za kigeni na badala yake shilingi yetu ndiyo itumike katika matumizi yote. Kufanya hivyo kutaleta heshima ya sarafu yetu na Taifa kwa ujumla. Jambo hili nililizungumzia katika Bunge lililopita lakini naona bado matumizi haya yakiendelea hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha Vijijini liko mbali na Ofisi za Halmashauri ambazo zipo Kibaha Mjini. Wananchi huteseka kutembea umbali wa kilometa 40 kuanzia Kata ya Magindu mpaka Kibaha Mjini kufuata huduma muhimu. Kwa maana nyingine, huduma wanainunua kwa gharama kubwa, huku kipato chao kikiwa cha chini. Wananchi hawa huacha shughuli zao mbalimbali za kujitafutia kipato na kufuata huduma hiyo. Nashauri ofisi hizi zihamishiwe Mji Mdogo wa Mlandizi kwani kuna maeneo hata ya kukodi ili kuwapunguzia Wananchi mzigo mkubwa. Ukizingatia hilo pia kuna tatizo la ukosefu wa benki, tunaishauri Serikali itoe msukumo ili tuweze kupata benki kuwapunguzia adha Wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuikumbusha Serikali ile ahadi ya Mradi wa Barabara nne kujengwa kutoka Kimara hadi Mlandizi, Mlandizi hadi Chalinze umefikia wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akija atueleze Mradi huu utanza lini na kukamilika lini? Vilevile napenda kuishauri Serikali kupitia Mradi huo, badala ya hizo barabara kuishia Chalinze basi Mradi huo uje mpaka Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kugusia jambo lililojitokeza siku za usoni; kumegundulika Ugonjwa wa Dengua ambao mpaka hivi sasa Serikali kupitia Wizara ya Afya, imekiri kuwa ugonjwa huo upo na hauna tiba kamili. Mpaka hivi sasa wananchi wanaendelea kuteseka na ugonjwa huo, wengine wameshapoteza maisha na wengine bado wamelazwa hospitalini. Naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kutafuta tiba ama njia mbadala ya kuuondoa ugonjwa huu kwani umekuwa tishio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato la Taifa katika mwaka 2013 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 mwaka 2012. Ongezeko hilo limetokana na ukuaji mzuri wa shughuli za huduma za mawasiliano, viwanda, ujenzi na huduma za fedha. Kutokana na ongezeko hilo, wastani wa pato la Mtanzania limeongezeka kutoka shilingi 1,025,038 mwaka 2012 hadi shilingi 1,186,424 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Mfumko wa bei umechangiwa na kupungua kwa kasi ya kupanda bei za bidhaa na vyakula hasa mahindi, mchele na aina nyingine ya nafaka. Hatuna budi kuipongeza Serikali kwa hatua hii na kuishauri iendeleze juhudi hizi ili nchi yetu izidi kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L.A KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu barabara ya Kidatu – Ifakara – Ifakara – Mlimba – Mlimba - Madeke - Njombe ambazo ni za changarawe na udongo na zimeharibika vibaya na mvua zinazoendelea na huko ndiko kwenye mashamba makubwa ya kilimo cha mpunga, cocoa na mahindi yaliko. Ni hatua gani za haraka zinachukuliwa kunusuru barabara zilizoharibiwa na mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachukua hatua gani za dharura ili kunusuru maisha ya wananchi wa Kilombero na Ulanga kwa kupeleka boti za kusafirisha abiria badala ya kuachia Halmashauri ambazo hazina uwezo wa kutosha kusafirisha wananchi ukizingatia mvua zinazoendelea hivi sasa. Ni juzi tu tarehe 6/5/2014, Nahodha wa mtumbwi amekufa akiwa safarini ndani ya mto Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji kujulishwa baada ya ujenzi wa daraja la Kilombero kusombwa na mafuriko. Je, Serikali haioni haja ya kuanza upya tathmini na upembuzi yakinifu kulingana na hali halisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi Wilaya ya Kilombero kati ya wananchi na JWTZ Chita, wananchi na Maliasili, wawekezaji Chita na wananchi wa Kata za Wilaya ya Kilombero ni lini Serikali itakwenda kumaliza migogoro hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia maafa, Mkoa wa Morogoro na hasa Wilaya ya Kilombero ambako barabara zote hazipitiki na kupelekea vifo na watu kukosa makazi, naomba upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha RCC Morogoro ilipitishwa hoja ya kugawa Wilaya ya Kilombero kuwa Majimbo mawili na kugawa Mkoa wa Morogoro kuwa na Mikoa miwili, mmoja Morogoro na wa pili Kilombero kwa kuwa una vigezo vyote. Je, ni lini sasa Serikali itakubali pendekezo hilo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la mchele na ushirika wa wakulima. Pamoja na wananchi wa Ifakara kuanzisha ushirika wa mazao lakini hawakupata msaada wa Serikali kwa mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunapitisha bajeti lakini haitekelezwi kwa wakati na kupelekea miradi inayoanzishwa kuharibika na fedha kupotea bure. Ifike wakati sasa kusimamisha miradi mipya na kukamilisha ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa kijiji kipya cha Meleta kilichopo Wilaya ya Kilombero wamechangishana nauli kuja kufuatilia ahadi yako ya ujenzi wa barabara na kuagiza TANROAD tarehe 17/10/2009, hivyo tunahitaji majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kushika mshahara wa Waziri Mkuu hadi nipate majibu kuhusu hoja nilizowasilisha.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu na Wizara zilizopo chini yake kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Manispaa ya Iringa. Hospitali hiyo ilijengwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wagonjwa lakini ni huduma ya OPD, jengo la wazazi (*maternity ward*) na *theatre*, ndio zinatoa huduma. Kuna fedha za ujenzi wa jengo la maabara na x-ray bado hazijaletwa. Pia tatizo la gari la wagonjwa ni kubwa sababu hakuna vyumba kwa ajili ya kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la Halmashauri zetu ni ucheleweshaji wa pesa za miradi. Ni vema pia Serikali ingetaja vigezo vinavyotumika kugawa hizo pesa za miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 33, miradi ya umwagiliaji, niipongeze Serikali kwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji lakini ipo miradi ambayo ipo katika Kata ya Isakalilo (*Mkoga Irrigation Scheme*). Miradi hii ni ya muda mrefu sana, kuna nguvu ya wananchi na kuna nguvu ya Halmashauri, naomba kupata maelezo vigezo vinavyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lipo daraja katika Jimbo la Iringa Mjini la Igumbilo kila mwaka linaleta maafa lakini uwezo wa Halmashauri ni mdogo kujenga daraja hili. Serikali ilileta Tshs.156m, tunaomba itoe kibali ili kujenga hata daraja la muda kwa sababu ili daraja hili liweze kukamilika zinahitajika Tshs.1.1 bilioni na Serikali imekuwa haileti pesa tena kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali iangalie katika bajeti yake kutenga pesa kwa ajili ya Wenyevidi wa Serikali za Mitaa na Vitongoji wapatiwe

posho za kutosha kwa sababu wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana na wengine hata ofisi hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa unakabiliwa na madeni makubwa sana ya wazabuni wanaotoa huduma katika magereza yetu na Jeshi la Polisi. Hawa wazabuni wana mikopo mikubwa katika benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itenge pesa za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za kiuchumi za Mkoa wetu kama vile ile inayokwenda Ruaha Jimbo la Kalenga, ile barabara ya Kilolo-Mwata inatengewa pesa kidogo sana. Niipongeze Serikali kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Dodoma-Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe Serikali itupe maelezo kuhusu ujenzi wa kiwanja cha Nduli. Katika bajeti ya mwaka jana tuliambiwa kipo katika orodha ya viwanja vitakavyofanyiwa marekebisho lakini hotuba ya Waziri Mkuu kiwanja hicho hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%.

MHE. ALHAJ MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kushukuru kwa kupata Wilaya mpya ya Ikungi lakini naomba sana matatizo yaliyopo kati ya Halmashauri ya Ikungi na Halmashauri mama yatatuliwe haraka, kuhusu mgawo wa fedha; mgawo wa mali za Halmashauri ya Singida Vijijini; mgawo wa watumishi na maslahi yao; stahili zinazowahusu watumishi waliohamia Halmashauri ya Ikungi – fedha za uhamisho na ikama za watumishi wa Halmashauri ya Ikungi itazamwe upya ili ikidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, RCC ya Mkoa wa Singida ilipitisha uamuzi wa kuiomba ofisi ya Waziri Mkuu isaidie ujenzi wa daraja la Minyughe ambalo ni kubwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi haina uwezo wa kulijenga. Mkurugenzi wa Ikungi aliwasilisha ombi hilo kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka jana. Aidha, mimi mwenyewe nilimuandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kusisitiza maombi hayo na niliambatanisha nakala ya barua ya Mkurugenzi na mchanganuo wa gharama. Naomba kujua ombi hili kama limewekewa fedha katika bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua lini ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Ikungi utaanza?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya uhamisho wa Walimu Wilaya Ikungi ni Tshs.2,500,000/=, haitoshi kabisa hii ni bajeti ya Mwalimu mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida haijapatiwa fedha zilizotengwa katika bajeti ya 2013/2014. Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya Hospitali hii zilizotolewa hadi sasa ni kiasi cha shilingi billion 1.8 tu. Naomba fedha hizi zipelekwe kabla ya mwisho wa Juni 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini masuala haya yazingatiwe.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu S.W kwa kunijalia afya njema na uwezo wa kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya Taifa. Kuna ajenda ya siri katika utoaji wa vitambulisho vya Taifa hasa Zanzibar na zaidi Pemba. Ajenda hiyo ya siri imesababisha urasimu mkubwa na usumbufu usio na mfano. Hii inatokana na mipango ya makusudi iliyoandaliwa ili kudhibiti kura za maoni katika Katiba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje kule Pemba mtu anaenda kutaka kupatiwa haki yake ya kiraia ya kupatiwa “kitambulisho cha Taifa” anajibiwa hawezi kupewa eti kwa sababu kitambulisho chake cha Uanzibari ukaazi kime-expire! Hivi Mzanzibari Uanzibari wake au Utanzania wake unapotea kwa sababu ya kipuuzi kama hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masheha pia wanakataa kuwapa barua za utambulisho wakaazi wa Shehia zao wasio na “Zan ID” ambao ni Wanzanzibari! Ama kwa upande wa ndugu zetu Watanganyika wanaoishi Zanzibar na Pemba wanapewa vitambulisho vya Taifa bila ya usumbufu na kwa kupembejewa (kubembelezwa) na wanafuatwa mpaka mashambani kuhimizwa na kubembelezwa. Tunahitaji majibu sahihi juu ya kadhia hii kwani kuna dalili za kupewa vitambulisho wageni kwani pia watu wanaoonekana si Wanzanzibari wa Pemba wakitoa rushwa ya Tshs. 5,000/= tu kwa Sheha wanapewa kitambulisho cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi. Hivi ni kweli kuna uwazi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali? Au hata ni kweli kuna nia ya dhati ya kutaka kuwepo uwazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Rasimu ya Katiba mpya, Sura ya Sita imependekeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi ziwe ni tunu za Taifa. Kama kweli kuna nia ya dhati ya kutaka uwazi katika shughuli za Serikali. Wajumbe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wanaounga mkono mawazo ya CCM ambao ni wengi katika Bunge hili na la Katiba wamekataa zisiwe tunu ya Taifa! Tunu ni kitu ambacho mtu anakitamani akipate na akikipata basi hukitunza sana. Bila ya kuwa na uwazi, uwajibikaji na ufanisi hatutaweza kuwa na “*Big Result Now*” bali tutakuwa tunajidanganya au tunaota ndoto za Alinacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya miundombinu ya masoko, uongezaji thamani na huduma za kifedha vijijini. Kwa upande wa Zanzibar na hasa Pemba katika Wilaya ya Chake Chake, Jimbo la Chonga hatujaona hata dalili za jambo hili. Kwa vile tulipewa barua kutoka ofisi ya Waziri wa Nchi, Sera na Uratibu tukitaarifiwa juu ya jambo hili jema, tunahitaji na watendaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambao fedha hizi za miradi hii zinapitia wapewe maagizo rasmi ya kuwashirikisha kikamilifu Wabunge kwa ujumla wao katika Wilaya husika. Kwa kufanya hivyo tu ndio tutatarajia ufanisi wa miradi hii kinyume chake tusebiri ujisadi wa mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, homa ya dengue. Tokea Januari, 2014 umelipuka ugonjwa huu mpya hapa nchini na hasa katika jiji la Dar es Salaam. Mpaka sasa kuna zaidi ya wagonjwa 200 na karibu wagonjwa 3-5 wamepoteza maisha. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu ugonjwa huu? Hotuba ya Waziri Mkuu haikugusia kabisa kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na uzoaji wa taka ngumu. Kuna tatizo katika Halmashauri hii kunakopelekea kero kwa wakazi maskini wa Manispaa ya Ilala. Kero ya kuwapandishia ada ya kuzoa taka ngumu kwa kaya kutoka shilingi 2,000/= mwaka 2012/2013 mpaka shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa kaya. Gharama zimepanda kwa asilimia mia tano (500%). Hili ni tatizo na ni ujisadi wa mchana. Kuna nini kimesababisha gharama kupanda kiasi hiki? Ni wapi duniani tumeiga jambo hili? Huku ni kuwapunguzia watu umaskini au ni kuwaongeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Housing*. Kuna dalili za wazi za ujisadi hasa katika ukarabati unaoendelea wa nyumba za bei ya wastani Kawawa Road Ilala Dar Es Salaam. Kampuni inayokarabati haijulikani na hakuna bango linaloonesha nani anafanya nini. Kuna vibarua wasio na ujuzi ndio wanakarabati na wamesababisha kero na adha kubwa kwa wapangaji wake hasa wakati huu wa mvua. Madirisha ya *aluminium* waliyoweka ni hafifu sana, hayana hata wavu wa mbu na la zaidi yanaingiza maji kama vile hakuna dirisha kabisa. Tuhahitaji Waziri Mkuu atupe majibu ya ujisadi huu na pia Bunge liunde Kamati Maalum kwenda kuangalia na kufanya tathmini ya matumizi mabaya ya fedha za umma kabla ya CAG!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ukanda wa Ziwa Tanganyika uunganishwe kwa ujenzi wa barabara kutokea Kata za Kalya na Buhingu kwenda Mpanda ili kuchochea biashara na uchumi ukanda huu pamoja na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli ya Liembe imezeeka, ina zaidi ya karne moja na Serikali inaadhidi kuleta meli miaka mingi bila mafanikio hata wananchi kupoteza imani. Meli ya Liemba leo inasafiri mara mbili kwa mwezi. Meli hii ni ajali inayotembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kati ndio uhai wa uchumi na maendeleo. Reli hii imezeeka na huduma ya usafiri ni duni kuliko nchi zote Afrika, hii ni aibu. Tunatumia pesa nyingi kukarabati barabara kutokana na reli duni. Mikoa ya Kigoma, Singida, Tabora imeathirika sana kwa uduni huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ukanda wa Ziwa Tanganyika ndio inaongoza kwa vifo vya mama wajawazito Afrika Mashariki kutokana na usafiri duni na ukosefu wa vituo vya afya vya uhakika hasa Kata ya Kalya. Nashauri Serikali isaidie kukamilisha kituo cha Kalya kiwe na huduma kusaidia hali ngumu ya afya eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuleta umeme Wilaya ya Uvinza bado unasuasua ingawa zimetolewa ahadi nyingi kwa muda mrefu. Nashauri hili lipewe uzito kwa kuwa hapa tunasafirisha tu umeme wa ziada toka Kigoma mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi wa IPTL na Serikali kupitia Wizara za Nishati na Madini, Hazina, Benki Kuu inapaswa maelezo yatolewe kwani ufisadi huu ni mkubwa wa zaidi ya dola 122 milioni hasa katika kipindi hiki ambacho TANESCO ina deni kubwa la zaidi ya bilioni 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji bado ni tatizo Kanda ya Ziwa Tanganyika hasa za Kalya, Buhingu, Simbo na Igahela. Pia Kata za Mganza, Mtego na Uvinza zote zina tatizo kubwa la maji ingawa zinazungukwa na mto Malagarasi na Ziwa Tanganyika ambalo lina zaidi ya asilimia 17% ya *fresh water* duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa eneo la Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza. Mkuu wa Wilaya kaelekeza Halmashauri ya Uvinza kuwa eneo lile ni mali ya Serikali Kuu na anagawa majengo wakati Halmashauri imekabidhiwa. Pia eneo la Makao Makuu limezungukwa na shamba la mwekezaji wa AGROSOL. Nashauri uamuzi wa Serikali kutoa shamba hili kwa mwekezaji ubatilishwe kwani migogoro ya eneo hilo haitakuwa salama kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gati la Buhingu zaidi ya miaka mitano ujenzi ulisimama na Dkt. Mwakyembe akaahidi kupatia ufumbuzi mpaka leo hakuna kinachoendelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho ya hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu mapitio ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2013/2014 na mwelekeo wa kazi zitakazotekelezwa, Mheshimiwa Hawa Ghasia atoe kauli kuhusu mambo/masuala yafuatayo:-

Kwanza, utawala bora. Waziri atoe kauli juu ya hatua zilizochukuliwa baada ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwasilisha ripoti ya ukaguzi wa Shirika la Usafiri (UDA) iliyobaini ufasidi na ubadhirifu.

Pili, uchaguzi wa Mitaa. Wizara ya TAMISEMI imefikia wapi katika kutekeleza maombi yangu ya kurekebisha kwa muundo wa Kamati za Mtaa - majukumu ya Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa, mamlaka ya Kamati na idadi ya wajumbe kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa Jijini Dar es Salaam. Aidha, hatua hiyo ifuatiwe na marekebisho ya uendeshaji wa uchaguzi wa mitaa kwa kuleta Muswada Bungeni na kuwezesha uchaguzi huru na haki utakaosimamiwa na sheria badala ya kanuni zitakazofungwa na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI (Waziri Mkuu).

Tatu, Wakala wa Usafiri Haraka Dar es Salaam (DART) anapaswa kushughulikia matatizo yaliyopo katika mradi wa BRT. Wafanyakazi wamerejea ofisini kwa vitisho sio kwa kuridhika kwa kuwa madai hayajashughulikiwa na Mkandarasi Strabag ambaye pia amepewa mkataba mwingine Arusha. Aidha, Serikali ieleze kiwango cha fedha kilichotumika mpaka sasa na sababu ya kiwango cha fedha kuzidi kilichokuwepo kwenye mikataba.

Hivyo maombi ya fedha za nyongeza bilioni 109 toka Benki ya Dunia ambazo ni za mkopo yasiridhiwe mpaka kwanza taarifa za kina za mradi awamu ya kwanza ziweze kutolewa. Pia, kasoro za kutokuweka njia mbadala wakati wa ujenzi, uharibifu wa miundombinu ya maji, kutokuweka mitaro na hivyo maji kujaa Magomeni.

Nne, mradi wa kuendeleza Jiji la Dar es Salaam (DMDP), ukarabati wa barabara hizo za mitaa zinazounganisha DART uunganishe na ya Kimara-Mavumnza-Bonyoko-Ilala ambayo ni ahadi ya Rais ya Mei 2010 kwamba ingefanyiwa marekebisho na ujenzi kwa kiwango cha lami mwaka huo. Barabara hiyo niliipendekeza kwenye DMDP hata hivyo mrejesho kamili haujatolewa.

Tano, utatuzi wa migogoro ya mipaka kati ya Halmashauri ya Kisarawe ya Mkoa wa Pwani na Halmashauri ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam kwa kufanya maeneo ya Kisopwa, King'azi na Mhoganzila yaendeleo kuwa Kinondoni ambako wananchi wanataka badala ya kudai kwamba wananchi hao wako Mkoa wa Pwani. Aidha, ufumbuzi pia upatikane kwenye mgogoro wa Msalanzi ambao niliwaandikia TAMISEMI.

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ni kati ya miji inayokuwa kwa kasi kutokana na biashara ya utalii na kwa kuwa ndio njia kuu ya kuingilia lango kuu la Mamlaka ya Ngorogoro na Serengeti. Kwa umuhimu wa watalii nchini hasa mapato tunayopata, hivyo ni wajibu wa Serikali kuhakikisha miundombinu ya usafiri wa uhakika inapokuwepo, ni jambo ambalo haliepukiki. Kwa umuhimu huo, Wilaya ya Karatu ina uwanja wa ndege wa Manyara ambao hautumiki wala kufanyika shughuli zozote. Je, ni lini uwanja huu utakarabatiwa na kuanza kutumika? Serikali itupatie majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme Vijijini. Kwa umuhimu huo wa Wilaya ya Karatu na biashara ya utalii, uwepo wa nishati ya umeme ni jambo muhimu sana. Wilaya hiyo ina vijiji 49 kati ya hivyo takribani vijiji 25 havina umeme. Serikali itupatie majibu ya uhakika mpango wa REA kwa Wilaya ya Karatu umefikia katika hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya Taifa. Zoezi la kuwapatia wananchi huduma hii kasi ni ndogo sana jambo ambalo linaleta mashaka sana endapo kuna uhakika wa Watanzania kupata vitambulisho vya utaifa. Kwa kuzingatia jioografia na idadi ya watu hapa nchini ni hakika kabisa kuwa jambo hili litachukua muda mrefu, hivyo ni muhimu sana kuchukua hatua za haraka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha zoezi hili.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika bajeti hii katika maeneo yahasuyo misamaha ya kodi na athari za uchumi wetu. Ni dhahiri kwamba suala la misamaha ya kodi ni jambo linalopaswa kuangaliwa upya ili kuwepo na mjadala mpana na makampuni makubwa hasa ya madini kuhusu upunguzaji wa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Taifa letu limekuwa na ombwe litokanalo na Serikali kutokuwa na nidhamu ya matumizi ya Serikali kwenye fedha za umma. Imekuwa ni kawaida kwa miradi mingi ya Serikali kupewa makadirio halisi ya miradi husika lakini cha kusikitisha ni muda mfupi tu miradi hii hulazimika kuongezewa fedha maradufu na wakati mwingine kuzidi hata kiwango cha awali cha miradi hiyo ilivyotengewa. Hili tatizo linazidi kukua kila siku zinavyozidi kwenda. Kuna mifano kadhaa ya kuthibitisha jambo hili. Naomba Serikali iwe makini na jambo hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi wa China na Tanzania Kurasini. Kwa muda kumekuwa na malalamiko mbalimbali ya wananchi waliohamishwa eneo la Kurasini Shimo la Udongo kupisha mradi huu mkubwa wa kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwalipe wananchi hawa wanaohangaika kufuatilia fedha zao za malipo. Hili ni jambo linaloleta mateso makubwa kwa raia hawa, kosa lao ni lipi? Tafadhali Serikali iangalie kwa uzito madhila wayapatayo raia hawa na familia zao.

MHE. DKT. PINDA H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wizara hazijatajwa katika hotuba ya Waziri Mkuu, ikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba kushauri *next time* iwemo kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 64 imetaja Vyu vya Maendeleo ya Wananchi kwa sentensi moja tu. Aidha, Wizara ina masuala ya *Women Development Bank*, uwezeshaji wa wanawake, usajili wa *NGO's*, Idara ya Mtoto, Jinsia na kadhalika, zote hazijatajwa. Ushauri na ombi *next time* masuala ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto yawemo kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wilaya zinazalisha sana mahindi. Wilaya hizi zipo Mikoa ya Rukwa, Njombe, Katavi, Songea na mteja mkubwa wa mahindi haya ni Serikali (*NFRA*). Changamoto ni ushuru wa mazao katika *Council* hizi mfano Ludewa. Je, fedha hizi za ushuru wa mazao zitalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maafa, Wilaya ya Ludewa, Kata ya Ruhuhu/Masasi Manda kulikuwa na mafuriko. Ombi, Idara ya Maafa iwasiliane na Mkurugenzi kwa ajili ya ku-*rescue* hali hii ya upungufu wa chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe-Ludewa-Itoni imekuwa ni changamoto sana. Ombi izingatiwe kwenye bajeti.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwasilisha shukrani za dhati kutoka kwa wananchi wa Mtwara kwa Serikali kukamilisha ujenzi wa daraja la Nangoo kwani hiki ni kiungo kizuri kwa biashara kati ya Tanzania na Msumbiji. Naipongeza sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, akina mama lishe wa Mtwara wanaishukuru TPDC kwa kuwapatia majiko ya gesi ambayo yameongeza tija katika biashara yao kwa kuwarahisishia kazi na kupunguza uharibifu wa mazingira kwani matumizi ya mkaa katika shughuli za kupika yamepungua.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, iharakishe matengenezo ya kipande cha barabara kilometa 15 kati ya Ndundu na Somanga ili kuondoa adha ya usafiri kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa Serikali ifuatilie suala la ujenzi wa barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala - Masasi ambayo ni barabara ya uchumi hasa kwa zao la korosho. Naiomba sana Serikali itekeleze ahadi ya ujenzi wa barabara hii kwani inalalamikiwa sana na wananchi wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isikilize kilio cha Wabunge kuhusu suala la maji na katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mtwara maji ni tatizo kubwa linalorudisha maendeleo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijipange vizuri kufanya tathmini ya Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015 na pia kupanga mikakati ya baada ya mwaka 2015 hasa kwa upande wa afya ya mama na mtoto na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuitaka Serikali iondoe kero za mfumo wa stakabadhi ghalani hasa kwa upande wa ucheleweshaji malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuiunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu. Aidha, naiomba Serikali kutekeleza yale yote ambayo wamepanga kutekeleza kama ilivyowasilishwa katika makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ofisi ya Bunge 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya wanyamapori bado kuna changamoto ya migogoro ya mipaka na vijiji. Katika marejeo ya Sheria ya Wanyamapori (2009), Serikali ilielekeza kupitia/kutafakari na kuona kama kuna hoja ya kuendeleza mapori tengefu 42 yaliyokuwepo wakati ule lakini hadi leo 2014 Serikali bado haijaleta jibu juu ya mapori tengefu hayo 42 ambayo mengine hayana hata tija badala yake kuleta adha kwa wananchi wa vijiji jirani. Nashauri Serikali kufuta baadhi ya mapori haya tengefu likiwamo pori la Kilombero ambalo linazungukwa na wananchi ambao wengi wako kule kihalali kwani vijiji vyao vimesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza kwa kutounga mkono hoja mpaka nipatiwe maelezo ya kina kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, hotuba ya Waziri Mkuu na mpango wa maendeleo havikugusa chochote juu ya maendeleo ya Mikoa ya Kusini (*Mtwara Corridor*).

Pili, Serikali imekaa kimya juu ya kilometa chache za barabara ya Kibiti – Lindi, lini zitakamilishwa? Tatizo liko wapi?

Tatu, kwa kipindi kirefu sasa Lindi na Mtwara shughuli za kisiasa (mikutano ya hadhara) imesimamishwa. Nataka kujua hii ni amri ya nani na ni kwa sababu zipi? Pia nijue ni kwa muda gani? Kuna maeneo mengi ambayo huwa yanatokea kuwa na vurugu na hata mauaji lakini mikutano inafanyika Lindi na Mtwara kuna ajenda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Waziri Mkuu mpaka nipatiwe maelezo ya kina kuhusu mradi wa uboreshaji miundombinu (CIUP). Miradi hiyo ya mkopo wa Benki ya Dunia umetokelezwwa kifisadi na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa hadi hii leo. Mfano rahisi ni Ilala, Kata za Buguruni, mitaa ya Malapa, Madenge na Mnyamani, Vingunguti, Mtakuja, Miembeni na Kombo kulikuwa na miradi ya barabara za changarawe, lami, mifereji, vizimba vya taka ngumu, taa za barabarani, kioski cha maji (DAWASCO).

Barabara za changarawe zimeharibika bila matengenezo, taa hazipo baada ya nguzo kuanguka, maji hakuna pamoja na DAWASCO kulipwa, vizimba vya taka ngumu havipo, mifereji imebomoka. Kama hapa Dar es Salaam panaonekana na wengi pako hali hii, Manispaa za pembezoni kama Lindi ambayo ipo kwenye mpango huu itakuwaje? Naomba maelezo ya kina na hatua zitakazochukuliwa kwa wote waliohusika na ufisadi huo.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Bahi unaendelea kukua kwa kasi na sasa ni miaka minne Halmashauri ya Wilaya wamekuwa wakiomba fedha za kuleta maji Tshs.1.5 bilioni toka Kijiji cha Mbwasa (Manyoni 43 km) lakini Halmashauri haijapewa fedha hizo. Je, ni lini Serikali itatoa fedha hizo kwa Halmashauri ili kumaliza tatizo la ukosefu wa maji katika Mji wa Bahi ambapo kwa sasa ni kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa takribani watumishi wote waliotakiwa kuhamia Halmashauri ya Wilaya ya Bahi tayari wamehamia lakini hawajalipwa fedha zao za uhamisho hadi sasa. Je, ni lini watumishi hao watalipwa fedha zao hizo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa yanaendelea lakini hadi sasa hakuna maelezo au ufafanuzi wowote au taarifa yoyote iliyotolewa kwa viongozi au wananchi ambapo kwa sasa wakulima na wananchi wamekuwa wakipigwa propaganda za uongo kuwa Bahi Mto Bubu utafungwa kujaza Bwawa hilo na wakulima wa umwagiliaji mpunga wa Bahi hawatapata maji kwa miaka minne. Je, Serikali itashirikisha kikamilifu viongozi na wananchi juu ya mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatoa fedha za kumaliza ujenzi wa Bwawa la Kongoro ambalo kwa miaka minne sasa halijakamilika pamoja na umuhimu wake kwa wakulima na wafugaji wa kijiji cha Bahi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwekezaji wa kiwanda cha kokoto katika kijiji cha Mpamantwa (Bahi) hatuelewi yupo pale kwa mkataba gani na toka kwa nani na wamekuwa ni wasumbufu kwa wananchi hata mambo waliyokubaliana na wananchi kuwa watafanya hawajafanya na hali ya usalama sasa eneo hilo inadolora kila siku kwa migogoro baina ya mwekezaji na wananchi, je, ni lini Serikali itaingilia kati mgogoro huo? Pamoja na kuwa mimi Mbunge tulishirikiana na DC-Bahi kwenda hadi TIC na Wizarani juu ya mgogoro huo lakini hadi sasa Wizarani au TIC haijatoa jibu la kutosha kwa wananchi. Tafadhali naomba ofisi yako itusaidie juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi ya DC-Bahi haina watumishi wa kutosha hadi sasa. Toka Wilaya hii ianzishwe ina watumishi sita tu kati ya 14 wanaotakiwa ikiwemo Dereva mmoja tu. Je, ni lini Serikali itarekebisha ikama ya watumishi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme mkubwa unaotoka Iringa kwenda Shinyanga (400) ambao pia utashusha umeme katika baadhi ya vijiji Wilayani Bahi (Kigwe na Mpamantwa) utekelezaji wake utanza lini na kwa sasa upo hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utoaji fedha za maendeleo kwa Halmashauri za Wilaya toka Serikali Kuu hauridhishi hata kidogo. Serikali ina mpango gani kurekebisha hali hii?

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu umetimiza miaka 50. Takwimu zinaonesha asilimia 90.6 ya watu wote wamezaliwa ndani ya Muungano na wanajua Tanzania.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Muungano, iandae makala na vipindi mbalimbali kuelezea historia na mafanikio yaliyokwishapatikana ndani ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Bahari Kuu: Sera zetu za uvuvi ziendane na mabadiliko ya kiuchumi na kuongeza Pato la Taifa. Umefika wakati tuangalie upya leseni zinazotolewa kwa meli za kigeni zinazojishughulisha na uvuvi katika Bahari Kuu. Utaratibu wa sasa unaotumika kulipia leseni tu bila ya kujua meli hizi zinavuna samaki tani ngapi; kwa nini tusiandae utaratibu tunapotoa leseni kufuatilia na kujua samaki wanaovuliwa na kulipiwa? Mfano halisi ni Samaki wa Magufuli waliovuliwa katika bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wapatiwe mikopo ya vifaa vya uvuvi katika vikundi vyao ili waweze kuvua katika kina kirefu cha maji waongeze mapato yao na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, haki za binadamu zisiachwe zikatumika vibaya. Tumeshuhudia baadhi ya Vyama vya Siasa, Vikundi na watu wakitumia vibaya haki hii na kusababisha kuvunja haki za wengine, Vyama hivi, vikundi au watu hao, Serikali iwachukulie hatua kali ili liwe funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kwa makusudi kabisa itambue kundi la watoto wanaoishi katika mazingira magumu kuwa lipo na linaendelea kukua.

Serikali ina mipango gani ya kulinusuru kundi hili? Leo ni watoto lakini kesho watakuwa na kuwa wazee wa mitaaani na kuendeleza mtandao huu. Tulisaidieni kundi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza yafuatayo:-

Naiomba Serikali nipate takwimu za kiasi gani kilipelekwa kwenye kila Halmashauri kati ya bilioni 8.7 zilizotengwa kutokana na vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipunguze maeneo ya kuhifadhi nchini na yagawiwe kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Capitation* iliyotolewa Meatu zilipelekwa shilingi ngapi?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Meatu wamepeleka shilingi ngapi za madawati? Ahsante.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza erikali kwa kuanzisha Mifuko ya Kuwawezesha Kiuchumi Akina Mama na Vijana. Kinachotakiwa ni kuongeza mitaji katika Mifuko hiyo. Lazima yatolewe mafunzo ili wahusika waweze kuisimamia Miradi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Wananchi wakashiriki katika Sekta ya Gesi na Mafuta, mmoja mmoja au kitaasisi. Hata nchi zinazotoa mafuta na gesi zimewahusisha Wananchi wao au Taasisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba shilingi milioni 650 za maji Mjini Pangani ziletwe Pangani ili Mradi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba Mivumoni na Kilimangwido yafutwe ili yagawiwe kwa Wananchi. Mashamba hayo yametelekezwa tangu mwaka 1989. Masuala hayo yako ofisini kwa Mheshimiwa Waziri tangu mwaka 2006 na bado hayajatolewa ufumbuzi. Wananchi wa Wilaya ya Pangani wanahitaji majibu katika masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi imeitaja Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo, yenye kilomita 178, kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, Mradi huu umefikia wapi? Wananchi wangependa kupata *feedback* ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa Mradi wa Umeme Vijijini. Kijiji cha Mhalamo tunaomba Kata za Ubungu na Bushini hasa Vijiji vya Kugurusimba vipatiwe umeme.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia. Naomba nianze kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atupe ufafanuzi sisi Wananchi wa Babati, juu ya migogoro ya ardhi iliyokithiri na ni ya muda mrefu sana. Bado migogoro mipya inazaliwa na hakuna hatua za dhati zinazochukuliwa, ni kazi za zima mota kila siku, Wananchi, Wawekezaji na Viongozi wanaishi kwa hofu ya kukamatwa na Vyombo vya Usalama wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu Bonde la Kiru kumetokea machafuko tena na mwekezaji amechomewa mali zake kwa mara ya pili na hana tatizo Wananchi. Viongozi wa vijiji wote wamekamatwa na wana hofu, matatizo

huanza kidogo kidogo, hatua za kisheria hazichukuliwi na ndiyo chanzo cha kuwa tatizo kubwa. Tume iliyoundwa miaka mitatu iliyopita, yenye Mawaziri watano, hadi leo mrejesho wake hatujaupata. Mimi kama mdau, mwakilishi na mwezeshaji, hadi leo sijawahi kuhojiwa wala kuombwa maoni ya jinsi ya kumaliza mgogoro wa ardhi Wilayani Bababati na zaidi Bonde la Kiru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro wa Wananchi wa Ayamango, Gedemar, Gidejabong na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Wananchi hao walipewa ardhi hiyo wakati wa Operesheni Vijiji. Wamekubali kutoka huko ilimradi wapewe ardhi mbadala na fidia stahiki, hadi leo tunaomba suluhu ya tatizo hili ipatikane mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo kubwa katika eneo la Nkaiti, Vilima Vitatu, kati ya mwekezaji wa utalii na wafugaji. Walishapelekwa Mahakamani na hadi leo masuala yanaendeshwa kisiasa. Hapo hapo Juhibu (WMA) wameingia mkataba na wawekezaji wa uwindaji katika kitalu pamoja na utalii wa picha. Wananchi wananyanyasika, sababu mifugo iliyokuwa inachungwiwa huko sasa hairuhusiwi, pia kuni na majani ya kujengea wananyimwa. Tunaomba Serikali itoe maamuzi ya kutatua migogoro hii mapema ili Wananchi wafanye kazi ya maendeleo kwa uhakika, wasiishi kwa wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali irekebishe Sheria ya Manunuzi mapema, tena hata haya marekebisho yaliyoletwa hayakidhi haja. Tunaomba kujua ni lini Serikali itamaliza tatizo hili la msururu wa kodi katika Sekta ya Kilimo? Mbali na juhudi za Bunge hili kuondoa baadhi ya kodi hizo, Serikali imekataa kutekeleza na inaendelea kukusanya kodi hiyo kinyume na utaratibu; kwa mfano, VAT kwenye matairi, matrekta, tela za matrekta na vipuri vya trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha pia sheria ya kuondoa kodi za malighafi za madawa za wenye ulemavu wa ngozi, bado kodi hizo zinakusanywa na serikali. Je, ni lini itaondoa na kutekeleza sheria tuliyopitisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Benki ya Kilimo itaanza? Leo ni mwaka wa tatu wakulima, wavuvi na wafugaji, wanasubiri. Kama bado, fedha hizo zingepolekwa kwenye Mfuko wa Pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza fedha za umeme vijijini (REA) kwa Mkoa wa Manyara aitatolewa lini kwani hadi leo hatujaona kinachoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kujua ni lini ahadi ya kujenga Daraja la Mto Magara itatekelezwa? Huko nyuma tulishaambiwa kuna fedha zilizotengwa, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Waziri wa Utumishi aliahidi kuharakisha suala la *re-categorization* ya watimishi wote wapate stahiki zao halali. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini wastaafu ambao hawajalipwa mafao yao watalipwa? Mwisho, tunashauri Ofisi ya Waziri Mkuu iangalie jinsi ya kuepuka majanga, kwa mfano, mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya mafuriko inakuwa kubwa na tukijenga mabwawa kwenye vyanzo vya mafuriko, tutaweza kuondokana nayo. Vilevile tutakuwa na bwawa la maji kwa ajili ya uvuvi, umwagiliaji na maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo. Pia zile gharama za kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko hazitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA), nusu yake zingetumika kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo yanayopelekewa chakula kila mwaka; itasaidia kuongeza chakula katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo mchango wake kwenye Pato la Taifa ni kiasi kidogo mno, kama mwajiri wa Watanzania wengi, inatakiwa kuboresha kilimo ili kiwe na mchango unaolingana na watu wengi wanaobebwa na kilimo, lakini itapandisha uchumi wa nchi kwa uendelevu zaidi (*consistence contribution*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo *favorable* kwa kilimo kama Rukwa, yanatakiwa yashughulikiwe kwa kuwezesha fursa hiyo itumike kuleta mabadiliko ya haraka kama vile kupeleka pembejeo kwa wakati na kwa wingi, matrekta makubwa na mengi ili kuleta mapinduzi katika maeneo yanayoruhusu kilimo. Viongozi wachapakazi ndiyo wapelekwe huko kwenye mwelekeo wa kuendeleza kilimo, *resource* fedha, watu na nyinginezo wapelekewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina uhaba wa Watumishi wa Sekta ya Afya, tunaomba Watumishi hao waongezwe. Madaktari, Wauguzi na Wataalam wa Maabara, waletwe Nkasi, Zahanati na Vituo vya Afya vinaendeshwa na Wauguzi na wakati mwingine *Medical Attendants*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya ujenzi wa barabara ni ndogo na ya polepole, isiyoeleweka, sijui sababu ni nini? Huku ni kutowatendea haki Wananchi ambao waliahidiwa na Rais wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara za Halmashauri ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi kuziwezesha mwaka mzima za Kilosi - Wampembe km 68, Nkana – Kala km 67 na Namanyere – Ninde km 40, hazijapata fedha ya kutosha kuzijenga. Huku ni kumdhallilisha Mheshimiwa Rais kwa vile aliahidi Wananchi. Barabara hizi ni kero na zinatakiwa kusaidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, REA wamesahau kupeleka au kuweka kwenye orodha vijiji vilivyoko Kata ya Kale vya Nkata, Ntemba na Nchenje na Vijiji vya Sintali, Nkana, Mkomanchindo na Kasapa.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inafanya kazi nzuri sana katika Sekta ya Barabara. Ukweli nchi yetu sasa inafikika kila sehemu, barabara za mikoa ni nzuri sana. Tunaipongeza Serikali hasa Waziri wetu wa Ujenzi pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, bila kuwasahau Watendaji wa Wizara hiyo, wakiwemo Wafanyakazi wa TANROAD wa Mkoa wa Iringa; ukweli kazi inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara ya Ujenzi kwa kufanya upembuzi yakinifu kwa Barabara ya Nyololo Igowole – Kibao – Mtwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini wanaipongeza sana Serikali kwa kukubali na kutekeleza mpango wa kuanza maandalizi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hiyo ni muhimu sana kiuchumi kwa Taifa zima, kwa sababu viwanda vikubwa vya chai, karatasi, mbao, pareto na wakulima wakubwa wapo Mgololo, ambapo Serikali imetoa msaada mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mgololo. Barabara hiyo ni ya muhimu sana katika kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua nyingi sana zinanyesha katika Jimbo la Mufindi Kusini, magari yanayosafirisha bidhaa ndani na nje ya nchi yanashindwa kupita kwa sababu barabara imeharibika sana. Naiomba Serikali iendelee na matengenezo ya kawaida ili kuwezesha usafiri wa barabara hiyo. Barabara ya Mafinga – Mgololo nayo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana TANROAD na nitaendelea kushukuru kama hatua za haraka zitachukuliwa kwa kutengeneza Barabara ya Nyolo – Mgololo, Mgololo – Nyigo – Makambako na Mafinga – Mgololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie kwa karibu bajeti zinazopitishwa na Bunge. Pesa iende Halmashauri kwa wakati na Miradi iliyoidhinishiwa fedha itekelezwe kwa muda na kwa kuzingatia viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imalize tatizo la mipaka kati ya Mkoa wa Manyara, Dodoma na Tanga na hatimaye migogoro kati ya Wilaya ya Kiteto na Kondoa, Chamba, Chamwino, Kongwa, Gairo na Kilindi iishe. Uhakiki na kuweka mawe ushirikishe pande zote husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ishughulikiwe kikamilifu kwa kuwa na *Programme ya Land Use Planning*, yenye fedha na kuwatengea Wizara ya Ardhi fedha ya kutosha kwa kazi hizo. *Programme* hiyo itenge na kusimamia matumizi husika ya makazi, huduma, kilimo, mifugo na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie utekelezaji wa hukumu ya Mahakama ya Rufaa ya Kesi Na 58/2010 inayohusu Embolieye Mwitangos Wilayani Kiteto. Serikali izingatie hukumu hii bila kupindisha kufuata matakwa ya *influence* ya wakulima wakubwa wanaofanya uhalifu kwa kulima ndani ya Hifadhi ya Jamii kinyume na hukumu ya Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa hukumu husika, watu wadogo na vibarua wamekamatwa, wamehukumwa na kufungwa. wakulima wakubwa na wanaondelea kufanya halifu, wameachwa huru bila kuchukuliwa hatua za kisheria! Hukumu isimamiwe bila ya upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kambi za makazi haramu yaliyoanzishwa na watu walioondolewa Mwitangos yavunjwe ili amani irudi katika maeneo hayo. Makazi haya haramu ni pamoja na Peri kwa Peri Namba moja (1) na mbili (2), Kisima Namba moja (1) na mbili (2) Kalikala.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI) ELIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenye dhamana ya Wizara yetu, naomba sasa nitumie muda huu, kutoa mchango wangu wa kutoa fafanuzi mbalimbali zilizojitokeza wakati wa bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza na Mheshimiwa Silinde, ambaye pia alitaka kujua mgongano wa mamlaka za uendeshaji elimu nchini kati ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu. Jambo hili nalirudia tena, kwa sababu katika session hii hii wakati wa Bunge la mwaka jana, niliwahi kutoa fafanuzi kwamba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

hakuna migongano mikubwa zaidi ya kwamba Wizara ya Elimu na TAMISEMI tunafanya kazi kwa ushirikiano na kila taasisi au kila Wizara ina majukumu yake bayana. Kwa kurudia, kwa manufaa ya wale wote ambao walikuwa hawakupata kusikia na wale ambao hawajafahamu, majukumu ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI kuhusu elimu ni kama ifuatavyo:-

Wizara ya Elimu kwa sasa kazi yake kubwa ni kuandaa sera ya elimu, kutoa miongozo ya elimu, tathmini na uhakika wa ubora wa elimu, kushughulikia elimu ya juu na Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya Ufundi Stadi kwa maana ya VETA, Idara ya Ukaguzi ambayo imezungumzwa na walio wengi na taasisi ambata kama vile Baraza la Mitihani la Taifa, NACTE, Bodi ya Mikopo, Taasisi ya Elimu, haya ndiyo maeneo ambayo Wizara ya Elimu inashughulikia pamoja na maeneo mengine wakati TAMISEMI tunashughulikia usimamizi na uendeshaji wa shughuli za kila za elimu kwa Kurugenzi ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunashughulikia ajira za Walimu na kuwapanga vituo vyao vya kazi, stahili mbalimbali za Walimu na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, lakini pia kushughulikia miundombinu, elimu maalum na yale yote yanayogusa Kurugenzi ya Msingi na Kurugenzi ya Sekondari. Jumla yote haya tunafanya kazi kwa pamoja kati ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba elimu yetu nchini inakuwa bora na ile ambayo imekusudiwa kutolewa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Silinde pia alitaka kujua mabadiliko ya mara kwa mara ya mitaala. Kama ambavyo nimeeleza majukumu tofauti ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI, jambo hili liko Wizara ya Elimu na Mheshimiwa Mhagama, atakapokuja kwenye bajeti yake atakuja kujikita kutoa ufafanuzi zaidi juu ya uendeshaji wa mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, alitaka kujua pia tatizo la Walimu katika Halmashauri ya Misenyi na kuwa ipo haja ya kulipa posho na mazingira magumu kwa Walimu wetu nchini. Ni kweli kwamba Serikali imeajiri Walimu na ni wajibu wa TAMISEMI kushughulikia maslahi yao pamoja na eneo ambalo Mheshimiwa wa Nkenge amelieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe taarifa kwamba mwaka huu tumeweza kuajiri Walimu wengi zaidi 36,380. Kati ya hayo Walimu hamsini walipelekwa Wizara ya Elimu kwa ajili ya shule za msingi na za mazoezi na za Sekondari. Pia Walimu 36,339 walipelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambazo ni Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya Kurugenzi ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawa tunashukuru sana mwaka huu wamesharipoti kwenye Halmashauri zetu. Nataka nitumie nafasi hii pia kueleza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

lile ambalo ameeleza Mheshimiwa Mbilinyi na Mheshimiwa Mwanjelwa juu ya tatizo ambalo linawagusa sana Walimu wapya na hili naamini Walimu wote nchini watakuwa wananisikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawa wamesharipoti kama nilivyoeleza mpaka tarehe 30 mwezi uliopita Walimu zaidi ya asilimia 92 walikuwa wamesharipoti kwenye vituo vya kazi. Maelekezo yetu kwenye Halmashauri zote nchini ni kwamba Walimu wanaporipoti watapata posho zao za siku saba, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge posho hizi walishalipwa za siku saba na tuliwalipa katika awamu mbili, lakini zote zimekwenda na tulitenga milioni 11.4 kwa ajili ya malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililoko sasa la kulipwa kwa mishahara, ya Walimu hawa wa ajira mpya linatokana na sababu mbalimbali. Moja ni kwamba, katika kuufanya mfumo huu uweze kulipa mishahara, Mwalimu mwenye ajira mpya ni lazima awasilishe vyeti halisi alivyokamilisha masomo yake. Baada ya kuwasilisha vyeti hivyo, ndio sasa vinaingia kwenye mitandao ili Utumishi waweze kuona pamoja na Hazina, lakini pia lazima waripoti kabla ya tarehe kumi ya mwezi ili waweze kuingia kwenye mfumo, baada ya hapo ni ngumu kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni kweli kwamba Walimu wetu kadhaa hawajalipwa mishahara ya mwezi wa Nne. Hii ni kwa sababu wengi waliripoti baada ya tarehe 10, lakini pia hata wale walioripoti kabla ya tarehe 10 kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwamba mishahara imeshatumwa, tatizo lililopo ni mfumo wa taasisi na Halmashauri zetu ili kuweza kuwalipa mishahara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumeshughulikia tatizo la Kibondo, tumeshughulikia tatizo la Igunga, lakini sasa hivi tulikuwa tunafanya mawasiliano na Mbeya. Tatizo la Igunga ni lile ambalo nimeeleza kwamba, ni kweli wapo Walimu hawajalipwa mishahara na ni wale ambao walikuwa wameripoti baada ya tarehe 10, lakini tumewasiliana na Halmashauri zote nchini, wahakikishe kwamba Walimu hawa ambao ni wageni kwenye Halmashauri zetu, Wakurugenzi watafute fedha ili waweze kuwapa fedha ambayo itawasaidia kujikimu huku wakisubiri kulipwa mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hilo linaendelea katika kila Halmashauri, najua kwamba kuna Halmashauri kadhaa hazijatekeleza hivyo, lakini tuna matumaini kwamba, Wakurugenzi watajitahidi na Halmashauri zao kutafuta fedha mahali pengine ili kuwawezesha hao Walimu wetu wageni waweze kuishi huku wakisubiri mishahara, lakini mishahara wa Mwezi wa Pili lazima wataupata kwa taratibu za utumishi. Kule Mbeya, tatizo la mishahara si Walimu peke yao,

taarifa ambazo tumepata sasa hivi kutoka kwa Mkurugenzi ni kwamba tatizo la mshahara Mkoa wa Mbeya...

MBUNGE FULANI: Kwa RAS.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI) ELIMU: Kutoka kwa RAS Mkoa wa Mbeya, ni kwamba Sekretarieti yake ya mkoa pamoja na Halmashauri ya Manispaa ni kweli hawajapata mishahara na hii ni kwa sababu ya wale watendaji ambao wako kwenye mitandao wote walikuwa kwenye bajeti Dar es Salaam lakini wamesharudi, jambo hilo linaendelea na mishahara itaweza kutoka kwa wale watumishi wote si walimu peke yao, kwa maeneo yote hayo mawili, Sekretarieti ya Mkoa pamoja na Manispaa ya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hii kwa ajira hii ambayo tumeajiri mwaka huu Wilaya ya Nkenge imeweza kufaidika kwa kupata Walimu 151 ambao tayari wamesharipoti. Pia alizungumzia suala la mazingira magumu ambayo Walimu hawa yanawakuta, lakini tunachosema ni kwamba, ni kweli kwamba, Serikali ilishaweka utaratibu wa kuwezesha Walimu ambao wako katika mazingira magumu, lakini uwezeshaji huu siyo mwalimu mmoja mmoja, tulichofanya ni kuboresha mazingira wanamofanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha wanayofanyia kazi, sisi tumeweka utaratibu mipango kadhaa ambayo itasaidia kuboresha mazingira haya, ili Mwalimu anapokwenda kufanya kazi, aone kabisa mazingira aliyoyakuta yanafaa kufanya kazi ya ualimu ikiwemo na ule mpango ambao tulishauanza wa ujenzi wa ukamilishaji wa shule 1,200 ambao niliueleza pia hata juzi wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kafulila, kwamba tumeanza na shule 264 kukamilisha miundombinu yote ikiwemo na nyumba ya walimu.

Kwa hiyo, *concentration* yetu ni ujenzi wa nyumba za Walimu ambao kazi hiyo imeendelea na sasa inakamilika. Awamu ya pili tutakuwa na shule 228 ambazo pia zitakua katika ukamilishaji huo huo kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na awamu ya tatu tutakuwa na shule 408, huo ni mkakati ambao tunao wa kuboresha shule 1,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa pili, ni kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu imetenga bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu, tunapeleka kwenye Wilaya zilizo katika mazingira magumu na tumeanza na Halmashauri 40 na kila Halmashauri imenufaika kwa kupelekewa milioni 500. Kwa hiyo, ni juu ya Halmashauri kujenga nyumba za Walimu kwa Kurugenzi ya Msingi na Sekondari na hasa maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mkienda kwenye Halmashauri zenu jambo hili mtalikuta na tunaamini tutaendelea kushirikiana ili kuhakikisha

kwamba Walimu wetu wanapata nyumba. Tunajua si rahisi kujenga nyumba za Walimu wote tulionao, lakini jitahada za hara zinafanyika na mikakati inafanywa ili kupata nyumba za kuwezesha Walimu waweze kuishi na hii ni kwa lengo la kuboresha mazingira haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ina mkakati wa kuunda Bodi ya Mishahara na Motisha iliyoko chini ya Ofisi ya Rais. Hili litaelezwa vizuri zaidi na Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, atakapoanza kuwasilisha bajeti yake jambo ambalo linawanufaisha watumishi wote kwa kuboresha mazingira yao.

Mheshimiwa Leticia Nyerere pia alitaka kujua Serikali imepeleka vitabu katika Wilaya ya Kwimba baada ya kupeleka Walimu 300. Jambo hili limezunguzwa pia na Mheshimiwa Christowaja Mtinda ambaye pia alitaka kujua tumepeleka vitabu kiasi gani kwenye maeneo haya.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Serikali tumenunua vitabu vya kutosha na tumesambaza kwenye shule zetu tumepunguza wastani wa kitabu kimoja na idadi ya watoto wanaosoma sasa kitabu kimoja wanasoma watoto watatu na jitihada zinaendelea kuhakikisha kwamba tunapeleka vitabu vya kutosha kwenye maeneo haya. Pia, hata Kwimba wamenufaika kwa kupata vitabu vingi vya kutosha na tunahakikisha kwamba Wilaya zote nchini zinapata vitabu hivyo kwa vile vichache vilivyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *capitation* lilijitokeza, tunapeleka *capitation* kwenye Halmashauri zetu. Mwaka wa fedha uliopita tumepeleka shilingi bilioni kumi na nne kwenye Halmashauri zetu ili zipeleke kwenye shule zetu za msingi na sekondari kwa ajili ya kuwasaidia Walimu kuendesha shule zao vizuri.

Pia eneo hili lilikuwa limezungumzia suala la BAE la vitabu hivi vilivyokwenda ni vya BAE lakini BAE ile pia inanunua na madawati na tayari usambazaji umeshaanza na kila Halmashauri itanufaika kupata madawati na vitabu kupitia BAE. Orodha iliombwa na Mheshimiwa Christowaja tunahakikisha kwamba, tutawapa orodha kwa sababu tunayo, tutawaletea mbele yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vullu alitaka kujua mkakati tulionao wa kusaidia kupunguza mdondoko wa wasichana mashuleni. Jambo hili linashughulikiwa kwa kujenga mabweni kwa shule zinazotakiwa kujengwa hosteli ili kupunguza mdondoko. Pia, tunawasihi wananchi kushirikiana na utekelezaji wa sheria ya kuwalinda watoto wetu wa kike ili kuwezesha wasichana hawa kumaliza shule zao. Jambo hili pia liliulizwa na Mheshimiwa Mkapa wa kule Masasi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome kutoka Iramba, alizungumzia tatizo la usafiri wa Idara ya Ukaguzi. Idara ya Ukaguzi iko Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Jenista Mhagama atakuja kueleza vizuri atakapokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba wote waliomba ufafanuzi wa namna ambavyo Serikali inasaidia kuondoa kero za Walimu hasa kwa kulipa madeni na maslahi mbalimbali. Nikiri kwamba, madeni yapo, Walimu wanatudai, lakini utaratibu tulioweka ni kufanya uhakiki kati ya bilioni 61 ambazo zimejitokeza, uhakiki unaendelea, wakati uhakiki unaendelea yale yaliyokubaliwa tunaendelea kulipa. Mpaka mwezi Februari, mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni 19 tumeshalipa za madeni haya na uhakiki unaendelea na tutaendelea kulipa. Kwa hiyo, Walimu waendeleo kuwa na matumaini kwamba kazi hii inafanywa na tutaendelea kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa kasoro kadhaa zimejitokeza lakini kasoro hizo pia tunataka kuzichukulia hatua. Kuna watu majina yanajirudia na kuna wengine wanaandika taarifa za juu sana tunataka tujue anayeandika taarifa hizi ni Mwalimu mwenyewe au Wakuu wa Idara pale kwenye Halmashauri na yeyote ambaye atakamatwa kwenye zoezi hili tutamchukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Msolla alitaka tutumie Juma la Elimu ambalo linaendelea sasa ili kuboresha elimu na kujitathimini kiasi kikubwa. Nataka nimhakikishie kwamba, Juma la Elimu ambalo linaendelea sasa ni njia mojawapo ya kujitathimini na kuona namna bora ya kuweza kukuza elimu nchini. Nataka nitumie nafasi kwa sababu Juma hili linaendelea na kilele ni tarehe kumi, naomba nitoe mwaliko kwa Waheshimiwa Wabunge wote tarehe kumi Jumamosi tuwe Uwanja wa Jamhuri na ndiyo siku ya kuhitimisha Juma la Elimu na mgeni rasmi siku ile ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, tumewaandalia viti vyenu karibu kwenye mabanda yale kuona shughuli zinazoendelea na pia kuhudhuria sherehe nzima ili mshuhudie tunapotoa zawadi na tuzo mbalimbali kwa waliofanya vizuri kwa Walimu, wanafunzi na hata pia shule ambazo zimefanya vizuri, kwa hiyo naomba niwakaribishe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faith Mitambo alizungumzia ukosefu wa vifaa vya maabara. Nataka nimhakikishie kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu imejipanga vizuri kuhakikisha tunapeleka vifaa vya maabara pale ambapo maabara zipo. Kwanza, tulishatuma shilingi milioni 36 kwa kila Halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara na hasa tulitumia *mobile laboratory*. Kama haitoshi kwenye ule mpango wa ujenzi wa shule 1200,

shule hizi tunajenga na maabara pia. Pamoja na maabara hizo, sasa mkakati ni kupeleka vifaa kwenye eneo lile. Vifaa tunavipata zaidi kupitia *capitation* ya sekondari kwenye asilimia 50 kuna eneo la kununua vifaa na vifaa hivyo ikiwemo na vile vya maabara. Kwa hiyo, suala la vifaa vya maabara vipo na vitaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Suzan Lyimo tena alisema mgawo wa Walimu siyo mzuri. Nataka nimhakikishe kwamba, mgawo huu ulitokana na mahitaji ya Halmashauri zenyewe na tuliwapelekea kulingana na mahitaji yao. Nataka kuhakikisha kwamba sasa tumepunguza upungufu mkubwa wa Walimu kwenye shule zetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, muda wako umekwisha!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Muda wangu umekwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana lakini majibu mengine yoyote tutayatoa kwa maandishi na tutawapelekea Mheshimiwa Wabunge ili muweze kuona namna ambavyo Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza jukumu lake kwenye sekta ya Elimu.

Ahsante sana kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aggrey Mwanri, dakika kumi na tano!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kabla sijaingia *speed*, niunge mkono hoja hii hata kama wakati nitakapomalizia nitaunga tena mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nizungumze la Wabunge wengi ambao wanatoka katika Mkoa wa Dar es Salaam ambao wamezungumzia kuhusu ujenzi wa Machinga *Complex* ambao umeshindwa kutatua tatizo la Wamachinga katika Jiji la Dar es Salaam. Jengo la Machinga lina vyumba 4,289 na lilijengwa kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara ndogo ndogo kufanya shughuli zao za kiuchumi. Pamoja na kugawanya vyumba, wapo ambao wameviacha wazi na wengi wanapendelea zaidi eneo la chini nje ya barabarani ambako wanaweka bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wafanyabiashara waliopo ni 1,200,000 na jengo lina uwezo wa kuchukua wafanyabiashara wapatao 4,289 na waliokubali kuingia katika vyumba hivyo ni 2,400. Hivyo, vyumba 1889 viko wazi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika sasa hivi kwa sababu kuna *point* ambayo inazungumzwa hapa ni kwamba, Halmashauri zote zilizoko katika Jiji la Dar es Salaam kwa maana *Municipalities* zote, zimefanya mambo yafuatayo:-

Wametenga maeneo kwa kila Halmashauri na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imetenga eneo la Kigogo *Fresh* ambalo linaweza likachukua wafanyabiashara 500, Kinyerezi masoko matatu wafanyabiashara 700, Kitunda wafanyabiashara 200, Tabata Masoko mawili ambayo yanaweza yakachukua wafanyabiashara 450. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni **Simu** 2000, wafanyabiashara 500, Mwenge wafanyabiashara 600, Mburahati wafanyabiashara 400. Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, TAZARA wafanyabiashara 1,000, Mbagala Zakhem wafanyabiashara 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itashirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kubuni mbinu za kutumia nafasi 1,889 zisizotumika kwenye Jengo la Machinga na pia kufanya kila Kata kuwa na eneo la wafanyabiashara wachache sambamba na kuwaelimisha wananchi ambao ndiyo wateja na wafanyabiashara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumza tatizo la udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma. Kushuka kwa hati na kulinganisha na mwaka 2008/2009. Hali hii inaonesha udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma. Bahati nzuri humu ndani tumeelezwa sisi wote na tumesikia tukielezwa hapa, kwamba suala la kusimamia fedha za Halmashauri kwamba tunangoja Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ndiyo isimamie kila kitu bila kuona kwamba sisi tunaingalia hii dhana ya *D by D*, then kazi yote hii itakuwa ni kazi bure.

Wabunge wetu ninyi ni Wajumbe katika Halmashauri zetu, tunachowaomba sisi ni kwamba tutumie nafasi zetu, katika Halmashauri zote ukiacha mtu anayeitwa Mkurugenzi Mtendaji, watumishi wale wengine wote na Wakuu wa Idara, wale wengine wote, Halmashauri hizi zinaweza zikawachukulia hatua na hatua zile zikawa zimefanyika na hivyo kuleta uadilifu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba, sisi kama *custodian* wa Halmashauri ni kweli kabisa litazungumzwa jambo hili na ndiyo maana mnatuona tukimaliza shughuli hapa wote tunatawanyika, Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi na Manaibu Mawaziri tunakwenda huko Mikoani kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Tunachozungumza hapa, tunahitaji kitu kinaitwa *consented effort* katika suala hili. Kama mtu anakwenda pale anakula hela za Halmashauri, anachukua vihela, anabeba tu anakula tu hela za Halmashauri, mtu huyu hafai.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi Mtendaji anakaa pale anashindwa kusimamia hela za Halmashauri, zinaliwa tu, zinatafunwa tu, Mkuu wa Idara anatafuna hela za Halmashauri, tunakaa hapa tunam-discuss hapa tunazungumza habari ya mtu anakula hela za Halmashauri. Mtu huyu ukifika pale ni Polisi unampeleka, habari imekwisha. Hatuwezi watu wazima tunakaa hapa mtu anakula hela za Halmashauri, tunasema mpaka tumsubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa aje achukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai, sauti hii ni msisitizo tu wa ninachosema. Hatuwezi mtu anakula hela za Halmashauri mahali pake ni Polisi, unamsukuma unampeleka pale. Tena siku hizi bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuambia hivi, mmalizane naye kwanza huko halafu ndiyo mniarifu. Hii ya kuja kumshtaki tena huko hakuna haja ya kufanya hivyo.

Kwa hiyo, tunawaomba sana sana Waheshimiwa Wabunge tusaidiane katika jambo hili kwa sababu uko mchwa unaingia katika Halmashauri. Fedha zinazoombwa hapa ni trilioni 4.9 ndizo zinazoombwa hapa. Tukifanya mchezo mchezo namna hii zitapita hivi, watoto wanakaa chini hawana madawati, nyumba zinavunjika, ufa, barabara hazitengenezwi, hela zimeondoka zimekwenda. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie Waheshimiwa na kama taarifa zozote tunaomba mtulettee hizo taarifa sisi tutachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumeulizwa swali hapa, kwa kipindi hiki kinachozungumzwa hapa, tumehangaika na Wakurugenzi sita wameondoka. Acha zile taarifa ambazo Waziri wa Nchi alikuwa amezitoa, akieleza hatua ambazo amechukua kwa wale Wakurugenzi Watendaji na Wakuu wa Idara ambao wemeonekana wamefanya mambo ya ajabu ajabu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo rai yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi hizi ni kweli kwamba inaonekana tumeshuka, lakini bado kutokana na juhudi hizi viwango vya utendaji katika Halmashauri vimeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka kama inavyohibitishwa na matokeo ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, miaka minne mfufulizo kuanzia mwaka 2009 mpaka 2010, ambapo Halmashauri ambazo zimepata hati safi zimekuwa zikiongezeka kutoka Halmashauri 66, sawa na asilimia 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2009/2010 Halmashauri 72 sawa na asilimia 54, mwaka 2010/2011 Halmashauri 104 sawa ma asilimia 78, mwaka wa 2011/2012 mpaka Halmashauri 112 sawa na asilimia 80 ya Halmashauri zote kwa mwaka 2012/2013. Kwa hiyo, imekuwa inapanda kwa sababu ya ushirikiano huo ambao tumekuwa tunapata kutoka kwenu lakini bado tunaona kwamba kuna haja ya kufanya jitahada zaidi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Henry Daffa Shakifu Mbunge wa Lushoto, alizungumza kwamba, fedha zinazotengwa kwa kwa ajili ya Mikoa na Halmashauri zipelekwe kama zilivyoidhinishwa ili kuwezesha utendaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Nataka niseme kabisa hapa, hata hela hizi za *Road Fund* wala hatupendi utaratibu wa kusema kwamba zipitie pale kwetu. Hakuna hela yoyote inayotoka *Treasury* ikitoka pale itakuja itakaa pale TAMISEMI. *In fact* mpaka sasa hivi ni kwa sababu Wizara ya Fedha yenyewe imetaka hizi hela zipite pale kwa ajili ya *accountability* na nini ili kuweza kuzisimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sisi hela zikiingia TAMISEMI *immediately* zinaondoka zinakwenda Halmashauri. Bahati nzuri zinakuwa zimeingizwa katika mafungu. Kwa hiyo, hii rai inayotolewa hapa wala si rai ambayo ni nzuri na hayo ndiyo mawazo tuliyonayo. Huwezi ukakaa na hela, hela zinazobaki pale TAMISEMI ni hela za *monitoring and evaluation* ndizo zinazobaki pale na zile nyingine ambazo zina miradi ambayo ina *nature* ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Majaliwa amezungumza hapa ameeleza habari ya vitabu na nini, tumelewa kwamba matatizo yalikuwa yanapatikana mpaka tukafika mahali tukaona vitabu haviendi, vitabu havinunuliwi. *Therefore*, ikatengenezwa *mechanism* ya kuhakikisha kwamba tunatengeneza utaratibu kutoka Wizarani ili kuweza kuimarisha *accountability*, lakini *otherwise* Wabunge wanachozungumza hapa ni jambo la msingi kabisa kwamba hizi ziende zote kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ya dhana yenyewe ya *Decentralization by Devolution*. Maana yake peleka madaraka kwa wananchi lakini wakati huo huo peleka na rasilimali watu, peleka na vifaa, peleka na fedha kule ambako kuna *functions*, ndicho kinachozungumzwa hapa. Kwa hiyo, hakuna haja ya kusema kwamba hela zibaki TAMISEMI *Headquarters* na wala Mheshimiwa Waziri Mkuu hana mpango huo kwamba hela zibaki *Headquarters*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengine wamezungumzia viongozi yaani baadhi ya Wakuu wa Wilaya wapunguze ubabe, kwa mfano, Mkuu wa Wilaya ya Korogwe ambaye alimweka ndani Diwani, hatua dhidi yake zichukuliwe na Serikali. Sisi hapa hatuna haja ya kumtetea mtu yoyote. Ukizungumza habari ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa ni msimamizi wa shughuli zote za Serikali katika Mkoa ule. Wanasema *he is incharge of all Government affairs* kama vile ambavyo iko kwa DC.

Kwa hiyo, kwa maneno mengine ni *representative of the President of the United Republic of Tanzania*, ndiyo nafasi yake anapoingia pale. Huyu umempa

majukumu mengi, kule ndani kuna purukushani nyingi ambazo zinaingia kule na kiwango cha nguvu kinachotumika kule kinategemeana na aina ya purukushani atakayokutana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, wala hatutaki kum-*defend* mtu yoyote hapa. Mtu ameshindikana huko utamwambia DC mkamate. Mtu ameingia mwendawazimu utamwambia DC nenda kamkamate. Kwa taarifa, *I was once upon the time a District Commissioner*, nimewahi kuwa Mkuu wa Wilaya, naelewa wanachozungumza hapa. Sisi *we take note* ya lile ambalo limezungumzwa kuhusu DC wa Korogwe na sisi tunaahidi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hili jambo ambalo limezungumzwa la Diwani hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunataka tuseme, wakati huo tunaposema haya yote, tuangalie pia kwamba huyu kiongozi tunaoyezungumza wa hii kada tunayozungumza, tumepa jukumu gani? Unafika mahali watu wame-*riot* pale, Kijiji chote kime-*riot* pale, nguvu itatumika lakini itatumika kulingana na kiasi cha *resistance* inayotoka pale. Ndicho tunachosema pale.

Kwa hiyo, tunachojibu hapa tutafuatilia jambo hili ambalo limesemwa na Mheshimiwa Mbunge kuhusu DC wa Korogwe ili kujua undani wake, kujua hilo jambo linalomhusu Diwani *and then* kama kutakuwa kuna tatizo lolote, mamlaka husika itachukua hatua kwa maana ya mamlaka ya uteuzi, lakini kwa sasa hivi hicho ndicho tunaweza tukajibu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakwenda haraka haraka, naomba nimalizie, mambo kama alivyosema Mheshimiwa Majaliwa na kama atakavyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwa kweli tunasema kwamba tutajibu kwa njia ya maandishi, madeni ya watumishi tunasema kwamba tutajibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya watumishi yalipwe na kurejesha ari ya utendaji kazi kwao na wapewe motisha. Yametoka maelekezo na Mheshimiwa Rais mwenyewe alishawahi kutoa maelekezo. Kama una Walimu wa kuwahamisha hapa, unataka kuwapeleka katika Wilaya nyingine, kama huna hela za kuwahamisha, maelekezo ya Serikali usiwahamishe. Unahamisha halafu unapeleka deni linakuwa kubwa, Walimu wanajisikia vibaya, Madaktari wanajisikia vibaya na Serikali yao, Watumishi wanajisikia vibaya. Hamisha watumishi wakati unapojua kwamba una fedha ya kuhamisha, ndiyo maelekezo ya Serikali. Kwa hiyo, tumesema kwamba habari ya ku-*accumulate* na kuweka madeni mengi, hili tuachane nalo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza anazungumzia mgao wa Mfuko wa Barabara, jambo hili limezungumzwa kwa muda mrefu. Tutaweka utaratibu, tumekaa katika vikao, huu Mfuko wa Barabara umeundwa kisheria. Anayehusika hapa ni Mheshimiwa Magufuli na ukizungumza naye atakwambia kwamba liko kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumekaa na wenzetu wa Ujenzi, tumezungumza na kweli imeonekana kwamba barabara zinazohusu *Local Government* sasa hivi mtandao wake umepanuka umeongezeka sana. Kwa hiyo, tume-*commission* watu ambao watasaidia kuangalia vizuri kufanya *feasibility study* na ku-*study* vizuri, waishauri Serikali ili tuweze kuona kwamba tunachukua hatua gani katika mgawo kwamba, uende kiasi gani. Kwa hiyo, haya ndiyo majibu ambayo tunaweza tukayatoa hapa kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahandisi katika Halmashauri wajengewe uwezo ili waweze kutimiza majukumu yao kwa ukamilifu. Wamezungumza pia na matatizo yao. Mheshimiwa Waziri wa Nchi huwa anakwenda Morogoro mara kwa mara tumekuwa na semina pale, tumewaita Wahandisi wote nchi nzima, tumezungumza nao. Tumezungumza hata haya masuala ya maadili ambayo yamezungumzwa hapa na kuwawezesha, lakini jambo wanalozungumza Wabunge hapa ni la msingi na tunakubaliana nalo na tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Watendaji wana vitabu viwili vya kukusanyia mapato na hivyo kuzikosesha Halmashauri mapato. Tunafanya uchunguzi kuhusu jambo hili, ni kweli kabisa inawezekana binadamu akafika mahali akatengeneza vibutu pale hela zikaingia katika Mifuko ya watu. Hili ni jambo ambalo tutaendelea kulifuatilia na tutatoa ripoti kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni Wakurugenzi wangapi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nimesema sita tumechukulia hatua hivi karibuni, Serikali imechukua hatua dhidi ya Maafisa Watendaji ambao wanashiriki kupokea rushwa na hasa katika maeneo ya Karagwe nako tutachukua hatua. Zaidi ya hapo Serikali ilipatia Halmashauri za Wilaya ya Misenyi, maji ya bomba tumeeleza hapo ukiangalia katika Majedwali yetu tutaonesha ni kiasi gani ambacho kimetengwa.

Mheshimiwa Rage amezungumzia kuhusu barabara za lami katika Manispaa ya Tabora. Hawa wamepata mradi mkubwa sana pale ambao utatengeneza kilomita kumi na mbili na gharama zake zitakuwa shilingi bilioni 9.6 kwa hiyo, tuna uhakika bilioni hizo zitafanyika katika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Kitete nayo imefanyiwa marekebisho makubwa na kuna msaada umetolewa pale. Kwa hiyo, tuna

uhakika kwamba hayo mambo yatakwenda vizuri kama ambavyo Mheshimiwa Rage amekuwa anashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ipatiwe fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Tumesema utaratibu ule wa *O and OD* ndiyo utumike katika kuleta mipango hii ili kuona jinsi ya kuweza kusaidiana nao katika kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hotuba na bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa namuita Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Hawa Ghasia!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ufafanuzi katika hoja ambazo zimeelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni suala la makusanyo katika Halmashauri na kwamba tumeelekezwa tufanye utafiti ili kuweza kubaini vyanzo vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni suala la makusanyo katika Halmashauri na kwamba tumeelekezwa tufanye utafiti ili kuweza kubaini vyanzo vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari ofisi yangu imeshafanya utafiti kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Halmashauri 30 na tayari tumepata, tathmini imeonesha vyanzo vipya ambavyo tunaweza tukavibuni na mikakati pia ya kufanya ili kuhakikisha kwamba, mapato yanaongezeka katika Halmashauri, viomeoneshwa ikiwa ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, ambayo na yenyewe pia itasaidia kuongeza wigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumezielekeza Halmashauri kuzipitia Sheria zake Ndogo ili na yenyewe pia ziweze kuona maeneo mapya ambayo yanaweza yakaongeza makusanyo, lakini katika kuhakikisha kwamba makusanyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yanaongezeka, tumeanza kuziweka Halmashauri zetu katika makundi, za Miji, Manispaa na Wilaya na kuziangalia zipi zinafanya vizuri na zipi zinafanya vibaya. Lengo ni kuhakikisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwamba zile zinazofanya vizuri tunazipa tuzo na zinazofanya vibaya, tunazichukulia hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeanzisha mifumo ya *ki-electronic* ya ukusanyaji wa mapato na kwa kuanzia tumeanza katika Jiji la Arusha na imeanza kuonesha matokeo mazuri. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunapeleka katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni suala zima la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ambapo kwa mtazamo wake anasema kwamba suala hili tumeanza kulitekeleza kinyemela na kwamba tunawatimia Mabalazi katika kuandikisha wapiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitamke rasmi kwamba, suala hili tuko katika maandalizi ya awali, na suala la uandikishaji wapiga kura, kwa mujibu wa Kanuni za Chaguzi za Serikali za Mitaa, huwa linafanyika siku 21 kabla ya uchaguzi. Kwa hiyo, kama kuna suala la uandikishaji linafanyika katika maeneo yao, ni suala la kawaida la ujazaji *registers* za vijiji au *registers* za mitaa. Kwa hiyo, hakuna suala la kinyemela na.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu wafahamu kwamba, kwa mujibu wa sheria zetu na kwa mujibu wa uchaguzi wetu, ni kwamba tunategemea mwaka huu mwezi wa 10, uchaguzi huo utafanyika na wakati ukifika, Waziri mwenye dhamana na Mamlaka na Serikali za Mitaa, atatangaza rasmi na Vyama vya Siasa navyo vitashirikishwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa aondoe hofu, ajiandae tu, na kama ana wasiwasi, basi afanye mikakati mapema, asije baaaye akasingizia kwamba tulianza mbio hizi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa upande wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni kuhusu suala la ugawaji wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo linahusu Manispaa ya Temeke na Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeulizwa ni Mabaraza yapi yalipendekeza, sasa napenda kumfahamisha kwamba, kwanza ofisi yangu haijapokea rasmi suala hilo, lakini taarifa ambazo tunazo, tayari Manispaa ya Temeke, wamekaa kwenye Halmashauri yao, wamekaa *DCC* na hata kwenye *RCC* walipeleka na kwenye *DCC* na kwenye Halmashauri wamekubaliana kuanzisha Wilaya ya Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala kwamba Ubungo wamekaa na kukataa suala la kuanzisha Halmashauri ya Kigamboni na ya kwao ya Ubungo kwa watu wa Kinondoni; nadhani si sahihi watu wa Kinondoni kuanza kujadili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

masuala ya Temeke. Kama Temeke wenyewe wameridhia kuongeza Wilaya nyingine, naomba msiwaingilie na kama nyinyi Ubungo hamjawa tayari, nimwombe Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kama Temeke wako tayari, atulettee. Sasa kama mlipiga kura huko Kinondoni, nadhani hizo kura si sahihi kuwapigia watu wa Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine, nimeona pamoja na kukataa, kuna ushauri mwingine wanaoutoa. Sasa niwaombe tu, kwamba, hapa si mahali pake, ingawa tumezoea kwamba Bunge Maalum la Katiba watu walikimbia, halafu Bunge la Bajeti ndiyo linafanywa Bunge la Katiba, lakini pia hapa si RCC ya kujadili mgawanyo wa maeneo mapya, si wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe mrudi kwenye Manispaa zenu, mkajadiliane huko, sisi tutapata taarifa hizo kupitia RCC zenu, ambapo tutaandikiwa rasmi TAMISEMI. Tunaomba msiharakishe, kama mkifika kwenye vikao vyenu hivyo mnachukua mpira mnaweka kwapani, mnakimbia. Msitumie vikao vingine vya shughuli nyingine kwa masuala ambayo mmeshindwa kuyatekeleza kwenye vikao rasmi ambayo mlipaswa kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa hapa na mchangiaji akiwa Mheshimiwa Msigwa, alizungumzia suala la fedha kwenye Manispaa yake kwamba kuna kipindi alikuwa anapokea shilingi bilioni 200, sasa hivi tumepunguza mpaka milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mfuko wenyewe wa barabara fedha zake zote mwaka jana bajeti ilikuwa ni bilioni 151. Sasa hizo ambazo wao walikuwawanapata bilioni 200, kidogo imenishangaza. Nina imani kabisa ni kwamba tu ulimi uliteleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine, amezungumza kwamba tunabagua, kwa sababu kule kuna upinzani. Nadhani hakusoma au hashiriki kwenye vikao vya Mabaraza kwenye Halmashauri yake. Kwa sababu kama angesoma nyaraka ambazo zipi au kama angekuwa anashiriki kwenye vikao vya Halmashauri yake, angejua kwamba Manispaa ya Iringa, kupitia mpango wa uendelezaji miji, imetengewa sh. 3,128,246,148.32 na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, haina ubaguzi na sisi tunavyopanga mipango yetu hatuangalii, huku kuna Mpinzani, huku kuna nani, kwa sababu ilani inayotekelezwa maeneo yote, bila kujali Jimbo limechukuliwa na Mpinzani au limechukuliwa na Chama cha Mapinduzi, ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo, yale tuliyoyaahidi, kuwatekelezea wananchi wetu tunatekeleza. Sasa napenda tu nimpe taarifa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetenga hizo bilioni tatu kwenye manispaa ya kwake. Sasa kwa vile hajasoma vitabu ndiyo maana anazungumza mengine. Kwa hiyo, ahudhurie vikao, kwa sababu mipango hii imepangwa kwenye Manispaa yake na akihudhuria pia, ashiriki na asikilize vizuri yanayozungumzwa pale, asiwaze kukimbia kimbia tu, kwa sababu ndiyo uzoefu wa wenzetu, kila mahali, lazima wakimbie.

Sasa sijui kama mwaka 3020 na ngapi huko, kama ikitokea wakachukua nchi, sijui na wenyewe watakuwa wanakimbia! Sijui watakapokuwa wanakimbia, sijui watakuwa wanamwachia nani vikao vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mgogoro wa ardhi kule Lindi, ambalo lilizungumzwa na Kamati, lakini pia na baadhi ya wachangiaji walilizungumza. Tayari tumetoa maelekezo, kwamba, mradi ule usimame, mpaka Tume, kama ambavyo Mkuu wa Mkoa alituambia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anataka kuunda Tume kwenda kufuatilia lile. Mpaka Tume ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itakapokuwa imetoa matokeo yake, ndivyo tutaelekeza vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari nimeshamwandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Lindi, lakini pia kupitia Bunge hili, napenda kuziagiza Manispaa zote pamoja na Wakuu wa Mikoa, wazielekeze Mamlaka zao za Serikali za Mitaa, kwamba Halmshauri haiwezi kuingia makubaliano yoyote ya kifedha bila kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na ni lazima tuone hayo makubaliano nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba miradi yote ya *UTT*, kwa sababu *UTT* kila wanapokwenda na niwaombe wenzetu wa *UTT*, waache kudanganya watumishi wetu kwamba tunachofanya sisi ni *MOU* tu, kwa hiyo, hakuna haja ya kupeleka kuomba ridhaa. Kwa hiyo, tunaomba miradi yote *UTT* isimame na iombe ridhaa kupita kwa Waziri mwenye dhamana. Kwa sababu mnapoomba ridhaa, ndipo tunapojua kwamba mmekubaliana kwa masharti yapi na kama hayo masharti yana manufaa kwa Halmshauri na wananchi wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililozungumza ni mgogoro wa Ilemela. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba suala hili tumeshamaliza, tumeshampelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu ataiandikia Wilaya ya Ilemela kuwajulisha matokeo ambayo tayari tumeyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, akisema kwamba takwimu zangu

zinajikanganya, kwamba kuna eneo tunaonesha kwamba, makadirio ni shilingi bilioni 362 na kwingine tunaonesha bilioni 324. Ni kweli makadirio ya mwanzo yalikuwa ni bilioni 362, lakini baada ya kufanya *mid year review*, makadirio yale yalipungua mpaka shilingi bilioni 324. Pia tunaporipoti makusanyo, mfano kama sasa hivi, tumeonesha makusanyo ya Halmashauri, mpaka mwezi Machi.

Sasa tutakapokuja mwakani, hatutaripoti tena ya mwezi Machi yaliyokusanywa mwaka huu, tutaripoti mpaka mwezi Juni; ndiyo kusema takwimu zitabadirika, zitaonesha ongezeko la *quarter* ya mwisho ambayo itakuwa imekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, Mheshimiwa Mustafa Mkullo yeye aliniletea kwa maandisi kwamba takwimu zilizoonesha kwamba Kilosa ilikuwa ya mwisho, hazikuwa sahihi. Kweli tumekwenda tumeangalia, tumeona ni kweli kwamba, Kilosa kwa muda wote wa miaka mitatu, wastani wao ulikuwa ni asilimia 64, kwa hiyo, tunaomba na wengine waangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi tunazitaka Halmashauri kila baada ya miezi mitatu watuletee taarifa ya makusanyo yao, ili tuweze kuzifuatilia na kuhakikisha kwamba zinafikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala ambalo lililetwa na Mheshimiwa Zuberi Mtemvu, akiomba kwamba Mweka Hazina tuliyempeleka Temeke ambaye alikuwa Manispaa ya Ilala akapelekwa Mvomero, tumwondoe. Ni kweli kwamba lilifanyika hilo, lakini maelekezo yalishatolewa na uhamisho huo Mheshimiwa Mtemvu umefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Msemaji wa Upinzani, pamoja na Naibu wangu kwamba aliisema, alisema kwamba, taarifa kuhusu usimamizi wa fedha, ni dhaifu mno na akasema kwamba taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, akiilinganisha mwaka 2008/2009 na mwaka 2009/2010 kwamba, asilimia ya hatisafi imepungua kutoka asilimia 58 hadi asilimia 59. Ni kweli kwa mwaka huo ilipungua, lakini napeda kumhakikishia kwamba, kuanzia mwaka 2009/2010 mpaka sasa tunapozungumza, masuala ya usimamizi wa fedha katika Halmshauri nyingi yamekuwa yakiboreshwa, pamoja na upungufu uliokuwepo na hata mwenyewe Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, amesema kwamba kumekuwa na mafanikio makubwa sana katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu 2013, imeongezeka kutoka Halmashauri 104, hadi 112, kutoka asilimia 78 hadi 80 na hii yote inatokana na kwamba tunafanya kazi, tunachukua hatua kwa wale ambao wanaonekana kwenda kinyume na matarajio yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mwenyekiti alilizungumza na Msemaji wa Kambi ya Upinzani walizungumzia suala la uwepo wa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam na kwamba lazima tuhakikishe kwamba tunachukua hatua kuondoa msongamano ule. Napenda kukuhakikishia kwamba suala hili tunalifanyia kazi na hatua tunazozichukua ni pamoja na ujenzi wa barabara za mzunguko (*ring roads*), utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka, pia uboreshaji wa barabara mlisho yaani (*feeder roads*), kwa kupitia mradi maalum ambao tumeuanzisha wa uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam, DMDP. Kwa wenzetu wa Dar es Salaam wanaufahamu huu mradi, lakini pia suala la ujenzi wa *flyovers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliombwa kwamba Halmashauri ambazo hazifanyi vizuri kwenye ukusanyaji wa kodi ya huduma, waende wakajifunze katika Halmashauri nyingine. Ushauri huo tunaupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo lilizungumzwa, kuhusu Mkurugenzi wa Ifilima, aondolewe na apelekwe sehemu nyingine. Huu siyo utaratibu wa kuwaondoa Wakurugenzi, tungekuwa tunafanya hivyo, kila mtu angekuja hapa anasema nataka yule aondoke. Kama Mkurugenzi anaonekana ana upungufu pale alipo, tunaomba mpitishie kwenye Baraza la Waheshimiwa Madiwani, mkipitisha kwenye Baraza na tuhuma zake hizo zielezwe, halafu ndiyo tuletewe, lakini siyo mtu mmoja mmoja. Kwenye Halmashauri kila kitu kinaamuliwa kupitia Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Cheyo, kama anaona Mkurugenzi ana matatizo hayo, pelekeni, mjenge hoja, mpeleke kwa Mkuu wa Mkoa, naye ataweza hata kutushauri nini cha kufanya.

Pia napenda nichukue nafasi hii kuelezea, kwa maeneo mengine, kwa sababu kumekuwa na uzoefu sasa hivi, mtu anaandika barua, Mkurugenzi huyu simtaki, mpeleke sehemu nyingine, Mweka Hazina huyu simtaki, mpeleke sehemu nyingine, DAS huyu simtaki, mpeleke sehemu nyingine. Aaa! Kama mtu hana uwezo katika eneo lake, sisi hatuna utaratibu wa kuhamisha wasioweza, kama hana uwezo achukuliwe hatua hapo hapo. (*Makofi*)

Kama hayupo katika mamlaka yenu kumchukulia hatua, basi tujulishwe ili na sisi, lakini lazima hoja zijengwe kupitia katika Mabaraza au mamlaka za nidhamu. Mfano kama DAS, RAS ndiyo mamlaka yake ya nidhamu, hakuna sababu ya kuturejeshea sisi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa, tulielekezwa kwamba, Halmashauri zetu zihakikishe kwamba zinatenga asilimia 60 mapato yao ya ndani, kuhakikisha kwamba zinakwenda kutekeleza miradi ya

maendeleo. Kwa kiasi kikubwa suala hili Halmashauri imelitekeleza na Wajumbe wa Kamati ya TAMISEMI na wenyewe ni mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa ni kwamba, tuwe na mazingira wezeshi kwa Wamachinga, tayari Mheshimiwa Naibu amelijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa ni suala la kuboresha sheria, kukosekana kwa sheria ndogo ya huduma, ambako kunasababisha kukosa mapato. Tumeshazielekeza Halmashauri zote, kupitia sheria zao ndogo ndogo, zile ambazo zimepitwa na wakati, basi wahakikishe kwamba wanazirekebisha zinaendana na mazingira ya sasa na wale ambao hawana sheria zinazoendana labda na utozaji wa huduma na wenyewe wahakikishe kwamba wanatunga ili waweze kupata kodi hiyo ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lilizungumzwa ni kwamba, Ofisi za Wakaguzi wa Nani wa Halmashauri ziwe nje ya boma la Halmashauri. Wakaguzi wa Ndani ni washauri wa Maafisa Masuuli, kwa hiyo, huwezi ukawatenganisha, ni sehemu ya Menejimenti ya Halmashauri na wamepewa meno ya kufanya kazi. Kwa hiyo, wanachotakiwa ni lazima wawepo katika majengo ya Halmashauri ili waweze kumshauri Mkurugenzi ili kuweza kuzuia matumizi mabaya katika Halmashauri waliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walisema, Wakurugezi wa Halmashauri, wapewe meno ya kuweza kuwachukulia hatua watumishi walio katika maeneo yao. Napenda kukuhakikishia kwamba, Wakurugenzi wa Halmashauri wana meno, Mabaraza ya Madiwani yana meno, tukiwemo pamoja na sisi, tunachotakiwa ni kushiriki na kuhakikisha kwamba tunatimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.
(Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nakushukuu sana. Sasa namwita Mheshimiwa Lukuvi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa muda ulionipa. Kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge, sisi tunachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo kama mnavyojua ilikuwa na maeneo matatu.

La kwanza, TAMISEMI ambalo Mheshimiwa Waziri wa Nchi ameeleza na Manaibu. La pili ni eneo la uwezeshaji na uwekezaji ambalo Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kesho atalitolea ufafanuzi, lakini eneo lingine ni eneo la sera, kwa

maana ya shughuli za uratibu wa utekelezaji wa Ilani ya Chama na uratibu wa shughuli za Serikali pamoja na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namsaidia, nachangia machache, lakini maeneo mengi makubwa katika eneo hili atamalizia mtoa hoja kesho. Kwa hiyo, naomba wale wote ambao hawatasikia maelezo yoyote kuhusu daftari na uandikishwaji wake, *biometric* na namna zake na jinsi litakavyokuwa na vifaa hivi vitakuwaje, vitatumikaje na masuala yote yale mliyozungumzia habari za mikutano ya Lindi na Mtwara na masuala ya mwisho ambayo Mheshimiwa Kafulila kasema Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho ataeleza ni nini Serikali inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza nataka nizungumzie eneo la maafa kwa ufupi. Kwanza, niwape pole sana watu wote waliofikwa na maafa ya aina mbalimbali mwaka huu na hasa yaliyosababishwa na mvua nyingi. Tulianza na Morogoro, tukaenda Dodoma, sehemu nyingi sana, hata kwangu kule Ismani tumepata maafa haya. Kwa hiyo, nawapeni pole sana, hakuna mtu aliyepanga lakini Mwenyezi Mungu ameamua mwaka huu kutupa baraka ya aina yake.

Sasa Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia juu ya haya na sehemu nyingi Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wamejitahidi sana kurudisha hali katika hali ya kawaida, kwa uwezo wao mdogo, lakini pia kwa misaada michache ambayo wamechangisha kutoka wananchi wa mikoa yao. Kwa hiyo, nawashukuru sana Viongozi wa Mikoa kwa sababu hawa ndio wenye watu, sisi tunaratibu tu huku juu, kwa kazi kubwa waliyoifanya na ndiyo hata sheria inataka kwamba shughuli zote za maafa kwanza ziwe zinashughulikiwa na Kamati za Maafa zilizopo katika maeneo maafa yalipotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu Wakuu wa Mikoa wametusaia sana katika mikoa yote ambayo maafa yametokea, lakini pia kulikuwa na hoja kwamba Jeshi la Wananchi liombwe lishiriki katika shughuli za maafa na hasa katika maeneo mbalimbali ya baharini. Nao nataka niwapongeze sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania, wameshiriki kila mahali walipoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tuliwaomba Morogoro, Mheshimiwa Bendera aliwaomba pale walikwenda wakamsaidia masuala mbalimbali ya *logistics* na tunajua kila mahali; iwe maafa ya baharini, nchi kavu ya mvua, ya njaa, kila mahali wanakwenda. Kwa hiyo, Jeshi la Wananchi tunawapongeza sana. Nataka kuwaambia kila tunapowaita wanakwenda na hata sisi Kitengo cha Maafa kwa taarifa yenu kinaongozwa na Luteni Jenerali wa Jeshi. Mheshimiwa Rais alimleta huyu kwa sababu alijua kwamba hawa jamaa wamejengeka katika mafunzo na ari yao, wako tayari kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yamezungumzwa maafa yaliyotokea Lindi na Mtwara kuharibiwa nyumba zao na maafa mbalimbali ya kuchomewa nyumba na mali. Nataka kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge waliozungumza haya kwa uchungu, hasa Mheshimiwa Anna Abdallah kwamba Serikali tunafahamu yaliyotokea na tumefanya tathmini. Kwa Mtwara tunajua kwamba mali zilizoharibika zina thamani ya shilingi bilioni nne nukta mbili na Lindi kwa Liwale peke yake ni kama milioni mia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali hizi ambazo zimeharibiwa, Serikali tumeshawasiliana na Kamati ya Maafa ya Taifa imeshapitia na tumepeleka mahitaji haya Hazina ili Hazina iweze kutoa fedha tuweze kurudisha mali hizi kuwa katika hali ya kawaida. Hata hivyo, kwa madai ya Mtwara, yale yanayohusu Mtwara yenyewe tu tumeyarudisha kwa RAS ili yahakikiwe zaidi na Mthamini Mkuu wa Serikali; lakini Lindi, kwa maana ya Liwale tumeyapokea na Masasi tunayo na tumeshayapeleka na tunaamini bila shaka Mungu atamjalia Mheshimiwa Waziri wa fedha atapata fedha hizi, tutawapa wanaohusika na tutafanya haya ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama tulivyosema kuhusu maafa kwa ujumla, ni kwamba, tunaangalia upya sheria ile ili angalau tuirekebishe vizuri iweze kujibu changamoto zote ambazo tumezipata sasa kupitia uzoefu tulio nao.

La pili imezungumzwa sana juu ya suala la mpiga chapa. Kwenye Kamati ya Katiba na Sheria wamezungumza sana hili, lakini tumekubaliana kwenye Kamati kwamba Mpiga Chapa ajitahidi, pamoja na ubunifu anaoufanya tutafute wabia wengine ambao wanaweza kuingia ubia na mpiga chapa ili tufanye kazi kwa pamoja, isibaki tu Mpiga Chapa kama mali ya Serikali. Tutaendelea kufanya zile *core function* za Serikali za Mpiga Chapa, lakini eneo lile ni kubwa na tunafikiri tunahitaji vile vile mwekezaji afanye kazi ya kuwekeza pale ili mitambo yetu na hadhi ya Mpiga Chapa iweze kufanana na hali halisi, Serikali peke yake haiwezi kwa sasa kukamilisha uwekezaji uliopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajitahidi, lakini tumempa kibali atafute wawekezaji ili tuone namna gani tunaweza tukaingia nao ubia waweze kuendesha shughuli zile. Hata hivyo, pia imetolewa rai kwamba Wizara ya Fedha wasicheleweshe fedha zao za *retention* ili kumwezesha Mpiga Chapa kuweza kutekeleza kazi za wateja wake kwa wakati. Kwa hilo tunaendelea kuwasilianana Hazina ili fedha anazozipata kwa kazi zake arudishiwe haraka ili aweze kufanya kazi zile ambazo zimempatia fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu linahusu CDA. Tunajua madhumuni ya kuanzishwa CDA na bahati nzuri hata kwenye Bunge la Katiba baadhi ya Wajumbe wamependekeza kwenye Katiba, ambalo halikupendekesha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kwenye rasimu, kwamba itamkwe kwamba Makao Makuu ya Serikali ni Dodoma. Nafikiri mpaka tutakapomaliza rasimu ya mwisho itakayokwenda kwa wananchi jambo hilo tutalipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi yamefanywa katika kipindi cha kuanzia 2011 mpaka 2014, Serikali kupitia CDA imetumia zaidi ya shilingi bilioni ishirini na tano nukta sita; lakini pia kwa Serikali nzima imetumia mara mbili kujenga miundombinu hapa, tumetumia bilioni ishirini na tano kupitia CDA, lakini tumetumia fedha kama hizi kupitia Manispaa ya Dodoma kwa ajili ya kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa CDA peke yake tumejenga kilomita 47.5 za lami, lakini tumejenga ujenzi wa mitaro ya maji yenye urefu wa kilomita 6.4, kufungua barabara zenye urefu wa kilomita 105, pia tumeweza kupima viwanja vipya 1850. Hata hivyo, mwaka huu wa fedha 2014/2015 tutaongezewa tena shilingi bilioni sita nukta saba kwa ajili ya kazi hiyo hiyo. Hii ni kuonesha kwamba bado nia ya Serikali ya kupafanya Dodoma kuwa Makao Makuu ipo, na kazi inayoendelea sasa ni kuimarisha miundombinu ili mahali Dodoma pawe pazuri na salama zaidi kuweka Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pia tumeshamaliza *master plan* mpya ya Dodoma, na sasa eneo ambalo limependekezwa kujenga makao makuu ni eneo ambalo linaanzia pale lhumwa, pale kwenye Kambi ya Jeshi mpaka Chamwino, kwa hiyo lile ndilo eneo litakalojengwa makao makuu ya Serikali kwa mujibu wa *master plan* mpya. Eeh! Hiyo kengele vipi, ya kwanza dakika zote hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele yako mzee inaota ota, inaotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu nataka nizungumzie kidogo juu ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Sisi tunajua, tunampongeza sana Mheshimiwa Jaji Mtungi, tangu ameingia amejitahidi sana kuwa karibu na Vyama vya Siasa na kufanya kazi nzuri, lakini limezungumzwa dogo juu ya TCB, tulikuwa hatupati fedha. Najua akina Mbatia na wengine ni wadau sana wa TCB, lakini mwaka huu kwa mara ya kwanza tumewatengea shilingi milioni mia nane kwa ajili ya kuimarisha kituo hiki.

Hata hivyo masuala yanayohusu kuzuiwa kwa mikutano Lindi na Mtwara kama Mheshimiwa Mbowe mlivyosema, nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho atatoa maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine jipya nilitaka kutoa taarifa tu kwamba sasa Vyama vya Siasa vilivyosajiliwa ni 22. Jana Mheshimiwa Msajiri wa Vyama Jaji Mtungi amesajili Chama kipya Pinzani kinaitwa *Change and Transparency*

Tanzania (ACT). Kwa hiyo tunawakaribisha sana chama hiki kipyua cha 22, kimekuja na nguvu kidogo. Tunakaribisha uwanjani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililozungumzwa linahusu Bunge. Nataka tu kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba kama mtakavyokumbuka juzi, kabla hatujaingia hapa siku ya Jumanne, tulijitahidi kutoa *briefing* ya mambo yote haya ambayo mmezungumza, habari ya bima na tumewaambia watu wa *Jubilee Insurance* wapite kwenye Kamati zetu mbalimbali kutoa ufafanuzi juu ya mambo yao ya bima. Kwa hiyo, naomba haya mambo ya Bunge tutaendelea kuyatolea ufafanuzi kwa kadiri tunavyoishi hapa.

Masuala ya UKIMWI yamesemwa mengi hapa, Mheshimiwa mmoja hapa amezungumzia hata dawa kwamba tuziache. Hatuwezi kuziacha, dawa lazima zitolewe, elimu itolewe, yote lazima yaendeleo, lakini naishukuru sana Kamati ya UKIMWI kwa kazi nzuri inayofanya ya kusimamia jambo hili. Tumekubaliana kwenye Kamati ya UKIMWI sasa watasimamia kwa dhati fedha zote na rasilimali zilizopelekwa kwenye Halmashauri na Wizara zote ambazo zinahusiana na mapambano dhidi ya UKIMWI.

Kwa hiyo Wizara wasishangae kuona Kamati ya Bunge au inakwenda katika Halmashauri halafu inaulizia habari ya fedha ya mapambano ya UKIMWI. Hawajafanya kazi kubwa sana, lakini sasa tumepeana changamoto kwamba, fedha zote na rasilimali zote za umma ambazo zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo lazima Kamati ya UKIMWI iende kuzisimamia kwa sababu ni jukumu lake la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu na nirudie tena labda kufafanua lile suala nililoanza nalo la maafa. Wengi wameuliza kwamba utaratibu wa namna ya kupata misaada ya maafa kwa kadiri inavyotokea. Labda utaratibu niwakumbushe kwamba, Waheshimiwa Wabunge mara nyingi mmekuwa mnaleta barua kwetu, lakini utaratibu wetu ni kwamba maafa yakitokea kwenye maeneo, *Government works on paper*, tungependa Kamati zile za Maafa za Wilaya ziandike, zifanye tathmini zipeleke mkoani, halafu mkoani ndio wanaandika kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa sababu mkituletea sisi moja kwa moja bado tungependa kwamba maelezo yanayoambatana na tathmini halisi lazima yatoke kwenye ofisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria tuliyoitunga, tunazo Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya. Kwa hiyo, mkitupa taarifa sisi, ingawa hatuwaambii, lakini mjue huwa tunazirudisha tena kule mikoani ili angalau watuletee tathmini ya kuanzia ili na sisi tuweze kushirikiana na mikoa kwa sababu kwa vyovyote vile, kama ni rasilimali, kama ni fedha lazima tutazipeleka mikoani ili ziweze kutekeleza wajibu huo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo, wakati mwingine inakuwa rahisi zaidi kama mkisikia jambo hapa ni vizuri kumpigia Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa au RAS itoke barua kule haraka, kwa sababu hata mkituambia sisi bado huwa tunarudisha sauti kule ili waweze kutuletea taarifa hizo ili tuweze kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu wote watatu waliotangulia, maelezo haya sisi tumeshaandika yote kabisa, maelezo yote na hoja zote tumeshaziandika. Tunachoweza kuahidi tu ni kwamba, kwa muda mfupi uliopo hapa, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho hataweza kutolea hoja hizi zote maelezo, lakini tutaziandika kwenye vitabu, halafu tutawagawia kabla ya Mkutano huu wa Bunge haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa William Mgimwa dakika mbili na nusu.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ningependa sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, kwa kunipa afya njema kuweza kuwepo mahali hapa, lakini vile vile ningependa sana kukishukuru Chama cha Mapinduzi kwa namna walivyoweza kutuunga mkono vijana kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kuliongoza Taifa letu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa sana kuenzi uongozi wote wa Chama cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya chini ya uongozi wa Rais wetu shupavu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, ningependa tu bila kusahau kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kalenga kwa kuwa wameniunga mkono kwa hali na mali kuhakikisha kwamba Jimbo la Kalenga linakuwa tena chini ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu na ninachoomba tu ni kuhakikisha kwamba, tutakwenda kuifanyia kazi, lakini vile vile ningependa tu kuhakikisha kwamba yale au changamoto zile ambazo zipo katika Jimbo langu zinakwenda kutimizwa na Chama cha Mapinduzi nina hakika kabisa kitakwenda kufanya kazi yake kwa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, kutokana na muda ningependa kurudisha kwa Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Ridhwan Kikwete!

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nigepele kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri mpaka leo hii bado nadunda. Pili, niwashukuru sana wazazi wangu kwa malezi waliyonipa, familia yangu hasa mke wangu mpendwa mama Aziza, Aziza na Aiman kwa mapenzi yao na baraka tele walizonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwanza kwa kuniamini, lakini pili kupigana kuhakikisha kwamba Jimbo la Chalinze linaendelea kuwa la CCM. Nakishukuru sana Chama changu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, japo si mwisho kwa umuhimu, wapiga kura wa Jimbo la Chalinze wamefanya jambo ambalo ndani ya Chalinze si geni, ni utaratibu wetu kushinda namna ile. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kuendelea kukipa heshima Chama cha Mapinduzi. Pia naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi wanavyoendelea kutupa ushirikiano wana Chalinze, japo yapo maeneo ambayo ningependa ninaposimama nafasi hii japo muda hautoshi niyagusie kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko eneo katika jambo zima la afya, ningependa sana, ili tuendeleo kushirikiana. Zipo changamoto katika eneo la elimu hususan kwenye madawati ya wanafunzi, nyumba za Walimu, lakini pia zipo changamoto katika miundombinu ya barabara.

Ninavyojua sisi kwetu ni waathirika wakubwa sana wa mafuriko na hasa mafuriko haya ningependa pia niwape pole wale wananchi wote wa Tanzania ambao kwa namna moja au nyingine wameathirika sana na mafuriko haya, hasa ndugu zangu, wajomba zangu wa kule Lindi na ndugu zangu wa Mbeya poleni sana, ndiyo kazi ya Mungu, kwenye neema nako kuna shari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme tu kwamba, naunga mkono hotuba nzuri ya Waziri Mkuu ambayo kwangu mimi kwa Jimbo la Chalinze inatoa neema mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kazi zote zilizopangwa leo zimekwisha. Malalamiko mengi yamekuja kwenye meza kuwa majina ya watu yamerukwa, ni kweli majina yalirukwa toka asubuhi. Wabunge humu ndani hamkai, mnakuja muda mnaotaka, mkiingia humu ndani mnataka kuharibu ratiba ya meza, meza haiwezi kuyumba, meza itafuata watu waliokuwa ndani,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

wale waliokuwepo ndio watakaohudumiwa. Ukichelewa ukirudi omba Mungu kama utapata nafasi.

Naomba kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 9 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*